

**UTENDAJI WA KIDRAMA WA RIWAYA YA *HAINI* YA
SHAFI ADAM SHAFI 2003**

**NA
ANNE MWARI MUNYIOKI**

**TASNIFU ILIYOWASILISHWA KWA AJILI YA KUTIMIZA BAADHI YA
MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI KATIKA CHUO KIKUU CHA MOI
KITIVO CHA SANAA NA SAYANSI JAMII IDARA YA KISWAHILI NA
LUGHA NYINGINE ZA KIAFRIKA**

CHUO KIKUU CHA MOI

NOVEMBA, 2018

IKIRARI

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijawahi kuwasilishwa kwa minajili ya utahini katika chuo kikuu chochote kile. Ni kosa kutoa nakala ya kazi hii bila idhini ya mwandishi na/au Chuo Kikuu cha Moi Eldoret.

Anne Mwari Munyioki**SASS/PGK/03/15**

TAREHE**WASIMAMIZI**

Kazi hii imewasilishwa kwa minajili ya kutahiniwa kwa ridhaa yetu kama wasimamizi wa Chuo Kikuu cha Moi.

Bw. Mumbo C.K**Idara ya Kiswahili****Chuo Kikuu Cha Moi**

TAREHE

Dkt. Magdaline N. Wafula**Idara Ya Kiswahili****Chuo Kikuu Cha Moi**

TAREHE

TABARUKU

Kwa:

Warren Van Genderen na mkewe Martha

(Opa und Oma)

SHUKRANI

Natoa shukrani zangu za dhati kwa wote waliochangia katika kufanikisha utafiti huu.

Kwanza kabisa nawashukuru wasimamizi wangu Dkt. Magdaline Wafula na Bw. Collins Mumbo kwa kujitolea na kutochoka kuisoma kazi yangu na kwa mawaidha ya busara waliyonipa. Nawashukuru wahadhiri wote wa Idara ya Kiswahili na Lugha Nyingine za Kiafrika ya Chuo Kikuu cha Moi kwa kunihamasisha nijiendeleze kitaaluma.

Nawashukuru vilevile wazamili wenzangu Joan, Jackline, Milkah, Kajuju na Kondoro; wanawake hoyee!

IKISIRI

Utafiti huu umeshughulikia utendaji wa kidrama katika riwaya ya *Haini* ya Shafi Adam Shafi (2003). Katika kuchunguza utendaji wa kidrama katika riwaya hii, tulibainisha vipengele vya utendaji vilivyotuwezesha kutathmini kuigizika kwa riwaya teule. Malengo ya utafiti huu ni pamoja na: Kubainisha lugha ya majibizano ilivyotumika na utendaji wa wahusika katika riwaya ya *Haini*, kuchanganua masimulizi ya kiutendaji na taswira za kifilamu katika riwaya ya *Haini* na hatimaye kutathmini ufaafu wa vipengele vya utendaji katika utendaji wa kidrama wa riwaya ya *Haini*. Kutokana na malengo haya, utafiti huu uliegemea nadharia tete kwamba lugha ya majibizano imetumika kwa kiwango kikubwa na wahusika watafanikisha utendaji wa kidrama wa riwaya ya *Haini*, kwamba masimulizi ya utendaji na taswira za kifilamu zimetumika katika riwaya hii na kwamba vipengele vya utendaji vitafanikisha utendaji wa kidrama wa riwaya teule. Utafiti huu umeongozwa na Nadharia ya Utendaji iliyoasisiwa na Wallace Bacon na kuendelezwa na Victor Turner na Richard Schechner. Nadharia hii inasisitiza kwamba pana uhusiano wa karibu kati ya utendaji na kazi ya kifasihi, na kwamba matini ya kidrama huwasilisha ujumbe wake vyema zaidi kupitia uigizaji wake kwenye jukwaa. Watafiti wa awali kuhusu suala la utendaji wameshughulikia utendaji katika fasihi simulizi, tamthilia na sanaa za maonyesho. Ingawa riwaya imetafitiwa kwa kina, tafiti nyingi ni zile zinazogemea fani na maudhui. Tofauti na tafiti hizi, utafiti huu umejikita katika utendaji wa kidrama katika riwaya, mintarafu riwaya ya *Haini* ya Shafi Adam Shafi (2003). Huu ni utafiti wa kiuhakiki, na hivyo mbinu zilizotumiwa kukusanya data ni utafiti maktabani ambapo tulisoma riwaya teule kwa makini na kudondoa vipengele vya utendaji kama vinavyojitokeza. Pamoja na maktaba ya Margaret Thatcher ya Chuo kikuu cha Moi, tulizuru maktaba zingine, zikiwa pamoja na maktaba za Chuo Kikuu cha Nairobi na Kenyatta. Tulisoma makala mbalimbali zilizoandikwa kuhusu mada ya utafiti, vitabu na majarida. Hatimaye, tulitembelea mitandao na tovuti mbalimbali zinazozungumzia utendaji pamoja na kupakua makala mbalimbali yanayohusu utendaji. Mbinu ya kithamano ilitumika katika uchanganuzi wa data tuliyokusanya na kueleza matokeo ya utafiti. Matokeo ya utafiti wetu yalidhihirisha kwamba iwapo baadhi ya vipengele vya utendaji tulivyobainisha katika riwaya ya *Haini* vitafanyiwa ukarabati, utendaji wa kidrama wa riwaya hii utafanikiwa iwapo itafanyiwa ufaraguzi na kutendwa kwenye jukwaa. Mbali na utafiti huu kuweka wazi suala la mwingiliano tanzu (riwaya na drama), utaongeza maarifa yaliyopo kuhusu drama na fasihi kwa jumla.

ABSTRACT

This research set out to examine the aspect of dramatic performance as portrayed in the swahili novel *Haini* by Shafi Adam Shafi (2003). To achieve this, the various dramatic elements in the novel have been identified and analysed, after which the performance of the novel *Haini* was evaluated. The study aimed at firstly, examining the success of characters and the deployment of dialogue in the novel. Secondly, investigating the cinematographic images and performance-description in the novel and finally, interrogating the success of its dramatic performance. Based on these objectives, the study was guided by the following hypotheses: one, that the characters in the novel *Haini* successfully contribute to its dramatic performance and that dialogue has been widely used in the novel, that cinematographic images and performance description feature in the novel and that its performance will be a success. The study is guided by the Performance theory by Wallace Bacon, which has also been expounded on by Victor Turner and Richard Schechner. The theory puts emphasis on the performance of literary works and claims that a bigger audience benefits from the performance than the reading of the same work. Most studies have focused on the performability the Swahili play as well as oral literature. However, very little has been done as regards the performance of the Kiswahili novel and based on that, this study sought to examine the aspects of dramatic performance in the swahili novel, *Haini*. This is a textual analysis research, hence most research basically took place in the library. The selected novel was critically read and the various performance aspects identified and analysed. We made use of other libraries-apart from the Margaret Thatcher library in Moi University-such as the University of Nairobi and Kenyatta University libraries. Here, we studied books, journals as well as various research works in regards to the study topic. We also made use of the internet and websites relevant to the area of study. Being a qualitative study, qualitative techniques were used in data analysis. From the study, we found out that if some of the aspects of drama we identified from the novel *Haini* are, improvised, then its dramatic performance will be a success. Aside from the study being based on intertextuality, it will add new knowledge to the existing knowledge of drama and Kiswahili literature in general.

YALIYOMO

| | |
|--|-----------|
| IKIRARI | ii |
| TABARUKU | iii |
| SHUKRANI..... | iv |
| IKISIRI | v |
| ABSTRACT..... | vi |
| YALIYOMO | vii |
| UFAFANUZI WA ISTILAHU | x |
| SURA YA KWANZA | 1 |
| MISINGI YA UTAFITI | 1 |
| 1.0 Utangulizi..... | 1 |
| 1.1 Usuli wa Suala la Utafiti | 1 |
| 1.2 Suala la Utafiti | 5 |
| 1.3 Malengo ya Utafiti | 5 |
| 1.4 Nadharia Tete..... | 6 |
| 1.5 Sababu za Uteuzi wa Mada..... | 6 |
| 1.6 Umuhimu wa Utafiti | 7 |
| 1.7 Msingi Wa Kinadharia..... | 8 |
| 1.8 Mapitio ya Maandishi | 14 |
| 1.9 Upeo Wa Utafiti | 26 |
| 1.10 Mbinu za Utafiti..... | 27 |
| 1.10.1 Uteuzi wa sampuli..... | 27 |
| 1.10.2 Mbinu za ukusanyaji data..... | 27 |
| 1.11 Uchanganuzi wa Data | 28 |
| 1.12 Hitimisho..... | 29 |
| SURA YA PILI..... | 30 |
| SHAFI ADAM NA UANDISHI WA <i>HAINI</i> | 30 |
| 2.0 Utangulizi..... | 30 |
| 2.1 Maisha ya Shafi Adam Shafi | 30 |
| 2.2 Shafi Adam Shafi na Uandishi Wake | 32 |
| 2.3 Historia ya Riwaya ya <i>Haini</i> | 38 |
| 2.3.1 Sababu za kuandikwa kwa Riwaya ya <i>Haini</i> | 38 |
| 2.4 Mukhtasari wa Riwaya ya <i>Haini</i> | 41 |

| | |
|--|------------|
| 2.5 Hitimisho..... | 44 |
| SURA YA TATU..... | 45 |
| LUGHA YA MAJIBIZANO NA WAHUSIKA..... | 45 |
| 3.0 Utangulizi..... | 45 |
| 3.1 Lugha Ya Majibizano | 45 |
| 3.1.1 Majibizano kama Nyenzo ya Kuhoji..... | 47 |
| 3.1.2 Majibizano kama Nyenzo ya Kupasha Habari | 52 |
| 3.1.3 Majibizano kama Nyenzo ya Kuliwaza | 56 |
| 3.1.4 Majibizano kama Nyenzo ya Kushawishi | 60 |
| 3.1.5 Majibizano kama Nyenzo ya Kuhamasishana | 61 |
| 3.1.6 Majibizano kama Nyenzo ya Kuendesha Mashtaka | 64 |
| 3.2 Wahusika..... | 68 |
| 3.2.1 Mahaini..... | 70 |
| 3.2.2 Mashahidi | 89 |
| 3.2.3 Wakubwa wa Magereza | 95 |
| 3.2.4 Washikadau Mahakamani | 98 |
| 3.2.5 Mahakimu..... | 103 |
| 3.2.6 Waathiriwa wa Uhaini..... | 105 |
| 3.3 Hitimisho..... | 110 |
| SURA YA NNE | 112 |
| MASIMULIZI YA UTENDAJI..... | 112 |
| 4.0 Utangulizi..... | 112 |
| 4.1 Masimulizi ya Utendaji..... | 112 |
| 4.1.1 Masimulizi Ya Utendaji Kuhusu Mateso | 113 |
| 4.1.2 Masimulizi ya Utendaji Kuhusu Usafiri..... | 118 |
| 4.1.3 Masimulizi ya Utendaji Mahakamani | 121 |
| 4.1.4 Masimulizi ya Utendaji wa Kifaraja | 125 |
| 4.2 Vimulimuli Na Kiza..... | 128 |
| 4.2.1 Vimulimuli | 128 |
| 4.2.2 Kiza | 134 |
| 4.3 Sauti na Kimya..... | 142 |
| 4.3.1 Sauti..... | 142 |
| 4.3.2 Kimya..... | 151 |

| | |
|--|------------|
| 4.4 Hitimisho..... | 157 |
| SURA YA TANO | 158 |
| TASWIRA ZA KIFILAMU | 158 |
| 5.0 Utangulizi..... | 158 |
| 5.1 Taswira..... | 158 |
| 5.1.1 Taswira za Kifilamu | 158 |
| 5.2 Mandhari | 166 |
| 5.2.1 Mahaini Walikozuiliwa | 171 |
| 5.2.2 Mahaini Wanakohojiwa na Kushawishiwa | 174 |
| 5.2.3 Mandhari Wanakotesewa Mahaini..... | 176 |
| 5.3 Maleba..... | 180 |
| 5.3.1 Mavazi Ya Mahaini | 181 |
| 5.3.2 Sare za Mahaini | 184 |
| 5.3.3 Mavazi ya Polisi | 184 |
| 5.3.4 Sare za Maafisa wa Usalama..... | 185 |
| 5.3.5 Mavazi ya Khadija na Familia Yake | 187 |
| 5.3.6 Wahusika Kuwa Uchi..... | 187 |
| 5.4 Hitimisho..... | 189 |
| SURA YA SITA..... | 190 |
| MATOKEO, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO | 190 |
| 6.0 Utangulizi..... | 190 |
| 6.1 Muhtasari Wa Utafiti | 190 |
| 6.2 Matokeo ya Utafiti | 197 |
| 6.3 Hitimisho..... | 197 |
| 6.4 Mapendekezo | 198 |
| MAREJELEO | 200 |

UFAFANUZI WA ISTILAHU

Sanaa za Maonyesho

Sanaa za Maonyesho ni sanaa ambayo kwa kiasi kikubwa huhusu utendaji hai, ambapo kitendo fulani hulenga kuibua hali ya kidrama.

Drama

Drama ni hali ya kuishi tendo fulani kwenye jukwaa au mahali popote pale pa kuigizia kwa kipindi maalum. Ni uigizaji wa kisanaa wa maisha ya watu katika jamii kwa lengo la kuwasilisha ujumbe maalum.

Utendaji

Utendaji ni kufanya jambo. Katika muktadha wa drama, utendaji ni uigizaji wa tendo fulani mbele ya hadhira. Yaani, uwasilishaji wa kazi ya sanaa mbele ya hadhira kwa lengo la kuwasilishia hadhira hiyo ujumbe maalum, mbali na kuiburudisha. Utendaji hujibainisha zaidi kwenye jukwaa.

Utendaji wa Kidrama

Kutokana na maelezo ya drama na utendaji hapo juu, utafiti huu unachukulia utendaji wa kidrama kama uwasilishaji wa matini za kuigizaji mbele ya hadhira. Uwasilishaji husika ufanywe kwa njia ya kidrama, kwa kujumuisha vipengele vya utendaji vinavyofanikisha aina hii ya utendaji.

Taswira za Kifilamu

Taswira za kifilamu ni hali au mchakato wa kujenga picha za kifilamu kwenye mawazo au fikra za hadhira. Kazi ya kisanaa ambamo taswira za kifilamu zimetumika humfanya msomaji kupata hisia za utazamaji filamu ya kazi husika ya fasihi na sio kuisoma au kuisigiza tu.

Maleba

Maleba ni mavazi au mapambo yanayotumiwa katika uigizaji ili kuwatambulisha wahusika. Maleba pia hutofautisha majukumu ya wahusika katika uigizaji. Hali hii husaidia kuwasilisha ujumbe.

Mapiku

Mapiku hujumuisha ngozi za wanyama kama vile chui, majitu, ndege, na zinginezo na hutumiwa katika drama kusisitiza tendo fulani pamoja na kuonyesha tukio lisilo la kawaida katika drama hiyo.

Riwaya

Riwaya ni kazi ya kisanaa iliyoandikwa kwa lugha ya nathari na husimulia maisha ya jamii kwa jumla. Inaweza kujengwa kwenye misingi ya kihistoria na hivyo kuibua mambo yaliyomo katika mazingira anamoishi mtu. Utunzi wake hutegemea uwezo wa mtunzi wa kuibua mambo yaliyomo katika mazingira yake.

Lugha ya majibizano

Hii ni lugha inayotumiwa aghalabu katika kazi za kidrama. Katika kazi za kinathari kama ilivyo riwaya, lugha ya majibizano hutumiwa kuipa uhai hadithi kwa kuwapa wahusika fursa ya kuwa watendaji. Hali hii huwezesha kueleweka zadi kwa masimulizi ya kinathari.

SURA YA KWANZA

MISINGI YA UTAFITI

1.0 Utangulizi

Sura hii ya kwanza inajadili usuli na suala la utafiti, sababu zilizopelekea kuteuliwa kwa mada ya utafiti, umuhimu wa utafiti, malengo ya utafiti huu, nadharia tete na nadharia iliyotuongoza katika utafiti wetu. Tumeleza vilevile yaliyoandikwa kuhusu mada yetu ya utafiti, upeo wa utafiti pamoja na mbinu za utafiti zilizotumika.

1.1 Usuli wa Suala la Utafiti

Wapo wataalam mbalimbali walioeleza dhana ya utendaji katika miktadha mbalimbali. Wapo baadhi wanaoeleza utendaji katika muktadha wa sanaa za maonyesho, wengine katika drama huku baadhi wakieleza utendaji kama dhana pana zaidi ya sanaa tendi.

Schechner (2013) anarejelea utendaji kama tabia mwigo. Anaeleza zaidi kwamba tabia mwigo ni tofauti na ile ya mtu mwenyewe. Ni kile ambacho mtu huambiwa afanye, kama kwamba yeye ni mtu mwingine. Tabia mwigo inajumuisha aina nyingi za matendo. Hakika, tabia zote huwa zimeigwa. Hujumuisha tabia na matendo ambayo huwa yameshafanywa tayari hapo mwanzo. Hata hivyo, wakati mwingi watu huwa hawajui kwamba washatenda [katika maisha yao ya awali kile wanachokitenda sasa]. Anachokiita tabia mwigo Schechner, katika maelezo yake haya, ndicho tunachokiita utendaji.

Soyinka (1976) anaeleza kuwa utendaji na hadhira ni vipengele vya kimsingi katika drama. Aidha, vipengele hivi havipatikani katika sanaa nyingine kama vile uchoraji. Hivyo, kwa maoni yake, sanaa za maonyesho ndiyo sanaa ya kimapinduzi zaidi

ijulikanayo na mwanadamu. Ni kweli kwamba sanaa za maonyesho huhusisha utendaji ambao umekusudiwa kuleta mageuzi, na huwa na athari kubwa kwa mwanadamu zaidi ya ilivyo katika sanaa zingine.

Madison na Hamera (2005) wanaeleza kuwa kwa upande mmoja, utendaji unaeleweka kama tendo la thieta. Hivi ni kusema kuwa utendaji unatazamwa kama drama au igizo kwenye jukwaa. Huu ni mtazamo finyu kuhusu utendaji kwani Ngugi wa Thiong'o (1986) anaeleza kwamba utendaji upo katika kila sehemu ya maisha ya binadamu, na sio lazima ufungamane na ukumbi wa maonyesho, yaani thieta.

O'Quinn (1981) anaeleza kuwa utendaji ni dhana pana zaidi ya sanaa za maonyesho kwani sanaa zote za maonyesho ni utendaji lakini sio aina zote za utendaji huwa sanaa za maonyesho. Dhana hizi mbili zinaweza kubainishwa kwa misingi ya hadhira. Sanaa za maonyesho huwa na mpangilio mahsusi na hubuniwa kwa lengo la kuathiri hadhira fulani. Kwa upande mwingine, aina zingine za utendaji hubuniwa kwa athari zake za kiroho kwa mtendaji wake. Aina hizi, kama ilivyo katika sanaa za maonyesho, huweza kuwa na hadhira ingawa haziigizwi kwa lengo mahsusi la kuathiri hadhira hiyo.

Kutokana na fasili hizi za wataalam mbalimbali kuhusu dhana ya utendaji, tunaweza kusema kuwa utendaji ni uwasilishaji wa tukio fulani kwenye jukwaa au mahali popote pa kuigizia mbele ya hadhira. Tukio hili linahusu maisha ya binadamu katika hali halisi. Utendaji unaweza kutokea hata katika kazi za kinathari; hadithi fupi na riwaya zikiwemo.

Schechner (1988) naye anaeleza kwamba upo utendaji uliojumuishwa katika drama. Kwamba, wakati mtu anaishi tendo fulani kwenye jukwaa mbele ya hadhira huwa

anatenda; hujiingiza katika utendaji wa mhusika anayetenda kwa niaba yake. Schechner katika kazi hii, anaeleza zaidi kwamba kucheza ngoma katika muziki kwa mfano ni namna ya utendaji. Kwake, utendaji sio uigizaji tu.

Anaeleza zaidi kwamba ipo tofauti kati ya utendaji katika drama na aina zingine za utendaji. Kwa mfano, utendaji unaodhihirika katika uchezaji ngoma na utendaji wa kidrama. Utendaji wa kidrama huwa na mpangilio zaidi ya utendaji usio wa kidrama. Ametoa mfano wa utendaji katika uchezaji ngoma ambapo baadhi ya mambo huenda yasitabirike hata na watendaji wenyewe. Katika utendaji wa kidrama kwa upande mwingine, mambo yanakuwa na utaratibu zaidi. Mathalan, kila mtendaji anajua anapoingilia na anapokoma ili kumpisha mwenzake, mwanzo na mwisho wa utendaji unafahamika, mahali pa utendaji, na vipengele vingine vya utendaji katika utendaji mahsusi wa kidrama huwa wazi.

Kutokana na maelezo haya ya Schechner tunabaini kwamba utendaji wa kidrama ni aina ya utendaji ambao huwa na mpangilio zaidi ya aina zingine za utendaji. Huyu ndiye mtaalam wa kwanza miongoni mwa tuliowarejelea ambaye anadai kwamba kuna utendaji ambao ni wa kidrama. Ni aina hii ya utendaji ndiyo tuliyoichunguza katika riwaya ya *Haini*.

Mtaalam mwingine anayehusisha utendaji na drama ni Wafula (2003) anayetumia neno drama kumaanisha somo linalohusu uigizaji wa hali fulani, iwe ni vitendo, hisia au tabia za binadamu kwa kufuata utaratibu maalum. Hapa, Wafula anatilia mkazo suala la utendaji, na kwa mara nyingine, tunapata utendaji wa kidrama ukihusishwa na utaratibu maalum.

Kuhusu dhana riwaya, Foster (1927) anaeleza kwamba riwaya ni masimulizi juu ya matukio yaliyopangwa kama yalivyotokea kiwakati. Mara nyingi kufaulu kwa mtunzi wa hadithi hutegemea uwezo wake wa kubuni na kupanga masimulizi. Kipengele cha kimsingi katika riwaya ni masimulizi ya tukio. Hiki ndicho kipengele cha kimsingi kabisa, na ambacho kisipokuwepo basi riwaya haipo. Hii ndiyo sifa inayobainika katika riwaya zote. Ni kweli kwamba kipengele cha kimsingi cha riwaya huwa ni masimulizi, japo sio lazima masimulizi yenyewe yafanywe kiwakati. Zipo riwaya zilizokiuka kaida hii, na kusimuliwa bila kuzingatia suala la matukio kusimuliwa kihatua, yaani kuanzia tukio la kwanza hadi la mwisho.

Kwa upande mwingine, utendaji katika kazi za kinathari kama ilivyo riwaya ni jambo ambalo kwa muda mrefu halijatafitiwa kwa kina. Tafiti nyingi zinazofanyiwa riwaya ya Kiswahili aghalabu huhusu maudhui na fani, huku suala la utendaji likiachwa nyuma. Kwa mfano, zipo tafiti mbalimbali zilizofanyiwa riwaya ya *Haini*, zikiwemo ‘Uhakiki wa *Haini* kama riwaya ya Kihistoria’ na vilevile Taswira ya Gereza inavyoendeleza Maudhui katika riwaya ya *Haini*.’ Utendaji wa kidrama katika riwaya ya *Haini* ni suala ambalo halijafanyiwa utafiti. Hii ni sababu moja iliyotufanya tutafitie suala hili.

Tumechunguza na kubainisha vipengele vya utendaji na hatimaye kutathmini utendaji wa kidrama wa riwaya hii. Baadhi ya vipengele tulivyochunguza ni pamoja na watendaji wanavyotenda, masimulizi ya utendaji na lugha ya majibizano miongoni mwa vipengele vingine. Hatimaye, tumetathmini utendaji wa kidrama wa riwaya hii iwapo itaandikiwa mchezo wa kuigiza na kuwekwa kwenye jukwaa.

1.2 Suala la Utafiti

Mada ya utafiti wetu ni Utendaji wa Kidrama katika Riwaya ya *Haini*, Shafi Adam Shafi, 2003. Ili kutafitia suala la utendaji wa kidrama katika riwaya ya *Haini*, utafiti huu umejikita katika kuchunguza, kubainisha na kuchanganua vipengele vya utendaji. Vipengele vya kimsingi vilivyochunguzwa ni pamoja na lugha ya majibizano, wahusika au watendaji, taswira za kifilamu na masimulizi ya utendaji. Pamoja na hivi, matumizi ya kimya na sauti, kiza na vimulimuli, mandhari na maleba vimechunguzwa. Tumetathmini namna vipengele hivi vinavyochangia kufanikisha utendaji wa kidrama wa riwaya ya *Haini*. Suala la utendaji katika kazi za kinathari na hasa riwaya halijafanyiwa utafiti wa kina. Watafiti wengi wanapotafitia suala la utendaji wa kidrama hujishughulisha hasa na utendaji katika fasihi simulizi na sanaa za maonyesho, huku riwaya ikiachwa nyuma.

Kuna tafiti mbalimbali zilizofanyiwa riwaya hii ya *Haini*. Kwa mfano, uhakiki wa *Haini* kama riwaya ya kihistoria na vilevile taswira ya gereza inavyoendeleza maudhui katika riwaya ya *Haini*. Hata hivyo, utendaji wa kidrama katika riwaya hii haujatafitiwa.

1.3 Malengo ya Utafiti

Kuna vipengele vinavyochochea utendaji katika kazi za kidrama. Vipengele hivi vinakuwa nguzo katika utendaji wa kazi hiyo, kwani kuwepo au kutokuwepo kwake huathiri kutendeka au kutotendeka kwa kazi hiyo ya kidrama. Utafiti huu wa utendaji wa kidrama katika riwaya ya *Haini* unakusudia kufikia malengo yafuatayo:

- (i) Kujadili lugha ya majibizano ilivyotumika na utendaji wa wahusika katika riwaya ya *Haini*.

- (ii) Kuchanganua masimulizi ya utendaji na taswira za kifilamu katika riwaya ya *Haini*.
- (iii) Kutathmini ufaafu wa vipengele vya utendaji katika utendaji wa kidrama wa riwaya ya *Haini*.

1.4 Nadharia Tete

Utafiti wa utendaji wa kidrama katika riwaya ya *Haini* umeegemea nadharia tete kuwa:

- (i) Lugha ya majibizano imetumika kwa njia itakayofanikisha utendaji wa kidrama na wahusika watafanikisha utendaji wa kidrama wa riwaya ya *Haini*.
- (ii) Masimulizi ya utendaji na taswira za kifilamu zimetumika katika riwaya ya *Haini*.
- (iii) Vipengele vya utendaji katika riwaya ya *Haini* vinafanikisha utendaji wake wa kidrama.

1.5 Sababu za Uteuzi wa Mada

Suala la utendaji linavyojitokeza katika kazi za kinathari na hasa riwaya halijafanyiwa utafiti. Watafiti wengi wanapotafitia utendaji hufungamanisha utafiti wao na ama tamthilia au sanaa za maonyesho na fasihi simulizi. Tafiti kadhaa zimefanywa katika riwaya ya *Haini*. Hizi ni pamoja na *Taswira ya gereza inavyoendeleza maudhui ya riwaya ya Haini*, na vilevile *Uhakiki wa riwaya ya Haini kama riwaya ya kihistoria*. Hata hivyo, suala la utendaji katika riwaya hii halijatafitiwa. Kutokana na hali hii, mada ya utafiti huu imeteuliwa ili kuhakiki suala la utendaji wa kidrama katika riwaya ya *Haini*.

Kazi nyingi za utafiti wa hivi majuzi zinaelekea kuchunguza Ubaada-usasa katika riwaya ya Kiswahili. Kwa mfano, kazi ya Elena, B. *'When Grandfather Came To Life Again: Said Mohamed's New Novel-Beyond Realism,'* inayoangazia suala la mizuka na mazimwi. Kutokana na mwelekeo huo, suala la utendaji linavyojitokeza katika riwaya ya Kiswahili halitiliwi maanani, huku likishabikiwa zaidi katika sanaa za maonyesho. Hii ndiyo sababu, tofauti na mwelekeo huu, utafiti wetu umechanganua utendaji wa kidrama katika riwaya ya *Haini*.

Tafiti za awali zimetafitia masuala ya maudhui na fani katika riwaya, huku utendaji ukitafitiwa katika tamthilia na sanaa za maonyesho. Tumeteua mada hii ili kutoa mwelekeo tofauti wa kuihakiki riwaya.

Uamuzi wa kutafitia mada hii ulichochea na namna mwandishi anavyosimulia tukio hili la kihistoria. Ametumia vipengele vya kidrama kama vile lugha ya majibizano inayochochea utendaji miongoni mwa wahusika pamoja na taswira za kifilamu zinazoteka hisia na mawazo ya msomaji, na kumfanya ajihisi kama anayetazama *'filamu ya Haini'* na sio kusoma riwaya yenyewe tu. Hivyo, katika utafiti huu, jambo la kimsingi lililochunguzwa sio tukio lenyewe la kihistoria bali namna tukio hilo lilivyosimuliwa na mwandishi, pamoja na vipengele vingine vya utendaji wa kidrama alivyotumia.

1.6 Umuhimu wa Utafiti

Kazi hii imetoa mwelekeo mpya wa kuhakiki riwaya ya *Haini*.

Utafiti huu umeongeza maarifa yaliyopo kuhusu drama na fasihi kwa jumla. Suala hili limetafitiwa kwa kina katika fasihi simulizi na sanaa za maonyesho, tofauti na hali ilivyo katika riwaya. Hivyo, kwa kutafitia utendaji wa kidrama katika riwaya ya

Haini, maarifa zaidi yatakuwepo kuhusu suala la utendaji ambayo yatawafaa watafiti, wasanii na watendaji wa siku zijazo.

Utafiti huu vilevile umeweka wazi suala la mwingiliano tanzu. Katika kutafitia suala la utendaji wa kidrama katika riwaya ya *Haini*, tumechanganua tanzu mbili tofauti za fasihi kwa pamoja na kuonyesha namna zinavyoingiliana na kukamilishana. Kwa mfano, tumebainisha namna riwaya ya *Haini*, inavyotegemea utendaji wa kidrama katika uwasilishaji wa ujumbe kwa hadhira lengwa. Aidha, tumeonyesha vipengele vya utendaji wa kidrama vinavyojitokeza katika riwaya hii na mchango wake katika kufanikisha utendaji wa kidrama wa riwaya ya *Haini*.

Utafiti huu wa utendaji wa kidrama katika riwaya ya *Haini* utahamasisha watafiti kutafitia suala la utendaji katika utanzu wa riwaya katika siku zijazo. Mpaka sasa, ni wazi kuwa utendaji wa kidrama katika riwaya haujafanyiwa utafiti kwa kina kama hali ilivyo katika sanaa za maonyesho na fasihi simulizi. Utafiti huu utakuwa kichocheo cha kutafitia suala hili katika riwaya kama ambavyo vipengele vingine vya riwaya vimetafitiwa.

Hatimaye, kwa kujadili utendaji wa kidrama unavyojitokeza katika riwaya ya *Haini*, kuna uwezekano wa riwaya hii kuandikiwa mchezo wa kuigiza na kuwekwa kwenye jukwaa na hivyo kupanua hadhira yake kama Bacon (1984) anavyodai katika maelezo yake kuhusu Nadharia ya Utendaji.

1.7 Msingi wa Kinadharia

Utafiti huu umeongozwa na Nadharia ya Utendaji iliyoasisiwa na Wallace Bacon (1984) na kuendelezwa na Richard Schechner na Victor Turner. Bacon (1984) anasisitiza kuwa uti wa mgongo wa utendaji ni mtagusano kati ya hadhira na matini.

Kulingana na Bacon, msomaji wa matini hunufaika yeye binafsi kutokana na ujumbe lakini katika uigizaji kwenye jukwaa, idadi kubwa ya hadhira hunufaika. Kazi ya drama inapoigizwa katika jukwaa, ujumbe huwafikia na kuwafaidi wengi na sio msomaji mmoja pekee.

Anaendelea kueleza kuwa drama sio jambo linalotokea jukwaani tu bali limejaa maana na linatumika katika viwango vingi vya maisha ya kila siku. Drama ilichukuliwa kuwa shughuli muhimu kama zilivyokuwa shughuli zingine na ilichota malighafi yake kutokana na shughuli hizo za jamii.

Sanaa ya utendaji hivyo basi hutilia mkazo kwenye vitendo au uigizaji ambapo watu halisi au waigizaji huchukua nafasi fulani za watu katika matini na kuigiza matendo yao kupitia mazungumzo na ishara mbele ya hadhira. Bacon anasisitiza kuwa tathmini ya kifasihi kwa msomaji ni tofauti na tathmini ya yanayoigizwa. Tofauti hii inatokana na hali kwamba msomaji hujitathminia anayoyasoma kivyake ilhali hadhira pana hutathmini matini tofauti, yaani inayotendwa kwenye jukwaa. Utendaji hutusaidia kushiriki katika maisha ya matini na huvuka mipaka ya ‘umimi’ inayodhihirika katika usomaji wa matini.

Bacon anaeleza mihimili ya Nadharia ya Utendaji. Anaeleza kwamba matini ya kidrama hupatikana katika njia mbili: Matini andishi na matini tendaji. Katika utendaji au uigizaji, mwigizaji, ambaye ni mtu halisi huwakilisha mhusika aliye katika matini. Ni hoja hii iliyopelekea uchanganuzi wa wahusika katika riwaya ya *Haini* kama kipengele cha kimsingi cha utendaji. Waigizaji huteuliwa kuwaigiza wahusika ambao wataweza kutekeleza matendo yao, na vilevile sifa zao kuwiana kwa kiwango kikubwa. Mwelekezi wa drama, kwa kuongozwa na namna Shafi Adam alivyowajenga wahusika katika riwaya ya *Haini*, atawateua watu halisi

watakaochukua nafasi za wahusika hao na kuwaigiza kwenye jukwaa. Ikiwa wahusika wamejengwa na kusawiriwa ipasavyo kutegemea kipengele hiki cha wahusika, basi riwaya hii itaigizika kwenye jukwaa. Ni katika msingi wa maelezo haya ndipo Nadharia ya Utendaji inakuwa mwafaka katika kutathmini utendaji wa matini za kidrama kwenye jukwaa.

Bacon (1984) vilevile anadai kuwa hadhira kubwa hunufaika kutokana na inayoyatazama katika uigizaji kuliko inayoyaelewa katika usomaji. Hii ina maana kwamba nadharia hii ya utendaji ni mwafaka katika kutathmini vipengele vinavyofanikisha na kuleta ukamilifu katika uigizaji. Vipengele hivi vimejadiliwa na kuchanganuliwa kama vinavyodhihirika katika riwaya ya *Haini*. Kwa kweli, kuwepo au kutokuwepo kwa vipengele hivi ndiko hubainisha ikiwa kazi fulani ya kidrama itaigizika kwenye jukwaa au la.

Nadharia ya Utendaji inashughulika kuifanya hai fasihi. Ni vigumu kufanya hivyo pasipo kuhusisha vipengele hivi vinavyofanikisha utendaji. Kazi ya fasihi hupata uhai inapoigizwa mbele ya hadhira kwenye jukwaa. Kwa hivyo, ni muhimu kuchunguza ikiwa kazi ya kinathari itaigizika au la, kutegemea vipengele mbalimbali vya utendaji. Nadharia hii, ingawa iliasisiwa na Wallace Bacon (1984), imepambanuliwa na Victor Turner na Richard Schechner.

Victor Turner (1982) anadai kwamba kwa jumla, matambiko na sherehe za mpito wa maisha zimejaa utendaji. Victor Turner, alikuwa Mwana-anthropolojia aliyeshughulikia zaidi matendo ya mwanadamu yenyewe. Anashikilia kwamba vipengele vya utendaji vinavyobainika katika matendo haya ya binadamu ama vinatokana na au vinahusishwa na matendo ya watendaji. Schechner naye, katika tafiti zake mbalimbali kama tulivyojadili hapa chini, anakubaliana na Turner (1982)

kwamba utendaji, iwe ni katika sanaa tendi, michezo ya kuigiza, muziki au katika maisha ya kila siku hujumuisha sauti na ishara za mwili. Schechner ndiye mtaalam aliyeiendeleza zaidi Nadharia ya Utendaji:

Schechner (2013) anaeleza kwamba katika taaluma ya Utendaji, matendo na tabia hushughulikiwa kitaaluma, na kwamba mwelekeo huu unatambua mambo mawili. Jambo la kwanza ni kuwa katika ulimwengu wa leo, tamaduni zinaingiliana kila siku, hivi kwamba hakuna kikundi cha watu ambacho kimejitenga na makundi mengine asilimia mia. Jambo la pili ni kwamba, tofauti baina ya tamaduni hizi zinabainika sana hivi kwamba hakuna Nadharia ya Utendaji ambayo ni bia. Nadharia moja haiwezi kueleza masuala ya utendaji katika tamaduni zote hizi.

Hata hivyo, Schechner (1985) anaeleza kwamba maswali muhimu ya kujiuliza kuhusu utendaji kwa jumla na kuhusu Nadharia ya Utendaji ni pamoja na:

- (i) Watendaji ni akina nani?
- (ii) Watendaji wanawezaje kutenda wahusika wanaowatenda?
- (iii) Hadhira ina umuhimu gani katika utendaji?

Schechner (1985) anadai kwamba maswali mengine yanayoulizwa yanaweza kuangazia mandhari, matumizi ya jukwaa au mahali pa kuigizia na maleba. Hivi ni baadhi ya vipengele vya utendaji ambavyo vimebainishwa katika riwaya ya *Haini* na kujadiliwa. Schechner (1985) anaeleza vilevile kwamba nguvu ya utendaji imo katika uhusiano mahsusi kati ya watendaji na ambao kwao, utendaji huo unatekelezwa. Kuhusu watendaji, Schechner (1988) anaeleza kwamba mtu anapoishi tendo fulani kwenye jukwaa mbele ya hadhira huwa anatenda; hujiinkiza katika utendaji wa mhusika anayetenda na hivyo kuyawasilisha maisha ya mhusika huyo kama kwamba

yanatukia katika ulimwengu halisi. Utendaji huu kwenye jukwaa ndio huipa kazi ya fasihi uhai na kunufaisha hadhira kubwa zaidi ya hadhira inayonufaika katika usomaji wa kazi hiyo hiyo.

Schechner, katika maelezo yake kuhusu Nadharia ya Utendaji anaeleza kwamba utendaji mzuri ni ule ambao hutumia kwa kubadilishana; sauti na kimya, na kwa kujumuisha matini, maleba, wakati na rithimu. Kwa pamoja, vipengele hivi vinajisuka katika ruwaza inayofanikisha utendaji kwenye jukwaa, na vilevile kuathiri hadhira. Hali hii inapotokea, basi utendaji wa kidrama huwa umefanikiwa kuwasilishia hadhira lengwa ujumbe uliomo katika kazi ya fasihi inayotendwa.

Bacon (1984) anasisitiza umuhimu wa vipengele tulivyotaja katika utendaji wakati akieleza kuhusu Nadharia ya Utendaji, jambo linaloendelezwa na Schechner (1985). Schechner anaeleza kwamba utendaji mzuri ni ule ambao umejumuisha vipengele anuwai vya utendaji, yaani watendaji, matini, maleba, mandhari, mahali pa utendaji, utendaji wenyewe, sauti na kimya. Schechner (2013) pia, kama vile Bacon (1984) anazungumzia hadhira katika utendaji anapodai kwamba Kinachochukuliwa kama utendaji hakitegemei jambo linalotendwa tu bali hutegemea pakubwa namna utendaji husika unavyopokelewa: wanaotazama utendaji fulani kwenye jukwaa wanafahamu kwamba ulimwengu wanaotazama sio wa watendaji bali ni wa wahusika ambao wanawakilishwa katika utendaji huo.

Kutokana na madai haya, tunaelewa kwamba ili kufanikisha utendaji, sharti mwelekezi au msanii ajumuishe vipengele vya kimsingi vya utendaji na avisuke kwa kipengele kimoja kufanikisha kingine kutoka mwanzo hadi mwisho wa utendaji husika kama Nadharia ya Utendaji inavyoeleza. Hii ndiyo sababu mojawapo ya kuchunguza namna vipengele anuwai vinavyobainika katika riwaya ya Haini

vinavyojisuka kutoka mwanzo hadi mwisho na uwezekano wake wa kufanikisha au kutofanikisha utendekaji wa kidrama wa riwaya hii kwenye jukwaa (iwapo itaandikiwa mchezo wa kuigiza).

Nadharia hii ni mwafaka katika utafiti huu kwa kuwa mbali na kwamba inatoa maelezo yanayofafanua umuhimu wa utendaji wa kazi za kidrama, tumeitumia katika mambo yafuatayo: Kwanza, kubainisha vipengele vya utendaji katika riwaya ya *Haini*. Kazi hii imechunguza na kubainisha vipengele vya utendaji katika riwaya ya *Haini* na kwa sababu hiyo, nadharia hii imetoa mwongozo katika kubainisha vipengele hivi vya utendaji. Kwa mfano, nadharia hii inatilia mkazo kwenye vitendo au uigizaji, ambapo watu halisi, au waigizaji huchukua nafasi za wahusika katika matini na kuigiza matendo yao kupitia mazungumzo na ishara mbele ya hadhira. Nadharia hii inabainisha wahusika, matendo (utendaji) na lugha ya majibizano, ambavyo ni vipengele vya kimsingi vya utendaji vilivyochanganuliwa katika utafiti huu.

Pili, nadharia hii imetuongoza katika kuchanganua data. Nadharia hii inaeleza kwa kina kuhusu vipengele ambavyo tumeshughulikia katika utafiti huu. Inaweka wazi namna vipengele hivi vya utendaji vinafaa kujumuishwa katika utendaji ili kufanikisha shughuli nzima ya utendaji husika. Katika kufanya utafiti huu, vipengele vya utendaji katika riwaya ya *Haini* vimechunguzwa na kubainishwa kama Nadharia ya Utendaji inavyoongoza.

Hatimaye, mbali na Nadharia ya Utendaji imetuongoza katika uchanganuzi wa data, imetuwezesha kutathmini utendekaji wa riwaya ya *Haini*. Tumegundua kwamba, baadhi ya vipengele vya utendaji katika riwaya ya *Haini* vimetumika kama Nadharia ya Utendaji inavyoelekeza na hivyo vitafanikisha utendaji wa riwaya hii katika

matukio ambamo vipengele hivi vimetumika. Kwa upande mwingine, tumetoa mapendekezo ya namna ya kutekeleza sehemu za riwaya (wakati wa utendaji wake) ambamo vipengele vya utendaji vilivyotumika havijajikita na madai ya Nadharia ya Utendaji.

1.8 Mapitio ya Maandishi

Sehemu hii inaangazia kazi mbalimbali zilizoandikwa kuhusu suala la utafiti. Kazi ambazo zimeangaziwa hapa zimeegemea kwa kiasi kikubwa riwaya, utendaji, sanaa za maonyesho na drama. Kazi hizi zinachangia katika kueleweka kwa suala la utendaji na vilevile kuweka wazi utendaji wa kidrama. Maoni ya wataalam mbalimbali kuhusu riwaya yameelezwa katika sehemu hii.

1. Yaliyoandikwa Kuhusu Riwaya

Senkoro (1982) anasema riwaya ni kisa ambacho urefu wake unakiruhusu kitambe na kutambaa vizingiti vingi vya maisha kama apendavyo mwandishi wake. Anaeleza zaidi kwamba riwaya ni hadithi ndefu ya kubuni inayojengwa kwa wahusika zaidi ya mmoja, visa vingi, na huzingatia kwa upana maisha ya jamii. Anachosisitiza mtaalam huyu ni kwamba riwaya sharti iangazie maisha ya jamii kwa undani.

Gromov (1996), akieleza kuhusu riwaya za miaka ya tisini anasema kwamba kazi nyingi za kinathari aghalabu zililenga kuelimisha. Anasema kuwa, katika fasihi hii iliyolenga kuelimisha, riwaya nyingi za miaka ya tisini na ambazo bado zipo ni riwaya zinazozungumzia uhalifu na masuala ya mapenzi. Anafafanua kwamba: Waandishi wengi wa riwaya hizi hufuata mtindo unaopatikana katika filamu aina ya thrila, huwa na ploti sahili, huwa na utendaji na taharuki, kama ilivyo katika riwaya ya *Tufani* ya Baker Mfaume (1993). Hata hivyo, wapo waandishi wanaochukua mikondo tofauti katika uandishi wa riwaya. Kwa mfano, Ben Mtobwa, mwandishi

maarufu wa riwaya pendwa, katika riwaya yake ya *Dar-es-Salaam Usiku* (1990) hakubuni wahusika kama walivyofanya waandishi katika riwaya za hapo awali. Wahusika katika riwaya hii wanapata sifa zao kutokana na mazingira yao ya kijamii ambayo ni magumu na yanawalazimu kuwa na hulka walizonazo.

Kwa mujibu wa Gromov (1996), mkondo aliochukua Mtobwa katika riwaya hii ni tofauti na uliotumiwa katika riwaya za miaka ya sabini na themanini. Anaeleza vilevile kwamba matatizo ya kijamii yalishughulikiwa kupitia riwaya. Akizungumzia maudhui, anaeleza kuwa maudhui yaliyotawala riwaya za kipindi hiki yalihusu maamuzi kati ya kutenda mema au maovu ambapo mema yalifungamana na maadili yaliyoongoza jamii. Mwisho wa riwaya nyingi ulikuwa wa kitanzia ambapo mhusika mkuu aliaga dunia baada ya kuadhibiwa kwa makosa aliyotenda.

Gromov (1996) anakuwa mtaalam pekee katika kazi hii aliyehusisha moja kwa moja riwaya na sifa za kifilamu. Anasema kwamba zipo riwaya zenye sifa za kifilamu hasa filamu aina ya thrila. Gromov (2008) anadai kwamba ni kweli kuna riwaya pendwa za Kiswahili ambazo kwa maoni yake huchukua mkondo wa ama thriller au mapenzi. Ingawa *Haini* sio riwaya pendwa, Tumejadili kwa kina suala hili la riwaya kuwa na sifa za kifilamu katika sura ya tano tunapochunguza taswira za kifilamu katika riwaya ya *Haini*.

Gromov (2004) alichukua mkondo wa baada-usasa katika kutafitia riwaya. Mbali na kuchunguza riwaya za baada-usasa, Gromov (2008) anashughulikia riwaya pendwa katika kipindi cha miaka michache iliyopita. Katika utafiti huu, tumechukua mwelekeo tofauti na wataalam tuliowataja kwa kutafitia utendaji wa kidrama katika riwaya ya *Haini*.

2. Yaliyoandikwa Kuhusu Utendaji

Soyinka (1988) anaona kwamba matumizi ya jukwaa yana athari chanya katika utendaji hasa kwa kuwa yanaathiri hadhira kisaikolojia na kimwili. Athari hizi hudhihirika hasa pale utendaji unapofanyika kwenye jukwaa, huku hadhira ikingoja kwa hamu kuona ikiwa mhusika mkuu ataepuka matatizo anayokumbana nayo kutokana na mpinzani wake au la. Haya hudhihirika katika utendaji kwenye jukwaa. Kama wataalam wengine waliotangulia, Wole Soyinka anafunga utendaji kwenye jukwaa, wazo ambalo linapingwa na Ngugi wa Thiong'o (1986) anayeeleza kwamba utendaji unaweza kutokea mahali popote pale palipo wazi. Huu ndio msimamo wetu, kwamba si lazima utendaji ufanyike kwenye jukwaa tu. Unaweza kutekelezwa mahali popote pale.

Kuhusu suala la utendaji wa fasihi, Madison na Hemera (2005) wanadai kuwa pana uhusiano wa karibu sana baina ya fasihi na utendaji. Tunakubaliana na wataalam hawa kwamba, sharti uigizaji ufanywe mbele ya hadhira ili ujumbe unaokusudiwa uwafikie watu wengi kwa pamoja. Hali hii haiwezi kutokea matini inaposomwa tu.

Mumbo (2012) anaeleza kwamba utendaji ni kipengele cha kimsingi cha kujieleza kinachodhihirika aghalabu katika nyanja zote za mawasiliano miongoni mwa wanadamu. Utendaji ni dhana inayolenga kujenga upya matukio fulani ili kutimiza lengo fulani mahsusi katika maisha ya mwanadamu.

Mtaalam huyu anaeleza zaidi kuwa sherehe hii ya *Vyalusa* huwa ya kidrama, inayohusisha waalikwa, jamaa na marafiki na kama wenyewe wanavyodhani, mtoto anayepewa jina, ambapo mtendaji mkuu huwa babu, na wengine hadhira.

Utafiti huu, kama inavyobainika, unafungamana na sanaa za maonyesho katika sherehe ya kumpa mtoto jina, *Vyalusa*, miongoni mwa Wamijikenda. Ijapokuwa utafiti wa Mumbo (2012) unajadili mbinu za uwasilishaji katika utendaji wa sherehe hii, Mumbo ametaja vipengele vya utendaji wa kidrama vinavyobainika katika sherehe hiyo. Kwa mfano, ametaja mtendaji, utendaji au uigizaji na hadhira. Tofauti na utafiti wake, tumechunguza na kubainisha vipengele hivi katika riwaya ya *Haini*.

Mlama (1981) ametafitia sherehe ya *Digubi* miongoni mwa jamii ya Wakaguru nchini Tanzania. Yeye pia anadai kuwa utendaji hudhihirika na kutawala sherehe hii. Kwa mfano anaeleza kuwa katika utendaji wa *Digubi* hasa, wacheza ngoma wote huwa wanawake ambao tayari wameshapita hatua hii ya maisha (yaani wameshafanyiwa sherehe ya *Digubi* zamani). Hawa hudhihirisha utendaji wanapocheza ngoma kwa kuyachezeshwa mabega na kuimba huku wakizunguka kwa mduara. Hadhira nayo hukaa katikati mwa duara hiyo ya wacheza ngoma.

Msichana hufanyiwa sherehe hii mara mbili; anapovunja ungo na siku moja kabla ya siku ya harusi yake. Katika sehemu moja ya utendaji wa sherehe hii, Mlama (1981) anaeleza kwamba mcheza ngoma mmoja huingia kwenye duara na kuchukua uhusika wa mke asiye na heshima huku akiigiza anavyoingia kwenye nyumba ya wakwe zake. Mcheza ngoma mwingine naye huchukua uhusika wa baba mkwe anayeingia chumbani mwake na kumpata mwanamke yule amekaa kwenye kiti chake (cha baba mkwe). Kwa kutojua la kufanya, anatoka nje. Baada ya muda, yule mwanamke anachoka kukaa kwenye kiti na anajilaza kitandani mwa baba mkwe, ambaye anaingia na kumpata kitandani. Kutokana na aibu ya kitendo hicho, anatoka nje kwa haraka.

Katika tukio hili, utendaji unadhahirika na kufanikishwa na kuwepo kwa vipengele muhimu vya kidrama kama watendaji, utendaji, na hadhira. Vipengele hivi, sawa na

vinavyobainika katika sherehe ya *Vyalusa* ya Mijikenda vinafanikisha utendaji wa sherehe hizi. Katika utafiti wetu, tumejadili namna vipengele hivi vimejitokeza na hatimaye ufaafu wake katika utendaji wa kidrama wa riwaya ya *Haini*.

Akifafanua mawazo ya Muhando na Balisidya (1976), Mumbo (1997) anasema wawili hawa wamethibitisha kwamba katika kusalia miungu, jando na unyago, mna matendo ya kidrama. Kwa mfano, wanaeleza kwamba katika kusalia miungu kwa Wakaguru (jamii ile ile yenye sherehe ya Digubi), tunapata uigizaji: watu hawa wanapokuwa katika maombi ya mvua, mwanaume mmoja na mwanamke mmoja ambao ni wa umri wa makamo huingia ndani na kukaa kwenye kitanda ambacho kimejengwa humo ndani kikiwa kama kitanda cha mungu. Wawili hawa wanachukua nafasi ya mungu na mkewe. Hapa, Mumbo (1997) anaeleza kuwa uigizaji unabainika wazi katika shughuli hii ya kusalia miungu, ambapo watu wawili wanamuigiza mungu na mkewe.

Kama ilivyo katika sherehe za *Vyalusa*, Mumbo (2012) na *Digubi*, Mlama (1981), shughuli hii ya kusalia miungu inadhihirisha utendaji, wakati wahusika wawili wanachukua nafasi za mungu na mkewe. Utendaji hudhihirika wazi zaidi katika sanaa za maonyesho kama ulivyojitokeza katika *Vyalusa* na *Digubi*, sababu inayowapelekea watafiti wengi kutafitia suala la utendaji katika fasihi simulizi na sanaa za maonyesho.

Schechner (1988) naye anasimulia namna utendaji hutukia katika sherehe ya *Thovil* katika jamii ya Korototan-Kijiji cha Sri Lanka. Anaeleza kwamba kuna mchezaji ngoma mmoja, ambaye anacheza kwa ustadi katikati ya duara. Duara katika utendaji huu ndiyo jukwaa, na matukio mengine hutukia katika sehemu hii iliyoachwa wazi na kuzungukwa na watu (hadhira) katika umbo la duara. Kuna wapiga ngoma wawili na waimbaji kadhaa. Mchezaji ngoma huyu anacheza huku akiruka juu na chini.

Mchezaji mwingine naye huingia kwenye duara hiyo huku amebeba mianzi ya moto na mchezaji ngoma, ambaye amekuwa kwenye duara akicheza tayari huja alipo mchezaji huyu anayeingia na hufanya kila awezalo kumnyang'anya mwenzake mianzi ya moto aliyoibeba. Anapofanikiwa hukatiza uchezaji wake kwa ghafla akiwa katikati mwa duara, bila kuhema wala kudhihirisha kwamba amechoka. Anafanya dua na kuondoka. Hadhira huwa watu takriban watu mia nne kwa kila utendaji, ingawa utendaji huu wa mchezaji ngoma huwa na watazamaji hata zaidi ya hao mia nne.

Katika utendaji huu, tunapata dhana inayotendeka ambayo ni kushindana katika uchezaji ngoma kwa ustadi zaidi bila kuonyesha kuchoka. Hii ni mojawapo ya sababu zinazomfanya Schechner kudai kwamba maisha tunayoishi kila siku ni utendaji, madai tunayokubaliana nayo. Mbali na dhana inayotendwa, tunapata kwamba utendaji huu huwa na wakati maalum wa kutendwa; mida kati ya saa kumi na dakika ishirini na tano na saa kumi na moja na dakika ishirini na tano alfajiri. Vipengele vya utendaji vinavyobainika katika utendaji huu ni pamoja na watendaji, hadhira na jukwaa, ambavyo tumejadili katika utafiti huu.

Tofauti na ilivyo katika tafiti hizi tulizoeleza, utafiti wetu umechunguza utendaji wa kidrama katika riwaya ya *Haini*. Kwa mfano, masimulizi ya utendaji na wahusika, ambavyo ni vipengele vya utendaji katika sherehe hizi (*Vyalusa, Digubi* na ya kusalia miungu miongoni mwa Wakaguru) vimechunguzwa na kubainishwa katika riwaya ya *Haini*, pamoja na vipengele vingine tulivyovitaja.

Toolan (1988) anaeleza kwamba katika miaka ya nyuma, istilahi utendaji ilitumiwa kueleza aina ya uwasilishaji wa kidrama wa masimulizi. Anasema, “wazo kwamba uwasilishaji wa masimulizi aghalabu huhusisha utendaji lilizuka katika kazi za Hymes na Goffman. Wazo hili linapambanuliwa zaidi na Wolfson (1982).”

Wolfson (1982) anaeleza kwamba kutenda hadithi ni kuiweka wazi zaidi kwa hadhira lengwa, kwa kuwa katika utendaji, tajriba ya hadithi husika inaelezwa kwa upambanufu zaidi. Vilevile, utendaji unakuwa sehemu muhimu sana katika kueleza na kuweka wazi visa katika hadithi husika. Anataja mambo kama: urudiaji, sauti, ishara na miondoko kwenye jukwaa. Dayalojia hutumiwa kuongeza habari ambazo hazikuwepo katika masimulizi. Hali hii huyapa uhai kwani msimulizi anapata kujibizana na watendaji wake. Katika kufanya hivyo, anaweza hisi kama vile huruma au kihoro, ambazo hazingebainika katika usomaji wa kisa kinachosimuliwa. Dayalojia vilevile hukatiza masimulizi marefu ya kibinafsi.

Wolfson anafafanua umuhimu wa lugha ya majibizano kwa kusema kwamba huipa uhai hadithi na huwawezesha watendaji kuonyesha hisia zao waziwazi, hisia ambazo hadhira isingepata kuzitambua katika usomaji au usimulizi wa kawaida (usiohusisha utendaji). Tunakubaliana na wataalam hawa katika maelezo yao kuhusu umuhimu wa utendaji, kwamba utendaji huwezesha uelewekaji zaidi wa kazi za kinathari, kwa kuzipa kazi hizo uhai. Ni kwa msingi huu ndipo tumetathmini utendaji wa riwaya ya *Haini* kwa mujibu wa vipengele vya utendaji tulivyobainisha na kuchanganua.

Mawazo haya yameungwa mkono na Epskamp (1984) anayesema kwamba usimulizi katika tamaduni za Kiafrika ni wa kidrama. Utendaji ni sehemu muhimu ya masimulizi, kwani hadithi haiwasilishwi kwa maneno tu bali huwasilishwa kwa matumizi ya viziada lugha, ishara, nyimbo na ngoma. Kinachosisitizwa zaidi ni namna ya uwasilishaji wa hadithi husika.

Akieleza kipengele kingine muhimu cha uwasilishaji wa masimulizi, Eskamp (1984) anasema kwamba maleba na mapiku yanatumiwa katika uwasilishaji wa masimulizi ili kuufanikisha usimulizi huo. Yanakuwa kipengele muhimu cha utendaji katika

uwasilishaji wa masimulizi au hadithi husika. Maelezo haya ya Eskamp yanazidi kuyakinisha madai yetu kwamba utendaji, katika tafiti nyingi, aghalabu hufungamanishwa na fasihi simulizi (hasa kipera cha hadithi na ngano), na sanaa za maonyesho. Tunakubaliana naye kwamba, maleba ni kipengele muhimu cha utendaji wa hadithi. Tumechanganua kipengele cha maleba katika riwaya ya *Haini*, na kutathmini mchango wake katika kufanikisha utendaji wa riwaya hiyo.

Francoise (1981), akizungumzia maleba, mapiku na vinyago anadai kuwa katika sherehe ya Midimu ya Wamakonde, ambayo huhusisha kuimba na kucheza ngoma, mapiku hutumiwa kuwasilisha ujumbe muhimu unaoelekezwa wanawake, ili kuwafanya wakubali jamii inayotawaliwa na mwanaume.

Tunatambua, kutokana na sherehe hii ya *Midimu* miongoni mwa Wamakonde kwamba sanaa za maonyesho, pamoja na kuburudisha, hulenga kuwasilisha ujumbe maalum kwa wanajamii. Katika kazi hii hata hivyo, tumetafitia suala la utendaji katika riwaya wala sio katika sanaa za maonyesho.

Akizungumzia sanaa za maonyesho na tamaduni, Ricard (2000) anaeleza kwamba miongoni mwa aina za burudani alizozizingatia Ebrahim Hussein katika utafiti wake, maonyesho ya taarab yalipewa umuhimu zaidi. Haya yalijumuisha uimbaji wa nyimbo za taarab uliokatizwa hapa na pale na maonyesho ya michezo mifupi mifupi ya maigizo, na aina hizi mbili; taarab na uigizaji ndizo njia mbili kuu za burudani kule Zanzibar na miongoni mwa jamii za Waswahili wa Pwani.

Kuhusu utendaji katika nyimbo za jamii ya Waswahili, Mwanakombo (2016) anajadili utendaji katika nyimbo za msondo. Katika kujadili utendaji huu, anachanganua utendaji wenyewe, hadhira na umuhimu wake, wahusika ambao

aghalabu huwa wanawake walioolewa tayari na wakati mwingine wari, maleba, ambayo hapo zamani yalikuwa lesa mbili, na sasa huwa nguo za kawaida na mhusika kujifunga lesa moja kiunoni. Anazungumzia vilevile jukwaa, ambalo huwa ukumbi kwenye chumba alimo mwanamke ambaye ameposwa na anaandaliwa kwa harusi yake. Anajadili vipengele anuwai vinavyobainika katika utendaji wa nyimbo za msondo.

Maelezo haya yanatudhihirishia zaidi kwamba kwa muda mrefu sasa, utendaji umehusishwa na fasihi simulizi katika vipengele vyake kama vile katika uwasilishaji wa nyimbo hizi za taarab.

Kufikia sasa, utendaji unahusishwa na kushughulikiwa zaidi katika sanaa za maonyesho. Utendaji hapo awali ulijibainisha katika uwasilishaji wa shughuli za kidrama katika jamii za Kiafrika. Shughuli hizi zilijumuisha matambiko, shughuli za kumpa mtoto jina, sherehe za harusi na hata mazishi.

Nyambura (2014) amejadili suala la utendaji katika tamthilia za *Sudana* na *Kimya Kimya Kimya*. Anachunguza na kujadili vipengele vya utendaji katika tamthilia hizi mbili, kwa lengo la kutathmini utendekaji wake. Vipengele anavyojadili ni pamoja na maelekezo ya jukwaa, mandhari, maleba, miondoko, uangazaji, sauti, kimya na mihimili. Amebainisha vipengele hivi katika tamthilia hizi mbili na kuvijadili huku akitoa mifano.

Kwa maoni yetu hata hivyo, Nyambura katika kazi yake hii amejadili vipengele visaidizi vya utendaji huku akiacha nyuma vipengele vya kimsingi. Mtaalam huyu hajataja wala kujadili vipengele kama wahusika na lugha ya majibizano ambavyo visipokuwepo katika kazi ya fasihi basi hapana utendaji.

Schechner (1988), akizungumzia masimulizi anaeleza kwamba masimulizi ya hadithi yalifanywa sio kwa maneno tu bali kupitia nyimbo, kucheza ngoma, na kupiga ngoma, na yalitukia katika mandhari maalum kama vile pango. Drama ikazaliwa kutokana na muungano wa tabia hizi zote.

3. Yaliyoandikwa Kuhusu Drama

Ngugi (1986) anaeleza kuwa chimbuko la drama ni mapambano kati ya mtu na mtu na vilevile kati ya mtu na mazingira yake. Kabla ya kuja kwa wakoloni, wakulima walifanya sherehe na matambiko ya kubariki vifaa vya uzalishaji mali (ukulima), walikuwa na sherehe za uzazi, tohara, ndoa na mazishi. Waliomba dhidi ya majanga yaliyowapata kama vile ukame, mafuriko na kifo. Matambiko yalikuwa mengi, na ingawa miungu hawakuonekana, waliigizwa na watu waliovaa mapiku. Drama ilikuwa sehemu ya maisha ya kila siku ya wanajamii. Ilichukuliwa kuwa shughuli muhimu kama zilivyokuwa shughuli zingine wakati ule, na ilichota malighafi yake kutokana na shughuli hizo za jamii. Drama iliburudisha, ilifunza jamii maadili na haikulazimu kufanyiwa katika kumbi za maonyesho, ilifanyiwa popote palipokuwa wazi.

Pamoja na kueleza chimbuko la drama, Ngugi wa Thiong'o anaeleza kwamba drama ni sehemu muhimu ya maisha ya jamii kwa kuwa ilifunza jamii maadili na kuburudisha vilevile. Katika utafiti huu, tofauti na alichorangazia Ngugi (1986) tumechunguza suala la utendaji wa kidrama, sio katika shughuli za maisha ya wanajamii bali katika riwaya ya *Haini*.

Wamitila (2008) anaeleza kuwa drama ni dhana inayorejelea kazi ya kifasihi iliyoandikwa kwa ajili ya kuwasilishwa jukwaani kwa njia ya maneno na ishara. Katika kueleza vipengele vya drama ya Kiswahili, Wamitila anataja usimulizi,

ambapo anaeleza kuwa drama hutegemea uwasilishaji wa maneno ya wahusika au waigizaji kimatendo. Pili, anaeleza kuwa kuna matumizi ya masimulizi ambayo ni mbinu ya kitendi au kiepiki katika muundo wa drama-ambao unasimulia matukio yanayopatikana katika tamthilia au kazi yoyote ile ya kidrama inayohusika. Tatu, anataja mazungumzo ya wahusika. Haya yanaweza kuangaliwa pia kama njia mojawapo ya uwasilishaji wa kisimulizi kwa sababu yanatekeleza dhima ya kusimulia kisa kikuu.

Vipengele hivi vya kidrama ndivyo Mwamzandi (2002) anavirejelea kama ‘mbinu za kitamthilia na kimaigizo’ na kuviangazia katika makala yake ‘*Majadiliano ya Tanzania katika Ushairi wa Kiswahili.*’ Anachunguza jinsi mtunzi Abdilatif Abdalla katika *Mnazi: Vuta N’kuvute* ametumia mbinu za kitamthilia na kimaigizo katika shairi hili. Amejadili vipengele vya lugha ya majibizano, ploti, wahusika na mandhari kama vipengele vinavyofanya utungo huu uwekwe katika medani sawa na tamthilia. Anaeleza kuwa katika utungo huu [Mnazi:Vuta N’kuvute], ushubiano wa wahusika unafanikishwa kupitia lugha. Alii anaposema, “Ndugu ulo mnazini...utashuka au la?” anauliza akitarajia kwamba Badi atamjibu ipasavyo. Abdilatif anamfanya Badi atoe kauli yenye mashiko, “Ndugu tini ya mnazi, nilo juu nakujibu.” Huu ni mtindo haloso wa kidrama ambao wahusika wanafanywa wajibizane na wawe watendaji wa sehemu walizopewa na msanii kwa kuzingatia muktadha waliomo.

Kutokana na madai haya tunapata kwamba lugha inayotumiwa katika tamthilia, ambayo ni lugha ya majibizano inawapa wahusika fursa ya kuwa watendaji wa matendo mbalimbali. Tumechukua mwelekeo huu tunapotafitia wahusika na lugha ya majibizano katika riwaya ya *Haini*. Mwamzandi pia amejadili kipengele cha wahusika ambacho ameshughulikia kwa kirefu huku akifafanua uhusika wa Alii na Badi, na

namna kupitia uhusika huu, wawili hawa wanafanikiwa kupitisha ujumbe kwa hadhira ya shairi hili. Kwa hivyo, lugha ya majibizano ni muhimu katika kupitisha ujumbe uliokusudiwa katika kazi za kidrama.

Mandhari ni kipengele kingine anachojadili Mwamzandi katika makala yake hii anapoeleza kwamba utungo wa Mnazi: Vuta N’kuvute umetumia mandhari moja ambayo inafafanuliwa na wahusika wenyewe. Maneno wanayotumia Alii na Badi ndiyo yanayotuelekeza kufahamu wahusika hawa walipo. Picha inayotujia katika bongo zetu ni kuwepo kwa mnazi kwenye jukwaa. kwenye mnazi huu ndipo tunapowaona wahusika hawa wawili; Badi akiwa juu, na Alii akiwa yu chini. Mnazi unatufanya tusaili umuhimu wa kuteuliwa kwake kama kifaa cha kimandhari ambcho kitendo kizima cha mchezo kinautegemea.

Tunaunga mkono kauli ya Mwamzandi kwamba tanzu mbili au zaidi zinaweza kushirikishwa katika kazi moja kutegemea ujumbe uliokusudiwa hadhira. Riwaya ya *Haini* kwa mfano ni mseto wa tanzu mbili kuu; riwaya na drama. Kinacholeta mseto huu wa kitanzu ni kuwepo kwa vipengele mahsusi vya tanzu husika. Katika utafiti wetu, tumeshughulikia vipengele hivi vya kidrama vinavyobainika katika riwaya ya *Haini*.

Mumbo (2014) naye anaeleza drama kama mtungo wa kisanaa unaotumia lugha ya majibizano baina ya wahusika katika kusawiri mawazo na migogoro inayoikabili jamii. Anakubaliana na Banks (1985) anayesema kuwa drama ni uwasilishaji wa maisha halisi ya watu. Utungo wa kinathari, kishairi unapowasilishwa jukwaani kwa njia ya matendo na maongezi inakuwa drama. Ricard (2000) anaelekea kukubaliana na Banks (1985) katika maelezo yake haya. Akieleza zaidi kuhusu utendaji wa maandishi, Ricard anaeleza ngojera ilibadilika na kuingia katika utendaji wa kidrama,

na hatimaye ikaja kuwa aina ya drama. Waandishi kama Peninah Muhando walitunga ngonjera kama walivyofanya waandishi kama Kezilahabi. Ngonjera, kupitia utendaji wake wa kidrama ikawa ikitumika zaidi katika drama za makampuni na shule mbalimbali kutokana na sifa yake ya ufunzaji.

Hapa, Banks (1985) akifafanuliwa na Mumbo (2014) anaeleza kwamba hata kazi za kinathari zinapowasilishwa kwa njia ya utendaji na lugha ya majibizano inaweza kuwa drama. Anaeleza zaidi kuwa drama iko katika njia ya uwasilishaji wa kimatendo na majibizano. Nawaunga mkono wataalam hawa kwamba drama, ni kazi yoyote ile ya kifasihi, kazi za kinathari zikiwemo, mradi uwasilishaji wake ufanywe mbele ya hadhira kwa njia ya kutenda na lugha ya majibizano itumike.

Vipengele alivyotaja Mumbo, lugha ya majibizano, maelekezo ya utendaji, na taswira ni baadhi ya vipengele ambavyo tumechunguza na kubainisha kama vinavyojitokeza katika riwaya ya *Haini* katika utafiti wetu.

1.9 Upeo wa Utafiti

Utafiti huu unahusu utendaji wa kidrama katika riwaya ya *Haini*. Tumehakiki riwaya moja ambayo ni *Haini* ya Shafi Adam iliyochapishwa na shirika la uchapishaji la Longhorn mwaka wa 2003. Tumejikita katika Nadharia ya Utendaji iliyoasisiwa na Bacon (1984) na kuendelezwa na Turner na Schechner. Utafiti huu umejikita katika kuchunguza na kubainisha vipengele vya utendaji katika riwaya hii. Vipengele vya utendaji vilivyobainishwa na kuchanganuliwa ni pamoja na lugha ya majibizano, wahusika, masimulizi ya utendaji na taswira za kifilamu. Pamoja na vipengele hivi, vipengele vingine vilivyobainishwa na kuchanganuliwa ni pamoja na kiza na vimulimuli, sauti na kimya, mandhari na maleba. Hivi, ingawa si vya kimsingi husaidia katika kufanikisha utendaji wa matini ya kidrama.

Eneo la utafiti lilikuwa maktabani ambapo pamoja na kufanya utafiti katika maktaba ya *Margret Thatcher* ya Chuo Kikuu cha Moi, tulizuru maktaba za Chuo Kikuu cha Nairobi na Chuo Kikuu cha Kenyatta. Hapa, tulisoma na kuhakiki tasnifu, vitabu na makala kadhaa kuhusu utendaji kwa jumla. Pia, tulifanikiwa kupata kanda za video za Shafi Adam akizungumzia maisha yake na hasa uandishi wa riwaya ya *Haini*.

1.10 Mbinu za Utafiti

1.10.1 Uteuzi wa sampuli

Katika utafiti huu, riwaya ya *Haini* imeteuliwa kimaksudi. Riwaya hii imetumia lugha ya majibizano miongoni mwa wahusika kwa kiwango kikubwa. Mwandishi huyu ana umahiri wa matumizi ya taswira katika kazi zake, ambazo hujenga picha waziwazi za yanayotendeka, hasa katika riwaya hii ya *Haini*.

1.10.2 Mbinu za ukusanyaji data

a) Utafiti Maktabani

Utafiti huu ni wa maktabani. Tuliisoma riwaya ya *Haini* kwa njia makinifu na kudondoa vipengele vya utendaji vilivyobainika. Vilevile tulisoma tahakiki zilizofanywa kuhusu riwaya ya *Haini* na zile zilizoandikwa na Shafi Adam Shafi kwa jumla. Pamoja na hayo, tulipitia makala mbalimbali zilizochapishwa na zinazohusu mada ya utafiti, pamoja na majarida yaliyotufaa katika kufanikisha utafiti wetu.

Tulitembelea tovuti na blogu mbalimbali kwenye mtandao ili kupata maarifa zaidi kuhusu yaliyoandikiwa utendaji kwa jumla na riwaya ya *Haini* pia. Tulisoma makala, vitabu na kazi mbalimbali za kitaaluma ambazo ni pamoja na tasnifu zilizoandikwa kuhusu utendaji. Vilevile, tulitazama kanda za video za Shafi akizungumzia uandishi wake na hasa riwaya ya *Haini*.

b) Vifaa vya Utafiti

Kuna vifaa tulivyohitaji ili kufanikisha shughuli nzima ya utafiti. Hivi ni pamoja na: Kamusi za fasihi katika kueleza na kufafanua dhana muhimu. Pili, tulitumia tarakilishi katika utafiti kwenye mtandao na tovuti mbalimbali. Vitabu na kazi mbalimbali za kitaaluma zinazoeleza vipengele mbalimbali vya utendaji wa kidrama katika kazi za kifasihi zilitusaidia sana katika utafiti huu.

1.11 Uchanganuzi wa Data

Tumeichanganua data kwa kuchunguza na kubainisha vipengele vya utendaji wa kidrama katika riwaya ya *Haini*. Usomaji makinifu ndiyo mbinu ya kimsingi iliyotumika katika uchunguzi wa vipengele husika vya utendaji. Tumekusanya na kupanga vipengele hivi vya utendaji pamoja kutegemea sifa za vipengele hivyo kama anavyoeleza Kothari (2004). Mtaalam huyu anaeleza kwamba, data zenye uhusiano au sifa sawa huwekwa katika kundi moja. Kwa hivyo, data yote iliyokusanywa huwekwa katika makundi kadhaa. Makundi haya hutegemea aina ya data na aina ya utafiti unaofanywa. Katika utafiti huu kwa mfano, tuliweka pamoja taswira za kifilamu tulizobainisha katika riwaya hii. Vilevile, tuliyaweka pamoja masimulizi ya kiutendaji tuliyodondoa katika riwaya hii.

Uchanganuzi wa data uliongozwa na Nadharia ya Utendaji iliyoasisiwa na Bacon na kupambanuliwa na Turner na Schechner inayoeleza kwamba matini ya kidrama hupatikana katika njia mbili: Matini andishi na matini tendaji. Nadharia hii inasisitiza kuwa tathmini ya kifasihi huwa tofauti na tathmini ya yanayoigizwa; hutusaidia kuhusika katika maisha ya matini. Hatimaye, inaeleza kuwa katika utendaji, mwigizaji ambaye ni mtu halisi anawakilisha mhusika aliye katika matini.

Katika uchanganuzi huu, tumetumia mbinu ya kimaelezo kwa kuzingatia mwongozo wa Kothari (2004) kama tulivyoieleza hapo juu na vilevile mihili ya Nadharia ya Utendaji kuonyesha namna vipengele vya utendaji vimebainika katika riwaya ya *Haini*. Vipengele hivi ni lugha ya majibizano, wahusika, masimulizi ya utendaji na taswira za kifilamu. Pamoja na vipengele hivi, tumechunguza kiza, vimulimuli, sauti, kimya, mandhari na maleba.

Hatimaye, kwa kuongozwa na Nadharia ya Utendaji, tumetathmini utendaji wa kidrama katika riwaya ya *Haini*. Utafiti huu ni wa kithamano, hivyo mbinu za kithamano zilitumika katika ukusanyaji na uchanganuzi wa data.

Baada ya kuchunguza vipengele vya kidrama katika riwaya ya *Haini*, vipengele vilivyobainishwa viliwekwa katika makundi. Kwa mfano, wahusika walikuwa katika kundi moja tofauti na lugha ya majibizano, masimulizi ya utendaji, taswira za kifilamu, mandhari, maleba, kiza, vimulimuli, kimya na sauti. Tulipiga hatua na kuchanganua kwa kina kila kipengele tulichobainisha. Mathalan, wahusika waliainishwa na kuchanganuliwa kulingana na majukumu waliyopewa na mwandishi. Kisha, tulifafanua utendaji wa wahusika hawa katika nafasi walizopewa na mwandishi kwa mujibu wa Nadharia ya Utendaji. Hatimaye, tulitathmini ufaafu wa vipengele hivi katika utendaji wa kidrama wa riwaya ya *Haini* iwapo itaigizwa kwenye jukwaa.

1.12 Hitimisho

Sehemu hii imechunguza msingi wa utafiti wetu. Tumeweka wazi suala letu la utafiti, malengo yetu, nadharia tete, sababu na umuhimu wa utafiti, msingi wa kinadharia, mapitio ya maandishi na uchanganuzi wa data. Sura ifuatayo inazamia maisha ya Shafi Adam na uandishi wake, hasa kilichompelekea kuandika riwaya ya *Haini*.

SURA YA PILI

SHAFI ADAM NA UANDISHI WA *HAINI*

2.0 Utangulizi

Sura hii kimsingi inaangazia maisha ya mwandishi wa riwaya ya *Haini*, uandishi wake, kilichompelekea kuandika riwaya ya *Haini* alivyoandika na hatimaye muhtasari wa riwaya ya *Haini*. Kuelewa maisha ya Shafi Adam Shafi ni muhimu kwa kuwa mwandishi aghalabu huchota malighafi ya uandishi wake kutokana na maisha yake na jamii alimokulia. Kufafanua uandishi wake kusaidia katika kuelewa anavyoandika kazi zake, lugha na mbinu anazotumia na sababu yake ya kufanya hivyo. Hii bila shaka ilituwezesha katika kuelewa zaidi riwaya ya *Haini*. Hatimaye, historia na muhtasari wa riwaya ya *Haini* ni muhimu katika kuelewa kilichompelekea Adam Shafi kuandika riwaya hii kama alivyofanya. Tumeleza ni matukio gani katika jamii halisi yalitomchochea kuandika kazi hii.

2.1 Maisha ya Shafi Adam Shafi

Shafi Adam Shafi anaeleza Diegner (2003) kwamba alizaliwa Zanzibar mwaka wa 1940. Alizaliwa kipindi cha tabu kwa kuwa Vita Vikuu vya Pili vya Dunia vilikuwa vikiendelea, hivyo akazaliwa katika hali hii ngumu ya vita. Akiwa mchanga, alitumia muda wake mwingi baharini, ama kwa mchezo, kuogelea au kuvua. Alitumia muda wake vilevile katika kutafuta matunda na kuwinda ndege na wanyama porini.

Alijiunga na shule ya msingi ya *French Comodian School* mwaka wa 1948 akiwa darasa la kwanza. Akasoma katika shule hiyo mpaka darasa la sita. Mwaka wa 1955 akajiunga na shule ya msingi ya Gulioni akiwa darasa la saba. Shule mbili hizo zilikuwa mjini Unguja, tofauti ikiwa kwamba *French Comodian School* ilikuwa katika mji mkongwe uliojulikana kama *Stone Town*; mji mkongwe wa Zanzibar,

wakati shule ya msingi ya Gulioni ilikuwa *Ng'ambo Area*, katika maeneo walimoishi wananchi wa kawaida.

Shafi alisomea shule ya msingi ya Gulioni kutoka mwaka wa 1955 mpaka 1956 alipomaliza darasa la nane. Alijiunga na Chuo cha Ualimu cha Seyyid Khalifa mwaka wa 1957 baada ya kufanya mtihani wake wa kitaifa wa darasa la nane. Masomo ya ualimu yalikuwa yakichukua miaka minne.

Alijiunga na chuo hiki cha Seyyid Khalifa, ambacho sasa ni Chuo cha Ualimu cha Nkurumah mwaka wa 1957, lakini akaondoka hapo mwaka wa 1960 kabla ya kumaliza mafunzo ya ualimu. Aliondoka kwa nia ya kwenda nchi za nje kutafuta masomo.

Shafi alipata mafunzo ya uandishi wa habari kutoka 1964 hadi 1965 mjini Prague nchini Czechoslovakia, ambayo sasa ni Jamhuri ya Czech, akapata mafunzo zaidi nchini Sweden mwaka wa 1982 na nchini Marekani mwaka wa 1983. Mwaka wa 1967 baada ya kumaliza masomo ya uanahabari, aliajiriwa na Chama cha TANU, ambako aliandikia magazeti mawili, *The Nationalist na Uhuru*.

Shafi Adam Shafi aliwahi kufungwa jela kwa miaka miwili, kutoka mwaka wa 1972 hadi 1974, baada ya kukamatwa na kushtakiwa kama mmoja wa waliohusika na tukio la uhaini lililopelekea kifo cha rais wa kwanza wa Zanzibar, Abeid Karume.

Shafi Adam Shafi alikuwa mwenyekiti wa Umoja wa Waandishi wa Vitabu Tanzania (UWAVITA) kutoka 1988 hadi 2002. Baadaye mwaka wa 2002, akachaguliwa kuwa mwenyekiti wa Baraza la maendeleo ya vitabu Tanzania (BAMVITA). Sasa tutazame jinsi mwandishi huyu alivyoanza kazi ya uandishi hadi alipofikia leo hii.

Kutokana na kuelewa maisha ya Shafi Adam, tunaelewa baadhi ya sababu zake za kuwaumba wahusika wake alivyofanya. Kwa mfano Hamza, ambaye ni mhusika mkuu katika riwaya ya *Haini* amepewa sifa za mwanahabari shupavu kama alivyokuwa Adam Shafi katika miaka hii tuliyoeleza. Ni uanahabari huu unaopelekea Hamza kukamatwa kwa madai ya kupanga mapinduzi ya serikali yaliyopelekea kuuawa kwa Kigogo.

2.2 Shafi Adam Shafi na Uandishi Wake

Shafi Adam Shafi anaeleza kwamba alianza kuandika akiwa mwanafunzi katika Chuo cha Ualimu cha Zanzibar. Hapa, aliandikia kijigazeti cha chuo kilichoitwa *Reveal*, ambapo mambo yaliyoangaziwa yalihusu jumla ya maisha ya pale chuoni. Shafi alikuwa mhariri wa kijigazeti hicho, huku mhariri mkuu akiwa Profesa Haroub Othman. Baadaye alienda Ujerumani Mashariki kusomea uanahabari na aliporudi akawa mwandishi wa habari katika magazeti.

Shafi Adam Shafi alifanya kazi katika gazeti la Chama cha TANU. TANU ilikuwa inatoa magazeti mawili wakati huo, moja la Kingereza likiitwa *The Nationalist* na jingine la Kiswahili likiitwa *Uhuru*.

Shafi Adam Shafi amefanya kazi ya uandishi wa habari kwa muda mrefu. Alipokuwa Moshi, anasema alifanya kazi katika shirika moja la kimataifa; *International Cooperative Alliance Regional Office for East, Central and Southern Africa*, shirika la vyama vya ushirika lisilo la kiserikali. Hapa, Shafi alishughulikia masuala ya elimu.

Akieleza kuhusu hadhira anayoandikia, Shafi anasema kwamba yeye anapoandika kazi zake huwa amewalenga Watanzania wote kwa jumla. Wasomi wa rika zote,

vijana na watu wazima. Anasema yeye huandika kwanza kwa Wazanzibari labda kwa sababu wanafahamu vizuri zaidi mazingira na mandhari, na lugha vilevile. Anawaandikia pia Watanzania wa bara ili waone raha na utamu wa Kiswahili cha Unguja. Kuhusu Kenya na Uganda, Shafi anaeleza kuwa anawaandikia Wakenya na Waganda ili waone Kiswahili kinavyoandikwa, na kwamba Kiswahili ni lugha inayoweza kutumiwa katika fasihi na ikapendwa na watu duniani kote.

Akieleza kuhusu lugha anayoitumia katika uandishi wake, Shafi anasema kuwa hutumia Kiswahili cha Unguja kwa vile ni lugha ya jazanda inayotokana na mandhari ya Unguja, iliyosheheni tashbiha na sitiari maalum. Anaeleza Kiswahili kama lugha yenye ladha yake, kwamba ina utamu wake, raha yake, na ni lugha ambayo mtu yeyote anaweza kuiandikia mtu anayeijua akasoma akaona raha, akaweza kuifananisha na lugha yoyote ile.

Ni wazi hivyo kwamba Shafi Adam Shafi huandikia hadhira pana, na vilevile anachangia pakubwa katika kukuza na kuendeleza lugha ya Kiswahili kwa kuichagua kama lugha yake ya uandishi. Baada ya kuangazia namna Shafi Adam Shafi alivyoingia katika uandishi, hadhira anayolenga na lugha anayoitumia katika uandishi wake na sababu zake, sasa tuangalie baadhi ya kazi za fasihi alizoziandika.

Shafi anadai kwamba yeye huandika riwaya. Hajaandika wala kujaribu kuandika mashairi na tamthilia lakini ameandika hadithi fupi kadhaa ambazo huenda zikachapishwa siku zijazo. Riwaya alizoziandika ni: *Kasri ya Mwinyi Fuad* (1978), *Kuli* (1979), *Vuta n'Kuvute* (1999), *Haini* (2003) na *Mbali na Nyumbani* (2013).

Kasri ya Mwinyi Fuad (1978) ndiyo riwaya ya kwanza aliyoandika Shafi Adam Shafi na ambayo ilichapishwa kwa mara ya kwanza mwaka wa 1978 na *Tanzania*

Publishing House na baadaye ikachapishwa na *Vide-Muwa Publishers* mwaka wa 2007. Riwaya hii imetafsiriwa kwa lugha tatu za Kizungu zikiwa ni pamoja na Kijerumani, Kifaransa na Kirusi. Katika riwaya hii, mwandishi anazungumzia watu wa tabaka la chini (watwana) na namna wanavyojaribu kujikomboa kutokana na dhulma za watu wa tabaka la juu (mamwinyi). Mwandishi anasimulia suala hili kupitia mhusika mkuu Fuad ambaye anarithi utajiri mkubwa baada ya kifo cha wazazi wake Bwana Malik (uk. 8) na Bibi Maimuna. Fuad, kama walivyokuwa mabwana wengine anawatesa wafanyakazi wake. Kutokana na mateso haya, wafanyakazi katika mashamba ya sehemu za mashambani na mjini wanafanya mikutano ambako wanajadiliana namna ya kujikomboa. Harakati za ukombozi zinaanza na kufaulu mamwinyi wanaponyang'anywa mashamba na mashamba hayo kugawiwa umma.

Katika riwaya hii, mwandishi anatetea wanyonge kwa kusimulia kwa kina kuhusu hali halisi ilivyokuwa nchini Zanzibar. Watumwa wanaungana na kuleta mapinduzi dhidi ya mabwana wao. Tukio hili liliwahi kutokea nchini Zanzibar, na mwandishi analiandikia riwaya kama anavyofanya katika riwaya yake ya *Haini*.

Kuli (1979), kama ilivyo *Kasri ya Mwinyi Fuad* ni riwaya inayoeleza kwa kina shida na madhila wanayopitia makuli. Wanaishi maisha ya umaskini, kufanya kazi ngumu na kupata mshahara mdogo wanaolipwa kule bandarini wanakofanya kazi ya kutwa ya ukuli. Hata pale kazi hii inaposababisha kifo cha mmoja wa makuli, wenye kampuni hizi pale bandarini hawawalipi chochote. Makuli hawa wanachoshwa na dhuluma hizi na wanaanza kupanga na kufanya mikutano ya kujadili namna ya kutetea haki zao. Wanafanya mikutano na kugoma kufanya kazi, jambo linalopelekea baadhi ya viongozi wa mikutano na migomo hii kukamatwa na kufungwa jela.

Katika matukio haya, yale yaliyotokea katika riwaya ya *Kasri ya Mwinyi Fuad* yanajirudia; wanyonge kupanga mikakati ya kujikomboa kutokana na dhulma za watesi wao. Mgomo huu ambao mwandishi amesimulia katika riwaya ya *Kuli* ni mgomo uliowahi kutokea nchini Zanzibar mwaka wa 1948, ambapo wafanyakazi nchini humo waligoma kutetea kuboreshwa kwa hali zao duni kazini pamoja na nyongeza ya mishahara. Mara tena, tunapata tukio la kihistoria ambalo mwandishi ameandikia kisa katika riwaya yake. Katika masimulizi yake, mwandishi ametumia mbinu ya taswira kwa ufanisi mkubwa; mbinu ambayo imejitokeza hata zaidi katika riwaya ya Haini, na tumejadili taswira hizi katika sura ya tano ya tasnifu hii.

Vuta N'kuvute (1999) ni riwaya inayoangazia maudhui anuwai ila yale ya kutafuta uhuru wa nchi, wa kibinafsi, wa makundi n.k yametawala kutoka mwanzo hadi mwisho. Mwandishi, katika riwaya hii amesimulia kutoelewana kati aya Wahindi na Waswahili kama ilivyokuwa wakati huo. Mwandishi anaeleza haya kupitia wahusika Yasmin (Mhindi) na Mwajuma (Mswahili) pamoja na wanaharakati kama Denge, Chande, Mambo na Sukutua.

Mwandishi anaonyesha namna Wahindi na Waswahili kule Zanzibar hawakuelewana, huku kila kikundi kikiwa na hisia hasi kuhusu kine. Shafi Adam Shafi anambuni mhusika mkuu Yasmin na kumfanya rafiki wa karibu wa Mwajuma (uk.8, 22). Mwandishi anamfanya Yasmin atoroke kwa mumewe Bwana Raza, ambaye ni Mhindi mzee aliyeozwa kwake na anakuwa na uhusiano wa kimapenzi na Denge, kijana Mswahili. Baadaye, anaolewa na Shahib ambaye anaaga dunia (uk.218) na hatimaye Yasmin anaishia kuolewa na Bukheti ambaye ni Mswahili.

Kwa upande mwingine, mwandishi anasimulia harakati za vijana wa Zanzibar kutaka kujikomboa kutoka kwa ukoloni wa Kisultan. Ili kudidimiza juhudi zao, vijana hawa

wanakamatwa, kuteswa na kufungwa jela, huku wakidaiwa kuwa Wakomunisti wasiomwamini Mungu (uk. 204).

Katika riwaya hii, Shafi Adam Shafi anafanikiwa kutatua mzozo kati ya Wahindi na Waswahili na vilevile kuendelea kutetea haki za wanaodhulumiwa. Kama tulivyoona katika riwaya zake za mwanzo, *Kasri ya Mwinyi Fuad* na *Kuli*. Shafi Adam, katika riwaya hii anatumia lugha ya majibizano kwa kiasi kikubwa, jambo linalochochea utendaji kama hali ilivyo katika riwaya ya *Haini*. Anasimulia visa katika riwaya hii kupitia majibizano miongoni mwa wahusika. Hii ni sifa mojawapo ya sifa kuu za riwaya ya *Haini*.

Mbali na Nyumbani (2013) ni riwaya ya kitawasifu inayosimulia maisha ya mwandishi na ujana wake, pamoja na kiu alichokuwa nacho cha kwenda Uingereza kutafuta elimu. Anaeleza kuhusu safari yake kutoka Zanzibar iliyojawa na changamoto chungu nzima na misukosuko ambayo yeye hakuitegemea. Anaanza safari yake kutoka Zanzibar mwaka wa 1960 (uk.12) kwa nia ya kwenda Uingereza kutafuta elimu. Kutoka Zanzibar, mwandishi anaeleza namna alivyofika Aden, Mombasa, Nairobi, Eldoret, Uganda, Sudan, akarudi Kenya; Bungoma, Kairo na hatimaye Ujerumani alikotaka kufika.

Ni kweli kama Walibora (2013) asemavyo kwamba tawasifu ya *Mbali na Nyumbani* ina upekee katika namna mwandishi anavyojimulika na kujiweka wazi mbele ya wasomaji wake. Ameifinyanga lugha hivi kwamba msomaji anatekwa kimawazo na kuungana na mwandishi katika safari yake hiyo ya kutafuta elimu, pamoja na changamoto zote anazokabiliana nazo. Taswira alizomchorea msomaji kama vile maelezo yake kuhusu mlima Elgon na mto Nile zinampa msomaji picha kamili ya

mwandishi alikopitia katika safari yake hii. Ni tawasifu iliyopita mipaka ya tawasifu zilizozeleka katika fasihi ya Kiswahili.

Kutokana na usomaji wa riwaya hizi za Shafi Adam, msomaji anapata kugundua mtindo wa uandishi anaoupendelea. Mtindo huu umesimikwa kwenye sifa za uandishi wake, na hivyo, mbali na kubainisha kazi zake, unambainisha yeye kama mwandishi wa kazi husika.

Kwanza, mwandishi mara nyingi anachukua tukio la kihistoria na ama kulitungia riwaya au kulifanya uti wa mgongo wa masimulizi ya riwaya husika. Riwaya zake; *Kuli*, *Kasri ya Mwinyi Fuad* na *Vuta N'kuvute* zinasheheni matukio ya kihistoria, ambayo kwa kweli yaliwahi kutukia nchini Zanzibar. Kupitia ubunifu wake, Shafi anayasimulia matukio haya katika riwaya zake hizi. Katika riwaya yake ya *Mbali na Nyumbani*, Shafi anasimulia kwa kina maisha yake kama yalivyokuwa; udhaifu wake, changamoto na ufanisi wake. Hivi ndivyo anavyofanya katika riwaya ya *Haini*, kwa kuchukua tukio la kuuawa kwa Abeid Karume na kuliandikia riwaya hii.

Pili, mwandishi anatumia mbinu ya taswira kwa wingi katika riwaya zake. Kwa mfano, katika riwaya ya *Kuli*, msomaji anaona namna makuli wanavyobeba mizigo, wanavyosukumana kwenye lango la bandari kila asubuhi na mateso anuwai wanayopitia wakiwa kazini. Katika riwaya ya *Mbali na Nyumbani*, taswira za mahali zimetumika kwa kina kumchorea msomaji picha kamili ya maeneo mbalimbali alimojipata mwandishi. Maeneo haya ni kama mlima Elgon na mto Nile. Tofauti na taswira katika riwaya hizi, Shafi ametumia taswira za kifilamu kusimulia mateso wanayoyapata mahaini kule gerezani. Taswira hizi zinaweka wazi namna hali ilivyo gerezani na namna mateso mbalimbali yanavyotekelezwa. Tumejadili taswira hizi kwa kina katika sura ya tano.

Hatimaye, mwandishi anapendelea matumizi ya lugha ya majibizano katika riwaya zake. Sifa hii ndiyo inayochochea utendaji katika riwaya zilimotumika. Mathalan, lugha ya majibizano imetumika kwa wingi katika riwaya ya *Vuta N'kuvute*, jambo ambalo, mbali na kuchochea utendaji linarahisisha usomaji wa riwaya hii. Hata hivyo, kilele cha matumizi ya lugha ya majibizano kinadhihirika katika riwaya ya *Haini*. Katika riwaya hii, mwandishi amewapa wahusika wake uwezo wa kujibizana kama inavyotukia katika tamthilia. Mazungumzo haya yametawala matukio mengi katika riwaya ya *Haini* kutoka mwanzo hadi mwisho, tofauti na ilivyo katika riwaya ya *Vuta N'kuvute* ambapo lugha ya majibizano imetumika katika matukio machache.

Sifa zote hizi zinazombainisha Shafi Adam zinapatikana katika riwaya ya *Haini*. Ametumia sio taswira tu bali aina tofauti ya taswira katika *Haini*, amechukua tukio kuu la historia ya Zanzibar na kuliandikia kisa na hatimaye lugha ya majibizano imetumika kwa kiasi kikubwa katika *Haini*. Kwa sababu hii, utendaji unachochewa zaidi katika riwaya ya *Haini* kuliko riwaya zingine za Shafi Adam, sababu mojawapo ya zilizotupelekea kuichagua na kuifanyia utafiti huu.

2.3 Historia ya Riwaya ya *Haini*

2.3.1 Sababu za kuandikwa kwa Riwaya ya *Haini*

Shafi Adam Shafi amehojiwa na vyombo vya habari na watu binafsi mara kadha wa kadhaa wakitaka kujua kilichomfanya akaandika riwaya ya *Haini*. Hii ni kutokana na riwaya ya *Haini* inavyosimuliwa pamoja na matukio yake ambayo yanachora picha kamili ya hali halisi ilivyo gerezani. Mwandishi anatoa mukhtasari wa kilichomchochea kuandika riwaya hii, ambapo anaeleza kwamba yalitokea mapinduzi nchini Zanzibar. Serikali ya mfalme iliyokuwepo iliondolewa kwa njia ya mapigano na umwagaji damu na ikaundwa serikali ambayo iliendeshwa na wanamapinduzi kwa

misilingi ya kimapinduzi. Kwa mfano, iliweka vyombo vya usalama ambavyo vilitumia nguvu dhidi ya raia wa kawaida nchini humo. Kwa sababu hii, watu wengi walikamatwa na kufungwa jela bila ya kupelekwa mahakamani. Yaani, serikali mpya haikufuata taratibu za kisheria zilizokuwepo wakati ule. Watu wengi wakaathiriwa na mfumo huu, huku wengi wakifungwa jela bila makosa.

Mfumo wa uongozi uliokuwepo ukapelekea kuwepo kwa matatizo mengi ya kijamii nchini Zanzibar. Kukawa na upungufu wa chakula na bidhaa zingine muhimu. Wananchi waliolalamikia hali hii walikamatwa na kufungwa jela, hivyo wengine wakawa wakiogopa kuzungumzia shida hizi hadi miaka ya 2000.

Hivi ndivyo hali ilivyokuwa wakati mapinduzi ya Zanzibar yalitokea mwaka wa 1972. Hali ya taharuki, hatari na hali ngumu kiuchumi, watu wakiogopa kusema wasije wakakamatwa. Katika mahojiano haya, Shafi Adam Shafi anafafanua kwamba watu waliogopa kuzungumzia matukio yaliyofuata baada ya kuuawa kwa Abeid Karume. Baada ya muda wakaanza kuyasahau hivyo lengo lake kuandika riwaya ya *Haini* lilikuwa kuhufadhi tukio hili, ili kazi hii iwe kumbukumbu kwa jamii.

Hii ndiyo sababu mojawapo ya zilizomsukuma Shafi Adam kuandika riwaya ya *Haini*. Alitaka kuhifadhi tukio hili la kihistoria na hali iliyofuata baada ya mapinduzi haya katika maandishi, ili riwaya hii iwe kama kumbukumbu kuwa mapinduzi haya yalitokea kweli. Alitaka kuzungumzia kile ambacho watu wengi wakati ule waliogopa kuzungumzia, kutokana na hali iliyokuwepo; hakukuwa na uhuru wa kusema, na aliyekashifu uongozi alikamatwa na kufungwa jela. Na alipata wapi mawazo ya kuandika riwaya ya *Haini* alivyoandika? Shafi Adam Shafi anaeleza kwamba alikuwa miongoni mwa watu ambao walikamatwa baada ya kifo cha rais wa kwanza wa Zanzibar, Abeid Karume. Alikamatwa siku ya pili baada ya mauaji hayo kutokea,

akapelekwa kwenye kituo cha polisi cha Malindi. Baadaye akapelekwa moja kwa moja hadi gerezani kama mmoja wa watuhumiwa wa upangaji wa mapinduzi ya serikali ya Zanzibar ambayo yalipelekea kifo cha Abeid Karume. Anaeleza zaidi kuwa alikaa gerezani kwa muda wa miaka miwili 1972-1974 na alikuwa mmoja katika washtakiwa walioshtakiwa kwa mashtaka ya kumuua Karume. Alifikishwa mahakamani. Hivyo aliandika kitabu cha *Haini* kama riwaya, kama hadithi ya kubuni, lakini hadithi ile ya kubuni inatokana na uzoefu au yale aliyoyaona katika miaka miwili aliyokaa pale gerezani. Alikaa magereza mawili. Gereza kuu la Kinoamguu lakini vilevile gereza la Usalama; *Maximum Security Prison*. Huko ndiko kulikuwa na mateso na madhila mengi. Hivyo, aliyoyaandika katika kitabu cha *Haini*, si yote, mengi ni mambo ambayo ameyaona, kuyashuhudia, au kusikia kutoka kwa wenzake aliokuwa nao kule gerezani.

Riwaya ya *Haini* hivyo ni riwaya ya kubuni (licha ya kwamba inaakisi tukio kuu la kihistoria). Kuna matukio ya riwaya hii ambayo ni ya kitawasifu. Kwa mfano, kuna baadhi ya wahusika ambao kwa kweli walikuwa katika Zanzibar halisi wakati ule mapinduzi yakitokea. Baadhi ya mandhari katika riwaya hii ni mahali panapopatikana kweli na vilevile baadhi ya matukio ni ya kweli, kama kesi ya watuhumiwa, na kwa mujibu wa maelezo ya mwandishi, ni kweli kwamba kesi yenyewe ilichukua mwaka mzima. Baadhi ya vipengele vya riwaya hii hata hivyo ni zao la ubunifu wa mwandishi mwenyewe.

Tulizozitaja ni baadhi ya sababu zilizompelekea mwandishi kuandika riwaya ya *Haini*. Kama tulivyoona, matukio mengi anayoyazungumzia mwandishi ni yale ambayo yalifuata baada ya kuuawa kwa rais wa kwanza wa Zanzibar; Abeid Karume, katika jaribio la kuipindua serikali. Kifo chake ndicho kilichozalisha hali ambayo

Shafi Adam anaeleza kwamba ndiyo iliyomsukuma kuandika riwaya ya *Haini*. Kama tulivyoeleza katika mukhtasari wa riwaya ya Haini baadaye katika sura hii, hali na matatizo yaliyotokana na kifo cha Abeid Karume ndiyo yametawala riwaya ya *Haini*. Kwa hivyo, mauaji ya Abeid Karume yanakuwa ndicho chanzo cha hali walimokuwa Wazanzibar, na vilevile kisababishi cha hali iliyomchochea Shafi Adam kuiandika riwaya ya *Haini*.

2.4 Mukhtasari wa Riwaya ya *Haini*

Katika riwaya hii, Shafi Adam Shafi anachukua tukio la kihistoria la kuuawa kwa Abeid Karume, rais wa kwanza wa Zanzibar mwaka wa 1972 kama tulivyoeleza hapo juu na kwa ubunifu wake, anasimulia kisa hiki kama alivyofanya. Masimulizi yanapoanza kuna hali ya taharuki na kama tunavyogundua baadaye katika riwaya, hali hii imesababishwa na kuuawa kwa Kigogo, ambaye ndiye kiongozi wa nchi ambayo katika *Haini* hajatajwa.

Katika sura ya kwanza, msimulizi anatanguliza kwa kutukutanisha na Hamza. Huyu ndiye mhusika mkuu, ambaye amemwoa Khadijah, na wiki mbili zilizopita walipata mtoto wa kike; Subira. Khadijah ameenda kwa wazazi wake Bi Farashuu na Mzee Maftah ambako dadake Zalhata pia anaishi. Hamza, ambaye yuko kwake na rafiki zake Kassim na Fadhil, anatoka na kwenda kwa akina Khadijah baada ya kusikia milio ya risasi na hali ya taharuki kuzuka. Ni kesho yake ndipo anapokamatwa akiwa Kisimamajongoo (alipo Khadijah na wazazi wake) na kupelekwa kwenye kituo cha polisi cha Malindi. Baadaye anapelekwa jela kuu ya Zanzibar; Kinoamiguu. Akiwa huko anakutana na Abdul ambaye anamjulisha sababu ya watu wengi kukamatwa; kwamba Kigogo ameuawa, na hao waliokamatwa ndio mahaini.

Mnaletwa mahaini zaidi katika chumba alimo Hamza, na kwa jumla wanakuwa 12. Hawa ni pamoja na Abdul, Shadidi, Sheikh Mandundu, Sururu, Masanja, Kondo, Fimbo, Bilali, Nassor, Sugu na Mzee Subet. Wakiwa chumbani wanatumia muda wao mwingi kupashana habari za walikokuwa kabla ya kukamatwa. Hali ya masimulizi inabadilika katika sura ya nne wakati mahaini hawa wanaanza kuhojiwa. Hamza kwa mfano anahojiwa kuhusu mwanajeshi Barakati, Hamduni na mauaji ya Kigogo. Anapigwa na kupelekwa kwa Ba Mkwe ambako anawekwa chumba kimoja na maiti ya Kidau. Baadaye, Doto analetwa katika chumba hiki. Kama ilivyobainika katika maelezo kuhusu kifo cha Karume hapo juu, wengi wa waliohusika na baadaye kukamatwa walikuwa wanajeshi. Hii ndiyo hali tunayoiona hapa, Doto anapowasiliana na wanajeshi wengine waliokamatwa kwa kugota ukutani.

Hamza anamweleza Doto kuhusu aina za mahaini waliokamatwa. Kwanza, kuna wanaopelekwa Kumbakumba na kukaa huko, wanaopelekwa Kumbakumba lakini huenda kwa Ba Mkwe mara kwa mara. Wapo pia ambao wanatolewa Kumbakumba wakapelekwa kwa Ba Mkwe na wakabaki huko kama alivyokuwa Hamza, na hatari zaidi ambao wanapokamatwa wanapelekwa moja kwa moja kwa Ba Mkwe kama alivyofanyiwa Doto. Katika harakati za mahaini kuhojiwa, Hamza anatolewa usiku wa manane na kutumbukizwa kisimani anakoteswa hadi anakubali kwamba atasema akijuacho. Baadaye katika sura ya saba, Hamza anapelekwa kwenye hoteli kwenye ufuo wa bahari kuhojiwa. Wanaomhoji hapa ni Kanali Bunju, Kanali Mapepe na Kanali Maisara. Anapokataa kuwa shahidi wa upande wa mashtaka kama wanavyomtaka makanali hawa, Hamza anapelekwa chumba cha kiza.

Hamza anakaa chumba cha kiza kwa zaidi ya wiki mbili na anapotolewa anarudishwa kwa Ba Mkwe. Anatolewa kwa Ba Mkwe na kupelekwa Kumbakumba ambako

wafungwa 655 wanaachiliwa. Wanaobaki 30, Hamza akiwemo wanarudishwa vyumbani kule Kumbakumba. Ni wakati wakiwa Kumbakumba ndipo baadhi ya wafungwa wanatoroka, tukio linalomfanya Sururu kuanza mpango wake wa ‘kata mbuga.’ Anakamilisha mpango huu pale anapotoroka siku kuu ya sherehe ya Ramadhani, Koplo Ngwali akiwa kwenye zamu. Msako wa kumtafuta Sururu unaanza na japo anakamatwa akiwa hai, Sururu hauawi kama wanavyofanyiwa wafungwa wengine waliojaribu kutoroka wakashikwa. Badala yake, anashawishiwa na Kifupi Nyundo na Meja Mapanga kwamba akubali kuwa shahidi wa mahakama. Anapokaidi anapata kichapo kama alichokipata Hamza. Baada ya kurudishwa kwenye vyumba kule Kumbakumba, Faraji, ambaye amesomea sheria, Hamza na Ambar wanatumia muda wao mwingi kujadili namna kesi yao ya uhaini itakavyokuwa.

Msimulizi anatumia kutoka gereza ambako matukio mengi yanatukia na kutupeleka aliko Khadijah. Tunaeleza kuhusu hali yake ya umasikini na jinsi anavyojaribu kila awezalo kumsaidia Hamza aachiliwe huru. Moja kwa moja tunapelekwa kwa Ba Mkwewe ambako mahaini walioteswa wakasalimu amri walipo. Hawa wameshaandaliwa kutoa ushahidi wa upande wa mahakama na ni pamoja na Mpakani, Sumbu, Marzuku, Mkadam, Vingosho, Zarikani, Pwacha, Kuchi na Haramia. Haramia anawashawishi wenzake kwamba wakifikishwa mahakamani wakane kwamba hawakuhusika, anasalitiwa na Pwacha anayemwambia Dude, ambaye anamwambia Kanali Mapepe, ambaye naye anamwambia Kanali Bunju. Kutuokana na uzito wa madai ya Haramia, kwamba wakubwa ndio walihusika katika mauaji ya Kigogo, Haramia anapelekwa *Mashakani Hotel* anakofungiwa chumba kimoja na chatu. Kwa bahati, Haramia anamwua huyo chatu na anachukuliwa na kurudishwa chumbani. Baadaye, mashahidi hawa wanakubaliana wote kwamba watakanusha ushahidi wao, Pwacha akawasaliti tena na mara hii wote wanapelekwa

kwenye makaburi yao ambako baada ya vitisho, wanakubali wote kwamba watashirikiana na akina Kanali Bunju. Wanatolewa makaburini na kupelekwa mahakamani ambako wanatoa ushahidi wao kama walivyotakiwa. Baada ya kesi kukamilika, wote wanahukumiwa kifo kwa kukubali kuwa walihusika katika mapinduzi yaliyosababisha kifo cha Kigogo.

Kesi ya uhaini inaanza mwaka mzima baada ya kifo cha Kigogo, na inachukua mwaka mzima kukamilika. Mahaini wanafikishwa mahakamani na mashahidi pia. Khadijah na wake wengine wa mahaini wanahudhuria vikao hivi vya mahakama. Hatimaye, uamuzi unatolewa. Wapo wanaohukumiwa kifo; wale mashahidi tisa pamoja na Mfaume, Doto na Heri Mahmoud. Wengine wanahukumiwa kifungo cha miaka kumi na mitano ambao ni pamoja na Sururu, Khalfan, Kondo na Ambar. Hawa walifungwa kwa kuwa na habari kwamba kulikuwa na mpango wa kumwua Kigogo ilhali hawakuwaarifu polisi. Walioachiliwa huru walikuwa Mabruki Issa, Faraji Majaliwa na Hamza.

2.5 Hitimisho

Sura hii imeeleza mtindo unaotumiwa na Shafi Adam katika riwaya zake tulizojadili. Aidha, tumeonyesha namna riwaya zake hizi zinaigiliana kimaudhui. Riwaya ya *Haini* imejumuisha sifa anuwai zilizomo katika riwaya zingine za Shafi. Tumeeleza historia ya kuandikwa kwa riwaya ya *Haini* na sababu zilizompelekea mwandishi kuiandika riwaya hii kama alivyoandika. Riwaya ya *Haini* ina sifa nyingi zinazochoecha utendaji ikilinganishwa na zingine za Shafi. Hii ndiyo sababu tuliichagua na sio nyingine yoyote aliyoiandika Shafi ili kuitumia katika utafiti wetu.

SURA YA TATU

LUGHA YA MAJIBIZANO NA WAHUSIKA

3.0 Utangulizi

Katika sura ya tatu, tumeshughulikia vipengele viwili vikuu vya utendaji; lugha ya majibizano na wahusika. Tumefafanua dhana lugha ya majibizano na hatimaye kuiainisha kwa mujibu wa majukumu ambayo yanatekelezwa na mazungumzo hayo katika riwaya ya *Haini*. Katika sehemu ya pili ya sura hii, tumeshughulikia kipengele cha wahusika ambapo baada ya kueleza dhana wahusika kwa kifupi, tumewaainisha wahusika kwa mujibu wa utendaji wao. Watendaji wa kipekee katika riwaya hii ndio wamepewa kipaumbele katika uchanganuzi wetu.

3.1 Lugha Ya Majibizano

Wataalam anuai wanatoa fasili tofauti ya dhana ya doyalojia au lugha ya majibizano:

Mumbo (2014) anafafanua kwamba dayalojia ni mtindo wa lugha ya majibizano ambao unatumika sana katika drama au tamthilia-ni kauli za majibizano. Lugha ya majibizano ndiyo nguzo kuu ya utunzi wa tamthilia na michezo ya kuigiza. Sifa kuu ya majibizano au dayalojia ya kidrama ni sentensi fupifupi kama ilivyo katika ushairi. Lengo la kutumia sentensi fupifupi katika drama ni kurahisisha uigizaji jukwaani, kwani mchezo wa kuigiza madhumuni yake ni kuwasilishwa kiutendaji mbele ya hadhira...dayalojia dhima yake si kuwasilisha ujumbe tu, bali inatekeleza majukumu mengine kama vile kubainisha taswira mbalimbali, kubuni miondoko jukwaani na kujenga ulimwengu wa matukio katika uigizaji.

Aina hii ya majibizano ndiyo tuliyochunguza na kubainisha katika riwaya ya Haini, huku tukifafanua namna ambavyo inawawezesha wahusika wanaoitumia kutekeleza utendaji wao.

Wamitila (2003) anaeleza kwamba mazungumzo hutumiwa kurejelea maongezi yanayopatikana kati ya wahusika wa kifasihi. Mazungumzo huhusisha mambo ambayo ni muhimu tu katika uendelezaji wa msuko wa kazi ya fasihi na yanapaswa kuwa na sifa za kutuwezesha kuwatambua wahusika wanaoshiriki katika maongezi kutokana na uteuzi wao wa maneno, lugha zao, matamshi yao.

Kutokana na fafanuzi hizi tunatambua kwamba majibizano au dayalojia huwa na umuhimu katika kazi za fasihi; kubeba ujumbe, kubainisha taswira mbalimbali, kubuni miondoko jukwaani, kujenga ulimwengu wa matukio katika uigizaji, kutuwezesha kutambua wahusika wanaoshiriki katika mazungumzo na kuendeleza msuko wa kazi husika ya fasihi. Hizi ni baadhi ya sababu zinazowafanya waandishi wa kazi za fasihi, hasa katika riwaya kuitumia mbinu hii ya uandishi, mbali na kwamba majibizano hupunguza uchovu wa kusoma masimulizi ya kinathari katika riwaya na hadithi fupi.

Bacon (1984) anasisitiza umuhimu wa lugha ya majibizano katika utendaji anapodai kwamba ili watendaji wafaulu katika utendaji wao, sharti wajumuishe majibizano na ishara. Majibizano ndiyo sifa kuu ya kazi za kidrama; tamthilia zikiwemo, na hivyo lugha hii inapotawala kazi ya kinathari kama vile riwaya huipa sifa za kidrama na hata zaidi kuchochea utendaji wake.

Shafi Adam ametumia dayalojia kwa kiasi kikubwa miongoni mwa wahusika katika riwaya ya *Haini*. Mazungumzo haya yanatekeleza majukumu ya kuendeleza maudhui

yaliyoangaziwa katika riwaya hii, pamoja na kutufafanulia hali mbalimbali wanamojipata wahusika wake. Mbali na hayo, majibizano haya yanarahisisha usomaji na hivyo hivyo kuchochea utendaji wake.

Katika kazi hii, tumeainisha lugha ya majibizano kulingana na majukumu ambayo inatekeleza. Kwa mfano, lugha ya majibizano imetumiwa na wahusika ili kujiliwaza, kupasha habari, kuhoji, kuhamasisha, kuendesha mashtaka na kushawishi kama tulivyojadili katika sura hii. Muainisho huu ni kwa mujibu wa Nadharia ya Utendaji. Bacon (1984) anafafanua kwamba ili watendaji wafaulu katika utendaji wao, sharti wajumuishe majibizano na ishara. Wahusika wametumia lugha hii ya majibizano kutekeleza majukumu ya kuliwaza, kupasha habari, kuhoji, kuendesha mashtaka, kuhamasisha na hata kushawishi. Wanafanya hivyo kwa kutumia lugha ya majibizano inayofanikisha kila jukumu linalotekelezwa.

Mwandishi ametumia majibizano ya kawaida ambapo anatumia maneno kama ‘akaeleza,’ ‘akafafanua,’ na kuna aina nyingine ambapo wazungumzaji wanazungumza kwa mfululizo bila ya maneno haya kutumiwa, ambayo Wamitila (2003) anayaita majibizano ya mkato. Katika sehemu zinazofuata tunajadili kwa mifano halisi matumizi ya lugha ya majibizano au dayalojia kama nyenzo ya utendaji katika riwaya ya Haini.

3.1.1 Majibizano kama Nyenzo ya Kuhoji

Mfano 3.1

...Alitaka kwenda chumbani kwa Khadija, kumbe Khadija naye akija ukumbini, wakakutana katika ujia wa katikati, “Nani?” Khadija aliuliza.

“Askari jeshi!” alijibu Hamza.

“Wanataka nini?”

“Sijui.”

“Fungueni haraka au tutavunja mlango!” aliamuru mmoja kutoka kule nje...

“Wewe nd’o Hamza?”

“Ndiyo!” alijibu kwa haraka, tena sasa kwa sauti ya hofu na wasiwasi.

“Wewe mwandishi wa habari?”

“Ndiyo!”

“Jana ulisikiliza BBC?”

“Sikusikiliza!”

“Hamduni unamjua?”

“Namjua!” “Yuko wapi?”

“sikumwona tokea tulipoachana jana mchana. Aliniambia anakwenda Mwanyanya kuna manuva!” Hamza aliyajibu maswali yao huku mikono amenyanyua juu, hofu imemjaa.

“Twende huku!”

“Wapi?” Hamza aliuliza.

“Wewe twende tu. Mbwa mkubwa, unaulizauliza nini?”...(uk. 7).

Katika tukio hili, Kigogo ambaye ni rais wa nchi ambayo mwandishi hajataja, ameuawa katika tukio la kihaini na watu wameanza kukamatwa na kufungwa gereza. Hamza, ambaye ni mhusika mkuu katika riwaya ya *Haini*, anakamatwa kutokana na uhusiano wake wa karibu na Hamduni, ambaye ndiye mshukiwa mkuu wa mauaji ya Kigogo. Maafisa wa polisi wanapomkamata wanamhoji kuhusu mambo kadha; yote yanayohusu kifo cha Kigogo ikiwa ni pamoja na habari za alipo Hamduni, mshukiwa mkuu wa mauaji hayo. Majibizano haya yanawawezesha askari wanaomkamata Hamza kutekeleza utendaji waliopewa wa kuhoji.

Lugha ya majibizano pia inadhihirika katika mifano ifuatayo:

Mfano 3.2

“Sasa tueleze!” alianza yule afisa wa usalama. “Hamduni yuko wapi?” Hamza alishangaa, hakujua la kujibu. Anavyojua yeye Hamduni amekufa. Hadithi zilizoenea Kumbakumba zinasema kwamba Hamduni aliuawa pale pale baada ya yeye kumpiga risasi Kigogo. Sasa ajibu nini? “Sijui” alijibu kwa sauti ya hofu, manyoya ya mwili yamemsimama, moyoni mwake akiomba, “Eh! Mungu! Nisaidie univue na balaa hili!” “Hujui?” aliruka yule askari wa usalama. Ana chungu ya makaratasi mkononi, akiandika. “Na Barakati unamjua?”

“Namjua!” Hamza akajibu. Pale pale ikamjia sura ya Barakati siku ile aliyokamatwa, akamkuta polisi ametiwa pingu za mikononi, uso umemvimba kama bunju.

“Yuko wapi?”

“Sijui!”

“Tueleze uhusiano wako na Hamduni.”

“Ni rafiki yangu wa kawaida tu!”

“Rafiki wa kawaida tu?”

“Ndiyo!” “Ukimwamini sana?”

Hamza akasita kujibu, akatulia makini akimtazama yule aliyemwuliza. Mara ikatoka sauti ya ukali kwa mwanajeshi mmoja, “Jibu!” “Sikuwa nikimwamini!” Hamza alijibu. Sasa ametulia, wasiwasi umeanza kumpungua pale alipokaa.

“Yeye akikuamini?”

“Sijui!”

“Kwani wewe ulikuwa humwamini?”

“Akishalewa alikuwa na tabia ya kusemasema ovyo!”

“Kwa hivyo wewe ulikuwa humwamini ili asije akasema ovyo kuhusu huu mpango wenu wa uhaini?”

Huu mpango wa uhaini mimi sina habari nao!”

“Sasa yeye husema nini ovyo?”

“Mengi tu!”

“Lipi moja kwa mfano?”

Sikumbuki hivi sasa, lakini husema maneno mengi tu!”

“Tueleze basi, moja tu katika hayo mengi.”

“Kwa mfano siku moja alilewa akasema atajitosa baharini.”

“Kwa nini ajitose baharini?”

“Sijui!”

“Wewe sasa unatutania ndiyo?” aliuliza yule askari wa usalama, sasa ameacha kuandika.

“Hapana, mimi sina utani na nyinyi!”

“Tueleze wewe unajua nini juu ya mauaji.”

“Mauaji gani?” aliuliza Hamza kwa mshangao.

“Wewe hujui mauaji gani? Mpumbavu mkubwa! Wenzako wameshakutaja hapa halafu wewe unajidai hujui mauaji gani!” alipiga kelele yule mwanajeshi mmoja, akapiga ngumi juu ya meza, akasimama, amehamaki.

“Mbona Hamduni katwambia na wewe umo?” aliuliza yule mkuu wa kile kikundi, kwa sauti ya utaratibu.

“Nimo wapi?” akauliza Hamza. Anashangaa kuhusishwa na jambo asilolijua. Tena jambo lenyewe si dogo. Ni mauaji, mauaji ya mkubwa. “Umo! Tena umo sana katika mpango wa mauaji ya mzee wetu!” alipiga kelele yule mwanajeshi wa pili, chumba kizima kikavuma, sauti yake imejaa mle tele.

“Sasa utasema au vipi? Aliuliza yule askari usalama.

“Kama kuna nnalolijua ntasema, lakini hayo ya mauaji mimi siyajui.” “Huyajui? Ngoja basi!”...(uk. 39-40).

Mfano huu unaonyesha namna Hamza anavyohojiwa. Miongoni mwa watu wanaomhoji ni askari jeshi wanne, askari polisi mmoja na afisa mmoja wa usalama, (uk. 37). Sita hawa wanamhoji Hamza kuhusu uhusiano wake na Hamduni na mauaji ya Kogogo. Hamza anahojiwa mara kadha wa kadha; wengi wa maafisa hawa wakiamini kwamba kwa kuwa yeye alikuwa rafiki wa karibu wa Hamduni, lazima na yeye alihusika katika mpango wa mauaji ya Kigogo. Katika mfano huu, wanamtaka aseme yoyote yale anayoyafahamu kuhusu mpango huo. Hata hivyo, Hamza hawaambii lolote la maana, na sita hawa wanamvamia kwa kichapo cha mipera, anateswa kikomo cha kuteswa na kuachwa, kama aliyekufa, (uk. 40-41).

Utendaji wa kidrama unadhihirika katika mahojiano kati ya Hamza na watu hawa sita. Wanaomhoji wanatumia sentensi fupifupi ambazo aghalabu ni maswali, naye Hamza kuwajibu. Majibizano katika mfano huu yanawawezesha wahusika hawa kutekeleza utendaji wao wa kuhoji.

Mfano 3.3

[Mzee Machale] Alipomaliza aliiweka chupa ya dawa chini akamtazama, “Wewe mzee mwenzangu uliingiaje katika mambo haya?” alimwuliza.

“Mambo gani?” Sururu naye akamwuliza. “Si haya mambo ya uhaini?” “Mimi simo,” Sururu alimjibu.

“Humo namna gani? Wasiokuwemo washatoka wote,” alimwambia, akimtazama, macho yake yameiva, masharubu yametawanyika, yametoa miche iliyotapakaa ovyoovyo puani mpaka mdomoni. Alimkaribisha Sururu sigareti naye akachomoa moja. Wote wamekaa wanavuta sigareti. Kimya, hapana anayesema na mwenzake. Mzee Machale akaanza tena, “Sasa wewe umejiinkiza katika haya mambo, watoto wako nje wanapata taabu.” “Mimi nakwambia simo! Tena sina mtoto.” “Huna mtoto?” Mzee Machale alimwuliza.

“Sina, sikujaaliwa kupata.”

“Na mke je?”

“Mke nnaye.”

“Sasa si anapata taabu huko nje?”

“Yeye keshazoea taabu. Huko tulikotoka maisha yetu ni tabu tupu.”

“Mimi nna watoto kumi na mbili. Dazeni nzima,” Mzee Machale

alijigamba. Sasa uso wake unaonesha tabasamu. Ni nadra sana kuwa hivyo.

“Ulikuwa unashindana na nani hata ukawa na watoto wote hao?”

“Siyo ushindani. Mimi mwanamme bwana.”

“Wako wapi watoto wote hao?”

“Wengine washaoa, wengine wameolewa. Mmoja Kapteni jeshini,” alijinata.

“Sasa watoto wote hao wewe ulitakiwa uwe nyumbani tu unastarehe...(uk. 129).

Mojawapo ya majukumu aliyopewa Mzee Machale ni ‘kuwatengeneza’ wafungwa kabla ya kukutana na wakubwa wa magereza. Katika majibizano haya, tunamwona Mzee Machale akimudadisi Sururu kuhusu kuhusika kwake katika mauaji ya Kigogo. Japo kuwahoji mahaini haikuwa kazi ya kimsingi ya walinzi wa magereza, waliwahoji wafungwa hawa wakiwa katika zamu zao, hasa katika mazingira ya kirafiki zaidi kuliko wafungwa wanapohojiwa na maafisa na makanali. Hii ndiyo sababu baadhi ya fungwa waliishia kuwafichulia walinzi hawa siri zao na kuishia matatani wanaposhtakiwa kwa wakubwa wa magereza kama inavyojitokeza baada ya Pwacha kuwasaliti wenzake kwa mlinzi Dude.

Ni baada ya kutayarishwa huku na majibizano haya kutokea ndipo Sururu anapokutana na Meja Mapanga, Kifupinyundo na wenzake, (uk. 131). Hawa wanataka Sururu akubali kushirikiana nao katika kuutoa ushahidi wa uongo kama walivyofanya Haramia na wenzake, na anapokataa, yanamfika makubwa; kuteswa, kuchapwa na kutupiliwa mbali akafilie huko, (uk. 133).

Nadharia ya Utendaji imeweka wazi umuhimu wa lugha ya majibizano hasa wahusika wanapotekeleza utendaji wao. Katika mifano tuliyotoa hapo juu, lugha ya majibizano imeshirikishwa katika utendaji wa kuhoji inavyofaa. Lugha dadisi na yenye maswali mengi imetumika ili kufanikisha shughuli ya kuhoji kama nadharia ya Utendaji inavyosisitiza.

3.1.2 Majibizano kama Nyenzo ya Kupasha Habari

Aina hii ya majibizano aghalabu inahusu wahusika na hasa mahaini wanapopashana habari na kusimuliana kuhusu mambo kama vile yanayotokea ama kwa Ba Mkwewe au Kumbakumba na vilevile nje ya gereza. Aina hii inajumuisha vilevile majibizano yanayotokea wakati mahaini wanakutana na kujuana na huku wakiambiana kuhusu mateso mbalimbali wanayokumbana nayo katika harakati za kuteswa kule gereza, pamoja na hali za familia zao zilivyo nje ya magereza. Wakati mwingine huwa wanaongea kila mtu anachokifikiria kuhusu hatima yao. Badala ya msimulizi kusimulia kwa njia ya moja kwa moja, anawapa wahusika katika riwaya hii kauli ambazo kwazo wanajibizana kama inavyobainika katika mifano ifuatayo:

Mfano 3.4

Mazungumzo haya yanatukia siku kadhaa baada ya Hamza kukamatwa na baadaye Abdul kupelekwa chumbani alimo Hamza. Abdul hana wasiwasi, ameishi Kumbakumba zaidi ya miaka miwili. Kwake, jela ni pahala pa kawaida tu.

“Hebu nieleze kumetokea nini?” aliuliza Hamza kwa hamu kubwa ya kutaka kujua kile kisa kilichomfanya awe anateseka ndani mle mpaka leo.

“Kigogo ameuawa.”

“Unasemaje?” Hamza aliuliza kama kwamba hakusikia.

“Kigogo ameuawa na watu chungu nzima wameshakamatwa. Na sisi ndo mahaini,” Abdul alieleza.

“Nani? Mimi? Mimi leo nishakuwa haini? Nani tena huyo aliyemwua Kigogo?” Hamza alizidi kudadisi.

“Hamduni,” Abdul alimjibu.

“Hamduni?” Hamza alizidi kupigwa na mshangao, macho ameyatoa kama maglobu.

“Naskia alikuwa pamoja na Barakati,” Abdul aliendelea.

“Na Barakati tulikuwa sote Malindi. Alikuwa ametiwa pingu,” alisema, Hamza ameshangaa.

“Nasikia walikuwa na Barakati, tena inasemekana walimfuata Kigogo palepale klabuni anapocheza dhumna.”

“Abdul!” Hamza alimwita kwa sauti ya kukata tamaa. “Sitoki! Sitoki tena ndani humu!”

Abdul alimtazama Hamza kwa macho ya kishujaa akamwambia,

“Sikiliza wewe. Humu gerezani hamna kaburi. Utatoka tu. Kama hutatoka mzima itatoka maiti yako. Tutatoka tu!”
Hamza alimtaazama Abdul na ghafla akamkumbatia. Akamtaazama tena. Akayarudia yale maneno yake, “Tutatoka tu.” (uk. 13-14).

Masimulizi ya riwaya hii yanapoanza, msimulizi haelezi sababu ya mambo yanayotendeka. Hamza na wenzake wanasikia tu milio ya bunduki, hali ya taharuki inatanda na hatimaye Hamza anakamatwa bila hata yeye mwenyewe kujua sababu ya kukamatwa kwake. Majibizano haya yanatekeleza jukumu muhimu la kumpasha Hamza pamoja na msomaji sababu ya hasa kukamatwa kwa watu, kwamba Kigogo ameuawa. Katika tukio hili, Abdul anampasha Hamza yaliyotokea, aliyemuua Kigogo na namna watu walivyokamatwa, wao wakiwemo.

Mfano 3.5

Majibizano haya yanatokea muda baada ya Hamza na Doto kupata afueni kutokana na kipigo wanachopata kutoka kwa maafisa wa kwa Ba Mkwe, (uk.48). Doto anapelekwa chumba Hamza alimo akiwa katika hali mbaya na Hamza anamwuguza. Baada ya hali yake kuwa na afadhali, wawili hawa ndipo wanapata nafasi ya kuzungumza, hivyo kuwepo kwa majibizano haya. Iliwachukua wiki nzima kupata nafuu. Hamza akajiona hajambo Doto haijambo. Ingawaje vitisho na vilio viliendelea kwa Ba Mkwe, kwao ilikuwa shwari. Sasa ndipo walipopata muda wa kukaa kwa utulivu wakapashana habari katika majibizano haya.

“Vipi Kumbakumba bado kumejaa?” Hamza alimwuliza Doto.

“Kumbakumba ndo nini?” Doto naye alimwuliza Hamza.

“Wapi?” akauliza Doto

“Huko Kumbakumba.”

“Mimi sikujui huko Kumbakumba.”

“Wewe umeletwa hapa moja kwa moja?” aliuliza Hamza kwa mshangao.

“Ndiyo, wamenichukua kwetu Jambiani mpaka hapa.”

“Basi yako wewe ni makubwa.”

“Kwa nini?”

“Wale wanaoletwa huku moja kwa moja huwa wale watuhumiwa wakuu.”

“Alaa! Alishangaa Doto. “Kwani hao wengine huwa vipi?” aliuliza.
 “Kuna watuhumiwa namna nne hivi, “Hamza alianza kueleza na Doto naye akimsikiliza kwa makini, ameegemea kwenye pembe ya ukuta. Miguu ameichanua kuzipa wasaa hasua zake.
 “Kuna wale wanaopelekwa Kumbakumba, kule mbele kule, gereza kuu.”
 “Ala! Kule nd’o kunaitwa Kumbakumba?” aliuliza Doto.
 “Ndivyo wafungwa wanavyokuita.”
 “Alaa! Ehen!” Doto akamtaka Hamza aendelee na maelezo yake.
 “Hao hukaa huko huko Kumbakumba. Hawaletwi huku. Hao wana afadhali kidogo.”
 “Ehen!”
 “Kuna wale walioko Kumbakumba lakini mara moja moja huletwa huku, wakahojiwa, wakapakwa mafuta kidogo, wakarejeshwa huko huko Kumbakumba.”
 “Hupakwa mafuta gani?” Doto akauliza.
 “Kupakwa mafuta nd’o kutandikwa mipera.”
 “Alaa!” alishangaa Doto. “Nd’o lugha ya huku hiyo?”
 “Hao nao pia wana afadhali kidogo,” aliendelea Hamza. “Kuna wale wanaofika Kumbakumba, wakaletwa hapa kuhojiwa, wakapakwa mafuta barabara, halafu wakaselelea hapa hapa, kama mimi. Hao...”
 Hamza akasita kidogo. “Hao ndio waliokabiliwa na balaa. Halafu kuna wale wanaoletwa hapa moja kwa moja, kama wewe.”
 “Ehen!” Doto akashangaa, amekodoa macho anamtazama Hamza.
 “Nyinyi nd’o wenyewe! Nyinyi nd’o wauaji! Nd’o mahaini hasa! Nd’o watoto wa nyoka!”
 “Sasa?” Doto akauliza, hofu imemzidi. Hamza amempa habari za kukatisha tamaa na kumwondolea matumaini. “Sasa tukae tu tushubiri mahaaliwa yetu,” Hamza alijibu.
 “Majaliwa yetu?” Doto akauliza...(uk. 51-52).

Kupitia majibizano haya, wahusika Doto na Hamza wanafanikiwa kupasha habari kwa kila mmoja wao na hata kwa hadhira. Kwanza, Hamza anampasha mwenzake Doto kuhusu hali inayowakabili. Anampasha Doto kuhusu aina nne kuu za mahaini katika magereza ya kwa Ba Mkwe na Kumbakumba. Pili, wakati Hamza akimpasha Doto habari hizi, hadhira pia inapata kuelewa ni kwa nini baadhi ya mahaini hupelekwa Kumbakumba wakaa huko, kwa nini wengine hupelekwa Kumbakumba, wakapelekwa kwa Ba Mkwe na kurudishwa Kumbakumba au wengine wakaachwa huko huko kwa Ba Mkwe, na hatimaye kwa nini baadhi yao wanapokamatwa

hupelekwa kwa Ba Mkwe moja kwa moja kama inavyomtukia Doto. Ikiwa tukio hili litatendwa kidrama kwenye jukwaa, mazungumzo haya yatafanikisha utendaji wake.

Mfano 3.6

Katika mfano huu, mahaini wanajipata wakizungumza kuhusu Zonga, mtu waliyedhani alikuwa mmoja wao kumbe alikuwa jasusi aliyewekwa miongoni mwao ili kuduhushi mambo.

Chumba chao [akina Hamza] kilifunguliwa na askari aliyekifungua chumba kile hakusema na mtu yeyote. Aliwatazama wote mmoja mmoja, halafu akamwita Zonga, “Wewe. Vaa nguo zako.” Baada ya Zonga kutoka tu Ambar akajigamba, “Niliona zamani kama Zonga atatoka.”

“Umeona atatoka kwenda wapi?” Sururu alimwuliza.

“Yule ni safari ya nyumbani tu,” alijibu.

“Umejuaje? Kama wanakwenda kumnyonga je?”

“Wakamnyonge yule?” Faraji aliingilia kati. “Yule mtu wao yule.

Wamemtia humu makusudi kuja kutuchuma, asikilize tunasema nini.” “Hata mimi nilikuwa na wasiwasi naye kuwa lazima ni kiwavi yule,” aliongeza Kondo.

“Tena ni shushushu aliyepa,” alithibitisha Khalfani. “Mimi nimeshawahi kumwona Pemba ndani ya gari la masekyuriti.” “Kwa nini usitubonyeze tukajua kama humu ndani tuna kidudu mtu?” aliuliza Hamza.

“Mimi nilidhani kwamba na yeye amekamatwa kama walivyokamatwa wengine, polisi, wanajeshi,” alijibu Khalfani.

“Basi kama aliletwa humu kuja kupeleleza, ameula na chua. Hana lolote alilolipata,” alisema Ambar. “Sasa wewe na ubingwa wako wote wa kutabiri hukujua kama mtu mbaya yule? Aliuliza Sururu. “Mimi haikunijia kabisa ndani ya akili yangu kama tunaweza kutiliwa mtu kama yule humu ndani,” alisema Ambar.

“Lakini mna hakika yule alitiwa humu kupeleleza, au mnadhani tu?” aliuliza Swedi.

“Ala! Wewe namna gani? Humwoni mtu mwenyewe alivyo. Tokea siku aliyotiwa humu ndani hatukusikia kauli yake. Yu kimya kama bubu. Kila wakati hujidai kulala kumbe anatusikiliza tunasema nini,” alisema Faraji.

“Lakini ni jambo la kawaida kwa wataalamu wa shughuli za ujasusi kuchomeka mtu wao pahala kama hapa,” alisema Hamza.

“Sasa wanatuletea mashushushu mpaka jela kuja kutafuta nini na wenyewe wanasema washamaliza uchunguzi? Washapata kila kitu, “aliuliza Khalfani...(uk. 115-116).

Mazungumzo haya yanafanikisha utendaji wa kupashana habari miongoni mwa mahaini. Mbali na mahaini wenyewe kupashana habari kwamba huenda Zonga akawa ametiwa mle waliko kwa minajili ya ujasusi, hadhira pia inapata habari hiyohiyo. Mazungumzo haya yanaweka wazi namna uchunguzi wa waliohusika katika mauaji ya Kigogo pamoja na mipango ya mahaini inavyokuwa wakati wakiwa vyumbani. Hapa, tunafahamishwa kwamba Zonga ni mmoja wa maafisa wapelelezi, na sio mfungwa kama walivyokuwa wenzake.

Kulingana na Nadharia ya Utendaji, waigizaji huchukua nafasi fulani za watu katika matini na kuigiza matendo yao kupitia mazungumzo na ishara mbele ya hadhira. Mazungumzo yametiliwa maanani katika utendaji wa kupasha habari. Wahusika wamepewa sentensi fupifupi zilizojaa habari muhimu kwa wahusika wenzao na wasomaji.

3.1.3 Majibizano kama Nyenzo ya Kuliwaza

Matukio mengi katika riwaya hii yanatokea gerezeni. Kinachotawala katika magereza haya ni mateso, ukatili, njaa, hofu na maumivu ya aina aina. Mwandishi hivyo amewapa wahusika hawa mahaini namna ya kujiliwaza, wakapeana nguvu, wakafufua matumaini yaliyokufa, na wakati mwingine hata wakacheka na kufurahia wakiwa mle vyumbani. Badala ya msimulizi kusimulia kwa njia ya nathari namna wahusika wanavyojiliwaza wenyewe, amewafanya wahusika hawa wajibizane moja kwa moja na katika kufanya hivyo, wakatulizana na kujiliwaza. Katika mifano ifuatayo tunaona jinsi wahusika wanatekeleza tendo la kuliwaza kupitia kwa mazungumzo yao.

Mfano 3.6

Msimulizi anaeleza kuwa baada ya kipindi kirefu cha kuugua na kuuguzana, maskini tena bila msaada wowote wa matibabu maalum, inshalla hali zao [Hamza na Doto]

sasa zilikuwa nzuri. Doto alikwishafanya mazoea ya kutembea huku miguu ameichanua. Madonda ya Hamza yaliwkishapona akabakia na makovu tu na Doto naye mzima, madhubuti. Doto alikaa pembe ya mkono wa kulia wa kile chumba na Hamza amekaa katikati, ameegemea mlangoni.

“Nani aliyekwambia karibu ?” Doto aliuliza. “Yule Mzee Machale ndio?” aliendelea.

“Ah! Yule mzee mkorofi kama nini sijui. Yeye ameniambia tutaozea humuhumu ndani!”

“Sasa umejuaje kama karibu tutatoka?”

“Wewe unafikiri watatuweka humu ndani mpaka lini? Watatutoa tu, lazima siku moja watatutoa, tena siku hiyo iko karibu sana,” Hamza alimweleza Doto kwa hamasa yake ile ile iliyojaa matumaini.

“Wewe bwana unapenda kujifurahisha.”

“Siyo kujifurahisha,” alijibu Hamza, akaendelea kumweleza Doto.

“Nilipokuwa kule Kumbakumba nilikutana na jamaa mmoja anaitwa Abdul. Abdul alinieleza maneno ya maana kwelikweli. Unajua aliniambiaje? Aliniuliza kama humu gerezani mna kaburi na mimi nikamjibu hakuna. Akaniambia basi tutatoka tu, kama hatukutoka tukiwa hai basi zitatoka maiti zetu....” (uk. 60)

Katika sehemu hii ya majibizano, Hamza anafanikiwa kumliwaza Doto pamoja na kumpa tumaini kwamba asikate tamaa hata mateso yanapozidi kwani watatoka tu. Msimulizi ameeleza kwamba wawili hawa wamekuwa katika hali mbaya kutokana na mateso na kichapo kwa muda mrefu sasa. Hali zao zimekuwa mbaya, lakini wanapata afueni. Mazungumzo haya yanapotukia, Hamza amekwishasahau yaliyomkumba, amesahau kwamba alipo ni mahali pa dhiki na mateso na amechangamka.

Anamhimiza Doto kufurahi vilevile kwa kuwa hakika watatoka. Hamza akamuuliza

Doto:

“Unajua kucheza dhumna wewe?” “Sijui,” Doto alimjibu.

“Ukiziona hizo dhumna zenyewe unazijua?”

“Nazijua sana, mimi naona wanaocheza mchezo huo ni wale watu wasiokuwa na kazi ya kufanya, kutwa wako vibarazani wakipigizana kelele,” alijibu Doto kwa dharau.

“Wewe huwezi kujua raha ya mchezo wa dhumna. Dhumna ni mchezo wa watu wa mjini, wewe mshamba utaujuaje,”

“Ndo maana nikakwambia huo ni mchezo wa watu wasiokuwa na kazi ya kufanya. Mshamba hawezi kupoteza wakati wake kutwa amekaa anacheza dhumna,” Doto alijigamba.

“Nani kakwambia?” Hamza aliuliza.

“Mimi mshamba, nayajua vizuri maisha yetu, hatuna wakati wa kupoteza, kukicha tu jembe begani kila mtu anaelekea kondeni kwake, sasa wewe unafikiri tutacheza dhumna saa ngapi?”

“Basi mimi nitakufundisha, ukitoka hapa ukawafundishe washamba wenzako,” Hamza alimtania Doto.

“Wewe Hamza tokea juzi nakuona kama mtu anayeota ndoto. Umeshika tutatoka, ukitoka, nikitoka, wewe unafikiri tutatoka humu?” Doto aliuliza amekata tamaa. “Kwa nini tusitoke?” Hamza naye akauliza.

“Hujui kwa nini? Kwa sababu sisi nd’o mahaini, tunaambiwa ati sisi nd’o tulomwua Kigogo. Unafikiri wewe Hamza dogo hilo?” “Mimi si haini wala sijamwua mtu. Kama Kigogo kauawa, wao wenyewe watamjua aliyemwua, mimi nitatoka tu.”

“Wewe unasema wewe si haini na huko nje watu wanasema sisi sote mahaini. Unafikiri Machale alipokwambia tutaozea humu ndani alikuwa akikutania?”

“Mzee Machale hata hajui alisemalo. Yeye mwenyewe ni mfungwa kama sisi, kutwa

kucha yumo humu, na yeye akili yake imeshakuwa kama akili ya walio humu ndani...”

“Tuyawache hayo, turudi kwenye dhumna,” Hamza aliyakurupusha yale mazungumzo. Alimfuata Doto pale alipokuwa amekaa. Amekichukua kifurushi chake cha vile vikaratasi. Vimeshakauka, “Tazama,” alimwonesha Doto vile vipande vya karatasi. “Hizi nd’o dhumna zetu,” alimwambia. “Angalia hivi vidoto,” alimfahamisha... (uk. 61-62).

Msimulizi amewapa mahaini uwezo wa kujifurahisha hata katika hali hii ya dhiki waliyomo. Wakati wakicheza michezo hii ndipo mazungumzo huanza na wakajibizana huku wakiliwazana. Hawakai wakasononeka bali hujifunza mambo, wakaliwazana, wakahimizana na kutiana nguvu; wakapata tumaini la kuishi na kutoka gerehani. Katika mfano ufuatao, baada ya Hamza kumfunza Doto namna ya kucheza dhumna, (uk. 62). Hamza anamfunza kucheza Chess vilevile na baadaye wanaanza kucheza wakati wakiwa mle chumbani. Wakichoka kuongea hucheza, wakichoka kucheza huongea, na hivyo siku hazijikokoti kama zilivyofanya hapo awali.

Majibizano haya, mbali na kuwaliwaza wao wenyewe huwapunguzia wasomaji dhiki ya kusoma mateso tupu. Tazama hali hii inavyojitokeza katika mfano ufuatao:

Mfano 3.7

Majibizano haya yanatokea chumbani nambari sita, (uk. 104), walikofungiwa akina Hamza baada ya wafungwa 655 kuachiliwa huru. Wamo katika hali ya kukata tamaa; hawana matumaini ya kutoka kule, kwani kama Sururu anavyomwambia Kondo, waliofaa kutoka washatoka. Isitoshe, hao waliobaki ni wale wanaohusishwa moja kwa moja na mauaji ya Kigogo, sababu tosha ya kuwakatisha tamaa. Hata hivyo, Hamza ameshikilia kauli aliyoambiwa na Abdul, (uk. 14), kwamba watatoka tu. Anaamini pia kwamba uchunguzi haujakamilika, na upo uwezekano wakaachiliwa.

[Kondo] Anamtazama Sururu, “Tutatoka?” alimwuliza.

“Wa kutoka washatoka, sisi ni wa kubaki,” alimjibu.

“Mpaka lini?”

“Mpaka siku litakapolia parapanda, wafu wakafufuliwa.” “Manake nd’o hatutoki?” aliuliza kama mtoto anayedadisi. “Wewe namna gani unauliza maswali ya kipuuzi. Nakwambia wa kutoka washatoka!”

Hamza alimtazama Kondo jinsi mabega yalivyompwaya, amekata tamaa. Ile haiba na ucheshi wake sasa hana tena, maisha kwake sasa yamegota. “Sururu mbona unamtisha mwenzako?” aliuliza Hamza. Yeye amelala juu ya kirago chake kule pembeni, karibu na mlango. Bado hali yake dhaifu kutokana na ile homa iliyomshambulia. “Namtisha?” aliuliza Sururu. “Kwani wewe unaonaje Hamza?”

Aliuliza.

“Mimi naona huu mchekecho bado haukwisha. Naamini kwamba tutatoka.”

“Siyo leo lakini. Wala siyo kesho. Wala siyo keshokutwa. Wala siyo mtondogoo.”

“Ndiyo, lakini tutatoka.”

“Mimi nakwambia hapa, mpaka mbono,” alisisitiza Sururu...(uk. 105)

Lugha ya majibizano katika mifano hii imetumiwa na wahusika kwa ufanisi mkubwa katika kutekeleza jukumu la kuliwaza. Maneno yenye tumaini yametumiwa ili kuwapa mahaini imani kwamba watatoka katika hali waliyomo hatimaye. Kwa

mfano, Hamza anakuwa mtendaji muhimu katika tukio hili, kwa kuleta tumaini na kuwaliwaza wenzake. Katika kufanya hivyo, lugha hii imewiana na maelezo ya Nadharia ya Utendaji kuwa majibizano ni kiungo cha kimsingi cha utendaji.

3.1.4 Majibizano kama Nyenzo ya Kushawishi

Mbali na kuliwaza, majibizano baina ya wahusika katika riwaya ya Haini yametumiwa katika kuwashawishi wahusika. Utendaji huu umedhihirika katika mifano ifuatayo:

Mfano 3.8

Haya ni majibizano yanayotokea kati ya maafisa wa gereza na mahaini wakati wakiwashawishi washirikiane nao katika mpango wa kuwa mashahidi wa upande wa mashtaka. Mazungumzo haya, tofauti na wakati wa kuwahoji mahaini, huwa yamejaa upole na utu, na hugeuka kuwa vita pale tu anayeshawishiwa anapokataa kushirikiana na wakubwa hawa. Faraji, (uk. 116) anadai kwamba ushahidi wa kesi ya uhaini umeshavurugwa, hivyo lazima kutafutwe mashahidi wa kuwasingizia watu. Hili ndilo lengo kuu la majibizano haya:

Ghafula mazungumzo yalisita, akaulizwa Hamza, “Utakunywa nini?” aliuliza yule aliyekaa kule kwenye meza. Hamza alishangaa. “Utakunywa nini? Soda, chai au kahawa?” “Soda,” Hamza alijibu. “Soda gani?” “Yoyote ile.” “Baridi.” “Na gilasi au bila gilasi?” “Vyovyote vile.” “Au tukuletee bia?”...(uk. 78).
... “Sikiliza Hamza,” aliingilia kati Kanali Mapepe... “Sisi tumekwita hapa kukuomba utusaidie. Utusaidie na sisi tutakusaidia, iwe nipe nikupe. Unasemaje?” aliuliza Kanali Mapepe. “Msaada gani?” aliuliza. “Sisi tunajua kwamba wewe huhusiki lakini ombi letu ni kukutaka ukubali. Ujidai kama vile umo na unawajua wengine. Tuna orodha ya majina hapa tutakupua, na wote hao tumeshawatungia hadithi

kuthibitisha vipi wanahusika,” alieleza Kanali Mapepe kwa sauti ya upole iliyojaa busara tele. “Halafu?” aliluliza Hamza.

“Halafu?” aliuliza Kanali Mapepe naye. “Halafu pale tutakapowafungulia mashtaka mahakamani wewe utakuwa shahidi wa upande wa mashtaka tu,” aliendelea.

“Shahidi tu?” alidadisi Hamza.

“Ndiyo, shahidi tu,” alijibu Kanali Mapepe.

“Mmmm!” aliguna Hamza, akiwaza kwa makini, “Nitakuwaje shahidi tu na mimi nimeshakubali kama nimo, nahusika?” aliuliza.

“Hayo tuwachie sisi, tunajua namna ya kuyatengeneza,” alisema Kanali Mapepe.

“Mtayatengenezaje?” aliuliza Hamza...(uk. 81-83).

Nia kuu ya mazungumzo haya ni kumshawishi Hamza, ambaye ni mshukiwa mkuu wa mauaji ya Kigogo, ashirikiane na maafisa hawa katika kutoa ushahidi wa uongo.

Kanali Mapepe anafanikiwa katika kutekeleza utendaji wake wa kumshawishi Hamza.

Anatumia lugha ya ushawishi tofauti na inayotumiwa katika kutisha au hata kuhoji.

Lugha yenye upole na iliyojaa ahadi imetumiwa na askari jela katika kuwashawishi mahaini. Lugha hii ya upole inatiliwa mkazo na matendo ya ukarimu wa makanali hawa kwa mahaini kama Hamza. Hali hii ndiyo Bacon (1984) aliyoitia kufaulu kwa utendaji. Yaani mhusika kuambatanisha ishara na lugha ya majibizano katika utendaji wake.

3.1.5 Majibizano kama Nyenzo ya Kuhamasishana

Katika mfano 1 hapo juu, Hamza anakataa kushawishika. Anakataa kushiriki katika mpango huu wa kukubali kwamba kahusika katika mauaji ya Kigogo na kuwataja wengine. Hata hivyo, kuna wale walioteswa wakakubali, na hawa wamewekwa katika hali nzuri kule gereza, tofauti na wenzao katika vyumba vingine. Hawa wamepewa michezo ya kucheza, wakapitisha wakati na kufanya siku zipite kwa haraka. Ni wakati wakicheza, na wakati mwingine usiku ndipo wao huzungumza kuhusu hali waliyomo, na kuhamasishana kwamba wakanushe madai kwamba wao walihusika katika mauaji ya Kigogo pale watakapofikishwa mahakamani. Wanajibizana wenyewe kwa

wenyewe pale chumbani, na kupitia mazungumzo yao, tunapata kujua msimamo wa kila mmoja wao kuhusu hali inayowakabili.

Mfano 3.9

“Sasa mnasemaje?” aliuliza Mpakani. Ametoka katika dimbwi la mawazo alilokuwa amezama.

“Tunalo la kusema,” alisema Pwacha. “Tuseme nini na tumeshaingia mtegoni, tumejaa tele,” aliendelea.

“Hapana!” Aliruka Haramia, ametoa macho, ameyatumbua. “Bado hatukuingia mtegoni. Tutaingia mtegoni tukikubali pale mahakamani, lakini kama tukikataa, tukasema kwamba sisi hatujui chochote, basi ujanja wao utakwisha.”

“Una maana tukifika mahakamani tukatae?” aliuliza Kuchi.

“Ndiyo,” alijibu Haramia. “Tena tukatae katakata.”

“Tutakataaje na tushatoa ahadi, tushakubali kila kitu, yashaandikwa yote,” alihoji Zarikani.

“Si tutasema tu kama yote tumeyaandika kwa kulazimishwa. Tutasema tu kama tumepigwa, tumeteswa,” alisema Haramia.

“Unajua wewe, sasa tunakula chakula kizuri, tunaletewa sigareti, tumepewa michezo tucheze chumbani, tunabembelezwa kama watoto wadogo, yote haya, halafu twende mahakamani tukakatae. Wa-llahi watatuuu,” alisema Zarikani....(uk. 155-156).

Mazungumzo haya yanachacha na kuendelea hadi (uk. 160). Mashahidi wote tisa wanashiriki, na michezo imekwama, kila mtu anatia na kutoa lake kuhusu ama kukubali au kukataa kutoa ushahidi wakati kesi ya uhaini ikianza. Jambo moja linalobainika katika mazungumzo haya ni kwamba hawakukubali kuwa mashahidi kwa hiari yao, au kutokana na ahadi ya kuachiliwa; wao wenyewe wanajua huo ni uongo, na haiamkiniki mtu akakiri kushiriki katika mauaji ya Kigogo kisha akaachiliwa huru. Waliteswa kikomo cha kuteswa, ndipo wakasema waliyoyasema na hatimaye kukubali kutoa ushahidi walioandaliwa na wakubwa wa mashtaka. Baadhi kama Pwacha hata hivyo wanaona kwamba kukataa kutoa ushahidi itakuwa sawa na kukosa fadhila kwa zile takrima zote wanazopewa kule gerezani. Baadaye wakati hukumu ya kesi hii inatolewa, tisa hawa wanahukumiwa kifo, (uk. 264) kama alivyowaeleza Marzuku katika sehemu tofauti ya majibizano haya:

“Sikilizeni nyie,” aliingilia kati Mpakani. “Nyinyi mnafikiri inaingia akilini kwamba ati sisi tunakwenda pale mahakamani, tunakubali kila kitu, ati kwa ushahidi wetu, ushahidi ambao nna hakika wataupinga kwa nguvu zao zote. Yanaingia akilni hayo?” aliuliza Mpakani. “Sisi twende tu mahakamani. Tukubali hivyo wanavyotaka wao, tutoe huo ushahidi wanaotaka wao, halafu tuone, watatuachia au watatuadhibu,” alisema Sumbu.

“Na unajua adhabu yetu nini kama watatuadhibu? Kifo,” alisema Marzuku.

“Kweli” aliuliza Kuchi. Kama aliyezindukana kutoka usingizini.

“Kweli?” aliuliza tena. “Manake! Manake! Yote yale tuloyasema, yote yale tulokubali hayatotusaidia kitu?”

“Yote yale tuloyasema, yote yale tulokubali, yatasaidia katika kukikaza vizuri zaidi kitanzi katika shingo zetu,” alisema Haramia....(uk. 157).

Mashahidi hawa wanazidi kuhamasishana kuhusu kukataa kwa pamoja kwamba wao walihusika kama mfano huu unavyodhihirisha zaidi.

Mfano 3.10

...Haramia akakohoa kwa nguvu kama mtu aliyepaliwa na mate. Zarikani akamwita kwa sauti ya kunong’ona, “Haramia.” “Hun!” Haramia akaitika.

“Umelala?”

“Ni macho.”

“Haramia!” Zarikani akamwita tena.

“Hun!” Haramia akamwitikia.

“Mimi nafikiri maneno yako ni sahihi kabisa.”

“Maneno gani hayo?” Haramia alimwuliza kwa sauti ya mtu aliye katika maruweruwe ya usingizi.

“Mimi nafikiri hakuna njia yoyote ya kutunusuru ila sote kwa umoja wetu tukatae.”

“Je! Umetumwa?” Haramia alimwuliza.

“Wacha upuzi wako Haramia, wewe unafikiri nani atanituma mimi?” Zarikani aliuliza.

Kila mtu mle chumbani sasa masikio yake yako wazi wanasikiliza Zarikani na Haramia. Mkadam akashindwa kujizuia, na yeye dukuduku limemkaa rohoni. “Tukatae sote,” na Mkadam naye akaingilia kati. “Tukikataa tumekwisha! Watatuu!” Mpakani naye akaingilia mazungumzo, amenyanyuka kutoka pale alipokuwa amelala. “Hawawezi, hawawezi kutuu manake bila ya sisi hakuna kesi,” Kuchi akampinga Mpakani.

Sasa kila mtu anasema lililomkaa moyoni, wakati umewadia, saa ya kuamua karibu itagonga, kila mtu roho anaiona tamu hakuna mwenye kutaka kuipoteza. Wote wakakubaliana, “Tukatae.” (Uk. 204-205)

Katika mazungumzo haya, mashahidi hawa tisa wanafanikiwa kuhamasishana kwamba wasikubali kutoa ushahidi wa uongo dhidi ya wenzao walioshtakiwa kwa kuhusika katika jaribio la kupindua serikali, tukio lililopelekea kuuawa kwa Kigogo. Wanahamasishana kwamba siku wakifikishwa mahakamani waseme kwamba walilazimishwa kutoa huo ushahidi. Japo hapo awali baadhi walitaka kuutoa ushahidi huo, wanapomaliza majibizano haya wamefanikiwa kuungana kwa kauli moja.

Kama mifano iliyotangulia, mifano hii ya kuhamasisha inaonyesha kwamba lugha ya majibizano inapotumika sambamba na ishara hufanikisha utendaji wa tukio inamotumika kama Nadharia ya Utendaji inavyoeleza.

3.1.6 Majibizano kama Nyenzo ya Kuendesha Mashtaka

Majibizano yanatumika zaidi ya usimulizi wa kinathari katika uendeshaji wa kesi ya uhaini. Majibizano yametumika kwa njia faafu katika kuendesha kesi hii, hasa kwa sababu kesi aghalabu huhusisha mshukiwa kuulizwa maswali huku akiyajibu, na hivyo kuzua hali ya majibizano ya moja kwa moja. Chopra, kiongozi wa mashtaka, anaanza kwa kuwaleta mashahidi. Hawa ni wale tisa ambao tumewajadili katika mifano iliyotangulia ya mazungumzo. Kama msimulizi anavyosimulia, walikuwa wameandaliwa; wataulizwa nini na watajibu nini hapo watakapoulizwa. tazama majibizano haya:

Mfano 3.11

Chopra akanyanyuka akaikaza tai yake, akaangalia huku na huku, akasema, "...Leo nitamleta mbele ya mahakama yenu tukufu shahidi wangu wa kwanza, Mkadam Bakari."

"Jina lako nani?" Chopra alimwuliza kwa sauti ya upole.

"Mkadam," alijibu.

"Mkadam nani?"

"Mkadam Bakari."

“Mkadam Bakari,” Chopra alimwita, akamtazama machoni bila ya kupepesa, “Maswali nitakayokuuliza yanahusu mambo yaliyotokea zamani kidogo kwa hivyo lazima ufikir kwa makini kabla hukuyajibu maswali yangu.”

“Nitafanya hivyo,” alimjibu Mkadam

“Barabara,” Chopra alimpongeza akaendelea. “Nataka mawazo yako yarudi nyuma kiasi cha mwaka mmoja hivi, ile siku aliyouawa Kigogo.”

“Sawa,” alijibu Mkadam.

“Siku hiyo saa kumi jioni wewe ulikuwa wapi?”

“Nilikuwa kwangu.”

“Kwako ukifanya nini?”

“Nikimsubiri mtu.”

“Mtu gani?”

“Mpakani.”

“Ukimsubiri kwa madhumuni gani?”

“Alikuwa aje kwangu kunipa habari muhimu sana.”

“Habari gani hiyo?”

“Habari ya mipango yetu ya kuiangusha serikali ya Kigogo....”
(uk. 238).

Kama walivyoandaliwa, Mkadam, mmoja wa wale mashahidi tisa waliotajwa, anatoa ushahidi wake. Anawataja wengine ambao aliambiwa awataje katika ushahidi wake; Mpakani na Kubwalao, na jinsi walivyopanga kuiangusha serikali ya Kigogo, jambo lililopelekea mauaji yake. Mashahidi wengine wanatoa ushahidi vivi hivi na wanaishia kuhukumiwa kifo kwa kukubali kwamba walishiriki katika mauaji ya Kigogo.

Mfano 3.12

Karani wa mahakama akasimama na kumkabidhi Akida Msahafu, Akida akaupokea kwa mkono wake wa kulia, karani wa mahakama akamwapisha Akida, “Wa-Ilahi n’tasema kweli, kweli tupu.” Karani wa mahakama akakaa, uwanja sasa wa Akida.

Musadiq alimtazama Akida kwa macho ya utulivu kabisa akamwuliza:

“Umeyasikia maelezo ya upande wa mashtaka?” “Nimeyasikia,” alijibu.

“Umeyasikia vizuri maelezo yaliyotolewa na mashahidi wa upande mashtaka?”

“Nimeyasikia vizuri,” alijibu Akida.

“Umeyasikia maelezo yako mwenyewe na yale ya washtakiwa wenzako kama yalivyosomwa hapa mahakamani?”

“Nimeyasikia.”

“Sasa mahakama hii inakuruhusu ujitetee, utoe maelezo yako bila woga au wasiwasi, na baada ya hapo mwendesha mashtaka atakuhoji.”... (uk. 247).

Baada ya Akida kumaliza utetezi wake, Chopra akanyanyuka ghafula kutoka pale alipokuwa amekaa... Aligeuka tena kumtazama Akida, akamwuliza, “Hebu ieleze mahakama hii, siku ya mauaji, pale mauaji yalipotokea ulikuwa wapi?”

“Nilikuwa baharini.”

“Baharini ulikwenda kufanya nini?”

“Kuvua.”

“Mwongo! Hukwenda kuvua!” Chopra alipiga kelele, anamtazama kwa macho makali kahamaki, “Ulikwenda baharini kuwasubiri wenzako kutoka Dar es Salaam.

“Sikuwa na mwenzangu yeyote kutoka Dar es Salaam siku hiyo.”

“Hukuwa na mwenzako kutoka Dar es Salaam siku hiyo?” aliuliza Chopra ametia mkono ndani ya mfuko wa suruali yake huku akimtazama Akida kwa dharau. “Si umeyasikia maelezo ya Mkadam akieleza kwamba wenzetu walikuwa wafike kwa mashua kutoka Dar es Salaam?”

“Hao labda ni wenzake yeye Mkadam si wenzangu mimi.”

“Wewe unasema hao si wenzako na gari yako ilionekana siku ya mauaji, kwenye tukio la mauaji!” “Iliyoonekana ni gari yangu siyo mimi.”

“Gari yako ilifikaje hapo?”

“Sijui.”

“Hujui vipi? Gari yako kwani alikuwa nayo nani siku hiyo?”

“Mara nyingi gari yangu anakuwa nayo dereva.”

“Kwa hivyo wewe ndiye uliyemtuma dereva kwenda kuwachukua hao wenzenu kutoka Dar es Salaam halafu awapeleke hapo mauaji yalipofanyika?”

“Nakwambia mimi sikuwa na mwenzangu kutoka Dar es Salaam au hunielewi Bwana Chopra?” Akida aliuliza kwa sauti ya utaratibu. Chopra alimtazama Akida akamkazia macho, akamwuliza, “Wewe koministi?” “Mimi si koministi.”

“Wewe ni koministi, mimi n’najua, na nyinyi makoministi hamna dini wala hamwamini Mungu.”

“Si umeniona nikishika msahafu nilipoapa? Sasa itakuwaje niwe sina dini wala siamini Mungu?”... (uk. 248-249).

Baada ya wale mashahidi walioandaliwa na maafisa wa gereza kutoa ushahidi wao na kuwataja mahaini walioambiwa kuwa wawataje, zamu ya washtakiwa inafika na wanapewa fursa ya kujitetea. Mmoja wao ni huyu Akida ambaye anatajwa na Mkadam katika ushahidi wake na maelezo kutolewa ya jinsi alivyoshiriki katika

mpango wa kumwua Kigogo. Akida, kama wengine waliotajwa, anakanusha madai haya. Suala la ukoministi linaibuka tena, mbali na suala na Ukomredi pale Hamza na Doto wanapozungumza, (uk. 71-72). Makundi haya mawili yanasingiziwa kuwa wafuasi wake hawamwamini Mungu na kwamba ndio walimwua Kigogo.

Majibizano haya vilevile yanadhihirisha uozo katika mfumo wa uongozi wa magereza, kwani Chopra mwenyewe anajua kuwa ushahidi uliotolewa dhidi ya Akida na wenzake hauna ukweli, na kwamba huo sio ushahidi wa Mkadam bali wa wakuuwa magereza (ambao labda kwa kweli walimwua Kigogo). Mkadam vilevile ametoa ushahidi huo baada ya mateso na vitisho vingi.

Mfano 3.13

Chopra akambana Hamza kwa maswali mara amtie huku mara amtoe kule, amzungushe hivi amzungushe vile, ambabaishe hivi ambabaishe vile, mara amletee kizungumkuti kile. Lakini Hamza alikuwa makini.

“Wewe unamjua Hamduni?” Chopra alimwuliza Hamza.

“Namjua.”

“Unamjua vipi?”

“Namjua kama n’navyokujua wewe.”

“Mimi unanijua vipi?”

“Wewe nakujua kama Bwana Chopra mwanasheria.”

“Na Hamduni unamjua vipi?”

“Namjua kama Hamduni mwanajeshi.”

“Mwongo! Unamjua zaidi ya hivyo! Yeye ni rafiki yako mkubwa na kila mtu anajua hilo,” alipiga kelele Chopra.

“Bwana Chopra nimeapa kwa kushika Msahafu kwamba nitasema kweli. Sikukataa kama namjua Hamduni wala sikukataa kama yeye ni rafiki yangu.”

“Wewe unauheshimu Msahafu?”

“Sana.”

“Unauheshimu Msahafu na wewe kila siku nakukuta Starehe Club unalewa.”

“Kwani wewe Bwana Chopra unapokuja Starehe Club huwa unakuja kusali?” (uk. 256).

Hamza, kama tulivyoeleza hapo awali ni mhusika mkuu, na vilevile mtendaji mkuu katika kesi ya uhaini. Alikuwa rafiki wa karibu wa Hamduni, mshukiwa mkuu wa mauaji ya Kigogo, hivyo siku aliyopandishwa kizimbani ilingojewa na wengi, wakiwemo Khadija na familia yake na wengineo waliokuwa na hamu ya kusigiza kesi ya uhaini. Majibizano haya kati ya Hamza na Chopra hivyo yalikuwa muhimu katika kufikia maamuzi ya kesi hii; ama kumwachilia huru Hamza au kumhukumu. Hamza alikuwa amejiandaa kukabiliana na maswali ya Chopra, na baadaye anaachiliwa huru, (uk. 264).

Bacon (1984), akieleza Nadharia ya Utendaji anadai kwamba utendaji hutekelezwa na watendaji kwa kuigiza matendo yao kupitia mazungumzo na ishara mbele ya hadhira. Mazungumzo hivyo ni nguzo kuu ya utendaji kwani haya ndiyo huwezesha utendaji husika kutekelezeka. Katika riwaya ya *Haini* kama tulivyoona, wahusika wamepeva kauli, na kupitia kauli hizo wanasemazana moja kwa moja, wanaambatanisha kusemezana huku na ishara na hivyo kufanikisha utendaji katika matukio wanamotenda.

Hali tunayoipata katika riwaya hii ni tofauti na ile ambayo tungepata katika muktadha ambapo msimulizi angeamua kusimulia kisa chenyewe kwa lugha ya nathari kutoka mwanzo hadi mwisho. Lugha ya majibizano iliyotumika kwa wingi katika riwaya hii ni kigezo mojawapo kinachoashiria kuigizika kwa riwaya hii ikiandikiwa mchezo wa kuigiza na kuwekwa kwenye jukwaa. Sasa tutazame kipengele cha wahusika, ambao ndio watendaji na wanaotumia lugha ya majibizano katika utendaji wao.

3.2 Wahusika

Wahusika ni kipengele muhimu katika kazi yoyote ile ya fasihi. Yapo maoni ya wataalam mbalimbali kuhusu wahusika wa kazi za fasihi. Kwa mfano, Foster (1927)

anawaita wahusika ‘watu,’ pamoja na kudai kwamba wahusika ndio watendaji wanaotumiwa na mwandishi kuwasilisha hadithi yake.

Tunaona kwamba wahusika ni vitu, viumbe au watu wanaoteuliwa na mwandishi wa riwaya ili kuiwasilisha hadithi yake kikamilifu. Wahusika hupata sifa zao kutegemea namna mwandishi anavyowaumba pamoja na majukumu wanayotekeleza katika riwaya husika. Hivyo, kunakuwa na aina nyingi za wahusika katika riwaya, na hutegemea wahakiki wa fasihi kutambua aina hizo za wahusika katika riwaya mahsusi.

Wamitila (2003) anafafanua wahusika kama sehemu muhimu sana ya fani ya kazi ya fasihi. Anawaeleza kuwa wahusika ni viumbe au watendaji wanaopatikana katika kazi ya kifasihi. Viumbe hawa ni kama (nguzo) mwega mkuu wa dhamira na maudhui. Kwa nini? Kwa sababu kila tendo lazima liwe na wa kulitenda. Wahusika wanafanana kwa kiasi kikubwa na binadamu katika maisha ya kawaida lakini sio lazima wadhibitiwe na kanuni zote za binadamu halisi...wahusika kuiwakilisha hali halisi ya maisha ya binadamu katika jamii fulani.

Kufikia hapa, tunaona kwamba Foster (1927) na Wamitila (2003) wanahusisha wahusika wa kazi za fasihi na utendaji. Wanashikilia kwamba, matendo yanayosimuliwa na msimulizi hutekelezwa na wahusika anaowateua kupitia utendaji.

Madai ya wataalam hawa yanawiana na kile wananadharia ya Utendaji wanachodai kuhusu watendaji wa kazi za kidrama. Bacon (1984) kwa mfano, anadai kwamba katika uigizaji, mwigizaji, ambaye ni mtu halisi huwakilisha mhusika aliye katika matini. Vilevile, waigizaji huteuliwa kuwaigiza wahusika ambao wataweza kutekeleza matendo yao, na vilevile sifa zao kuwiana kwa kiwango kikubwa. Ikiwa

riwaya ya *Haini* itafanyiwa ufaraguzi na kuigizwa kwenye jukwaa, mwelekezi wa mchezo husika anafaa kuwateua watu halisi ili wachukue nafasi za wahusika kama Hamza na kuzitenda kwenye jukwaa. Watu hawa wanastahili, kwa mujibu wa madai haya ya Bacon, kuwa na sifa zinazowiana na za mhusika wanayemwakilisha kwenye jukwaa, na vivyo hivyo, waweze kutenda kama anavyotenda mhusika fulani kwa kiwango kikubwa.

Katika utafiti huu, tumeainisha wahusika wa riwaya ya *Haini* katika makundi kadhaa kutegemea utendaji wao, kuwajadili na hatimaye kutathmini utendaji wao kama unavyobainika katika riwaya yenyewe. Makundi hayo ni pamoja na: mahaini, mashahidi, wakubwa wa magereza, washikadau mahakamani na waathiriwa wa uhaini.

3.2.1 Mahaini

Mahaini ni wahusika ambao wanakamatwa punde baada ya kuuawa kwa Kigogo. Wanapelekwa gereza la Kinoamiguu, almaarufu Kumbakumba. Wapo wasiojua sababu za kukamatwa kwao, lakini baada ya kupatana kule Kumbakumba wanapashana habari na ndipo wanajua kwamba wao ndio washukiwa wakuu wa mauaji ya Kigogo; wao ndio mahaini. Kwa jumla, mahaini hawa ni pamoja na Hamza, Abdul, Shadidi, Sururu, Shekhe Mandundu, Masanja, Sugu, Kondo, Fimbo, Mzee Subet, Bilali na Nassor, Faraji na Doto.

Kwa mujibu wa msimulizi, mahaini hawakuwa watu wa kuhurumiwa bali watu waliwadharau na kuwaona kama najisi. Ikawa haramu kusema nao na kucheka nao, na huruma kwao ilikuwa kujitafutia balaa, (uk. 92).

Wananchi walikuwa wamesigiza uvumi na propaganda nyingi kuwahusu mahaini hawa, hivi kwamba walikuwa na mtazamo hasi dhidi yao. Baada ya kesi ya uhaini kuanza msimulizi anaeleza kwamba:

Masikio ya watu wote ndani ya nchi yalikuwa wazi yakisikiliza kesi ya uhaini. Muda mrefu umepita watu wakizua na kudhani. Hakuna aliyewaonea huruma isipokuwa wale waliowahusu na walio karibu nao. Wengi walikwisha tabiri hukumu ya kifo kwa wote wale wala hakukuwa na tegemeo la yeyote katika wale kunusurika na adhabu hiyo. Chuki dhidi yao ilijazwa ndani ya nyoyo za watu ikajaa tele ikawa ishara yoyote ya kuwaonea huruma ni usaliti mkubwa...(uk. 230).

Kwa jumla, hii ndiyo hali iliyowakabili mahaini. Miongoni mwa wahaini kumi na wanne tuliowataja, tumejadili wale wakuu ambao ni Hamza, Sururu, Doto, Shekhe Mandundu na Faraji. Mahaini hawa, ndio wanaowasilisha maudhui mengi katika riwaya ya *Haini*, na kutokana na utendaji wao wanaathiri msuko wa masimulizi kwa kiwango kikubwa. Matukio mengi yanayowahusu mahaini yamewazunguka na hivyo kuwapa umuhimu mkubwa wakilinganishwa na wenzao. Tuwatazame watano hawa.

1. Hamza

Hamza ni mhusika mkuu miongoni mwa mahaini wote tuliowataja. Ndiye mhusika wa kwanza tunayepatana naye katika (uk. 1), akiwa kwake na marafiki zake wakati Kigogo anauawa bila wao kujua yanayoendelea kule nje. Wanakimbilia usalama wao na Hamza anaenda Kisimamajongoo kwa wakwe zake aliko mkewe Khadija. Huku ndiko anakokamatwa kama inavyotukia katika (uk. 7-8):

Hamza aliongoza mbele, mikono juu, akahisi sasa kweli shari imemkabili. Hakujua Hamduni amezua balaa gani. Kikosi kizima cha wale askari kimemfuata nyuma na bunduki zao wamezikamata imara mikononi... Hamza aliingia ndani ya gari, akawekwa katikati, mikono juu. Askari wote wamemzunguka bunduki mkononi kila mmoja, zote zimemwelekea yeye. Gari likapigwa moto, likanza safari...akiwa amejaa tele katika mawazo ya Hamduni, gari limeshafika Darajani linaelekea Malindi. Kufumba na kufumbua,

wakajikuta wameshafika kituo cha polisi cha Malindi, “Haya shuka!” aliamrisha. Akashuka, akasindikizwa mpaka ndani ambako alikaribishwa kwa kofi kubwa alilopigwa na mkuu wa kituo...”Mtieni ndani!” mkuu wa kituo naye akaamrisha...(uk. 8).

Baada ya kutiwa ndani katika kituo cha polisi cha Malindi, Hamza anapelekwa katika gereza la Kinoamiguu ambako anafahamishwa na Abdul, ambaye pia ametiwa ndani kwamba Kigogo kauawa na Hamduni, na kwamba wao ndio washukiwa wakuu, yaani mahaini, (uk. 13). Hapa ndipo Hamza anapobaini sababu za kutafutwa kwa Hamduni.

Ni wakati huu akiwa Kumbakumba ndipo anakumbana na mateso ya kule gerezani. Kama mume na baba, Hamza anakuwa na mawazo kuhusu familia yake; mke na mwanawe, (uk.30). Anatolewa Kinoamiguu na kupelekwa Ziwani; gereza kuu nchini ambalo wafungwa katika riwaya hii wanaliita Kwa Ba Mkwe. Anahojiwa kuhusu rafiki yake Hamduni na uhusiano wao ulivyokuwa, pamoja na kila kitu akijuacho kuhusu mauaji ya Kigogo, (uk. 37-39). Hamza anakataa kwamba alihusika katika mauaji ya Kigogo, ingawa askari wale wanadai kwamba na yeye katajwa, (uk. 40). Hamza anashikilia msimamo wake kwamba hakuhusika kwa namna yoyote ile na hapo anapata kichapo ambacho nusura kimtoe uhai, (uk. 40-41).

Siku yake ya kwanza kwa Ba Mkwe inakuwa yenye mateso na udhalimu, (uk. 42). Baada ya kichapo hiki, Hamza anawekwa chumba kimoja na maiti ya Kidau, rafiki yake wa siku nyingi ambaye ameuawa kule kwa Ba Mkwe, iwe funzo kwake kuwa huenda yaliyompata Kidau yakampata ikiwa hatashirikiana na wale askari waliokuwa wakimhoji. Hamza, mwili unamuuma, ana vidonda kutokana na kuchapwa, na akili nayo inakuwa kama ya mwendawazimu, (uk. 43).

Katika (uk. 64-65), Hamza anatolewa chumbani alikofungwa pamoja na Doto na kupelekwa sehemu asiyoijua. Huko, mateso yanaanza, anapigwa mpaka pumzi

zikampaa, akatiwa kizibo mdomoni asiweze kusema, akazongwa kamba mwili mzima na kutupwa kisimani anakoning'inia, huku anatupiwa risasi afe au apone. Akasalimu amri na kukubali kusema askari wale walichomtaka akiseme, akanusurika, (uk. 66). Tukio hili kwa mtazamo wetu halionyeshi kwamba Hamza alikuwa hana uwezo wa kuvumilia bali mateso ndiyo yalipita mipaka, akafanya kile ambacho mtu yeyote katika hali hii atafanya katika hali halisi.

Askari wa kwa Ba Mkwe wanazidi kumshawishi Hamza, ambaye bado anashikila msimamo wake kwamba hakuhusika kwa namna yoyote ile katika mpango wa kupindua serikali uliopelekea kuuawa kwa Kigogo. Wanabuni mbinu nyingine na mara hii, wanakubaliana na Hamza kwamba wao pia wanafahamu kuwa hakuhusika katika tukio hilo la uhaini. Hata hivyo, wanamtaka awe shahidi katika kesi ya uhaini, na awataje wengine 'waliohusika,' tazama:

“Sisi tumekwita hapa kukuomba utusaidie. Utusaidie na sisi tutakusaidia, iwe nipe nikupe. Unasemaje?” aliuliza Kanali Mapepe. Hamza alishangazwa na kauli ile. Kauli ya kuombwa msaada na watu waliomtia mikononi wakamdhiti sawasawa, “Msaada gani?” aliuliza. Sisi tunajua kwamba wewe huhusiki lakini ombi letu ni kukutaka ukubali. Ujidai kama vile umu na unawajua wengine. Tuna orodha ya majina hapa tutakupa, na wote hao tumeshawatungia hadithi kuthitisha vipi wanahusika,” alieleza Kanali Mapepe kwa sauti ya upole iliyojaa busara tele... Walidhani Hamza angelikubali tu, lakini walipomwona si wa kunyera walikaa juu, “Sikiliza wewe!” aliyarukia maneno Kanali Bunju. Mkali kama moto. “Sasa utakubali hukubali?” “Potelea mbali!” Hamza alipiga moyo konde akaamua, “Mimisiwezi kukubali mtego huo,” alisema Hamza...”Mpelekeni chumba za kiza!” aliamrisha Kanali Bunju. (uk. 81-83).

Hamza, hata baada ya kushawishiwa kwa kila hali na Kanali Bunju na kikosi chake kwamba ashirikiane nao, anakaidi na kushikilia kwamba yeye hawezi kukiri kwamba kashiriki mambo ambayo yeye mwenyewe hayaelewi. Hii inampelekea kuwekwa

kwenye chumba cha kiza ambacho kipo gereza la Kinoamiguu. Huku, anateseka kwa joto jingi, njaa na hatimaye anakuwa mgonjwa. Msimulizi anaeleza kwamba:

[Hamza] Alikaa, akasimama, akachutama. Kila alivyofanya aliona sivyo. Akiegemea, kuta zinaunguza. Akikaa, sakafu inaunguza. Vile alivyosimama, nyayo nazo zinaungua. Afanye nini? Yumo katika nakama. Jahanamu ya hapa hapa duniani...usiku ule aliupitisha kwa mashaka makubwa, kucha akisononeka kwa joto, njaa na mbu...(uk. 86).

Baada ya kupelekwa chumba cha kiza, anapatwa na njaa kali kwa kuwekwa kwa muda mrefu bila chakula chochote. Baadaye Koplo Usi na kikosi chake wanapoleta chakula, wanamtilia Hamza sahani nusu, hali inayozidi kumweka katika hali ya njaa. Habari zinapoenea kule Kumbakumba kwamba Hamza yupo chumba cha kiza, Hamadi Matope, mmoja wao, anamwauni:

“Hamza!” alitwa tena. “Chukua huo mpira nyonya! Nyonya kwa nguvu! Fanya haraka!” Hamza alijiburura mpaka akafika pale chini ya dirisha akachukua ule mpira akaupachika mdomoni. Alidhani yatakuwa maji na alikwisha shukuru kwani kiu kali ilikuwa imemshika. Alivuta kwa nguvu mpaka alipoweza kunyonya. Alinyonya rojo ya maharagwe iliyochanganywa na wali. Kama uji. Tena ilikolea chumvi na pilipili. Alizidi kunyonya na kila aliponyonya rojo na wali ulitiririka...akanyonya, akala mpaka akashiba. Mwisho akaletewa maji, akanyonya mpaka kiu yake ikakatika, mpira ukavutwa nje...(uk. 88).

Katika tukio hili, Hamza analetewa chakula kwa mpira na Hamadi Matope, mmoja wa wafungwa. Inatarajiwa kwamba baada ya kukaa kwa njaa kwa siku nyingi, Hamza angetenda kama alivyotenda, kunyonya ule mpira kwa nguvu na pupa hadi ashibe, kuunyonya tena akinywa maji na kupumzika tu pale ambapo amekata kiu yake. Huu ndio uhalisia, na mtu akajipata katika hali kama hii katika maisha halisi angefanya namna Hamza alivyofanya. Hamza anakuwa mhusika wa kuaminika, na ambaye matendo yake yanaweza kuigizika kwenye jukwaa.

Akiwa katika chumba cha kiza anakopelekwa kuteswa na kufanywa asalimu amri, anavamiwa na ugonjwa na hali yake ni mbaya:

[Koplo Usi] Alipofungua mlango kwa vishindo kama kawaida yake, Hamza alikuwa amelala. Amelalia ubavu wake wa kulia, kichwa amekilaza juu ya kiganja cha mkono. Amejikunyata kama anayeona baridi. (tukumbuke kuwa chumba cha kiza kama tulivyoeleza hapo juu kilikuwa na joto kupita kiasi. Hivyo kujikunyata kwa Hamza kama ambaye anaona baridi ni dhahirisho kwamba kweli anaugua), Gamba jeusi la taka limemwota tokea usoni mpaka tumboni, mweusi kama mwuza makaa. Tongo zimemjaa machoni na alipoyafumbua macho yake kumwangukia Koplo Usi, alimwona kama aliyesimama nyuma ya chandarua. Alimwona kwa mbali, kama anayeyeyuka ndani ya ukungu wa alfajiri, “ A-aaa-amka!” Koplo Usi alimpigia kelele. “Naumwa Koplo,” Hamza alilalamika kwa unyonge. (uk. 91).

Mateso anayokumbana nayo Hamza ni mengi, na yanaishia kubadilisha hali yake ya mwili. Amebadilika, hayupo alivyokuwa siku alipokamatwa. Hamza, licha ya mateso hayo yote, bado hajasalimu amri. Anateseka, kumia, kuugua lakini bado ameshikilia kwamba yeye hakuhusika na mauaji ya Kigogo. Amewekwa katika hali ngumu ya maisha, hali ambayo msimulizi anaeleza kama ‘mtafaruku uliomzongazonga [Hamza] ukamweka katika hali ya kusalimu amri.’ Ameamua kusimamia ukweli, liwe liwalo.

Kama mtendaji mkuu katika kikundi cha mahaini, tunamwona Hamza akikabiliana na mateso ya kukatisha tamaa na kupambana na hali ngumu ya maisha ya gerezani. Anakuja kuyazoea maisha hayo, na ingawa wakati mwingine anaishiwa na matumaini ya kuwahi kutoka (kama ambavyo mahaini wengine wanaishiwa) anashikilia tu kwamba hata asipotoka yeye, itatoka maiti yake, (uk. 59). Amejitafutia njia za kujiliwaza, kuyaondoa mawazo yake kule gerezani na hata zaidi, kumfurahisha. Yapo baadhi ya matukio ambayo Hamza anaelezwa kwamba amefurahi, hali ambayo haitarajiwi kwa mtu kama Hamza.

Hamza ni mhusika ambaye ameshikilia msimamo wake kwamba yeye hakuhusika katika mauaji ya Kigogo. Msimamo wake huu umemsababishia taabu na mateso kule gerezani. Yapo matukio ambapo Hamza anateswa, anaumwa, anapata njaa, anakata tamaa, anaota na wakati mwingine kuwa kama mwendawazimu mambo yanapomzidi. Uhusika wake ni wa kihalisia, unaaminika na unaweza kuigizika kwenye jukwaa. Schechner (1988) kwa mfano anadai kwamba mtu anapoishi tendo fulani kwenye jukwaa mbele ya hadhira huwa anatenda, kwa kuwa hujiinkiza katika utendaji wa mhusika anayetenda. Bacon (1984) naye anadai kwamba waigizaji huteuliwa kuwaigiza wahusika ambao wataweza kutekeleza matendo yao, na vilevile sifa zao kuwiana kwa kiwango kikubwa. Kutokana na madai haya, tunaweza kusema kwamba inawezekana kumteua mtu halisi akatenda uhusika wa Hamza, na kwamba uhusika huu utatendeka kwenye jukwaa.

Msimulizi amemweka Hamza sio tu katika matukio na utendaji wa kutamausha bali pia katika matukio ya kupumzisha kutokana na madhila anayokumbana nayo. Kwa mfano, Hamza akiwa katika chumba chao na Doto, anatafuta namna ya kupata vifaa vya kuchezea wakiwa pale chumbani, shughuli inayoweka wazi zaidi utendaji wake.

Wanacheza dhumna na hata chess kutokana na ubunifu wa Hamza. Tazama:

Asubuhi Hamza alikuwa mashughuli akibaka mbu...alihangaika chumba kizima kuwafukuza pale waliporuka huku na kule, akiwatafuta wale walioshiba vizuri..Hamza alikuwa akihangaika, kufukuza mbu, akiwabaka mmoja mmoja. Aliwakusanya chungu nzima, akawapanga kitita kama fungu la dagaa. Alichota gao zima la maji kutoka katika ile ndoo ndogo ya sandarusi iliyokuwepo katika pembe ya chumba akawamwagia, akafanya kama aliyetaka kuwakaanga. Aliwatumbua tumbua akaikusanya damu yao, akafanya kidimbwi kidogo cha damu hiyo...alikusanya damu ya kutosha ya kuviremba vile vipande vya lile bango alivyovikata. Kalamu yake ilikuwa ujiti wa njukuti alioukata kutoka katika ufagio wa mle chumbani. Aliuchovya ule ujiti ndani ya kile kidimbwi cha damu kama vile anavyochovya mtu kalamu ndani ya kidawa cha wino. Alikuwa akiviremba vile vikaratasi kwa vidoto vidogo vidogo,

ameshughulika na kibarua kile. Aliinua macho yake akamtazama Doto akamuuliza, “Unajua kucheza dhumna wewe?” (uk. 60-61)

[Hamza] alimfuata Doto pale alipokuwa amekaa. Amekichukua kile kifurushi cha vile vikaratasi. Vimeshakauka... “Hizi nd’o dhumna zetu,” alimwambia. “Angalia hivi vidoto,” alimfahamisha...(uk. 62).

Katika mfano huu, tunamwona Hamza katika muktadha tofauti na matukio ya dhiki ambayo tumemzoea akiwemo. Hapa, anashughulika kuhakikisha kwamba wamepata vifaa vya kucheza, ili wapunguze hofu na wajenge imani kwamba ipo siku watatoka jela.

Hatimaye, baada ya kukumbana na dhuluma za gerezani, kesi ya uhaini inaanza. Kama wahusika wengine wanavyojitetea, Hamza anapewa fursa ya kujitetea (uk. 254256), jambo ambalo anafanya kwa ukakamavu na usahihi kutokana na kuwa makini wakati ushahidi ukitolewa.

...Hamza naye aliapa kama atasema kweli, kweli tupu na hakuna kingine chochote isipokuwa ukweli mtupu...Hamza anaangaza kila pembe kuwatazama wale walioijaza mahakama ile. Akawaangalia mahakimu. anaonekana amechoka hali yake amedhoofu, kichwa kimekuwa kidogo baada ya nywele zake zote kukatwa. “Waheshimiwa mahakimu,” Hamza alianza kutoa maelezo yake kwa sauti ya upole...(uk. 253-254).

Hamza akaacha kumtazama Chopra akaelekeza macho yake mbele kuwaangalia mahakimu na akamaliza maelezo yake kwa kuwaomba mahakimu wale wahukumu kwa kufuata haki na siyo chuki na sumu iliyomwagwa kila mahali dhidi ya washtakiwa...(uk. 255).

Katika mifano hii, Hamza anapopewa fursa ya kujitetea anafanya hivyo bila woga, amekuwa makini wakati wa ushahidi na anajua yepi yalisemwa kumhusu na yepi aseme katika maelezo yake. Anafanya haya kwa ujasiri, utulivu na akiwa makini, na katika (uk. 264), anaachiliwa huru, jambo linalozua mtafaruku, tukizingatia uhusiano wake na Hamduni.

Akaelekea nyumbani kwake katika (uk. 267). Mhusika Hamza anakuwa kielelezo cha mvumilivu hula mbivu. Amevumilia mateso, na hatimaye anaachiliwa huru, tofauti na waliotaka maisha ‘mazuri’ pale gerezani, wakajitia kuwaponza wenzao nao wakaishia kuhukumiwa kifo. (uk. 265).

Hamza anawakilisha watu katika ulimwengu halisi ambao hujipata mashakani kutokana na watu wanaohusiana nao. Amesimamia ukweli aujuao, akateswa na kudhalilishwa lakini hatimaye kuachiliwa huru. Kama tulivyoeleza hapo awali, Hamza ni mhusika ambaye kutokana na sifa alizopewa, namna alivyojengwa kisaikolojia na kimaumbile, tajriba za maisha yake na maarifa ya maisha, anakuwa wa kuaminika na ambaye uhusika wake unaweza kutendeka kikamilifu kwenye jukwaa mbele ya hadhira. Haya ni baadhi ya mambo ambayo yanayosisitizwa na Nadharia ya Utendaji.

2. Sururu

Msimulizi anatueleza kwamba Sururu alikuwa kuli ambaye alitetea haki za wafanyakazi katika vyama vya makuli. Alikuwa na umri wa takriban miaka hamsini, mwenye kipara na mvi kwenye sehemu za kichwa zenye nywele. Alikuwa na pengo la meno matatu yaliyong’oka katika harakati za kuteswa na kupigwa kule kwa Ba Mkwe, (uk. 20).

Anapolewa chumbani walimo akina Hamza, analetwa kwa kishindo baada ya kichapo kikubwa nje ya Kumbakumba. Masaibu yake yanaanza mara tu anapokamatwa, na hapa alipo hata meno yashang’oka. Msimulizi anatueleza kwamba baada ya kutupwa mle chumbani anaanguka chali katikati ya chumba, uso ukiwa umechanika huku nguo zake zimeloa damu. Amepigwa kwa mipera iliyochanachana

mwili wake, na pale Abdul na wenzake wanapomhudumia analalama kwa uchungu, (uk. 21).

Sururu, kama mifano ifuatayo inavyodhihirisha ni mhusika ambaye anaafikiana na maelezo ya Nadharia ya Utendaji kuhusu wahusika kwamba katika utendaji, wajumuishe lugha ya majibizano na ishara. Yeye amepewa uwezo wa kueleza hisia zake na kuzionyesha wazi wazi huku akiziambatanisha na matendo. Sururu anajipata katika mateso mengi humu gerezani, na hivyo uhusika wake ni wa dhiki na majonzi. Kwa mfano, mahaini wote wanatolewa nje ya vyumba vyao kule Kumbakumba katika mchakato wa kuwaachilia huru wale ambao hawahusiki na keshi ya uhaini. Askari wa kwa Ba Mkwe walipoingia, yule aliyemkaribia Sururu masimulizi yanatuarifu kwamba:

Sururu alimwangalia kwa hasira, uso ameukunja, amekaa kama mbwa mwitu kwa vile sharafa ya ndevu nyeupe ilivyouzunguka uso wake na mvi zilivyomjaa kichwani mwake zikabakisha kile kipara tu kikimetameta utosini...(uk. 101).

Katika mfano huu, Sururu anashirikisha ishara za uso katika utendaji wake. Anatenda kwa namna inayodhihirisha hisia zake za ndani, hivi kwamba msomaji anafahamu ikiwa amekasirika au la.

Sururu anapopata habari kwamba wafungwa watatu sugu wametoroka jela, (uk. 111-112), anapata kiu ya kutaka kutoroka. Anaanza kupanga mpango wa 'Kata Mbuga,' (uk. 114) na baada ya kutagusana na Polo (mfungwa sugu ambaye amekwishatoroka jela mara kadha akikamatwa), Sururu ari ya kutoroka inamzidi. Hatimaye, mahaini wanapotolewa nje kusherehekea siku kuu ya mwezi wa Ramadhan, anautekeleza mpango huu (uk. 119). Msimulizi ameweka wazi namna alivyotekeleza kutoroka

huku, kwa namna inayotufanya tumwone mhusika Sururu katika utendaji wa kutoroka kutoka mwanzo hadi anapofanikiwa kutoka nje ya gereza:

...Alikwenda mpaka ilipo ngazi, akaishika na kuitikisatikisa ili kujaribu umadhubuti wake. Ilikuwa madhubuti, ina uwezo wa kuhimili uzito wake bila ya wasiwasi wowote. Aliiparamia mpaka akafika juu kabisa pale alipopambana na waya wa senyenge uliotanda mbele yake, umechanua miba yake tayari kumraruararu... Aliukamata waya wa senyenge akajaribu kuuparamia na kila alipousukuma huku na kutaka kuukiuka afike upande wa pili wa ule waya ncha zake zilimchoma na kumtoboatoboa, mikono na miguu. Alinyanyua mguu kutaka kuukiuka, ncha moja ikamchana paja, ncha nyingine ikamchana mkono pale alipojaribu kuuparamia. Aliuparamia hivyo hivyo, akaulalia juu yake, ncha nyingine ya waya ikamraru tumboni kama aliyekakwa na kisu kikali, damu chururu, mikononi, miguuni na tumboni. Alipokuwa anauburusha ili apindukie upande wa pili, waya wote ulilala na alipogeuka upande wa pili, waya wote ulilala upande mmoja. Koplo Ngwali aliuona vile ulivyokuwa ukitikisikatikisika na alipogeuka kuangalia kule kwenye mtikisiko akamwona Sururu, keshauparamia waya tayari kuruka nje ya ukuta, "Weee!" alipiga kelele. Alimfyatulia risasi ikapita "zzuuuum!" Juu ya kichwa chake. Sururu akajiachia, akaanguka chini kwa kishindo kikubwa. Ameshafika nje ya gereza. Damu zinamchirizika, mguu umeteguka, mauti yamemkabili, Koplo Ngwali anazifyatua risasi kama mwendawazimu. Sururu alipotea vichakani kama paa, hakujali damu wala mguu kuteguka, mpango wa Kata Mbuga umeanza...(uk. 121-122).

Anahangaika msituni anakokimbilia kutafuta msaada kutokana na maumivu aliyoyapata wakati akitoroka, shughuli ambayo inazidi kuweka wazi utendaji wake.

Tunasimuliwa kwamba:

...alijiburura hivyo hivyo, akapenya vichakani kuufuata ule mwanga, lakini kila alipoufuata aliuona kama unamkimbia, uko kulee, hafiki asilani...Sururu alitaka kumziba mdomo. Kabla hakuwahi kufanya hivyo yule mwanamke aliufunga mlangokwa nguvu Sururu akakimbia upesi kabla halijamzuka balaa jingine...alikurupuka kama nguruwe anayefukuzwa na msasi, akaingia vichakani asijue aendako ndani ya usiku ule wa kiza uliojaa nuksi na mikosi...(uk. 124-125).

Sururu anakamatwa kesho yake, (uk. 124, 125). Anapelekwa kwa Ba Mkwewe ambako anashawishiwa kwamba aungane na mashahidi wa upande wa mashtaka, na akifanya

hivyo akina Meja Mapanga watamwachilia huru. Katika kile kikao cha kushawishi, tunasimuliwa kwamba:

Sururu alinyamaza kimya. Hana la kujibu, akaona leo ndiyo leo. Ya huku anayajua vyema, huanza hivi hivi, taratibu, kwa viswali vidogo vidogo yakamalizwa kwa kipigo kikubwa. “ Bwana Sururu, “ Meja Mapanga alimwita. [Sururu] ameshtuka, tokea siku aliyokamatwa hakuwahi kuitwa bwana...Meja Mapanga akatoa jalada akamrushia Srururu. “Ninaruhusiwa kusoma?” Sururu alilivuta lile jalada akalifungua...Sururu aliliinamia lile jalada akasoma neno moja moja, wote wamekaa wanamtazama. “Sikiliza wewe! Sisi hatupo laibrari hapa, tukusubiri wewe usome mpaka umalize! Utatia saini au hutii saini?! Sururu alimtazama, uso umembadilika, jasho linamtoka kaliinamia jalada. Yaliyoandikwa mle yamemshitua. Yanamtokomezwa kabisa, “Sitii!” alijibu Sururu, amechachamaa...(uk. 133).

Katika mfano huu, tunaona namna Sururu anatenda katika tukio lote hili la kushawishiwa kwake. Kutokana na hali ya hofu iliyomzingira chumbani mle, amejikalia kimya akiwaza ni balaa gani zimezuka. Anapopewa jalada lenye maelezo ya ushahidi anaotakiwa kutoa, tunamwona anavyolisoma kwa makini, na japo anafahamu hatari inayomkabili, anakuwa mkakamavu na kukataa kutia saini kwenye jalada hilo. hata baada ya kichapo anachopata na mateso yanayomkabili baada ya kukataa kushirikiana na upande wa mashataka, bado Sururu hakati tamaa ya kutoroka, anaiona kama njia ya pekee ya kuyaondokea mateso ya pale gerezani, (uk. 197-198).

Sururu anatumiwa kuonyesha mateso anuwai wanayoyapitia wafungwa, na zaidi wale wanaojaribu kutoroka wakashindwa au wakapatikana baadaye; hakuna mateso hajaonja, si Kumbakumba si kwa Ba Mkwe, na ni haya mateso yanayomkosesha tumaini la kutoka huko, hadi anahiari kutoroka.

Wakati wa kesi ya uhaini, Sururu anahusika kwa kiasi kikubwa kwa kuwa anatenda hata akiwa pale walipoketi, tofauti na baadhi ya mahaini. Kwa mfano, Chopra

anapodai kwamba mahaini hao ‘walifinywafinywa’ Sururu anasimama alipo, analivua shati lake na kuwaelekezea mahakimu mgongo wake wayaone makovu na michaniko ilivyotamba mgongoni mwake na kuwauliza ikiwa huko kweli ni kufinywa, (uk. 261). Kesi hii inapokamilika, hukumu inatolewa kwa kila mmoja wao na Sururu ni mmoja wa wale waliohukumiwa kifungo cha miaka kumi na mitano. Kila mmoja wao aliipokea hukumu yake kivyake. Kuhusu Sururu, msimulizi anataeleza:

Sururu aliposikia jina lake limetajwa akasimama. Alitaka kusema lakini maneno hayakutoka kinywani, yamemkwama, uso umembadilika. Alinyanyua mikono juu na kushukuru Mungu, akakaa, (uk. 263).

Sururu ni haini ambaye ni msemaji wakati akiwa na wenzake kule vyumbani, wenzake wakimhusisha sana na shari anayoizungumzia zaidi ya heri. Upekee wake unatokana na namna anavyoshirikisha matendo katika usemaji wake. Hasemi tu akiwa amekaa bali anatenda hivi kwamba inabainika kwa wazi namna alivyofanya matendo husika. Hii ndiyo nguvu ya utendaji, ambayo Schechner (1985) anaeleza kuwa imo katika uhusiano mahsusi kati ya watendaji na ambao kwao, utendaji huo unatekelezwa.

Sururu anafanikiwa kujenga na kuendeleza maudhui ya mateso anuwai wanayoyapitia wafungwa, na zaidi wale wanaojaribu kutoroka wakashindwa au wakapatikana baadaye. Kufaulu huku kunatokana na namna anajumuisha matendo au ishara katika kusema kwake, na kama Nadharia ya Utendaji inavyoeleza; utendaji mzuri na unaofanikiwa ni ule ambao hujumuisha lugha ya majibizano na ishara. Uhusika wa Sururu unaweza kutekelezwa na mtendaji atakayechukua nafasi hii kwenye jukwaa.

3. Doto

Doto anaelezwa kama mhusika ambaye alikuwa kijana mwenye umri wa kati ya miaka 20-30. Alikuwa sajini aliyesifika katika kikosi chake kwa ujasiri na ukakamavu wake. Kabla hajakamatwa na kuhusishwa na mpango wa uhaini, Doto alikuwa kwao Jambiani baada ya kuacha kazi ya jeshi na kuanza kufurahia maisha ya baharini. Alitumia muda wake mwingi akivua baharini usiku na mchana, na wakati akiwa baharini, saa nane za usiku ndipo alipokamatwa, kuteswa na kupelekwa moja kwa moja hadi kwa Ba Mkwe.

Mateso na kichapo anachopokea baada ya kukamatwa kinaathiri utendaji wake katika riwaya hii. Kwa mujibu wa msimulizi, Doto alikuwa jitu lenye ujasiri na ukakamavu, sababu zinazomfanya msomaji kutarajia kwamba matendo yake yatakuwa na sifa hizi za ukakamavu na ujasiri. Hata hivyo, masimulizi yanazidi kutufahamisha kwamba katika kule kuteswa, Doto aliteswa, askari wa kwa Ba Mkwe wakamtimba na kumfirigisa, ule ukakamavu wake ukamwisha. Anapotupwa chumbani alimo Hamza, ambapo anaanza kutenda moja kwa moja:

Alianguka chali akihema, pumzi zimempaa ziko juujuu kama mtu aliye katika sakarati-el-mauti, ameshika makorodani yake, ameyakumbatia akikenya meno, akionesha mwenye maumivu makali. Alikuwa amevaa fulana isiyo na mikono tu, amevuliwa suruali yuko uchi ameyabana makorodani yake hayawachii, anajinyonga na kujibenua akirusharusha miguu. Ameroa damu mwili mzima na nyingine imetapakaa sakafuni, anapiga mikambi na kukidunda kichwa chake chini kama aliyepandwa na pepo. Amekuwa mawenge kabisa. Hamza alijaribu kumzuia, akamwinua asiumie kichwa kwa vile anavyokidunda sakafuni lakini alirusha miguu, akatupatupa mateke, hakamatiki asilani. Palikuwa na ndoo ya maji pembeni, Hamza akachukua akachota gao jingine, akampakata na kumnyweshwa, akachota gao jingine, akampangusa usoni. Akatulia kama mtoto mchanga anayebembelezwa akapata usingizi taratibu. Hamza akaendelea kumnyweshwa maji mpaka alipotulia kabisa, akamlaza juu ya sakafu, bado ameyakumbatia makorodani yake, miguu ameichanua...(uk. 46-48).

Katika mfano huu, tunamwona Doto katika hali ya maumivu. Ni wazi kwamba ameumizwa vibaya kutokana na namna anavyotenda. Anashirikisha sehemu nyingi za mwili; kichwa, mikono, miguu na hata ishara za uso hivi kwamba utendaji wake unadhihirika kikamilifu. Doto alipoamka anaanza mazungumzo na Hamza ambapo tunasimuliwa hali ya Doto ilivyokuwa:

“Wameniumiza! Wameniumiza sana!” alilalamika, akisononeka kwa mateso aliyoyapata...kila tako alilolikalia lilimtonesha. Akarudi kulala chali. Na mgongo nao unamtonesha. Akalala vilevile, miguu ameichanua chanu, kama anayetaka kuzaa, bado ameyakamata makorodani yake kama mwenye kuhisi yatadondoka sasa hivi...(uk. 49).

Katika utendaji huu, Doto bado ana maumivu, hali anayoidhihirisha kutokana na anavyo kaa, kulala na kushikilia makorodani yake kwa namna inayoonyesha kwamba kweli ana maumivu. Tukirejelea kauli yake wakati akimwambia Hamza kwamba ameumizwa, zile kauli zinaambatana na hisia na matendo, na vyote hivi vinaonyesha kwamba anaumia. Huyu ni mhusika mzuri na ambaye utendaji wake utafanikiwa kwa mujibu maelezo ya Bacon, Schechner na Turner katika Nadharia ya Utendaji.

Upekee wa Doto kama mmoja wa mahaini ni ule uwezo wake wa kuwasiliana kwa kugota ukuta. Amekuwa jeshini kwa muda mrefu na hivyo ana uwezo wa kuwasiliana na majeshi wenzake waliokamatwa na kuwekwa vyumba tofauti na alimo. Anamfunza Hamza, na wawili hawa wanaweza kuwasiliana na wenzao kupitia kugota ukuta; wakawapa wenzao habari nao wakapokea chochote kigeni kutoka kwa wenzao:

Ule mlio wa ukuta ukaendelea. Doto akausikiliza kwa makini, akamwuliza Hamza, “Mna mwanajeshi humu?” “Wengi,” Hamza akamjibu. Ule mlio ukaendelea na baada ya muda kidogo ukasita.

“Anayegonga ni mwanajeshi,” Doto alisema. Anazungumza kwa ishara za morse”...sauti ya ule mlio wa ukuta. Ukaanza tena, tu, tu, tu. “Sikiliza!” Doto aliamrisha kama sajin anayeamrisha kuruta.

Alisikiliza kwa makini mpaka alipomaliza kugonga. Naye Doto akagonga. Akagonga kwa muda, naye akasita kugonga...(uk. 52).

Doto ni bingwa wa kuongea kwa ishara za vidoto. Sehemu ya redio ya kikosi chao humtegemea sana kwa shughuli hiyo na hapo tena alijigamba na kujitapa kwa Hamza jinsi alivyokuwa bingwa katika fani hiyo...(uk. 53).

Sifa yake hii ndiyo inayompa utendaji mpana na wenye umuhimu. Anaweza kuzungumza na wanajeshi wenzake ambao wamekamatwa, na baada ya kumfunza Hamza namna ya kuwasiliana kwa vidoto, wawili hawa wanapata namna nyingine ya kujipunguzia upweke wakiwa chumbani, (uk.58).

Doto anashirikiana na Hamza kwa mengi, ikiwemo kule kuzungumza na wenzao kwa kugota kuta za chumba, kucheza dhumna na vilevile kuuguzana mateso ya kwa Ba Mkwe yanapokithiri, uk. 50-62.

Doto ni mmoja wa mahaini 30 wanaobaki baada ya wale 655 kuachiliwa huru. Hawa 30 wanahusishwa na kesi ya uhaini moja kwa moja, na wanapofikishwa mahakamani na kesi ya uhaini kukamilika, Doto anahukumiwa kifo.

4. Shekhe Mandundu

Shekhe Mandundu ndiye mhusika wa nne kupelekwa Kumbakumba baada ya Hamza, Abdul na Shadidi. Anaelezwa kama mtu mfupi, mnene tipwatipwa mwenye uso mdogo na sauti kali nyembamba. Kama jina lake linavyoashiria, Shekhe Mandundu ni mfuasi dhabiti wa dini ya Kiislamu. Utendaji wake wakati akiwa kule gerezani unajitokeza zaidi na kwa njia ya kipekee kutokana na tabia yake ya kuhusisha dini katika kila jambo.

Anapoingia chumbani katika (uk. 16), badala ya kukasirika au kufanya vituko kama alivyofanya Shadidi, yeye anashukuru Mungu na kukubali kwamba kuwepo kwake katika chumba kile ndiyo majaliwa yake. Magharibi inapoingia anawaomba wenzake wajiunge naye katika swala ya jioni ile:

Yule mgeni [Shekhe Mandundu] alisimama mlangoni ameshangaa, akanyanyua mikono yake juu akashukuru, “Al-hamdu lillah! Nimekosa nini miye?” aliuliza...Magharibi imeingia! Tuswalini jamaa! Aliamrisha. “Nataka kutawadha!” alisema. “Hamna maji humu,” Hamza alimjibu kwa upole. “Basi tutayammam.” Walimnyamazia kimya wakamtazama. Akapiga mikono yake juu ya sakafu akajipangusa uso na mikono, akasimama, “Nye hamsali?” aliuliza. Hakuna aliyemjibu. alifunga sala, akarukuu, akasujudu, akamaliza rakaa zote tatu za swala ya Magharibi, akabakia pale pale akivuta uradi...(uk. 16-17).

Mhusika huyu amepewa utendaji wa kidini. Katika chumba hiki, yeye ndiye anayetekeleza wajibu wa kufuata swala zote za siku, kuomba mabaya na shari ipite mbali na chumba chao, na kila balaa inapotokea, yeye anakuwa wa kwanza kupiga dua kwa mwenyezi Mungu. Japo wengine huenda wasiwe na imani kama yake, yeye amejitwika jukumu la kuomba na kuwaomba wenzake chumbani mle (uk. 17). Ana bidii ya dini na anaamini kwamba Mungu pekee ndiye mwenye uwezo wa kuwaondoa kwenye balaa ile kama msimulizi anavyoeleza zaidi:

...Na Shekhe Mandundu naye matumaini yake yote yalikuwa juu ya ujudi wa Mungu. Yeye ni kuvuta uradi tu. Amechukua uzi wa gunia ameufunga mafundo madogo madogo kwa namna ya mudawari akawa ni kuvihesabu vile vifundo na kumunyamunya mdomo. Kamba hiyo ilimtosha kuwa ndiyo tasbihi yake ya gerezani, akiomba na kuomboleza, “Mungu atutoe katika janga hili!” (uk. 24).

Mbali na kupiga dua na kuvuta uradi mle chumbani, yeye huwa msimulizi wa hadithi za kidini, (uk. 33). Anaposimulia hadithi hizo ndipo anapozidisha dua na kuomba mwenyezi Mungu awanusuru. Anakuwa kiungo kati ya Mungu na wale wafungwa,

wakajifunza dini kutoka kwake na baadaye wakaomba. Japo yeye pia anateseka na hali yake ya mwili kudhoofika kila siku, Shekhe Mandundu anawahimiza wenzake waombeane kheri na kuoneana huruma; mmoja asimtie mwenzake katika matatizo zaidi, janga linalowakabili linatosha, (uk.91).

Kutokana na tabia yake hii, wenzake mle chumbani wameshamzoea, na wakiwa na hofu au shida zinapokithiri humwendea na kumwomba awapigie fat-ha, kama inavyotukia wanapopata habari kwamba Hamza yumo chumba cha kiza, (uk. 89).

Shekhe Mandundu anajipata miongoni mwa mahaini 30 wanaoandaliwa kesi ili kufikishwa mahakamani. Kabla hajarudishwa chumbani alikuwa ameketi uwanjani akiomba na kupiga dua, (uk. 100). Wanaporudi chumbani, tunasimuliwa kwamba mahaini hawa wanasoma na kuomba:

Shekhe Mandundu alikuwa amekaa, miguu ameisuka kama mwalimu wa chuoni anavyokaa juu ya jamvi...kofia yake ameishika mkononi anaonekana wazi wazi ni mtu mwenye wasiwasi, ni kumunyamunya midomo akiomba dua tu, (uk. 102).

Shekhe Mandundu amepewa nafasi ya kukuza maudhui ya dini na kuwafanya mahaini wengine kuweka tegemeo lao kwa Mungu, ambaye ndiye anayeweza kuwaondolea balaa inayowakabili. Shekhe Mandundu anatekeleza uhusika wake huu kwa ufanisi mkubwa, kutoka mwanzo wa mazimulizi hadi mwisho.

5. Faraji

Faraji mwanasheria mashuhuri; ana digrii mbili za sheria kutoka Chuo Kikuu cha Lumumba cha mjini Moscow. Hajapata kazi ya uanasheria lakini alikutana na Kapera, Afisa mkubwa katika Idara ya Usalama, na huyu ndiye aliyempa kazi ya kumtafutia habari; kutafuta nani anasema nini, nani anafanya nini, kwa ujira wa shilingi mia

mbili kila mwezi. Yeye ndiye aliyempelekea Kapera habari za mpango wa kuuawa kwa wakubwa, lakini akazipuza. Hivyo, ilipotukia kwamba Kigogo kauawa, Faraji alikuwa miongoni mwa watu wa mwanzo kukamatwa, akateswa na kulazimishwa kusema kila alichokijua kuhusu mauaji ya Kigogo lakini hakuwa na zaidi ya kueleza. Akateswa na kudhalilishwa, akaishia kutupwa chumba nambari sita alikokuwa Hamza na wenzake, (uk. 107).

Yeye ndiye aliyekabidhiwa utendaji katika masuala yote ya sheria chumbani mle. Anamuunga Hamza mkono kwamba wote watashtakiwa, na kutokana na elimu yake ya sheria, anajua namna ile kesi ya uhaini itakavyoendeshwa, na anajua hatima yake vilevile. Anamweleza Sururu kwamba hii haitokuwa kesi ya kufanyiwa mzaha. Hii ni kesi ya mauaji, tena mauaji ya mtu mkubwa...ukipatikana na hatia ni kifo tu! Itakuwa kesi ya uhaini...(uk. 108).

Wakati wenzake wanashtushwa na habari za kwenda mahakamani, yeye hukaa na kuichambua kesi yenyewe akilini, akajiuliza maswali anayotarajia kuulizwa na kujijibu mwenyewe, (uk. 108, 109). Anapotolewa Zonga, yeye ndiye anayewaambia wenzake kwamba yule hakuwa mmoja wao bali alikuwa ametiwa ndani mle kusigiza tu wanayoyasema na wenzake; Khalfani na Kondo wanamuunga mkono, (uk. 115). Japo Faraji ni bingwa wa sheria, mateso ya gerezani yanamzidi na kubadilisha haiba yake; amedhoofu hali yake, mbavu zote zipo nje unaweza kuzihesabu. Hatimaye, Faraji Majaliwa anapatikana bila hatia na kuachiliwa huru.

Katika sehemu hii, tumewachunguza mahaini watano wenye umuhimu zaidi katika masimulizi ya riwaya ya *Haini*. Tumewaangazia Hamza ambaye ni mshukiwa mkuu wa mauaji ya Kigogo, Doto; mwanajeshi, Sururu; Kuli na mtetezi wa haki za wafanya

kazi, Shekhe Mandundu; kiongozi wa kidini na hatimaye Faraji; mtaalamu wa masuala ya sheria.

3.2.2 Mashahidi

Mashahidi ni miongoni mwa mahaini waliokamatwa na kushawishiwa watoe ushahidi wakiwa upande wa mashtaka. Wanakiri wenyewe kwamba wamekubali kushirikiana na wakubwa wa magereza baada ya kushindwa kustahimili mateso wanayokumbana nayo pale gerezani. Hawa wameandaliwa, wamwewekwa vizuri, wanasubiri siku ya kesi tu, watoe ushahidi; ambao tayari umetayarishwa. kama Kanali Mapepe anavyomwambia Hamza:

“Sisi tunajua kwamba wewe huhusiki lakini ombi letu ni kukutaka ukubali. Ujidai kama vile umo na unawajua wengine. Tuna orodha ya majina hapa tutakupa, na wote hao tumeshawatungia hadithi kuthibitisha vipi wanahusika.”...(uk. 82).

Haya ndiyo Hamza anayowaeleza wenzake baada ya kurudishwa Kumbakumba kwa kuhusiana na kesi ya uhaini moja kwa moja:

Mimi nadhani sisi sote tutashtakiwa na tutapelekwa mahakamani, manake washaandaliwa watu kuja kuwa mashahidi wa serikali. Wako huko wamewekwa, wanakula biriani kwa kuku, sio kama sisi, asubuhi muhogo, mchana muhogo...(uk. 106).

Mashahidi hawa wameandaliwa kwa kuwa watu wamekamatwa kwa kushukiwa kuwa wameshiriki kwa njia moja au nyingine katika kuuawa kwa Kigogo, lakini kesi yenyewe haina mashahidi. Faraji anamwambia Khalfani kwamba:

Aliyemwua Kigogo naskia naye kauawa hapo hapo. Wenzake aliokuwa nao walisakwa kama nguruwe, wakauawa mmoja mmoja wakamalizwa wote. hapana hata mmoja aliyekamatwa yuhai. Sasa huo ushahidi uko wapi? Ushahidi madhubuti wa kesi hiyo umeshavurugwa. Sasa lazima wautafute ushahidi wa kusingizia watu...(uk. 116).

Kutokana na mifano hii, tunafahamu kwamba mashahidi hawa sio mashahidi halali bali ni wale ambao wameandaliwa na kutungiwa maelezo watakatotoa siku wakifikishwa mahakamani. Mashahidi waliopo ni tisa, (uk. 153), ambao ni: Mpakani, Sumbu, Marzuku, Mkadam, Vingosho, Zarikani, Pwacha, Kuchi na Haramia. Hawa wanaishi upande wa pili wa kule kwa Ba Mkwe ambako wanalishwa vyakula vizuri, kupewa michezo ya kuwaondolea uchovu wa mchana kutwa pamoja na kutunzwa vizuri; wanadekezwa kwa sababu ya umuhimu wao katika kesi ya uhaini inayotegemea ushahidi wao ili kufaulu. Wahusika wakuu katika kikundi hiki ni Haramia na Pwacha. Yanayowatukia mashahidi hawa yanategemea matendo na misimamo ya wawili hawa.

1. Haramia

Haramia, kabla ya kuuawa kwa Kigogo alikuwa akimtafutia Kanali Bunju habari. Alikuwa mmoja miongoni mwa wengine wengi ambao Kanali Bunju alisambaza kila mahali, wakimtafutia habari na kumpelekea. Siku aliyuawa Kigogo, Haramia, kama inavyosimuliwa katika riwaya alikamatwa, akabinywa, akachapwa mbuda sawasawa, akaboboja aliyoyabwabwaja, na sasa ni mmoja wa wale tisa. Alipo anajuta, na anawashawishi wenzake wakatae kila kitu, iwe sio tena bali ni Kanali Bunju na wenzake, (uk. 164).

Huyu ndiye Haramia tunayekutana naye. Anawaambia wenzake ukweli aujuao kuhusu wao kukubali kutoa ushahidi wa uongo:

... “Hapana!” aliruka Haramia, ametoa macho, ameyatumbua. “Bado hatukuingia mtegoni. Tutaingia mtegoni tukikubali pale mahakamani, lakini kama tukikataa, tukasema kwamba sisi hatujui chochote, basi ujanja wao (Kanali Bunju na wenzake) utakwisha...(uk. 156).

Haya ndiyo wanayoyajadili, (uk 156-160), na Haramia anajaribu kuthibitisha kwamba kweli Kigogo kauawa na wakubwa wenzake, Kanali Bunju akiwemo. Haramia karibu na wakubwa hawa, akifanya kazi nao, hivyo pana uwezekano akajua waliohusika katika kupanga na kutekeleza mauaji ya Kigogo.

Wapo wanaoyaamini madai ya Haramia lakini wapo wanaohofia kukataa kusema waliyoambiwa waseme siku kesi ikifunguliwa wakajitia matatani. Kitendo hiki cha Haramia kuwashawishi wenzake wasikubali kutoa ushahidi huu ndicho kinachomletea maafa yanayomkuta baada ya kusalitiwa na Pwacha, (uk. 160).

Haramia anatolewa mle chumbani na Dude, kwa amri ya Kanali Bunju:

“Vaa shati lako,”Dude alimwambia. Wote sasa walimtazama Haramia. Haramia sasa amebabaika analitafuta shati amesahau kama ameliweka mchagoni. Alipoliona alilivaa kwa haraka akawatazama wenzake hajui awambie nini. Awaage? Anajiuliza. “Tuombeane dua!” aliwambia akatoka chumbani kumfuata Dude. (uk. 166).

Anamfuata Dude hadi ofisini mwa Ba Mkwe na baadaye kupelekwa *Mashakani Hotel*, ambako anafungiwa chumba kimoja na chatu na kuachwa humo; hajijui hajitambui, aliwe na huyo chatu, yake yaishie hapo:

Alipokuja kujitambua alijikuta ndani ya chumba kikubwa akazindukana taratibu, anadorora kama anayeamka kutoka katika usingizi wa nusukaputi. Alijihisi kama aliyezongwa na mauzauza ndani ya chumba cha ujinini miongoni mwa majini na mashetani ambayo yeye hawezi kuyaona...akajihisi sasa amefika. Yupo Mashakani Hotel, nyumba ya mashaka kweli kweli siyo mashaka ya mzaha... “Nini tena kile?”alijiuliza. Alisimama akalinyemelea taratibu. alipoligurubia, alirudi nyuma ghafla akiwa na mshtuko mkubwa. Alirudi kinyumenyume mpaka pale alipokuwa amekaa, pale kwenye pembe ya chumba. Macho yake yote yako kule liliko lile furushi. Moyo unamwenda mbio unadunda kama ngoma. Macho kayatumbua, kinywa kakiwacha wazi, anataka kupiga kelele lakini anaogopa. Mwili unamsisimka, manyoya ya mwili yamemsimama, viungo vyote vimekufa ganzi. Alikaa chini taratibu amelikodolea macho. Chatu! (uk. 169-172).

Katika mfano huu, Haramia anazinduka na kujipata tayari amefika *Mashakani Hotel*, amefungiwa chumba kimoja na chatu. Haramia anatenda namna ambavyo mtu akijipata katika hali kama hii anatarajiwa kutenda. Damu inamwenda mbio, hajui la kufanya, ameogopa kikomo cha kuogopa. Baadaye katika tukio hili, yule chatu anaamka na Haramia anatenda zaidi ya matarajio ya msomaji na hata wakubwa wa magereza anapomkata yule chatu kwa meno, (uk. 173-174). Tumeleza tukio hili kwa kina katika sehemu ya taswira za kifilamu, sura ya tano.

Huu ndio utendaji wa kutisha zaidi uliosimuliwa katika riwaya ya *Haini*, jambo linalomfanya Haramia kuwa mhusika muhimu zaidi miongoni mwa mashahidi wote.

Katika masimulizi yote katika riwaya hii, hakuna haini anayechukuliwa kuwa hatari kiasi cha kukutana na Ba Mkwewe mwenyewe isipokuwa Haramia kwa kuwa anapanga kuwaponza wakubwa, hivyo adhabu yake ikawa kuachwa chumba kimoja na chatu; afile mbali, (uk. 173-174). Haramia anaporudishwa chumbani anayamaza, hasemi chochote na yeyote kwa kuhofia kwamba mle chumbani mna jasusi wasiyemfahamu. Anabadilika na kuacha ile tabia yake ya kusemasema.

Licha ya hatari inayomkabili, Haramia anashikilia kwamba hata kubali kutoa ushahidi wa uongo akawaponza wenzake:

“Wa-llahi sikubali! Hata wakinifanya nini,” Haramia anaapa na kula yamini. “Itakuwaje niwaponze wenzangu, niwaingize katika janga kwa jambo wasilolijua!” Kauli hiyo imejaa tele ndani ya kifua chake, inavuma kama moto wa makuti makavu, (uk. 202).

Wanajadiliana na kusafiana nia, na sasa wanayaongea haya ya kutoshirikiana na Kananli Bunju waziwazi, (uk. 205). Japo wanadhani kwamba wote wamekubaliana kwamba siku wakifikishwa mahakamani wakatae, hawajui kwamba anayewasaliti ni

Pwacha. Huyu ndiye anayewasababishia taabu inayowapata kwa kuwasaliti kwa Dude.

2. Pwacha

Pwacha anaelezwa kama mhusika mvivu, mnene, mwenye tumbo kubwa; manyama ya tumbo yameteremka na kufanya mapeta, ambayo humfanya ajihisi mzito, (uk. 160).

Huyu anakinzana na Haramia. Wakati Haramia anapanga mikakati ya kuvuruga mpango wa kutoa ule ushahidi waliopewa, na kuwaona Kanali Bunju na wenzake kama watu dhalimu ambao watawaua hatimaye, Pwacha anawaona kama wenye huruma kwa zile fadhila wanazowapa; chakula kizuri na michezo, (uk. 156). Wakati Haramia anaona kwamba wakitoa ule ushahidi watawaponza wengine ambao huenda hata hawakuhusika katika mauaji ya Kigogo, Pwacha hajali hayo, (uk. 157).

Pwacha anamsaliti Haramia kwa kumwambia Dude (mmoja wa walinzi wa pale kwa Ba Mkwe) madai ya Haramia; kwamba wakubwa wamo katika mauaji ya Kigogo, (uk. 160). Baada ya kumponza Haramia na yaliyompata kumpata, Haramia anarudi chumbani na ule mjadala wa kukaidi mpango wa Kanali Bunju unanza upya. Wote wamekubaliana kuchukua msimamo huo isipokuwa Pwacha kama msimulizi anavyosimulia:

Pwacha akabaki amefadhaika, hajui asimame wapi amebaki mguu nje, mguu ndani. Mazungumzo yote yale ya jana usiku yeye aliubana du, hakutia lake. Sasa anajiuliza. Wapi? Huku au huku? Akatae kama wenzake wote au akubali. Wenzake ndio hao, washajitolea, na liwe litakalokuwa...lakini mnafiki haachi unafiki kwani ni ila isiyosarifika. Pale pale ukamjia unafiki akasema kimya kimya, “Mbele ya kifo hakuna unafiki wala uzandiki.” (uk. 205).

Pwacha anaamua kuiokoa nafsi yake na kuwasaliti wenzake tena, (uk. 205) na wakati huu, wote, yeye akiwemo wanajipata mashakani. Wanapelekwa upenuni ambako

kaburi zao zimeandaliwa. Wakati kila mmoja wao amesimama mbele ya kaburi lake, na nyuma yao kuna askari mwenye bunduki tayari anayengoja tu amri aifyatue, uzandiki wa Pwacha unamzidi:

Pwacha alichomoka mbio pale alipokuwa amejipanga na wenzake akaenda mpaka chini ya miguu ya Kanali Bunju, akapiga magoti na kuikumbatia miguu hiyo, “Nakushika miguu! Nakushika miguu Mheshimiwa!” Amejitupa chini ameinua macho yake juu, yamejaa hofu tele, anamtazama Kanali Bunju usoni... Pwacha akaanguka chali, tumbo juu, shuka aliyojifungakiunoni imefunguka, mikojo inamtoka...Pwacha aligaragara pale chini akilia na kuomba, “Msalieni Mtume! Msalieni Mtume!” Lakini hakuna hata mmoja aliyetaka kumsalia Mtume... (uk. 209).

Mfano huu unadhihirisha zaidi kwamba Pwacha ni mzandiki, anataka sana kushirikiana na akina Kanali Bunju kwa namna anavyowapigia magoti na kuwabembeleza, tofauti na mashahidi wenzake. Hata hivyo, hamna anayemsigiza, na anawekwa katika hali moja na wenzake. Wote wanateswa kisaikolojia, kuchapwa na kudhalilishwa hadi wanaapa kutoa ushahidi kama walivyokubaliana hapo awali, (uk. 208-210), jambo linalopelekea wao kuhukumiwa kifo.

Pwacha na Haramia wanatekeleza majukumu yao kwa ufanisi mkubwa kwa mujibu wa maelezo ya Nadharia ya Utendaji. Haramia kwa mfano, anajipata amefungiwa chumba kimoja na chatu ambapo mmoja wao lazima amuue mwenzake. Haramia anajikaza anamvamia yule chatu na kumkata vipande vya nyama huku akiitema hadi anamkata vipande viwili na chatu huyo anakufa. Namna Haramia anvyotekeleza tukio hili imewekwa wazi na mwandishi. Kwa upande mwingine, Pwacha anadhihirisha utendaji wake katika matukio kadha, hasa pale ambapo anamwangukia Kanali Bunju miguuni na kumwomba awaepushe na matuti. Utendaji wake unaaminika hasa hali aliyomo ikizingatiwa. Kutokana na maelezo ya Nadharia ya Utendaji kuhusu wahusika na utendaji wao, tunaweza kusema kwamba wahusika hawa wanatekeleza

majukumu waliyopewa kikamilifu. Ni wahusika ambao matendo yao yanaweza kutekelezeka kwenye jukwaa mbele ya hadhira. Sasa tuwatazame wkubwa wa magereza.

3.2.3 Wakubwa wa Magereza

Hawa ni wahusika muhimu katika uendeshaji wa shughuli zote zinazoendelea gerezani. Matukio mengi ya riwaya ya *Haini* yanatukia gerezani, hivyo kikundi hiki kinakuwa muhimu katika kufanikisha matukio hayo mbalimbali. Sifa zao za jumla ni ukatili, udhalimu na hawana utu wala huruma. Hizi ndizo zinawawezesha kutekeleza mambo wanayoyafanya kama vile kuwadhulumu wale mahaini kama wanavyofanya, bila ya chembe hata ya huruma. Ni mtu wa aina hiyo pekee ndiye atakayemtendea binadamu mwenzake wanayoyatenda na asione tatizo lolote wala nafsi yake kumsuta. Hawa ni pamoja na: Meja Mapanga, Kifupinyundo, Kanali Bunju, Kanali Maisara na Ba Mkwe.

Hawa ndio wakubwa wa magereza, na wote wako chini ya Ba Mkwe, ambaye ndiye mkubwa wa gereza la Ziwani, al maarufu kwa Ba Mkwe. Hawa ndio wenye ukatili, udhalimu na hawana huruma wala utu. Kutokana na masimulizi vilevile, upo uwezekano kwamba wapo kati yao waliohusika katika mauaji ya Kigogo wakitarajia kwamba wangerithi kiti chake, (uk. 158). Wana sifa tofautitofauti kama za kimaumbile lakini hushirikiana, wakawahoji wafungwa, wakawatisha, kuwashawishi, kuwafirigisa na hata kuua pale inapobidi. Japo tumetaja wakubwa watano, yule aliyepewa nafasi ya mhusika mkuu katika kikundi hiki ni Kanali Bunju. Yeye anahusika katika matukio mengi yanayohusu kesi ya uhaini, na kauli au msimamo wake unaathiri msuko wa matukio katika yale magereza.

1. Kanali Bunju

Kanali Bunju ni mhusika mkali na mwenye hasira nyingi katika matukio anamohusika, (uk. 81). Kulingana na msimulizi, Kanali Bunju alikuwa rafiki wa karibu zaidi wa Kigogo; akiandamana na Kigogo kila alipoenda. Hivyo Kigogo alipokufa, Kanali Bunju akawa kama aliyefiwa zaidi ya kila mtu nchini, tukio ambalo pia linabainisha ufanisi wa utendaji wake:

Kilio alichokiangusha siku ya mazishi ya Kigogo, chozi likamchirizika mpaka likadondokea kifvani, akajigaragaza chini kama aliyepandwa na pepo, akajifanya hapana aliyefiwa wa kumshinda yeye, hapana mwenye majonzi wa kumshinda yeye, hapana aliyefikwa na msiba wa kumshinda yeye...(uk. 161).

Katika tukio hili la mazishi ya Kigogo, Kanali Bunju anaomboleza na kutupatia taswira hasa ya mtu aliyefiwa. Hata ingawa kuna tetesi kwamba huenda alihusika katika mauaji ya Kigogo kwa nia ya kurithi kiti chake, kuomboleza kwake huku kunashawishi kwamba kweli aliona uchungu kufiwa na rafiki yake Kigogo.

Kanali Bunju anafanya kila juhudi ya kumtafuta muuaji wa Kigogo, na ndio maana yupo katika mstari wa kwanza katika kuwahoji na kuwashawishi mahaini; mradi kesi ya mauaji ya Kigogo ifanikiwe. Katika mfano ufuatao; yeye ni mmoja wa wale wanaomhoji Hamza:

Kanali Bunju alikuwa anajikuna upara wake kwa dole la kati, akimwita [Hamza] kwa dharau, “Umeshakaa ndani siku nyingi,” alimwambia... “Lakini Hamza kuna wenzako waliokutaja,” aliendelea. “Nani?” Hamza aliuliza, hana wasiwasi. “Wenzako,” Kanali Bunju sasa amewacha kujikuna upara wake, anafikichafikicha mikono yake huku akimtaazama Hamza bila ya kupepesa. “Wenzako wamekutaja,” aliendelea. “Sifikiri kama kuna mtu aliyenitaja.” “Ebo!” Kanali Bunju alizipandisha nambari zake, macho kayakaza, makali. “Sasa unataka kutwambia sisi waongo siyo?” (uk. 81).

“Mimi siwezi kukubali mtego huo,” alisema Hamza. “Unasemaje?” aliruka Kanali Bunju, akasimama kutoka pale alipokuwa amekaa.

Aliinyanyua bastola yake akafyetua risasi mbili. Zote zikapiga ukutani. Kama “Cow boy” aliyeingia baa kufanya fujo. Kanali Bunju kaja juu, “Ntakushut sasa hivi!” alipiga kelele. Wenzake wote wamesimama wanamsihi atulie...(uk. 82).

Katika mfano huu, mbali na Kanali Bunju, wengine wliopo ni pamoja na Kanali Mapepe na Kanali Maisara. Hata hivyo, anayeongoza ushawishi huu ni Kanali Bunju, ambaye anaanza kwa upole na pale Hamza anapokataa kushirikiana naye anapandwa na hasira na kuamrisha kwamba Hamza apelekwe chumba cha kiza ateseke mpaka asalimu amri, (uk.84-85).

Mbali na kusababisha Hamza awekwe kwenye chumba cha kiza, anampeleka Haramia *Mashakani Hotel* na kuakiza kwamba awekwe chumba kimoja na chatu, amle Haramia ili huo uwe mwisho wake kwa kutaka kumponza yeye Kanali Bunju, (uk. 163-164). Hatua hii inazidi kutudhihirishia kwamba Kanali Bunju ni katili, na kwamba yupo tayari kufanya lolote ili kuhakikisha kwamba waliohusika na mauaji ya Kigogo wameadhibiwa. Anafanya hivi kwa hadhari kubwa asije akatajwa na mmoja wao kwa kuwa kuna tetesi kwamba na yeye alihusika katika mauaji hayo kwa nia ya kurithi kiti cha Kigogo, (uk.83).

Haramia alipotoka *Mashakani Hotel*, alikutana tena na Kanali Bunju na Ba Mkwe, wakamhoji kuhusiana na aliyoyasema. Kanali Bunju ndiye anayefanya sehemu kubwa ya hayo mahojiano:

“Sasa tueleze Haramia,” alianza Kanali Bunju uso umembadilika ameshaivaa ile sura yake ya nuksi na kisirani. “Tumesikia unasema kwamba wewe utakataa kila kitu utakapopeleka mahakamani. Kinyume na vile tulivyokibaliana. Tumesikia vilevile kwamba eti unawatajataja wakubwa kwamba na wao wamo. Kweli hayo Haramia?” Kanali Bunju alimwuliza Haramia huku akimtazama, ameegemea kiti kuonesha dharau.(uk.177).

Kanali Bunju anafahamu namna ya kuwafanya mahaini na mashahidi hawa kufanya kama atakavyo yeye. Hii ndiyo sababu ya kimsingi ya kuogopwa kwake. Japo Haramia na wenzake bado wanakubaliana kwamba wakanushe madai ya kuhusika kwao, Kanali Bunju anaamrisha wachimbiwe makaburi ambako baada ya wao kuomba msamaha wanatoa ushahidi kama walivyokubaliana. Tunasimuliwa:

Kanali Bunju aliwaangalia wale wanajeshi akanyanyua mkono wake juu. Kwa pamoja wakazikorokocha bunduki zao kuinkiza risasi katika chumba chake cha kufyatulia. Ule mlio wa “korokocho” wa bunduki zote zile kwa pamoja ulilidondoa lile tone la mwisho la matumaini lililobaki ndani ya moyo wa kila mmoja wa watu tisa wale. Sasa wanasubiri maumivu makali ya kifo cha risasi. Lakini kabla ya Kanali Bunju hakushusha mkono wake chini kutoa ishara kwa wale wanajeshi wafyatue risasi zao, alinyanyua sauti yake juu akawauliza kwa kelele, “Nakuulizeni mara ya mwisho! Mtakubali mtakataa!” “Tutakubali!” wote walijibu kwa umoja wao...(uk. 209-210).

Mifano hii inazidi kudhihirisha namna Kanali Bunju alivyostadi wa kutesa, kimwili na hata kisaikolojia. Kanali Bunju ana sifa ya kuwatesa mahaini kisaikolojia hadi wakajiona wazimu ilhali wana akili zao timamu. Msimulizi anaeleza kwa mfano kwamba, wakati Kanali Bunju amefika kule kwa Ba Mkwe, yeye huzungumza kwa sauti ya juu makusudi kuwashtua akina Hamza, (uk. 96).

Kanali Bunju, kwa mujibu wa Nadharia ya Utendaji ni mhusika ambaye ikiwa mtendaji atachukua nafasi yake na kuitenda kwenye jukwaa mbele ya hadhira atafanikiwa. Ameweza kuwasilisha sifa za mkuu wa gereza ambaye ni katili na ambaye anajua namna ya kushughulikia mahaini na kupata habari anazotaka kutoka kwao.

3.2.4 Washikadau Mahakamani

Washikadau mahakamani ni wahusika ambao utendaji wao umejikita katika kuendesha na kufanikisha kesi ya uhaini mahakamani. Wahusika wakuu hapa ni

wanne; Chopra, ambaye ndiye mwendeshaji wa mashtaka, na mahakimu watatu; Pandu, Jongu na Musadiq. Chopra anatawala matukio yote ya kesi hii, na inapokamilika anawaachia nafasi mahakimu kutoa hukumu.

1. Chopra

Chopra anaelezwa kwamba alikuwa mtu mfupi. Ana uso mwembamba, pua ndefu na macho madogo yanayodhihirisha ujanja wake. Chopra pia amepewa sifa ya ubarakala kwa sababu kwamba kila serikali mpya inapochukua hatamu, yeye hujibadilisha na kufanya kazi nayo. Kwa mfano, tunasimuliwa kwamba wakati wa utawala wa Elizabeth wa Pili, alikuwa mwanasheria wa kupigiwa mfano katika serikali hii. Sultan alipochukua hatamu, Chopra akawa mshauri mkuu wa mambo ya kisheria, na Sultan alipotolewa mamlakani na Kigogo kuingia uongozini, Chopra akapewa cheo cha Mwanasheria Mkuu wa serikali yake, wote hawa akifanya nao kazi kwa utiifu na uaminifu, (uk. 230-231).

Mbali na huku kutumikia serikali tofautitofauti kwa uaminifu, msimulizi anabainisha wazi kwamba Chopra anakipawa cha Uanasheria, ni mwanasheria wa kupigiwa mfano:

Alikuwa ni mwanasheria aliyejaaliwa kipawa cha hali ya juu na ustadi mkubwa wa kazi yake ya uanasheria. Jinsi alivyokuwa bingwa wa kazi yake hiyo, aliaminiwa sana na mahasimu wote watatu waliokitawala Kisiwa cha Zanzibar...Kwa hivyo alikuwa na kipaji cha ajabu kwa kazi yake ya uanasheria...(uk. 230-231).

Kutokana na ustadi wa Chopra katika kazi yake ya uanasheria, anastahiki uhusika aliopewa, wa uendeshaji mashtaka. Tajriba yake katika uanasheria inamfanya Chopra atekeleze utendaji wake kwa njia ya kuaminika na msomaji. Anafanikiwa katika namna anavyoingia kortini, anavyosoma maelezo katika majalada anayobeba, (uk.

231), anavyowahoji watuhumiwa, (uk. 238) na anavyoendesha kesi ile kwa jumla.

Chopra anapopishwa na karani wa korti tunasimuliwa kwamba:

...zamu ya Chopra ikafika. Akasimama kwa mikogo na kuikaza vizuri tai yake shingoni. Alijipinda kidogo kama mtu mwenye kutaka kurukuu, hiyo ikiwa ni ishara ya heshima kwa mahakimu. Aliwatazama mahakimu akaanza maelezo yake. “Waheshimiwa mahakimu. kwa heshima kubwa niliyonayo kwenu, napenda kuwasilisha kwenu mashtaka ya serikali dhidi ya watu wale waliokaa mbele yenu,” alionesha kidole kule walikokaa washtakiwa, na yeye akageuka kuwatazama kwa jeuri... Alikuwa akisema kwa hanjamu na kila alipoendelea kutoa maelezo yake ndipo jazba ilipozidi kumpanda na sauti yake kuipaza ikavuma ukumbi mzima. Alisita kutoa maelezo, kijasho chembamba kinamtoka. Alitoa kitambaa cha hankachifu kutoka katika mfuko wake wa koti akajifuta jasho kwenye kipaji cha uso wake, akaendelea...Chopra alisita kidogo akameza mate. Akageukia kule walikokaa washtakiwa akawatazama. Halafu akawageukia mahakimu, akaendelea na maelezo yake, (uk. 233-234).

Chopra anatoa maelezo yake kwa mahakama na katika kufanya hivyo, uhusika wake unajibainisha huku utendaji ukijidhihirisha waziwazi. Anaelewa kazi iliyomkabili vizuri, anatambua uzito wa kesi hii ya uhaini na hivyo amejandaa kutoa maelezo yake ili kuwashawishi mahakimu kuwachukulia hatua kali wale washtakiwa. Anapoyaeleza waliyoyafanya washtakiwa, anakuwa katili, na anapowageukia mahakimu anazungumza kwa upole. Msimulizi anaeleza kwamba Chopra aliposema, sharti umsikilize, kwa jinsi alivyokuwa na umbuji. Tazama:

Wote ndani ya ukumbi ule wa mahakama walinyamaza kimya wanamsikiliza Chopra kwa makini na Chopra umbuji tu, alikuwa nao. Anaposema ukitaka usitake utamsikiliza...Chopra alishusha pumzi akapumua kama mtu aliyechoka. Alitia tena mkono mfukoni akatoa kitambaa cha hankachifu akajiofuta uso. Akaendelea na maelezo yake, lakini sasa kwa sauti ya upole na unyenyekevu. “Waheshimiwa mahakimu. Nakuombeni mwisikilize kesi hii huku mkiyazingatia kwa makini sana ukweli niliouwasilisha kwenu kwa maelezo yangu haya. Nitaleta mbele ya mahakama yenu tukufu mashahidi 58 ili kuthibitisha ukweli wa maelezo yangu haya... (uk. 235).

Hivi ndivyo Chopra anavyotanguliza kesi hii ya uhaini. Kwa namna anvyotoa maelezo yake; sauti na ishara anazoshirikisha katika tukio hili bila shaka zinamfanya Chopra kuwa mhusika mwafaka zaidi kutekeleza nafasi hii ya uendeshaji wa mashtaka. Baada ya kutoa maelezo kuhusu kesi ile, anawaleta wale mashahidi tisa walioandaliwa kwa ajili ya kesi hii. Chopra ndiye mwenye jukumu la kuwahoji ili waeleze mahakama kuhusu kuhusika kwao katika mpango wa mauaji ya Kigogo.

Msimulizi anatueleza namna Chopra anavyofanikiwa katika kutekeleza shughuli hii:

“Mkadam Bakari,” Chopra alimwita, akamtazama machoni bila kupepesa, “Maswali nitakayokuuliza yanahusu mambo yaliyotokea zamani kidogo kwa hivyo lazima ufikiri kwa makini kabla hukuyajibu maswali yangu.” Hapo tena Chopra akamwandama Mkadam kwa maswali juu ya huo mpango wa kuangusha serikali ya Kigogo na Mkadam yanamtoka tu... Chopra anaruka pale aliposimama, kijasho chembamba kinamtoka, kamshika Mkadam kwa maswali, “Ehen, unaweza kuieleza mahakama hii mipango yenu hatua kwa hatua.”...Chopra akafurahi kwa kazi nzuri waliyoifanya mashahidi wake... Kila shahidi aliyepanda kizimbani alizidi kuthibitisha ukweli wa maelezo ya Chopra na hakuna hata mmoja aliyethubutu kutoa maelezo yoyote yaliyopingana na yake. (uk. 238-240).

Mashahidi wote 58 wanapomaliza kutoa ushahidi, Hamza akaleta vithibitisho vya kusisitiza ushahidi uliotolewa. Chopra amepewa jukumu la tatu, la kusomea mahakama maelezo ya washtakiwa. Anapofanya hivi, hasomi tu yaliyoandikwa bali anajumuisha utendaji katika shughuli yote hii:

Chopra akasimama, akakaza tai yake shingoni, akatazama huku na huku. Kwanza aliwatazama washtakiwa kwa jicho la kuwakejeli, halafu akageuka na kuwatazama mahakimu, akasema, “Waheshimiwa mahakimu. nimewasilisha mbele ya mahakama yenu tukufu mashahidi 58 kama nilivyoahidi. Nimewasilisha mbele ya mahakama yenu tukufu vithibitisho vyote vilivyotakiwa kuwasilishwa mbele ya mahakama hii.” Chopra alisita kidogo, akaomba radhi baada ya kukohoa, “Excuse me!” akaendelea na maelezo yake...Chopra alipomaliza maneno yake alikaa...(uk. 242).

Katika mfano huu na katika masimulizi yanayofuata, Chopra anawasilisha mbele ya mahakama maelezo anayodai kwamba yalitolewa na washtakiwa wenyewe, tena kwa hiari yao. Baada ya kukamilisha shughuli hii, washtakiwa wanapewa nafasi ya kujitetea. Jukumu la nne na muhimu zaidi la Chopra hapa ni kuwauliza maswali na kuhakikisha kwamba maelezo yao yanawiana na ushahidi uliotolewa pamoja na maelezo aliyosomea mahakama. Hapa pia, ustadi wa Chopra unadhihirika:

...Chopra akiwaandama [washtakiwa] kwa maswali makali makali...Chopra mara huwa mkali mara hushuka matao ya chini akaongea kwa upole. Huwababaisha na kuwazungusha washtakiwa kwa maswali yake na washtakiwa nao huwa makini wanapomjibu...(uk. 250).

Chopra anawahoji washtakiwa hawa kwa ustadi kama alivyotekeleza shughuli zake za awali. Hata hivyo, inapofika zamu ya Hamza, tunaona udhaifu wa Chopra ulipo:

Chopra akambana Hamza kwa maswali mara amtie huku amtoe kule, amzungushe hivi amzungushe vile, ambabaishe vile, mara amletee kizungumkuti hiki mara kizungumkuti kile. Lakini Hamza alikuwa makini...Chopra akaduwa, hana la kujibu, mara hii badala ya kukasirika, alicheka. Akarudi juu ya kiti chake akakaa...(uk. 256).

Vilevile, Chopra anashindwa kuwashawishi mahakimu kumfunga mshtakiwa kama Hamza, ambaye amekuwa mshukiwa mkuu, kutokana na ile tabia yake ya hasira na papara ya mambo. Kwa mfano, anatoa kauli tuliyonakili hapo juu, ambayo Hamza anaitumia kumkejeli wakati akijitetea. Kwa mtazamo wetu, Chopra alianguka kwa hili. Ufanisi wake ungekuwa kuhakikisha kwamba mahaini hawa, hasa wale wakuu kama Hamza wote wamehukumiwa. Mbali na hayo, Chopra ni mhusika wa kukubalika kwa mujibu wa Nadharia ya Utendaji; ameshirikisha vipengele anuwai ambayo wananadharia hii wanadai ni muhimu katika kufanikisha utendaji. Maneno yake, ishara, mpumuo, maleba, vyote amevishirikisha katika uhusika wake.

Mahakamani, Chopra anapomaliza majukumu yake anawakabidhi mahakimu fursa; wao ndio waamuzi wa kesi ile, tuwatazame:

3.2.5 Mahakimu

Mahakimu watatu ndio waliohusika kikamilifu katika kesi ya uhaini. Hawa ni pamoja na Pandu, Jongo na Musadiq. Kwa mujibu wa ya msimulizi tunaelewa zaidi kwamba:

Umri wao ulikuwa wa rika moja la baina ya miaka hamsini na tano na sitini na wote walipewa kazi hiyo ya uhakimu na Kigogo mwenyewe pale alipozivunja mahakama zote za mahakimu wanaovaa majuba na nywele za bandia, akafuta utaratibu wote wa kimahakama wa watetezi wanaovaa makoti meusi na tai. Akawaita mahakimu na mawakili wa mahakama hizo malaghai, mabingwa wa kuugeuza ukweli ukawa uongo na uongo ukawa ukweli. Akaunda mahakama zake mwenyewe, akaziita mahakama za wananchi. Mahakimu wa mahakama hizo akawateua yeye mwenyewe na watatu katika hao ndio hawa walipo hapa, mwuza samaki, mwuza maziwa na mwalimu wa chuoni. Wanahukumu kesi ya mahaini waliomwua Kigogo mwenyewe, mfadhili wao aliyewatoa huko walikotoka kwenye soko la samaki, mikeka ya chuoni na kwenye kibao cha baisikeli, akawaweka juu ya viti vile vya heshima, akawapa satua ya kutoa hukumu waitakayo kwa kesi yoyote ile...(uk. 232-233).

Maelezo haya yanamfanya msomaji kutilia shaka utendakazi wa mahakimu hawa, hasa ikichukuliwa kwamba hii ni kesi muhimu, ya mauaji ya kiongozi wa nchi.

Pandu ni mmoja wa mahakimu katika kesi ya uhaini. Kwa mujibu wa msimulizi, Pandu hajasoma, ni mbumbumbu wa kutupwa, na katika maisha yake ya awali, alikuwa mwuza samaki katika soko la Hajitumbo. Jongo naye ana sifa ya uendeshaji wa baisikeli kwa kasi, hasa alipokuwa akifanya kazi yake ya kuuza maziwa:

Kutwa [Jongo] akiranda katika vichochoro vya mitaani na baisikeli yake, amebeba tangi la maziwa juu ya chanja ya baisikeli yake. Kengele ya baisikeli yake akiigonga mlio maalum na washitiri wake walipousikia tu mlio huo wa kengele walijua Jongo yupo mitaani...(uk. 232).

Musadiq ndiye kiongozi wa jopo hili la mahakimu. ameketi katikati ya Pandu na Jongo. Kama msimulizi anavyotueleza, Musadiq ni mwalimu wa chuoni, mchana akisomesha Kurani na usiku akisomesha darasa. Ni gwiji wa masuala ya elimu na dini, (uk. 232). Huyu ndiye anayekabidhiwa jukumu la kutoa hukumu juu ya kesi ya uhaini kama inavyobainika hapa chini:

...Kwa hivyo, mahakama imeridhika kwamba mna hatia na inakuhukumuni nyote adhabu ya kifo isipokuwa wafuatao. Hawa wamehukumiwa kifungo cha miaka kumi na mitano kila mmoja kwa kosa la kutoarifu polisi juu ya mpango wa uhaini ambao wao waliujua ijapokuwa hawakushiriki; Sururu, Khalfan, Kondo na Ambar. Na wafuatao, hawa wao mahakama imewaona hawahusiki hata kidogo na mpango huu wa uhaini na imedhihirika kabisa kwamba wao hawana hatia na kwa hivyo mahakama inawaachilia na wanaweza kwenda zao sasa hivi; Mabruki Issa, Faraji Majaliwa na Hamza. Waliobaki ni waliohukumiwa kifo; Haramia Habib, Mpakani, Sumbu, Mkadam Bakari, Marzuku, Vingosho, Zarikani, Pwacha na Kuchi (wale mashahidi). Wengine ni Mfaume, Doto na Heri Mahmoud... (uk. 263-264).

Sifa ambazo mahakimu wamepewa haziafiki mahakimu waliohitimu. Wawili hawajasoma, na aliyesoma hajasomea Uanasheria; yeye ni mwalimu wa chuo. Hakuna miongoni mwao mwenye tajriba katika uanasheria, na msomaji anashawishika kutoamini kwamba watatoa hukumu faafu kwa kila mshtakiwa. Baadhi ya watuhumiwa wa kesi hii ya uhaini vilevile wana wasiwasi kuhusu utendakazi wa mahakimu hawa. Tazama mawazo yao:

“Kesi, kesi,” alikejeli Sururu. “Mahakimu wenyewe wale? Wengine wauza samaki wameokotwa sokoni? Pana kesi hapo?” aliuliza Sururu, (uk. 107) ...Faraji alimtazama Sururu akashangaa. Kwa Faraji, kwake yeye hakimumu si lazima yule anayevaa nywele za bandia na joho kubwa jeusi, “Hata akiwa nani, hakimumu ni yule mwenye kutazama la haki na lisilo la haki,” alisema Faraji. Unafikiri hawa mahakimu waliookotwa vichochochoni wanajua la haki na lisilo la haki?” Aliuliza Sururu. “Utasikia wakimwuliza mtu. Unawaona wale? Anaonesha wale watu wanaopita nje ya mahakama. Mbona wao hawakuletwa hapa kizimbani? Mbona wewe upo hapa? Hayo nd’o maswali yao. Unafikiri watu kama hao wana cha haki? Aliendelea Sururu... (uk. 108).

Hata hivyo, wanatenda kinyume na matarajio haya, pale ambapo kila mshtakiwa anapewa hukumu anayostahili. Kabla ya kufikia uamuzi wao, Musadiq anaieleza mahakama kwamba:

“Tumezingatia kwa makini sana ushahidi wote uliowasilishwa na upande wa mashtaka...tumezingatia kwa makini ushahidi wa shahidi mmoja mmoja pamoja na maelezo yote yaliyotolewa na upande wa mashtaka. Kadhalika, tumezingatia kwa makini maelezo yote ya washtakiwa kama yalivyosomwa mbele ya mahakama hii, tukatilia sana maanani maelezo ya washtakiwa wenyewe pale walipokuja kujitetea...Baada ya kuzingatia yote hayo, tumeamini kabisa kwamba kweli ulikuwepo mpango wa kutaka kuipindua serikali, mpango ambao baada ya kushindwa ulisababisha mauaji ya Mheshimiwa Kigogo... (uk. 262-263).

Wanatekeleza wajibu wao kama mahakimu ambao wamesomea uanasheria na kupata tajriba kubwa ya kutatua masuala ya kesi kama hizi. Msimulizi hata hivyo anawaacha wasomaji katika taharuki, kwani hatujui ikiwa wale mashahidi tisa watakubaliwa kukata rufaa ili kujitetea upya mbele ya mahakama. Hawa walilazimishwa kutoa ule ushahidi, wakahukumiwa kifo kwa kukubali kuhusika katika mauaji ya Kigogo. Ukweli hata hivyo ni kwamba, hawakuhusika, hata ushahidi waliotoa ulikuwa bandia. Baada ya kuchunguza mahaini, wakuu wa magereza, mashahidi na washikadau mahakamani, sasa tuchunguze walioathiriwa na hili suala la uhaini japo hawakuhusishwa na mchakato wenyewe moja kwa moja.

3.2.6 Waathiriwa wa Uhaini

Wakati Kigogo aliuawa katika mpango wa kuipindua serikali yake, nchi nzima ilijawa na hali ya taharuki. Mambo hayakuwa kama yanavyokuwa siku za kawaida; watu wakajawa na hofu, wasiwasi na hawakujua yaliyokuwa yakiendelea ila milipuko ya risasi ilisikika mara kwa mara, polisi walikuwa kila mahali na watu walikuwa wanakimbilia makwao, (uk. 5). Nchi nzima iliathirika. Kila mtu aliathirika kwa

namna moja au zaidi. Mbali na wananchi kukumbana na matatizo ya njaa, gharama ya juu ya bidhaa, watu kukamatwa ovyo na hali ya taharuki na hofu kutanda, wapo wahusika ambao waliathirika zaidi. Baadhi ya hawa ilikuwa familia iliyoishi jirani na alipoishi mshukiwa Hamduni, (uk. 252-253).

Wengine walikuwa wake za mahaini waliokamatwa wakawaachiwa kazi za nyumbani na malezi ya watoto peke yao. Nassor anamwambia Abdul, “ Kama wewe unataka kujitolea muhanga, basi utajitolea muhanga peke yako! Sisi wengine tunajali maisha yetu. Wake zetu wanapata tabu, watoto wetu wanapata taabu kwa balaa lililofanywa na watu wengine...” (uk. 89). Mkewe Khalfan naye anasemekana kwamba amepata shida, maisha yakamwia magumu akakata tamaa; akadai talaka yake na sasa ameolewa na mwanamume mwingine...(uk. 134).

Wengine ni pamoja na Aziza, ambaye mume wake, kama msimulizi anavyosimulia, amezama kwa Ba Mkwe siku kadha sasa, tokea ile siku aliyochukuliwa nyumbani, usiku wa manane, akapotea moja kwa moja asimwone tena. Naye anahangaika usiku na mchana...(uk. 218). Mhusika mkuu katika kundi la waathiriwa na hasa wake za mahaini ni Khadija.

1. Khadija

Khadija ni mkewe Hamza, ndio kwanza ameolewa na kupata mtoto, hata wiki haijakamilika, Hamza akakamatwa, (uk. 1-7). Ameachiwa kazi ya kulea mwanawe Subira peke yake, kinyume na hali ilivyokuwa hapo awali, yeye akikaa tu na Hamza akikimu mahitaji yake. Amebaki mama na baba, (uk. 144). Khadija anakabiliana na matatizo ya aina mbalimbali. Kwanza, baada ya Hamza kukamatwa, maisha yanakuwa magumu kiuchumi, na kama Hamza anavyoarifiwa akiwa gerezani, Khadija amekwishafukuzwa kutoka nyumba walimoishi kwa kushindwa kulipa kodi,

akarudi kwa wazazi wake Kisimamajongoo. Kwao nako anapata umaskini kama unaomtoa kwake. Tunasimuliwa kwamba:

Jana walilala mkiwa hamna hata senti moja ndani ya nyumba, ulitima umewapiga. Khadija kichwa kinamzunguka, amekaa chumbani, amezama katika bahari ya luja juu ya shida zake...mtoto hana maziwa, mkate wa kunywea chai hakuna. Khadija yumo katika mashaka makubwa...(uk. 144), umaskini umemwandama, hana pesa analazimika hata kukopa, (uk. 147).

Kutokana na changamoto anazokabiliana nazo, Khadija anabadilika; tuliye naye hapa ni Khadija tofauti na yule tunayepatana naye masimulizi ya riwaya ya Haini yanapoanza. Msimulizi anatueleza hali yake ya sasa katika (uk.152).

Mbali na umasikini, Khadija anakabiliwa na changamoto ya unyanyapaa kwa kuwa yeye ni mke wa haini. Azizi anaposimama kwa madai kwamba anataka kumsaidia Khadija, Khadija hasadiki kwa kuwa wakati ule, wake wa mahaini walionekana kama watoto wa nyoka, (uk. 148). Hali hii tunaiona waziwazi siku ya Ukoo pale duka linapofunguliwa. Msimulizi anasema kwamba waliomjua Khadija walinong'onezana na kumsengenya; yeye ni mke wa haini! (uk. 179). Kama kwamba kubaguliwa huku hakutoshi, mkewe Baraka anamzungumzia Khadija vibaya wakati akienda kumtafuta Baraka (sahibu mkubwa wa Hamza) kwa kudhani kuwa Khadija anamwandama mumewe, labda kwa kuwa mumewe ni mmoja wa mahaini, (uk. 183).

Shida nyingine inayomkabili Khadija ni kutongozwa na Azizi, (uk. 148). Huyu ni mwanasiasa mkuu, kamishna wa shirika la kusafirisha dagaa nchi za nje. Anadai kuwa ana salamu zake (Khadija) ambazo Khadija anakisia huenda ni habari kumhusu Hamza, hivyo anashawishika kukutana na Azizi:

Khadija, usingizi hauji pale kitandani. Kila akimuwaza Azizi hamwishi. Ati wakaonane Jumamosi, Forodhani, chini ya mti wa Mabaniani, saa moja usiku. "Azizi ana nini hasa? Anataka nini?"

Anajua nna shida, anataka nijisalimishe kwake kwa ajili ya shida zangu?” Khadija anajiuliza. Hulala kifudifudi akajigeuza huku na huku akajiuliza tena, “Yeye mkubwa, kutwa yumo ndani ya magari ya SZ. Waheshimiwa wote anawajua yeye. Atanisaidia kumtoa Hamza jela?” (uk. 187).

Kama alivyotarajia Khadija, kumbe Azizi amekuwa akimtamani na alitaka kuzini naye, (uk. 191-192). Naye Khadija nusura anaswe na mtego huu kwa kuwa, kama msimulizi anavyosimulia katika (uk. 144), joto kali la mapenzi ya mumewe linafukuta ndani ya moyo wake. Khadija, anatarajia kwamba huenda Azizi anamtaka ajisalimishe kwake kwa kuwa anafahamu kuwa ana tatizo ambalo anaweza kumtatulia. Khadija, akijua hatari anayojiinkiza kwayo bado anakubali kukutana na Azizi kwa matumaini kwamba atamsaidia kumtoa Hamza jela. Pale Azizi anapomtaka kimapenzi, Khadija anakataa; anakuwa mwaminifu kwa Hamza. Anamheshimu vilevile, licha ya kwamba yupo gerezani. Anamwambia Azizi:

“Ndo salamu zenyewe hizo ulizoniitia?” Khadija aliuliza. “Sikiliza bwana, mimi ni mke wa mtu, n’na mume wangu na mume wangu amefikwa na matatizo yuko jela kwa muda mrefu sasa. Sina hakika kama yu hai au amekufa, ameniachia mtoto mchanga. Wewe kama kweli binadamu nisaidie kwa shida yangu hiyo. Nisaidie mume wangu atolewe,” alisema Khadija, uso sasa umembadilika, umejaa majonzi...(uk. 190-191).

Kwa mujibu wa masimulizi, Khadija anakuwa mhusika ambaye utendaji wake unaaminika na uliofaulu; maneno anayoteua, anavyotenda na namna anavyodhihirisha hisi, vyote hivi vinachangia katika kufanikisha utendaji wake.

Wapo wanawake wengine waliokabiliwa na matatizo sawia na haya ya Khadija na wakakata tamaa kama alivyofanya mkewe Khalfan, (uk. 134). Khadija hata hivyo anayavumilia yote hayo. Anamuwaza mumewe na kufanya kila awezalo kumkidhi mwanawe ikiwepo kukopa. Anamshughulikia Hamza kwa vyovyote awezavyo.

Tazama:

[Khadija] amekazana buibui analivalia njiani. Siku ile alikuwa na shughuli nyingi za kuranda huku na kule kushughulikia mambo ya mumewe. Anamuwaza, anamfikiri, anamuota usingizini, hana raha hana furaha. Yumo katika msiba usiokuwa na mwisho, kila siku majonzi mapya huyafukuza majonzi yaliyokuwepo siku iliyopita, hana chochote cha kumliwaza, amezama ndani ya uchungu...Watu humpa moyo wa matumaini na kujaribu kumpoza joto lake la roho wakimtaka asubiri lakini sasa amechoka kusubiri na subira yake imefika kikomo. Sasa atayatafuta mwenyewe ayajue. Mume wake yupo wapi? Yu hai au amekufa? Amekosa nini? Kimya kimekuwa cha muda mrefu, sasa wakati umefika, lazima ayajue. Amechoka kusikiliza porojo la mitaani...(uk. 178).

Khadija anamtafuta Baraka amsaidie kumtoa Hamza gerezani lakini anaishia kudanganywa kwamba hayupo, (uk.183). Anaenda hadi kwa mganga, (uk. 185) na kuweka nadhiri ya sadaka atakayotoa mtaa mzima siku Hamza akitoka jela. Wakati wote Hamza akiwa gerezani, Khadija haishi kumuwaza mumewe. Ana wasiwasi na kihoro kwa kuwa hajui yepi atarajie leo wala kesho yake. Babake anaposikia kwamba Hamza na mahaini wengine wamenyongwa anataabika kujua atakavyomweleza Khadija kwa kuwa; 'Khadija mwenyewe kila wakati roho iko juu juu, wasiwasi umempamba mpaka akawa akili hana wazimu hana, yupo tu, amezongwa na masaibu ya dunia.' (uk. 214). Wakati kesi ya uhaini inapoanza, Khadija anahudhuria ili kuifuatilia kesi ile, na kujua hukumu atakayopewa mumewe, (uk. 231-232). Yeye, kama walivyo wote waliofahamu uhusiano wa karibu waliokuwa nao Hamza na Hamduni, anaona huenda ikawa vigumu Hamza kuachiliwa:

Khadija amejumuika na ule umati wa watu walio nje, amejibanza chini ya upenu wa jumba linalotazamana na lile jengo la mahakama. Mtoto wake amembeba ubavuni amemzuia barabara kumnusuru na zahama na zogo la pale nje. Moyo wake una mchanganyiko wa hofu na tamaa ijapokuwa dalili yenyewe ya tamaa anaiona kwa mbali sana. Maelezo ya Hamza, siku ile aliyopanda kizimbani yalimpa moyo mkubwa akaiona hiyo dalili ya tamaa, akaamini kwamba Hamza kweli hayumo. Lakini kweli Hamza hayumo yeye na Hamduni walikuwa kama ambari na zinduna? Khadija anajuliza, na hilo ndilo linalomtia hofu. (uk. 258, 259).

Mbali na hofu, tashwishwi na majonzi aliyokuwa nayo Khadija, anamtaabikia mumewe hadi pale Hamza anapoachiliwa huru, (uk. 265). Haya yote ni dhahirisho, sio tu la mapenzi ya Khadija kwa mumewe, bali la wanawake kuwa nguzo ya jamii pale waume zoa wanakumbwa na majanga.

Khadija anatekeleza utendaji wake kikamilifu, na ingawa yapo matukio ambapo anajutia kuolewa na Hamza, kumzalia na kujipata katika hali aliyomo, (uk. 151), hakati tamaa. Anavumilia, kuhudhuria kesi siku zote hadi pale Hamza anapoachiliwa huru.

Kwa mujibu wa Nadharia ya Utendaji wahusika tuliowajadili wamejengwa kwa namna ambayo inawezesha utendaji wa kidrama wa riwaya ya *Haini*. Mathalan, namna ambavyo mtunzi amesawiri tabia zao, sifa zao za kimaumbile, matayarisho ya kisaikolojia aliyowajengea, mandhari ya utendaji aliyowachorea, migogoro wanayokabiliana nayo, tajriba na maarifa aliyowapa, taswira alizozijenga, ishara alizowabunia kutumia na mazingira mwafaka aliyoyaunda yanawapa fursa nzuri ya kutekeleza utendaji wao. Kama vile utendaji wa Haramia kumrarua chatu unatangulizwa na matayarisho ya kisaikolojia, ama utendaji wa Kanali Bunju au Chopra kortini.

3.3 Hitimisho

Katika sura hii, tumejadili namna wahusika katika riwaya ya *Haini* wanatekeleza utendaji wao, na kutoa mifano iliyotuwezesha kuthibitisha hayo. Wahusika walioteuliwa wanaafiki nafasi walizopewa. Kwa maoni yetu, wahusika hawa wanaweza kuigizika kwenye jukwaa kikamilifu. Schechner (1985) anaeleza kwamba maswali muhimu ya kujiuliza kuhusu utendaji kwa jumla na kuhusu Nadharia ya Utendaji ni pamoja na: Watendaji ni akina nani? Watendaji wanawezaje kutenda

wahusika wanaowatenda? Na Hadhira ina umuhimu gani katika utendaji? Katika uteuzi wa watendaji watakaochukua nafasi za wahusika tuliowajadili, ni muhimu maswali haya yazingatiwe. Watendaji waweze kutekeleza nafasi hizi kama wahusika wenyewe walivyofanya. Watendaji ndiyo nguzo kuu zaidi ya utendaji; kwani wasipokuwepo basi hakuna wa kutenda.

Katika sura hii vilevile, tumechunguza namna lugha ya majibizano imetumika katika riwaya ya *Haini*. Tumejadili kwa mifano maridhawa matumizi ya lugha ya majibizano katika kufanikisha utendaji mahsusi katika riwaya teule. Kwa mfano, majibizano yametumika kama nyenzo ya kuhoji, kupasha habari, kuliwaza, kushawishi, kuhamasisha na kuendesha mashtaka. Wahusika wamefanikiwa kutenda matukio ambamo majibizo haya yametumika. Lugha ya majibizano kwa mujibu wa Nadharia ya Utendaji, yanapojumuishwa na ishara huwa nguzo kuu ya kufanikisha utendaji.

SURA YA NNE

MASIMULIZI YA UTENDAJI

4.0 Utangulizi

Sura hii imejikita katika uchanganuzi wa masimulizi ya utendaji, matumizi ya kiza na vimulimuli na matumizi ya sauti na kimya kama yanavyobainika katika riwaya ya *Haini*. Hivi ni vipengele ambavyo hufanikisha utendaji ikiwa vitatumika kwa njia faafu pamoja na vipengele vingine vya kimsingi vya utendaji. Hivyo, vipengele hivi huenda visichangie katika kufanikisha utendaji ikiwa vitajisimamia au kutumika kwa njia isiyofaa. Vipengele vya kimsingi vya utendaji kama vile lugha ya majibizano, wahusika na utendaji wenyewe husaidiwa kufanikisha utendaji na vipengele hivi. Japo umuhimu wa vipengele hivi visaidizi hauwezi kulinganishwa na wa vipengele vya kimsingi, huenda vikasababisha kufaulu au kutofaulu kwa utendaji kwenye jukwaa. Shafi Adam amevitumia vipengele hivi katika riwaya ya *Haini*.

4.1 Masimulizi ya Utendaji

Goldfarb na Wilson (2002) katika kujadili suala la utendaji wanauliza nini tofauti kati ya utendaji kwenye jukwaa na utendaji kwa ajili ya filamu au runinga? Wanadai kwamba, katika aina hizi mbili za utendaji, sharti mtendaji ajenge mhusika ambaye ni tofauti na alivyo yeye (mtendaji mwenyewe); aigize maneno na matendo ya mtu tofauti na alivyo yeye. Mtendaji katika miktadha hii sharti akariri maneno ya mhusika anayemwigiza, miondoko yake na nafsi yake na vilevile aweze kutangamana na watendaji wengine wakati wakiigiza. Maelezo haya yanatia mkazo madai ya Bacon (1984) kwamba waigizaji huteuliwa kuwaigiza wahusika ambao wataweza kutekeleza matendo yao, na vilevile sifa zao kuwiana kwa kiwango kikubwa. Utendaji hivyo,

hufaulu pale ambapo mtendaji anayeteuliwa anaweza kutenda kama anavyotenda mhusika anayemwakilisha kwenye jukwaa.

Katika tamthilia, maelezo ya utendaji hubainika moja kwa moja kwa kuwa huandikwa na mwandishi mwenyewe kwenye mabano kwa hati mlazo. Maelezo haya ndiyo hutuarifu namna mwigizaji atakayechukua uhusika fulani anafaa kutenda ili kuleta athari iliyokusudiwa pamoja na kufanikisha utendaji wa igizo husika.

Katika riwaya hata hivyo, maelezo ya namna tukio fulani linafaa kutendwa hutolewa na mwandishi kama sehemu ya masimulizi ya riwaya hiyo. Ikiwa mwandishi anakusudia hisia fulani zionyeshwe, miondoko kwenye jukwaa, namna ya usemaji na mabadiliko ya sauti, huyaeleza yote katika masimulizi ya riwaya hiyo, na riwaya hii inapoandikiwa mchezo wa kuigiza, maelezo haya ya utendaji huchukua nafasi ya yale yanayoandikwa mabanoni katika tamthilia.

Katika riwaya ya *Haini*, msimulizi ametoa maelezo anuwai ya utendaji ambayo tumejadili na kuyatolea mifano katika matukio yafuatayo:

4.1.1 Masimulizi Ya Utendaji Kuhusu Mateso

Haya ni masimulizi ya utendaji yanayoweka wazi namna mahaini na wafungwa wengine wanateswa. Matukio mengi katika riwaya ya *Haini* yanatukia gerezeni. Msimulizi amefafanua namna askari, maafisa wa usalama na wakubwa wa magereza wanatekeleza yale mateso dhidi ya wafungwa walio chini ya ulinzi wao. Haya ndiyo masimulizi ya utendaji yanayoeleza mateso haya, na ikiwa kazi hii itaandikiwa mchezo wa kuigizwa na kutendwa kwenye jukwaa, matendo hayo yatatekelezwa ili kufanikisha utendaji wenyewe. Mifano ya masimulizi haya ya utendaji ya mateso ni pamoja na lile tukio ambapo Sururu anapigwa na kutupwa chumba walimo Hamza.

Inaelezwa waziwazi namna kipigo kile kinatekelezwa na Sururu mwenyewe alivyo kufikia pale anapotupwa chumbani. Tazama dondoo lifuatalo:

Mfano 4.1

Ghafula, lango la Kumbakumba lilifunguliwa kwa vishindo visivyo vya kawaida, wakasikia askari wakiamuru kwa sauti za kikatili, “Twende! Twende mbwa wee!” Na sauti nyingine ikiwajibu kwa hasira, “Makatili! Wauaji!” watu walichungulia milangoni wakaona jinsi kiumbe yule alivyokuwa akipondwa kwa mateke bila huruma, akabururwa kitikiti, akanyanyuliwa juujuu, chumba cha akina Hamza kikafunguliwa, akatupwa ndani kwa vishindo, halafu mlango ukafungwa kwa hasira na vishindo, askari hao, wakaenda zao, milio ya viatu vyao ikafifia taratibu mpaka wakatoka Kumbakumba. Alianguka chali katikati ya chumba, uso wake umechanikachanika anavuja damu. Nguo alizovaa, nazo zimeloa damu chepechepe. Amelala chali anatweta kama mwenye kukata roho...(uk. 19).

Msimulizi anaeleza namna Sururu analetwa kule Kumbakumba, majibizano kati yake na waliokuwa wakimpiga, namna alivyokuwa akipigwa kwa mujibu wa waliochungulia kwenye mlango na kuona yaliyokuwa yakiendelea, na hatimaye alivyoanguka mle chumbani baada ya kutupwa humo. Masimulizi haya yanaeleza namna watendaji wanafaa kutekeleza tukio hili.

Hamza anaitwa kuhojiwa kuhusu anayoyajua kuhusu mauaji ya Kigogo. Huyu ni mshukiwa mkuu katika kesi hii kutokana na urafiki wake wa karibu na Hamduni; anayeshukiwa kwamba yeye ndiye aliyemuua Kigogo. Anapokosa kushirikiana nao, wale askari wanaanza kumpiga, popote pale bila kujali lolote. Msimulizi anaeleza utendaji wa tukio hili ifuatavyo:

Mfano 4.2

Yule askari usalama akalivuta gongo la mpera alilokuwa ameliweka chini ya meza akamtwanga nalo Hamza kichwani kwa nguvu zake zote. Damu, mwaa, ikamwagika kama iliyotoka kwenye chemichemi. Ikatapaka juu ya makaratasi, nyingine imemwagika chini, nyingine inamchururika usoni. Hakuwahi hata kuguna, wengine nao wakamwingilia, kama nyuki waliochokozwa. Alitolewa

mle ofisini akatupwa nje juu ya ule uwanja wa sakafu na hapo ikawa piga, piga, kinyang'anyiro, kobe. Alijaribu kuyakinga yale magongo na kukimbia lakini alizongwa akawa kama aliye ndani ya uzio, hapana hata mwanya wa kupenya. Alipigwa mpaka akashindwa kusimama. Hakuna aliyechagua pa kupiga. Walipiga popote pale. Usoni, kichwani, tumboni, mgongoni. Hamza akapondwapondwa, kachiri saga. Akaanguka kifudifudi. Hapo hapo wakamwinua na kumshika huku na huku kama mwenye kutaka kusulubiwa. Wakamchapa mgongoni shati lote likararuka nyambunyambu. Wakamrudisha kule ofisini. Kamba madhubuti ya mkonge ishafungwa. Kitanzi kinaning'inia kwenye kikuku juu ya boriti ya darini. Alivishwa kitanzi shingoni wakamburura huku na huku na yeye akawafuata kama ng'ombe aliyevishwa shemere. Damu ikimwagika, denda inamchururika. Alipiga kelele kuomba huruma mpaka sauti ikampotea ikawa haitoki tena. Lakini huruma itoke wapi ndani ya nyumba ile. Alibaki kukoroma tu. Sasa wakaona wamnyonge. Wakampandisha juu ya kiti na kitanzi chake shingoni. Waliivuta ile kamba mpaka wakahakikisha kitanzi kimembana sawasawa shingoni, wakampandisha juu ya kiti halafu wakakipiga teke kiti, Hamza akawa ananing'inia na wao wanavuta kamba. Alipiga mikambi, macho yamemtoka, mikojo inamchururika kama mtoto mdogo. Walimning'iniza mpaka akakaribia kukata roho ndipo walipoiachilia kamba. Hamza akaanguka chini. Alinyanyuliwa akatupwa nje na baada ya kutua juu ya ile sakafu tu wakam'mwagia ndoo nzima ya maji kumfufua arudi tena duniani. Walipomwona anazindukana wakaanza tena, "Sasa utasema." Wote wamemzunguka, wamejaa tele pale uwanjani. Hamza amelala chali, povu la kinywa linamtoka. Ameloa damu, anatweta kama mtu anayekata roho sasa hivi na kitanzi bado anacho shingoni. Suruali yote imejaa mikojo. Aliwatazama lakini hakuona watu ila aliona umande mtupu, umetanda tele ndani ya nyumba ile. Yeye mwenyewe hajijui wala hajitambui. Alizisikia sauti zao kwa mbali, mmoja wao akisema, "Tummalize." Akapigwa teke la uso kwa kiatu cha jeshi, na hapo akapoteza fahamu kabisa, akawa kama aliyekufa fo fo fo. Aliwachwa pale pale uwanjani jua la mchana kutwa likimpiga yeye kama ng'onda aliyeantikwa. (uk. 40-41).

Masimulizi haya yanaeleza waziwazi namna Hamza anavyopokea kile kichapo kutoka kwa wale askari; wanavyompiga, anavyoning'inizwa kwenye kitanzi, anavyotolewa nje na kichapo kwendelezwa na hatimaye kuachwa nje kama mfu. Masimulizi haya yanatueleza namna ya kutekeleza igizo hili kwenye jukwaa, na vilevile kudhihirisha mateso ambayo washukiwa wa uhaini waliyoyapitia, Hamza akiwa mmoja wao.

Doto ni mhusika mwingine anayekumbana na mateso yanayosimuliwa kiutendaji kama yalivyotukia:

Mfano 4.3

“Mshike mikono! Mkamate miguu! Mtie kamba!” Naye yule mtu akirusha ngumi na kuwatukana, “Mbwa wakubwa! Washenzi! Wauaji!” Hamza alitega masikio kusikiliza vurumai ile mpaka yule mtu alipotupwa pale uwanjani na kubumundwa. “Utasema! Leo ni moja tu, utasema au tutakuu,” sauti zilizojaa hasira na uchungu zilisikika zikimwambia. Zikiambatana na kipigo kikubwa. Kipigo chote hicho, yule mtu hakuguna wala kunung’unika. Alihimili mateso yake kijabari akadhihirisha usugu mkubwa. Kwa ghafla kile kipigo kilisita, naye usugu ukamwisha akaanza kulia na kupiga mayowe kwa sauti ya mtu mwenye kuhisi maumivu makali, “Yalla! Mnania! Ya Rasulallah!”

“Sasa utasema!”

“Mnaniuniza!”

“Sema! Unayajua!”

“Ngojeni! Ntasema! Ntasema!”

Alitolewa kule ofisini akatupwa uwanjani, Hamza akamsikia akianguka kwa kishindo kikubwa na hapo hapo akawasikia wakimlaani na kumtukana, na matusi na laana zao zikienda pamoja na dharuba kali za kipigo kwa mipweke mizito mizito. Aliishiwa na nguvu zote. Hali, halalami, hakoromi. Anatweta na alipopumua pumzi zilitoka kwa mlilo wa kifirimbi kama mgonjwa wa pumu.

“Anakufa!” Hamza alimsikia mmoja wao akisema.

“Bado! Alisema mwingine.

“Tummalize!” mwingine aliingilia kati.

“Tumwache, kama hakusema leo atasema kesho. Atasema tu! (uk. 47-48).

Doto anapigwa nusura afe kwa kukataa kusema ayajuayo kuhusu mauaji ya Kigogo. Katika hali ile ya kukata roho, anabebwa na kutupwa chumba alimo Hamza, na hapa ndipo Hamza anamwuguza. Masimulizi haya, kama yaliyotangulia, yanaeleza na kudhihirisha namna tukio lile linavyotendwa; kule kupigwa na kuteswa anakoteswa Doto. Wakati mwelekezi akielekeza utendaji wa tukio hili, azingatie masimulizi ya utendaji kama yanavyobainika katika mfano huu.

Hamza anatolewa nje ya chumba chao na Doto alfajiri kabla ya kiza kutoweka.

Yanayofuata yameelezwa na msimulizi katika masimulizi ya utendaji:

Mfano 4.4

Hamza aliongozwa mpaka chini ya mti mkubwa na hapo akakuta watu wanne wanamsubiri... “Mnanipeleka wapi?” Hakujibiwa lolote ila alipigwa kofi kubwa na kabla hata hakutulia vizuri kutoka katika zahama za lile kofi alilopigwa, alivamiwa, akashikwa mikono yote miwili, akafungwa kamba kwa nyuma. Alifungwa kitambaa usoni kikakazwa barabara akasukumwa kwa vishindo ndani ya gari. Gari liliondoka pale kwa kasi, likayumba huku na huku, baadaye likatulia katika mwendo wa kasi. Hamza alilisikiliza lile gari linavyonguruma, likipanda na kushuka vilima na mabonde. Alibanwa huku na huku, ametiwa katikati, hana nafasi hata ya kupumua...(uk. 64).

Kutokana na masimulizi haya ya utendaji, tunamwona Hamza akitolewa chumbani na kuandamana na watu asiowajua. Anapouliza anakopelekwa anapigwa na kufungwa kamba kisha anatupwa kwenye gari. Anafikishwa mahali ambapo baada ya gari lile kufika mwisho wa safari, anapigwa na kuteswa; mateso ambayo msimulizi anaeleza kwa taswira ya kifilamu, naye kama mwenzake Doto, anakiri kwamba atasema yote anayoyajua ili kujinusuru. Ni hapo anapotolewa kwenye kisima alikoning’inizwa, (uk. 65-64).

Baada ya Sururu kukamatwa akitoroka na kurudishwa kwa Ba Mkwe, siku tatu baadaye anaitwa na Meja Mapanga. Namna anavyohojiwa imeelezwa kwa masimulizi ya utendaji. Kwa mfano, anapopewa jalada ili atie sahihi, Sururu anauliza:

Mfano 4.5

“Ninaruhusiwa kusoma?”

“Usume nini na hayo maelezo ni yako mwenyewe! Usitupotezee wakati wetu sisi tuna kazi nyingine za kufanya!” Alisema kwa sauti ya juu Kifupinyundo.

“Soma,” Meja Mapanga alimruhusu

Sururu alilivuta lile jalada akalifungua...Sururu aliliinamia lile jalada akasoma neno moja moja. Wote wamekaa wanamtazama yeye

anavyosoma, ukurasa baada ya ukurasa. Ikapita nusu saa nzima. Kifupinyundo akashindwa kustahimili, “Sikiliza wewe! Sisi hatupo laibrari hapa, tukusubiri wewe usome mpaka umalize! Utatia saini au hutii saini?” Sururu alimtaazama. Uso umembadilika, jasho linamtoka kaliinamia jalada. Yaliyoandikwa mle yamemshitua. Yanamtokomezwa kabisa, “Sitii!” alijibu. Sururu ameliinamia jalada, anatikisa kichwa, jasho linamchirizika, “Haya yote mmeyatoa wapi?” aliuliza... “Nakuombeni msinitie katika ushahidi wa uongo.” Ushahidi wa uongo! Nani mwongo? Sisi waongo?” alipiga kelele Kifupinyundo na chumba kizima kikajaa sauti yake. “Utatia saini au hutii?” alimwuliza Sururu amemkazia vile vijicho vyake, uso ameukunja, “Unajua kama wewe kwanza ni mtoro, umetoroka, wewe ulistahili tukupige risasi kule kule ulikokamatwa, uchimbiwe shimo, ufukiwe, kama tulivyowafanya wenzako. Tumekuonea huruma tumekuleta hapa sasa unathubutu kutuita sisi waongo. “Mpumbavu we!” alisita, akamtazama, akawatazama na wenzake mmoja mmoja, akamgeukia tena Sururu, “Nakuuliza tena. Utatia saini au hutii?”... (uk. 132-133).

Msimulizi anaeleza kwa kina namna tukio hili linavyotendeka, kutoka Sururu anapoletwa waliko akina Kifupinyundo hadi anapokataa kutia saini kwenye jalada alilopewa. Hapo ndipo anapopigwa kinyama na kutupwa chumbani.

Mifano tuliyotoa ni baadhi tu ya matukio ambayo utendaji wake umewekwa wazi. Matukio haya yanasimuliwa namna yanavyotukia hivi kwamba utendaji wake kwenye jukwaa unakuwa rahisi.

4.1.2 Masimulizi ya Utendaji Kuhusu Usafiri

Wafungwa wanatolewa sehemu moja hadi nyingine wakipelekwa wanakoteswa. Uendeshaji wa magari unafanywa kwa njia isiyo ya kawaida kwa kuwa wanaosafirishwa sio watu wa kawaida, ni mahaini wanaostahili kifo kama Chopra anavyodai. Uendeshaji huu vilevile unafanywa kwa fujo, vishindo na vitisho huku utendaji wenyewe ukiwekwa wazi kupitia masimulizi ya utendaji. Tazama mfano ufuatao:

Mfano 4.6

...Pembeni liliegeshwa gari na alipokaribia gari hilo Hamza alisita...alifungiwa kitambaa usoni kikakazwa barabara akasukumwa kwa vishindo ndani ya gari. Gari liliondoka pale kwa kasi, likayumba huku na huku, baadaye likatulia katika mwendo wa kasi. Hamza alilisikiliza lile gari linavyonguruma, likipanda na kushuka vilima na mabonde...Gari limekolea mwendo, gia zinatiwa na kutolewa, Hamza hajui anakokwenda, amepoteza mwelekeo hajui mashariki wapi magharibi wapi. Kwa ghafla gari lilipunguza mwendo, dereva akachomeka gia kubwa, gari likanguruma mngurumo wa kunung'unika likapandisha kilima kikubwa...Mle ndani ya gari hamkuwa na chochote ila hofu tupu na jasho likimvuja mwili mzima, likayachokoza yale makovu yaliyomjaa mgongoni, yakamchonota kama aliyemwagiwa upupu...Gari likapiga breki, likasimama kwa ghafla. Waliomo ndani wakayumba kwa mtikiso mkali wa lile gari na kabla hata hawajatulia vyema kwa mtikiso ule, milango ilifunguliwa, Hamza akavutwa nje, ameshikwa huku na huku, mikono yake yote miwili bado imefungwa kwa nyuma...(uk. 64-65).

Katika mfano huu, Hamza anatolewa chumbani na anapelekwa mahali asipopajua na huko anateswa na kurudishwa chumbani asubuhi akiwa taabani. Uendeshaji wa magari na namna shughuli yote ya usafiri huu inafanywa ni ya fujo na vishindo kama inavyobainika. Katika utendaji wa riwaya hii, tukio hili litekelezwe kulingana na masimulizi haya ya utendaji.

Mfano 4.7

Tukio hili linatukia pale ambapo mashahidi wale tisa wanapelekwa mahakamani ili kushuhudia kwamba wao pamoja na wenzao wengine walihusika katika mauaji ya Kigogo. Mauaji ya Kigogo ni makosa ya kihaini, hivyo walipewa ulinzi uliostahili mahaini kama wao.

Hii sasa haikuwa safari bali ni msafara uliotimia. Land Rover ya mbele ina kimurumuri chekundu juu yake, kinametameta kuwatahadharisha walio mbele huku king'ora kilichonguruma njia nzima kupiga sumile, walio njiani wakae pembeni kuupisha msafara huo. Askari waliokuwemo ndani ya gari na mbele waliheuka nyuma kulenga bunduki zao mbele kwenye karadinga hilo hilo. Ulinzi hasa wanaostahili mahaini waliomwua Kigogo. Msafara uliingia mjini

kama umeme ukawafadhaisha watu majiani asubuhi ile wakaulizana, “Kumezidi nini?” Magari yanakwenda mbio kama yanayoendeshwa na wendawazimu, kimurimuri kinametameta, king’ora kimehanigiza, askari na bunduki mikononi, “Nini tena Toba ya Rabi?” Watu wanaulizana. Kila ulipopita msafara ule, walio ndani walitoka nje na wasioweza kutoka nje walichungulia madirishani kuona rabsha ile. Ulipopita Darajani, wauza mihogo na viazi waliopanga biashara zao pale marikiti waliacha biashara wakasimama pembeni, msafara ukawapita “vuup,” ukawacha vumbi tu nyuma yake...Askari walishuka kutoka katika yale magari yaliyowachukua kwa vishindo wakatawanyika kila mahala na kufunga njia inayopitia pale mahakamani, wa huku hendi kule na wa kule haji huku. Hali ilikuwa ya kutisha...(uk. 210-211).

Utendaji wa tukio hili utafanikiwa ikiwa mwelekezi wa utendaji kwenye jukwaa atazingatia masimulizi haya. Namna magari wanayosafiria mashahidi yanaendeshwa yanazua hofu sio kwa mashahidi wale tu bali kwa wote wanaoayaona. Yanatangaza hatari moja kwa moja kama ilivyoelezwa katika mfano 2 hapo juu. Hali ya hofu na taharuki ijengwe wakati wa utendaji. Hebu tutangulize kwa yanayothibitishwa kwa mfano huu wa tatu:

Mfano 4.8

...Ndani ya basi mlikuwa na askari sita wa kuzuia fujo, watatu nyuma na watatu mbele, kila mmoja na bunduki mkononi. Wakajaa [mahaini] ndani ya basi, msafara ukaanza. Ulikuwa msafara mrefu, uliotanguliwa na mapikipiki manane mbele. Mapikipiki yale yalifutwa na gari la aina la Land Rover lililokuwa na king’ora na kimurimuri chekundu, na gari hilo lililiza king’ora chake njia nzima huku kimurimuri chekundu kikimetameta. Magari sita yasiyokuwa na kipaa yalisheheni askari wa kuzuia fujo wote bunduki zao wamezilenga kule kwenye lile basi lililowachukua mahaini. Hayo yalikuwa mbele. Magari mengine sita yaliyosheheni askari vilevile, nao pia bunduki zao wamezilenga kwenye lile basi, yalikuwa nyuma. Vyombo vyote viliwasha taa kuashiria hali ya hatari. Njiani kulikuwa hakuna hata mdudu wa mtu na mwendo wa msafara ule ulikuwa wa kasi sana. Ulipita uwanja wa gofu ukatokeza Mivinjeni, gari zinakwenda marshi marshi utadhani wanakimbilia mwisho wa dunia. Walipita V.I.Lenin Hospital kwa kishindo na walio hospitali wakabaki wakiulizana, “Kumezidi nini?”(uk. 229).

Katika mfano huu, kama walivyosafirishwa wale mashahidi, mahaini wamekwekwa chini ya ulinzi mkali, magari yanaendeshwa kwa kasi bila kujali, na msafara wote ule

wa magari unatangaza hatari tupu. Utendaji wa shughuli yote hii unajibainisha. Safari hii inarudiwa kila wakati mahaini hawa wanapopelekwa mahakamani kutoka kwa Ba Mkwe hadi kesi inapokamilika na hukumu kutolewa. Hivyo, ni muhimu ikiwa mwelelekezi wa utendaji wa kidrama wa tukio hili atahakikisha kwamba hali tunayopatana nayo katika riwaya imewasilishwa ipasavyo kwenye jukwaa.

Bacon (1984) anaeleza kuwa sanaa ya utendaji hutilia mkazo kwenye vitendo ama uigizaji. Kufikia hapa, tunaona namna masimulizi ya utendaji yanavyobainika katika riwaya ya *Haini*, ithibati kwamba msimulizi ametilia mkazo matendo na utekelezaji wake. Hii ni kwa sababu anachukua muda mwingi kuweka wazi namna kila tukio linavyotokea na matendo ya wahusika yanavyofaa kutekelezwa. Aidha, masimulizi haya ya utendaji yanaweka wazi tukio linatendwa wapi na lini. Hali hii itarahisisha utendaji wa kidrama wa riwaya ya *Haini* ikiwa itaigizwa kwenye jukwaa.

4.1.3 Masimulizi ya Utendaji Mahakamani

Masimulizi haya yanahusu namna kesi ya uhaini inaendeshwa. Kesi hii inaanza na tunasimuliwa wazi wazi namna inavyoendeshwa. Wahusika wake; mahakimu, karani wa mahakama, mwendeshaji mashtaka, washtakiwa na mashahidi wanadhihirisha utendaji kwa njia moja au nyingine kutoka mwanzo hadi kesi inapokamilika na mahakimu kutoa hukumu:

Mfano 4.9

Chopra, mwendesha mashtaka wa serikali aliingia peke yake, amebeba majalada kwapani akakaa juu ya kiti kilichokuwa karibu na kizimba...(uk. 230).

Saa nne juu ya alama karani wa mahakama akainga, naye amebeba furushi la makaratasi kwapani. Aliingia kwa kupitia mlango wa kule jukwaani na baada ya kukaa juu ya kiti chake, pembeni mwa ile meza kubwa, hakutaka kumwanganalia mtu yeyote ila alishughulika kupekuapekua makaratasi yaliyokuwa mbele yake...(uk. 231)

Kimya kilichokuwemo ndani ya ukumbi wa mahakama kilipotea kidogo pale askari wawili walipoingia na kuwafungua pingu washtakiwa. Kimya kikarudi upya pale kwenye ukumbi wa mahakama mpaka pale mahakimu watatu walipoingia kwa kupitia mlango wa kule liliko jukwaa. Wote waliokuwemo ndani ya ukumbi wa mahakama wakasimama kuwapa mahakimu heshima yao. Wote watatu wakakaa juu ya vile viti vikubwa...(uk. 232).

Washikadau wa mahakama wanavyoingia mahakamani kiutendaji ni jambo lililowekwa wazi. Wanaonekana waziwazi namna kila mmoja wao anaingia na kukaa mahali pake kabla ya kesi ile kuanza rasmi. Tukio hili linapotendwa kwenye jukwaa, watendaji watakaochukua nafasi za wahusika hawa waingie kwenye jukwaa kama inavyosimuliwa.

Mfano 4.10

Chopra akasimama, akakaza tai yake shingoni, akatazama huku na huku. Kwanza aliwatazama washtakiwa kwa jicho la kuwakejeli, halafu akageuka na kuwatazama mahakimu, akasema, “Waheshimiwa mahakimu. nimewasilisha mbele ya mahakama yenu tukufu mashahidi hamsini na nne kama nilivyoahidi. Nimewasilisha mbele ya mahakama yenu tukufu vithibitisho vyote vilivyotakiwa kuwasilisha mbele ya mahakama hii.” Chopra alisita akakohoa kidogo, akaomba radhi baada ya kukohoa, “*Excuse me!*” Akaendelea na maelezo yake. Wote ndani ya mahakama ile wanamsikiliza yeye, “Leo waheshimiwa mahakimu nataka kuwasilisha mbele ya mahakama yenu tukufu, maelezo ya washtakiwa yaliyotolewa na washtakiwa wenyewe, kwa hiari yao...(uk. 241).

Washtakiwa walipanda na kushuka kizimbani na Chopra akiwaandama kwa maswali makali makali, kila mshtakiwa akieleza jinsi alivyoteswa na kudhalilishwa, na wale waliokubali kama walishiriki katika mpango wa uhaini wakaeleza jinsi walivyoteswa mpaka wakakubali mambo ya uongo na kuwataja watu ambao hawajui lolote juu yao...Chopra mara huwa mkali mara hushuka matao ya chini akaongea kwa upole. Huwababaisha na kuwazungusha washtakiwa kwa maswali yake na washtakiwa nao huwa makini wanapomjibu...(uk. 250).

Baada ya wahusika wote kuchukua nafasi zao, Chopra, ambaye ndiye mtendaji mkuu katika uendeshaji wa kesi hii anaianza rasmi kesi yenyewe. Msimulizi anaeleza

namna anatenda katika kusoma maelezo ya ile kesi, kuwahoji mashahidi na mahaini na hatimaye anapotoa maelezo yake ya mwisho kuhusu kesi hii.

Baada ya kuwahoji washtakiwa na kuwaongoza mashahidi katika kutoa ushahidi wao, Chopra anatekeleza jukumu lake la mwisho; kutoa maelezo ya jumla na kauli yake kuhusu kesi ile. Anatekeleza hili kwa njia iliyojaa utendaji, bila haraka yoyote ile, anawaomba mahakimu kuwatosha washtakiwa wale baharini wakafie humo kwa kosa la kihaini walilofanya na hatimaye anakaa, (uk. 260-262). Uamuzi anawaachia mahakimu.

Mfano 4.11

Chopra anapomaliza kutoa maelezo yake mahakimu wanachukua hatamu. Wao ndio wenye mamlaka na wajibu wa kuwahukumu washtakiwa wale kwa mujibu wa maelezo yaliyotolewa, ushahidi na kujitetea kwao wenyewe. Kiongozi wa wale mahakimu, Musadiq, ndiye anatenda kwa niaba ya wenzake Pandu na Jongo:

Musadiq alitoa karatasi kutoka katika mfuko wa ndani wa koti lake akaiinamia akiisoma kwa makini. Wote waliokuwemo ndani ya ukumbi wa mahakama wametulia kimya, saa ambayo kila mtu akiisubiri kwa muda wa miaka miwili sasa, imefika. Na washtakiwa pia wametumbua macho wanaitazama ile karatasi wanajua kwamba mle ndimo yalimo majaaliwa yao na kila mmoja wao sasa hivi atajua kama ni wa duniani au wa ahera. “Tumezingatia kwa makini sana ushahidi wote uliowasilishwa na upande wa mashtaka,” Musadiq alianza kutoa hukumu. Macho yake yote yapo kwenye ile karatasi.

Hataki kumwangukia mtu. Labda akifuata ule usia wa, “Ukitaka kumwua ngedere usimtazame usoni.” “Tumezingatia kwa makini ushahidi wa shahidi mmoja mmoja pamoja na maelezo yote yaliyotolewa na upande wa mashtaka. “Kadhalika, tumezingatia kwa makini maelezo yote ya washtakiwa yaliyosomwa mbele ya mahakama hii, tukitilia sana maamani maelezo ya washtakiwa wenyewe pale walipokuja kujitetea.” Alipofika hapo Musadiq alinyanyua uso akawatazama washtakiwa. Akaendelea. “Baada ya kuzingatia yote hayo tumeamini kabisa kwamba kweli ulikuwepo mpango wa kutaka kuipindua serikali, mpango ambao baada ya

kushindwa ulisababisha mauaji ya Mheshimiwa Kigogo.” (uk. 262-263).

Utendaji katika tukio hili unaingiliana. Ule wa Musadiq unatukia kwa wakati mmoja na ule wa washtakiwa:

“A-a-a-a-a!” washtakiwa wote walilalamika kwa pamoja. Musadiq akawatazama mpaka walipomaliza kulalamika, akaendelea. “ Kwa hivyo mahakama imeridhika kwamba mna hatia na inahukumuni nyote adhabu ya kifo isi...”

“Dhuluma! Dhuluma! Mnatudhulumu!” walipiga kelele washtakiwa wote kabla Musadiq hakumaliza hukumu yake. Mahakamani pale pakazuka zogo mpaka askari wa kuzuia fujo ikawabidi waje wasimame mlangoni ili kuchukua hadhari washtakiwa wasije wakamduru mtu. “Mungu atatuhukumia!” waliendelea kupiga kelele...(uk. 263).

Hii ndiyo hali inayojitokeza katika utendaji mahakamani. Kwa mfano, Chopra anapopendekeza kwamba washtakiwa watoswe baharini kutoka kwa helikopta wafie humo, na anapoendelea na maelezo yake, (uk. 248-262), washtakiwa wanaingilia kati, kulalamika au kupiga kelele. Musadiq anapochukua hatamu, washtakiwa wanafanya vivyo hivyo hadi pale hukumu inapotolewa, (uk. 263-265).

Utendaji unaotukia mahakamani hivyo unawashirikisha wahusika wote waliomo. Wanaingiliana na kupokezana zamu hivi kwamba tunapata picha kamili ya namna kesi ile ilivyoendeshwa. Kwa kiasi kikubwa, kesi hii inafanywa kama inavyotendeka katika hali halisi. Wahusika wote wanatenda wanavyotarajiwa kutenda, karani wa mahakama anavyowaapisha mashahidi na washtakiwa, (uk. 247-248), Chopra anavyoiendesha ile kesi, mahakimu, mashahidi na washtakiwa wanavyotoa maelezo yao na vilevile maafisa wa usalama wanavyoingilia kati wakati zogo likizidi pale mahakamani. Wanakamilishana na kufanikisha utendaji huu.

4.1.4 Masimulizi ya Utendaji wa Kifaraja

Japo matukio mengi katika riwaya ya *Haini* ni ya huzuni na simanzi, wahusika wametafuta namna ya kujifurahisha, wakapata raha pasipo na raha. Msimulizi ameeleza utendaji wa baadhi ya matukio haya kama inavyobainika katika mifano ifuatayo:

Mfano 4.12

Hamza akakaa juu ya ile sakafu iliyoanza kupata joto la jua. Akakabiliana na Mzee Machale uso kwa uso. Mzee Machale alichukua kile kipande cha sigareti alichokuwa akikivuta. Kimejaa mate kule nchani, amekikamata kwa ncha za vidole, “Shika.” Hamza alikipokea kile kipande cha sigareti kwa wasiwasi. Akamtazama Mzee Machale, akakipachika mdomoni taratibu. akaikupua mkupuo mdogo, akaupuliza moshi taratibu kupitia mdomoni. Ilikuwa sigareti kali na alizisikia nishai zake kwa mbali. Alivuta mkupuo mwingine na mara hii akaikupua barabara, akayajaza mapafu yake moshi tele halafu akaupuliza kwa nguvu kutokea puani. Siku nyingi zimeshapita Hamza hakuvuta sigareti, hata funda moja la moshi. Alivyoikupua ile sigareti kwa pupa alijihisi kama aliye katika zilizala, dunia yote inazunguka inataka kumwelemea. Hamza ameshavuta tumbaku na tumbaku. Hata buruma nalo amekwishalikupua lakini hakuwahi kupata nishai kama hizi alizozipata leo...sigareti ile ilimlevya Hamza akawa yuko chopi, kama aliyemaliza chupa nzima ya viski. Alijivuta nyuma taratibu mpaka pale ulipo ule ukuta, akaegemea ukutani na kipande chake cha sigareti mkononi. Alidorora kwa muda mpaka kile kizunguzungu kilipoanza kufifia, akaiona dunia ikikaa sawa pole pole. Sasa aliivuta ile sigareti kwa hadhari na kutoa moshi taratibu...(uk. 54-55).

Katika mfano huu, Hamza ametolewa nje na Mzee Machale na wawili hawa wanavuta sigara. Uvutaji huu wa sigara huwa kitulizo cha nafsi cha Mzee Machale. Hamza, ambaye kabla ya kukamatwa alikuwa mvutaji mashuhuri wa sigara anakaribishwa na Mzee Machale na wawili hawa wanavuta huku wakiongea. Namna uvutaji huu unatekelezwa, pamoja na athari zake umesimuliwa hivi kwamba utendaji unadhihirika waziwazi, kama kwamba unatekelezwa kwenye jukwaa.

Mfano 4.13

Wahusika wanafarijika kupitia ndoto wanazoota wakiwa vyumbani. Katika ndoto hizi, wahusika hawa wanatenda mambo ambayo wangetenda wangukuwa huru, wanafurahia nyumbani na shughuli za maisha yao nje ya gereza. Katika ndoto hizi, utendaji unajidhihirisha kama msimulizi anavyosimulia. Mojawapo ya ndoto hizi ni ile anayoiota Hamza akiwa pale gerezeni. Kila kinachoendelea katika ndoto hiyo kinaweza kutendwa kwenye jukwaa. Utendaji wake ni dhahiri, kama walivyo wahusika katika dondoo hili:

Usingizi ulimchukua nao ukamtoa nje ya lile gereza ukampeleka kwake moja kwa moja. Huko kwake akajihisi amejinyosha kitandani, amezama ndani ya godoro la danlopilo, kiunoni amejifunga kanga safi bado inanukia udi uliofukizwa jana. Sigareti ameipachika mdomoni anaikupua taratibu, moshi akiupuliza kwa maringo. Pankaboi lilikuwa linapepea kutoka katika pembe ya kile chumba na upepo wake uliukorogakoroga ule moshi ukatokea dirishani. Chumba kilijaa harufu ya kiwanda alichokuwa akikikaanga Khadija kule jikoni, ameshughulika kumtayarishia mumewe chai. Mtoto alikuwa akilia,

“Ng’aa! Ng’aa!” Kelele zimehanigiza nyumba nzima.

“Eh! Mtoto kilizi huyu! Sijapata kuona! Alilalamika Khadija. “Mpe ziwa anyonye, labda ana njaa,” Hamza aliamrisha, amestarehe na sigareti yake mdomoni.

“Hana njaa chochote, sasa hivi nimemnyonyesha,” alisema Khadija.

“Basi tu, mtoto mwenyewe kilizi,” aliendelea.

“Mbebe basi.”

“Ntambebaje na mimi nna kazi mkononi? Njoo umbebe wewe, umekaa tu huko, kazi kutoa amri.”

Khadija alimbeba mtoto akampeleka chumbani akamweka chini ya ubavu wa baba yake, “Huyo hapo mwanao. Mbembeleze.”

Hamza alimchukua, akamvinyavinya na kumrusharusha, akamlaza juu ya kifua chake akicheka naye, “Chu-chuu-chu-chuuu!”

Kitoto kilitabasamu, vijino viwili vimechomoza juu ya ufizi wake wa chini. Hamza alimnyanyua, akamrusha juu, akamudaka, akamwimbia.

“Pole mwanangu nyamaza Ukilia waniliza, hoya Wanikumbusha ukiwa. Hoya...”

Khadija alikuwa ameegemea mlangoni, amefurahi, anamwangalia mumewe vile anavyobahashuka na mwanawe, “Kumbe na wewe unajua kubembeleza mtoto enhe? Aliuliza.

Hamza alishtuka. Hakujua kama Khadija alikuwa akimwangalia, “Njoo umchukue.”

“Hebu kaa naye kidogo mwanao. Huoni alivyofurahi.”

Khadija naye alikwenda akakaa ubavuni mwa Hamza. Pale Hamza akajiona ametimia, yuko kamili...Hamza alimvuta karibu naye akitaka kumbusu midomo yake. Mlango ukafunguliwa kwa kishindo, “Vaa nguo zako.” (uk. 97)

Kwenye jukwaa, utendaji wa tukio hili pamoja na matukio mengine yanayohusu ndoto unaweza kurekodiwa na wakati wa utendaji wa mchezo wa kuigiza, tukio hili likachezwa na kuonyeshwa kwenye projekta. Utendaji huu ufanywe kama msimulizi anavyosimulia. Hii itaarifu hadhira kwamba matukio haya hayatukii katika hali halisi au kwenye jukwaa haswa bali mtendaji aliye kwenye jukwaa ndiye anayeota yale wanayoyatazama. Ni muhimu ikiwa hadhira itaelewa yanayoendelea kwenye jukwaa. Haya ndiyo Schechner (1985) anayofafanua anaposema kwamba nguvu ya utendaji imo katika uhusiano mahsusi kati ya watendaji na ambao kwao, utendaji huo unatekelezwa.

Katika mfano wa tatu ufuatao, wafungwa wapo katika hali ya kutamauka, wameshapelekwa kule kwa Ba Mkwewe. Hawajui yatakayojiri. Wamejikunyata kama wagonjwa, hakuna anayesema na mwenzake. Katika hali hii, Hamza na Faraji wanajipata kimawazo katika mazungumzo ya kujifurahisha. Wanayakumbuka maisha yao kabla ya kukamatwa na kuselelea gerezani kwa zaidi ya mwaka mzima sasa. Katika kumbukumbu yao hii, wanasahau kwa muda mateso yanayowakabili na mengine yanayowasubiri. Wanaondoa hofu na kujipa raha. Mazungumzo yao haya yamejaa utendaji hasa unaoweka wazi namna walivyokuwa wakitengeneza ile *Martini* kama unavyodhihirika katika dondoo hili:

Mfano 4.14

“Unaonaje ubaridi kama huu ukapata chupa ya wiski?” Hamza alimtania Faraji. Anamjua vyema jinsi anavyopenda pombe.

“Ya nini wiski. Hata chupa ya tende inatosha.”

“Tena tende yenyewe uitengeneze ule mkorogo nilioutengeneza siku ile nyumbani. Unakumbuka?” Hamza alimkumbusha Faraji zile hafla zao za manywaji zisizokwisha, siku zile wenyewe walizoziita za uhuru. Pale wote wawili walipokuwa wajane.

“Unachukua chupa yako ya tende unaitia ndani ya dishi, unaichanganya na divai, tena divai yenyewe iwe Martini. Unachanganya na maji ya madafu, kiasi ya madafu mawili hivi. Unaikatiakatia machungwa, tena usiyamenye, hivyo hivyo na maganda yake ili kukata ile harufu ya tende. Ukipata na nanasi kidogo mambo yanakuwa mazuri zaidi. Halafu unajaza mapande ya barafu.” “Hiyo inaitwa Punch, tena nishai zake hupanda taratibu, hazina haraka,” alisema Faraji.

Khafani alikuwa amekaa pembeni anawasikiliza vile walivyokuwa wakikumbushana zama zao za starehe, akatabasamu.

“Lakini zikikaa kichwani zimekaa,” aliongeza Hamza. “Asubuhi ukiamka lazima unaamka nazo.”... (uk. 110-111).

Masimulizi ya utendaji yanatubainishia namna wahusika wanatenda uhusika waliopewa. Wahusika katika riwaya hii wanatekeleza utendaji wao kwa njia ya kuaminika na hadhira. Kutokana na masimulizi ya utendaji, msomaji anapata picha ya namna wahusika wanatenda kama ambao wapo kwenye jukwaa, wanavyoingia na kutoka kwenye jukwaa, wanavyodhihirisha hisia kupitia kauli zao, na ishara za uso, na vilevile wanavyopokezana zamu. Mwandishi amefanikiwa katika masimulizi ya utendaji, ambamo nguvu ya utendaji imesimikwa.

4.2 Vimulimuli Na Kiza

Kiza na vimulimuli hutumiwa katika utendaji kuleta athari kadhaa ambazo tumejadili kwa kina. Mwandishi wa riwaya ya *Haini* ametumia vipengele hivi viwili kufanikisha utendaji wa kidrama wa riwaya hii kama inavyodhihirika katika mifano ifuatayo:

4.2.1 Vimulimuli

Vimulimuli ni aina ya uangazaji uaotumiwa katika utendaji, hasa kwenye kumbi za maonyesho. Wakati vimulimuli vikitumika katika utendaji, mwangaza unaweza

kuongezwa au kupunguzwa kwa mfano ili kuashiria kipindi cha mchana wakati jua likiwa kali au kupunguzwa ili kuashiria wakati wa jioni jua likichwea.

Rangi ya mwangaza inaweza kubadilishwa kutegemea hali na mandhari yanayohitajika. Kwa mujibu wa Goldfarb na Wilson (2002) vimulimuli hutumiwa katika utendaji kwa sababu zifuatazo: Kwanza, huwezesha kuona. Vimulimuli huwezesha watendaji kuonana kwenye jukwaa na vilevile hadhira kuona kinachotendwa kwenye jukwaa. Mwangaza huwezesha maingiliano baina ya wahusika pamoja na kuyafanya mandhari yaonekane.

Pili, vimulimuli hutumiwa ili kubainisha mahali na wakati. Rangi ya mwangaza, aina na wingi au uchache wake huweza kubainisha ni wakati gani wa siku. Kwa mfano kuongezeka kwa mwangaza huashiria wakati wa mchana huku kiza au kutokuwepo kwa mwangaza kukiashiria kwamba tukio linatendeka usiku. Kwa kutumia vimulimuli, mahali huweza kujulikano iwapo kwa mfano tukio linalorejelewa linatokea nje au ndani mwa jengo.

Tatu, vimulimuli hutumiwa kuleta hali fulani. Vimulimuli vikitumika pamoja na mandhari husika, na maleba huwezesha kubainisha au kuleta hali fulani katika utendaji. Kwa mfano, mandhari, maleba na vipengele vingine vya utendaji vinapotumika huleta hali ya huzuni, kutisha, hofu au wasiwasi kutegemea kazi husika ya drama.

Vimulimuli hutumiwa kusesitiza utendaji. Mwangaza unaweza kuelekezwa katika sehemu maalum ya jukwaa ili kusesitiza tendo moja na kulipa umuhimu zaidi ya lingine. Hapa, tendo muhimu kuliko lingine ndilo husisitizwa, hasa ikiwa kuna matendo zaidi ya moja kwenye jukwaa yanayotokea kwa wakati mmoja.

Katika utafiti huu, tumeainisha vimulimuli na kiza kwa mujibu wa majukumu yake katika utendaji wa matukio ambamo vimulimuli na kiza vinatumika. Katika riwaya ya *Haini*, vimulimuli vinatumiwa kutekeleza majukumu mbalimbali kama vile:

a) Kuwezesha kuona

Kama ambavyo mwangaza ulitumika zamani katika sanaa za maonyesho ili kuwezesha kuona, drama za kisasa hutumia mwangaza kuwawezesha watendaji kuonana wakati wakitenda kwenye jukwaa. Shafi Adam amedhihirisha matumizi haya ya mwangaza katika riwaya yake ya *Haini*. Tutazame mifano hii:

Mzee Machale akawamurika kwa kurunzi usoni mmoja mmoja, akifyonya na kutukana, “Wapumbavu! Wajinga! Akafunga mlango kwa nguvu akaondoka... (uk. 175).

Tukio hili linatendeka baada ya Haramia kurudishwa kwa Ba Mkwewe baada ya kutolewa kule *Mashakani Hotel*. Kutokana na kule kuwekwa katika chumba kimoja na chatu, hofu imemjaa na alipo anaota na kupiga kelele kwamba mna nyoka mle chumbani. Wenzake wanamwunga mkono na kumsababisha Mzee Machale kwenda waliko. Anamulika kwa ile kurunzi yake na nyoka huyo anapokosekana anawamulika wote usoni, kuwatukana na kuondoka.

Usiku pale Forodhani, Khadija na Azizi wamekaa wakiitazama bahari. Japo ni usiku, wanawezeshwa kuona na mwangaza wa mwezi uliopo usiku ule. Tunasimuliwa kwamba:

Hakuna anayesema kitu, wote wanaiangalia bahari, imetanda mbele yao mpaka kule kwenye upeo wa macho ambako nuru ya mwezi inamulika kwa nguvu zake zote, mwanga wake umechora mstari mkali baina ya mbingu na bahari, unameremeta kama fedha...(uk. 188).

Katika utendaji kwenye jukwaa, hasa ikiwa utendaji unatukia mchana, tukio hili linaweza kuashiriwa kupitia mchoro wa mwezi huku mwangaza wake umechora mstari baina ya mbingu na bahari. Utendaji ukitukia usiku, hali hii inaweza kuwasilishwa kupitia vyombo vya kiteknolojia. Kwa mfano, chombo cha kuangazia chenye umbo la mwezi kinaweza kutumiwa kuangazia jukwaa.

Khadija na Azizi wanaondoka na kwenda chumba cha Azizi cha kupokea wageni. Chumba chenye kabla hawajafika kilikuwa na kiza, hadi Azizi anapobonyeza swichi. msimulizi anaeleza kwamba:

Mwanga wa taa ya chumbani ukajaa chumba kizima na kufufurika, mwingine ukamwagika huku nje ukakipunguza kidogo kiza cha pale nje. Azizi alimkaribisha Khadija chumbani...Baada ya kufika ndani, Azizi alifunga mlango, Khadija kasimama amepigwa na mshangao anakiangalia kile chumba. Chumba ni kikubwa, mwanga wa taa ni mkali, kinang'ara, kuta zinameremeta...(uk. 189).

Ni baada ya Azizi kuwasha taa ya chumba chake ndipo Khadija anaweza kuona vilivyomo. Wawili hawa vilevile wanapata uwezo wa kuonana wakiwa mle ndani. Chumbani walimo mashahidi ni kiza tupu, na asubuhi inapoingia na kufukuza kiza kizito kinachotawala kila usiku wanaweza kuonana na hata kuendelea na michezo yao ile waliyopewa kwa kukubali kutoa ushahidi, (uk. 205).

Haramia anapopelekwa kule *Mashakani Hotel*, anafungiwa kwenye chumba chenye taa inayotoa mwanga hafifu na ambayo huwaka kutwa kucha. Kama tunavyosimuliwa, hoteli ile ilikuwa imezungukwa na msitu mkubwa na kutawaliwa na kiza. Hivyo, taa ile iliwekwa pale kuwezesha kuona pamoja na kumfanya aliye ndani kutojua majira ya siku; hali haibadiliki na mtu hawezi kujua ikiwa ni mchana au usiku, (uk. 169).

b) Kuleta tumaini

Vimulimuli, mbali na kuwawezesha wahusika kuonana wakati wa utendaji, vimetumiwa kuwapa wahusika waliokata tamaa tumaini. Matukio mengi katika riwaya hii yanatukia gerezani, hivyo yametawaliwa na mateso na mambo ya kukatisha tamaa. Vimulimuli vinatumika kuashiria tumaini hata pale pasipo na tumaini lolote.

Koplo Fataki anapowatoa wafungwa nje wakaoge na kukatana nywele, anawaambia kwamba wasiwe na wasiwasi kwa kuwa watatoka gerezani wote. Msimulizi anaeleza:

[Koplo Fataki] Alikwenda zake akawaacha wakifurahia siku ile iliyojaa nuru ya jua na matumaini tele. Ya ngapi leo hawajaiona nje? Siyo ile nje ya mtu kwenda na kurudi apendavyo, la! Ile nje ya chumba tu, wakaliona jua wakafurahi nalo. Siku ile walikoga wakatakata. Wakakatana nywele, kila mmoja mtindo aupendao na wengi wakanyoa kipara. Wakafua, wakaota jua, wakatamani jua lile lisitue, libaki pale pale mpaka litakapowakifu...(uk. 35).

Katika dondoo hili, jua limetumiwa kama ishara ya tumaini. Kwa mara ya kwanza tangu walipokamatwa, tunawaona wafungwa hawa wakiwa na furaha japo wamezungukwa na dhiki. Ule mwangaza wa jua ambalo hawajalionga kwa siku nyingi unawachamngamsha na kuwarejeshea tumaini lililokuwa limeanza kufifia.

Wafungwa hawa wanatolewa kule Kumbakumba na kupelekwa kwa Ba Mkwe. Wanapofika nje ya lango la gereza, msimulizi anaeleza kwamba, ‘nuru ya jua ilimwagika usoni kwa ghafula, mboni za macho yao zikafunga kwa haraka kwa kutozowea mwanga mkali kama ule kwa muda mrefu, wakatamani kusimama pale waote joto la lile jua baada ya kuvumbikwa chumbani kwa siku zote zile.’ (uk. 195). Japo hawajui yanayowakabili waendako, lile jua linawachangamsha kiasi cha kutamani waruhusiwe wakae pale kwa muda zaidi.

Sururu anapoporomokea upande wa nje wa ukuta wa gereza, anatorokea msituni. Ameumia mikono, miguu, na tumbo, damu inamtoka yuko taabani. Wakati akitafuta pa kwenda bila tumaini, anaona mwangaza kwa mbali na kuelekea mwangaza huo unakotoka. Msimulizi anasimulia:

Kwa mbali akaona mwangaza hafifu, akahisi pale lazima pana uhai, na hapakosi kiumbe mwenye huruma atakayemuafu maisha yake. Alijiburura hivyo hivyo, akapenyapenya vichakani kuufuata ule mwanga lakini kila alipoufuata aliuona kama unamkimbia, uko kulee, hafiki asilani...ule mwanga aliokuwa akiuona kwa mbali akadhani unamkimbia ulikuwa unakuja karibu naye taratibu, taratibu kama vile alivyokuwa akijikongoja, akichechemea, chehegu chehegu mguu umevimba unamwuma maumivu makali...(uk. 124).

Mwangaza huu unampa Sururu tumaini la kupatana na binadamu mwenzake akamsaidia kuuguza yale maumivu yake.

c) **Kuashiria hatari**

Vimulimuli vimetumika katika riwaya hii kuashiria hali ya hatari. Japo katika matukio machache sana, mwandishi amefanikiwa kuashiria hatari miongoni mwa wahusika na watazamaji. Wafungwa waliobaki kwa Ba Mkwe, ambao pia wanahusishwa moja kwa moja na kesi ya uhaini wanapelekwa mahakamani kwa msafara wa magari. msimulizi anaeleza kwamba ulikuwa msafara mrefu uliotanguliwa na pikipiki nane, hizi zikafuatwa na gari aina ya 'Land Rover' lililokuwa na king'ora na kimurimuri chekundu ambacho kilimetameta njia nzima. Hili lilifuatwa na magari mengine sita.

Magari haya yote pamoja na pikipiki hizo yaliwasha taa kutoa ishara ya hatari. Kutokana na hili, watu waliouona msafara huu walijawa na hofu, wakabaki kuulizana tatizo lilipokuwa, (uk. 229 na 246).

4.2.2 Kiza

Malas (2012) anadai kwamba:

Kiza kinapotumika kwenye jukwaa hutawala mahali pote ambapo kila kitu humezwa na kiza hicho na humwezesha mwigizaji kutagusana na nafsi yake mwenyewe, na waigizaji wengine au kutagusana na matukio ya mchezo wa kuigiza katika ngazi zake mbalimbali, hivyo kuvuka mipaka ya mahali na wakati... Kiza kinatumika katika maingiliano kati ya wahusika kimatendo, kifikra na kimawazo, na hili huwezesha athari za kisaikolojia kuwepo katika tamthilia husika kama alivyokusudia mwandishi. (T.Y)

Kiza, kama inavyobainika katika maelezo ya mtaalam huyu kinatumika kama kipengele cha kidrama ambacho huathiri ploti, ujenzi wa wahusika na hivyo kuchangia pakubwa katika kujenga hali mbalimbali katika utendaji.

Katika utendaji, aghalabu matukio maovu hutukia usiku au kwenye sehemu yenye kiza. Mathalan, kiza hutumiwa wakati mhusika akitekeleza mauaji, au kumtesa mwengine. Vilevile, mwandishi wa kazi ya kidrama anaweza kutumia kiza katika kazi yake kuibua woga. Katika riwaya ya *Haini*, kiza kimetumiwa kiutendaji ili kubainisha wakati, kuashiria mateso na uovu na kuonyesha kutamauka.

(a) Kubainisha Wakati

Kiza kimetumiwa katika riwaya ya *Haini* ili kubainisha au kutobainisha wakati. Kiza kimetumiwa kubainisha matukio yanatendeka wakati fulani wa siku. Hata hivyo, baadhi ya matukio hayatambuliki yanatendeka wakati gani kutokana na kiza kuwepo wakati wote. Hali hii inaifanya hadhira kutojua ni wakati gani wa siku tukio hilo mahsusi linatendeka. Kiza kimetumika katika riwaya hii kubainisha wakati katika matukio yanayosimuliwa katika mifano ifuatayo:

Haukupita muda mrefu, mnamo saa za magharibi, mwanga umetoweka na kiza hafifu kuingia chumbani mle, wakati kunguni walikuwa wameanza kutoka katika maficho yao na mbu wanavuma,

wote wanajitayarisha kwa karamu yao ya usiku kucha, mlango ulifunguliwa kwa kishindo...(uk. 15).

Tukio hili linatokea chumbani alimopelekwa Hamza punde baada ya kukamatwa. Baada ya kukaa mle peke yake, Abdul akaletwa na wakati huu wa magharibi ndipo Shadidi anapoletwa. Tunafahamu kwamba aliletwa wakati wa jioni kwa kuwa maelezo yanasema kwamba ‘kiza hafifu kinaingia na mwanga kutoweka taratibu.’

Kama aliyepandwa na pepo halafu akamtoka kichwani, ndivyo alivyokuwa Hamza pale alipokaa. Akabakia vilevile kuiangalia siku inavyopotea, nuru ya mchana ikififia na kiza kikiingia mpaka kikajaa tele chumbani. Na sasa chumba kile kikawa kaburi hasa, labda aliyekosekana katika kaburi ile ni Munkar na Nakir kumhoji maiti, mema na mabaya yake...(uk. 43).

Wakati wa tukio hili umebainishwa na kuwepo kwa kiza. Tunafahamu kwamba tukio hili linatendeka usiku. Katika utendaji wake kwenye jukwaa, taa zinaweza kuwashwa na mwangaza kuwa mwingi ili kuashiria ni mchana, halafu mwangaza huo ukafifia polepole hadi kuwepo kwa kiza ili kuashiria usiku unavyoingia hadi kuwa usiku mpevu.

Tazama mfano huu vilevile:

Lile jua lililowatesa mchana kutwa pale uwanjani limezama, limekuchwa na kupotea na nuru yake, huku nyuma likikiwacha kiza nacho kikijitawanya na kutapakaa kila pahala. Kiza kikawameza walio vyumbani, hawaonani. Wenyeji wa mle vyumbani wakawakaribisha wageni wao kutoka Kumbakumba katika hali ile ya kiza kilichostadi...(uk. 196).

Tukio hili linatokea wakati wa usiku mchanga, punde baada ya kuchwea kwa jua na kiza kuingia. Wanaopatana katika chumba kimoja, kwa kuwa hawaonani, wanalazimika kujitambulisha kwa sauti. Kesho yake asubuhi kiza kinapotoweka na mwangaza kuingia ndipo wanapoonana. Katika utendaji wa tukio hili, kiza kinaweza

kutumiwa kwa kuzima taa kisha taa zikawashwa kwa mwangaza hafifu na kuuongeza hadi mwangaza mkali uwake kwenye jukwaa. Mabadiliko haya yataashiria kwamba kulikuwa usiku lakini kumekucha.

Tazama mfano huu mwingine:

Kiza cha usiku ule kilikifunika kila kitu, kimezagaa kila pahala na mle chumbani wamezama ndi, ndani ya kiza hicho, hawaonani. Hakuna aliyelala, usingizi umewaruka, kila mmoja anawaza lake. Chumbani kimya, sauti za mbu tu ndizo zilikuwa zikisikika wakivuma kutafuta watu wawanyonye damu. Zarikani amelala chali, ametumbua macho lakini hakuna chochote anachokiona ila kiza tu, kimezunguka kila pembe...(uk. 204).

Kisa hiki kinatendeka waliko mashahidi wale tisa, Haramia na wenzake. Wote wana hofu. Ni usiku huu, katika kiza hiki ndipo wanapojadili na kusafiana nia. Wote isipokuwa Pwacha wana kauli moja, na asubuhi inapoingia msimulizi anasema:

Usiku ulipomalizika asubuhi ikaingia, chumba chao kilikuwa kama bahari iliyokuwa imechafuka kwa mawimbi na dharuba, sasa imetulia, shuari kabisa. Nuru iliyokuwa ikiingia chumbani taratibu asubuhi ile haikuingia ili kukifukuza kiza kizito kilichokuwa kimetanda chumbani mle jana usiku tu bali pia kuwaondoshea udhia, kisirani na ukorofi uliokuwemo chumbani mwao...(uk. 205).

Kutokana na mifano hii miwili, inabainika kwamba tukio hili la mashahidi hawa kukaa na kujadiliana kuhusu msimamo wao wa kukataa kutoa ushahidi linachukua usiku mzima, tangu kiza kinapoingia hadi kinapoondoka na kupisha asubuhi.

Schechner (1988) anaeleza kwamba utendaji mzuri ni ule ambao kwa kutumia vipengele anuwai vya utendaji hubainisha wakati ambapo matukio husika yanatukia. Hii ndiyo hali katika riwaya ya *Haini*. Kwa matumizi ya kiza, mwandishi amefaulu katika kutubainishia wakati matukio tuliyotaja yanatukia.

(b) Kuashiria mateso na uovu

Katika riwaya ya *Haini*, mbali na kiza kutumiwa kubainisha wakati, kimetumika kubainisha matukio ambayo yameshamiri ama mateso au uovu wa aina fulani dhidi ya baadhi ya wahusika. Kiza kinatumika kama mbinu ya kutesa anayehusika na wakati mwingine kinatumika katika utendaji ili kufanikisha tukio ovu. Matendo mengi maovu aghalabu hutekelezwa usiku au kwenye kiza, na hii ndiyo hali tunayopatana nayo katika riwaya ya *Haini*. Kiza kimetumika kwa ufaafu pale Haramia anapopelekwa *Mashakani Hotel*. Jumba lile limewekwa kizani makusudi ili kuzidisha mateso ya anayepelekwa huko. Wanaopelekwa huko ni wale ambao wamevumilia mateso ya kwa Ba Mkwe, na sasa wanawekwa katika hali mbaya zaidi ya huko, ikiwa pamoja na kuwekwa kwenye kiza. Mfano ufuatao unashadidia wazo hili;

[Haramia] alitega masikio kusikiliza kama kuna ishara ya uhai ndani ya jumba lile lakini hakuna chochote alichokisikia ila kimya cha mfululizo, kimemzunguka pale alipo, hajui yuko wapi, hajui saa ngapi, hajui kama ni mchana au ni usiku. Chumbani mle hampambazuki ukajua kumekucha. Kila wakati kumekuchwa. Ni usiku tu. Chumba wala hakina habari na kupanda au kushuka kwa jua. Humo halifiki asilani. Limezingiwa na lile chaka halina nafasi ya kupenyeza miali yake hata kidogo. Haramia alikuwa akikitazama kile chumba ana wingi wa hofu. Ule ushujaa wake wote aliokuwa nao kule kwa Ba Mkwe, akijigamba na kujitapa mbele ya wenzake sasa umekwisha. Anajuta...(uk. 170).

Kutokana na mfano huu, tunaona namna Haramia anavyopata dhiki kutokana na hali aliyomo hadi anajuta laiti asingewashawishi wenzake wakatae kutoa ushahidi. Hamza vilevile anapelekwa katika chumba cha kiza kwa kukataa kushirikiana na Kanali Bunju na maafisa wenzake. Kanali Bunju anamwambia, “Tunakupeleka chumba cha kiza. Tutakapokutoa huko uwe umeshaamua kimojawapo. Kukubali tulivyokwambia au kifo!” (uk. 84).

Mbali na kiza kwenye chumba cha kiza, kuna joto jingi hivi kwamba chumba chenyewe kinakuwa ni dhiki tupu. Huku ndiko anakokaa Hamza kufunzwa adabu hadi anapotolewa baada ya siku kumi akiwa hoi; hajiwezi...(uk. 92,93).

Katika matukio mengine, uovu unatekelezwa wakati kiza kimeshitadi. Matendo kama haya, ikiwa yatatendwa kwenye mwangaza huenda yasifaulu wala kuaminika kama yanavyoaminika na kufaulu yanapotendwa kwenye kiza. Huu hapa mfano:

Kiza kilikuwa kimegubika usiku gubigubi, kutotoro. Kila kitu kimetulia pale kilipo. Katikati ya usiku ule Hamza alisikia watu wakinyatia nyatunyatu. Hatua moja moja, wakinyemelea kama wezi. Alikuwa katika usingizi mwepesi na mnyatio ule aliusikia kama aliye ndani ya njozi za gerezani. Alishangaa, akajiuliza, “mwizi gani tena atakayekuja iba gerezani, tena gereza lenyewe kwa Ba Mkwe?”...Mwili ulimsisimka, hofu ikamjaa tele moyoni, moyo unamwenda mbio. Hakujua nani kati yao, wawili walio mle. Yeye au Doto. Doto amelala wa juzi, hana habari na wenda usiku wale. Mlango ulifunguliwa taratibu, mwanga wa kurunzi ukampiga usoni moja kwa moja pale kwenye pembe ya chumba alipokuwa amejibanza. Aliyaziba macho yake kwa viganja vyake viwili kujikinga na baka la mwanga wa kurunzi lililomwagika ghafla usoni mwake na kuzipadhiki mboni za macho yake yaliyokwishazoea kiza kwa muda mrefu. “Toka nje!” aliitwa kwa sauti ya chini. Kama ya mwizi anapozungumza na mwizi mwenzake wanapokuwa katika wizi wao. “Toka nje!” aliitwa tena. Sasa alijihisi kama aliyezugwa, kama mtu aliye usingizini, lakini hakulala usingizi. Aliinuka taratibu akasimama kuangalia pale mlango. Alitoka nje ya chumba. Mlango ulifungwa taratibu kama vile ulivyofunguliwa. Hofu ilimzidi akaona leo siku yake imefika. Matumaini yake yote ya kutoka yalivia pale. Yeye amekwishasikia hadithi za waliochukuliwa kutoka humo usiku usiku, wakatotea hivi hivi watu wasijue wameyeyukia wapi. Lakini akajikaza kiume, akasema na moyo wake, “Siku ya kufa ni moja tu, ikifika imefika.” Ule mlango wa chuma wa kutokea kwa Ba Mkwe ulikwishafunguliwa naye akaongozwa nje kwa hatua za kunyatia asiamshe waliolala. Nje kiza kizito kilikuwa kimeatawi baina ya mbingu na ardhi, kimejitandaza na kujimwaga mwaaa! Kimetapakaa kila kipenu na kichocho. Kimejaa tele ndani ya usiku wa siku ile...(uk. 63-64).

Katika dondoo hili, Hamza anatolewa chumbani, usiku wa manane wakati kiza kinatawala kila mahali na watu wamelala. Anatolewa kimya kimya na kupelekwa

mahali upenuni ambako anateswa na kushurutishwa aseme yote anayojua kuhusu mauaji ya Kigogo. Anateswa kule hadi anakubali kusema, (uk. 65-66) na asubuhi inapokaribia anarudishwa chumbani alimomwacha Doto. Tunasimuliwa kwamba:

Doto alidhani yake yalikuwa makubwa, lakini haya ya leo yametia fora. Haya ya kuchukuliwa usiku usiku ukarudishwa alfajiri umefundwafundwa. “Haya, tsubiri lijali!” Doto alisema akashusha pumzi kwa nguvu...(uk. 67).

Kiza kimetumika katika tukio hili kuwezesha tukio la uovu kutendeka. Mateso mengi, yasiyo na utu yanatukia wakati wa usiku; kiza kikishameza kila kitu. Hivi ndivyo Hamza anavyochukuliwa, kuning'inizwa kisimani kichwa chini miguu juu na kulipuliwa kwa risasi alizonusurika hadi akakiri kusema wanayotaka ayaseme.

Si Hamza pekee anayefikiria kwamba kutolewa nje usiku mpevu kama ule uliojaa kiza ni ishara ya kupelekwa wanakouawa watu wasijulikane waliko. Sururu anapokamatwa baada ya mpango wake wa utoro kutofaulu, anawekwa chumbani mwenyewe bila kusemeshwa lolote. Tunasimuliwa kwamba:

Siku ya tatu Mzee Machale aliufungua mlango alfajiri. Bado kulikuwa kiza hakujapambazuka vizuri. Hizo ndizo saa za kunyonga wale waliohukumiwa kifo. Sururu akaona siku yake imefika, bora atoe shahada...(uk. 127).

Kupitia Sururu kutolewa nje wakati ule; alfajiri kiza kikiwepo, tunapata kufahamu kwamba wakati huo ndio wanaponyongwa waliohukumiwa kifo. Wakati kiza bado kipo ndio wakati mwafaka wa kutekeleza mauaji, tofauti na mchana kwenye mwanga. Matukio mengine yanayotendeka kikamilifu kizani ni yale yanayohusu matumizi ya mihadarati miongoni mwa wafungwa. Tuangalie tukio hili:

Usiku ulikuwa umeshaingia, kiza kimejaa tele vyumbani. Walio Kumbakumba ni wakati wao wa kuchimba kufuru. Wavuta bangi huo ndio wakati wao wa kuyasokota mabomu yakawashwa moja

moja na kupelekwa duru wavutaji wakaisifu bangi hiyo, “Joz minal Hindi.” Harufu ya bangi hujaa Kumbakumba nzima ukadhani labda humo bangi imehalalishwa. Hata kama haikuhalalishwa kwa wafungwa hao sheria za kuvunjwa ziko nje tu na wao washazivunja na ndiyo maana wamo jela. Kwao jela hakuna sheria. Na wavuta sigareti nao hivyo hivyo. Sigareti hukatwa vipande vipande na kila kipande huvutwa na watu kadha kila mmoja apate angalau mikupuo miwili mitatu. Kipande cha sigareti huvutwa mpaka kikawa hakishikiki tena kwa ncha za vidole na huongezwa urefu kwa msokoto wa karatasi ya gazeti ili kuhakikisha kwamba inavutwa yote, mpaka inakwisha kabisa, hakibaki chochote cha kutupwa. Humo sigareti na bangi ni vitu azizi na mwenye navyo ni mfalme, kama gerezani kuna ufalme...Humo vyumbani, usiku ndio wakati wa kwenda chooni kupakua choo kilicholimbikizwa mchana kutwa matumboni mwao...(uk. 142).

Dondoo hili linaeleza namna wafungwa wanavyoinkiza dawa za kulevya gerezani kupitia njia zao za kwendea haja na wanavyozipakua dawa hizo usiku. Dawa za kulevya haziruhusiwi gerezani na ndio maana wafungwa hawa kiza kitakapoingia ndipo wazitumie. Ili tukio hili liaminike sharti litendwe usiku au wakati kiza kimestawi. Utendaji ukitukia mchana, jukwaa liwe na michoro ya nyota kuweka wazi kwamba japo ni mchana, tukio mahsusi linafaa kutendwa usiku. Kiza hivyo kinakuwa mwafaka kutumika katika tukio kama hili.

(c) Kuonyesha kutamauka

Kiza kimetumika katika riwaya ya *Haini* kama ishara ya wahusika kutamauka. Wamezongwa na balaa, tabu na walipo hawana tumaini. Wamekata tamaa, na kiza kinatumiwa kuashiria kutamauka huko. Kwa mfano, Hamza na watu wengine wanapokamatwa, wanakuja kujua baadaye kwamba wao ndio washukiwa wa mauaji ya Kigogo, kwamba wao ndio mahaini. Jambo hili linawafisha moyo kwa kuwa hilo halikuwa kosa dogo, na aliyepatikana na hatia hukumu yake ilikuwa kifo tu. Akieleza hali yao msimulizi anasema:

Ulikuwa mkusanyiko mkubwa wa watu. Wanaume, wanawake, vizee na vijana. Hakuna aliyezungumza na mwenzake kila mmoja

akihofia maisha yake, kwani hakuna hata mmoja aliyeweza kutabiri hatima yake katika hali ya kutisha kama ile. Kila mmoja aliona kiza kitupu mbele yake, kiza ambacho hakuna aliyejua kinaelekea wapi. Hakuna aliyekuwa na matumaini kwani matumaini yote yalipeperushwa na shutuma za kutuhumiwa kwa kosa ambalo hakuna yeyote katikaumati ule uliokata tamaa aliyelijua... (uk. 9).

Kwingineko, Hamza na Faraji wanakumbushana maisha yao ya awali yalivyokuwa ya raha mustarehe. Walipo sasa hivi wamezungukwa na dhiki na tabu. Wao pia wamo kwenye kiza kama inavyodhihirika hapa:

“Zile zilikuwa siku za raha. Maisha yalikuwa matamu kama asali. Tulizungukwa na raha tupu. Pombe, wanawake na muziki,” alisema Hamza na Faraji akimtazama vile anavyokubuka zama zile. “Lakini tazama maisha yalivyobadilika. Kama taa iliyozimwa ghafla. Sasa hivi tulikuwa katika nuru, tukizona anasa zote za maisha, sasa tuko kizani, hatuoni kitu chochote isipokuwa dhiki, shida na mateso.” (uk. 111).

Mhusika mwingine aliyetamauka na yupo kizani ni Khadija, mkewe Hamza. Amefanya kila awezalo kumtoa Hamza gerezani lakini hajafanikiwa. Yupo katika hali ya kutamauka, amezungukwa na kiza cha maisha. Msimulizi anasema:

Nuru yote ya mwezi iliyokuwa imezagaa kila pahala usiku ule kwake [Khadija] haikumulika kitu chochote na alichokiona yeye ni kiza cha maisha kimetanda mbele yake, kimetanda nyuma yake, kimemzunguka kila pahala. (uk. 192).

Ni bayana kwamba katika riwaya ya *Haini*, kiza kimetumika kikamilifu katika utendaji wa matukio hasa tuliyoyajadili katika mifano tuliyoitoea. Matukio hayo yanakubalika na kuaminika zaidi yanapotendeka kizani kuliko yakitendeka kwenye mwangaza. Mwandishi amefaulu katika matumizi haya ya kiza katika riwaya hii.

Vipengele vya kiza na vimulimuli vinapotumiwa pamoja na vile vya sauti na kimya kwa njia ifaayo husaidia katika kufanikisha utendaji. Tutazame vipengele hivi; Sauti na kimya.

4.3 Sauti na Kimya

Matumizi ya sauti na kimya, kama ilivyo matumizi ya vimulimuli na kiza huathiri ufanisi wa utendaji wa kidrama kwenye jukwaa. Mwelekezi, baada ya kupitia matini ya kidrama, anapaswa kubainisha ni wapi sauti au kimya kinatumika na kuelekeza matumizi ya vipengele hivi kwa njia ambayo itafanikisha utendaji.

4.3.1 Sauti

Goldfarb na Wilson (2002) wanaeleza yafuatayo kuhusu matumizi ya sauti.

Kuna sababu mbili za kimsingi zinazolazimu matumizi ya sauti katika utendaji. Kwanza, kuleta athari za kimazingira na athari zinginezo zinazohitajika katika utendaji. Vilevile, sauti hutumika kusisitiza yanayozungumzwa au utendaji wa kimmelodrama.

Wataalam hawa wanaeleza kwamba sauti zinazosikika nje ya alipo mtendaji kama vile sauti ya mtu akitembea, gari likipita barabarani au mlango ukifunguka na kufungwa huwa muhimu katika utendaji. Hizi ni sauti za kimazingira ambazo ni sehemu ya maisha ya kila siku, na sharti zijumuishwe katika utendaji. Sauti katika utendaji husisitizwa kwa matumizi ya vipaza sauti. Hivi hupaza sauti ya mtendaji ili isikike na watazamaji wake wote akiwa kwenye jukwaa.

Sauti zinazohitajika kufanikisha igizo fulani zinaweza kurekodiwa na kucheza wakati utendaji ukiendelea. Kwa mfano, rekodi ya vyombo kuvunjika jikoni inaweza kucheza waigizaji wakiwa tuseme sebuleni na sauti hiyo ikaathiri mkondo wa matukio yatakayofuata, kama vile mhusika kwenda ilikotokea.

Vipaza sauti wakati mwingine huwekwa katika sehemu mbalimbali za ukumbi na sauti inaweza kusikika kutoka upande wowote ule inakotakiwa kutoka. Mwangwi unaweza kusikika kutokana na sauti ya maneno yanayosemwa kucheza. Wakati

mwingine, hadhira inaweza kusikia anachowaza mwigizaji kupitia sauti ya anayowaza kurekodiwa na kucheza wakati utendaji ukiendelea.

Mumbo na Mwari (2016) wanaeleza kwamba sauti hutumika katika utendaji wa kidrama ili kutekeleza shabaha maalum na kuleta athari muhimu za sanaa za maonyesho. Athari hizi aghalabu hukusudiwa kuibua hisia fulani za kimaumbile, kimazingira, kiutambuzi na kisaikolojia miongoni mwa hadhira.

Kama tulivyoeleza hapo awali, hadhira ni muhimu katika utendaji kwa kuwa hiyo ndiyo inayotendewa na kuwasilishiwa ujumbe katika kazi mahsusi ya kidrama. Ni muhimu hivyo ikiwa kipengele cha sauti kitatumika kufanikisha utendaji husika.

Katika riwaya ya *Haini*, sauti kama vile ya makanali wakicheka maofisini mwao inaweza kurekodiwa na kucheza, huku vyumbani tukionyeshwa namna sauti hiyo ya kicheko inavyowatia hofu mahaini. Shafi Adam amejumuisha matumizi ya sauti katika riwaya hii ili kuleta athari mbalimbali katika utendaji. Athari hizo ni kuzua hofu na wasiwasi, kuashiria hatari, kuwapa wafungwa tumaini na hatimaye kufanikisha mawasiliano.

1. Kuzua Hofu Na Wasiwasi

Baadhi ya matukio katika riwaya ya *Haini* yanaibua hofu kutokana na namna sauti ilivyotumika katika matukio hayo. Sauti fulani inapotumika, matokeo yake yanakuwa ni hofu na wasiwasi miongoni mwa hadhira na wahusika wenyewe. Tazama dondoo lifuatalo:

“Watangazaji wamelala nini?” aliuliza Hamza kwa mzaha. Kabla hata hakujiibiwa ulisikika mlio uliokuwa na kishindo tu-tu-tu.

“Hivi hawa Mabaniani hawana habari kwamba hairuhusiwi kuliza fataki siku hizi?” aliuliza Fadhil...

“Hizo si fataki wala si fashfash. Hizo ni risasi, tena zenyewe ni za mashingan,” alieleza Pango, mwanajeshi wa siku nyingi aliyeanzia ukuruta mpaka sasa kafika cheo cha u-sajini...(uk. 1-2).

Tukio hili linatokea saa chache baada ya kuuawa kwa Kigogo. Nchi nzima imo katika hali ya hatari. Redio haitangazi chochote isipokuwa kucheza muziki wa kijeshi, hali inayozidisha hofu na taharuki. Wote wanatoka na kutorokea makwao, kila mmoja wao akiwa na wasiwasi; hakuna ajuaye kumetokea nini ili kusababisha milio ile ya risasi. Baadaye (uk. 5) ndipo redio inapotangaza kwamba hairihusiwi mtu yeyote kuonekana nje baada ya saa kumi na mbili. Tangazo hili linazidisha wasiwasi miongoni mwa hadhira na wahusika kama vile Hamza na wenzake na vilevile Khadija.

Wanajeshi na polisi wanapokuwa maofisini mwao wakiongea na kupanga mikakati mbalimbali kuhusu wafungwa wao, sauti zao zinasikika kule vyumbani na kuzua hali ya wasiwasi na hofu. Msimulizi anasimulia kwamba:

Ilipofika saa nne, kwa Ba Mkwe kulikuwa kumetimia. Wakubwa wamejaa maofisini, wanajeshi na polisi, tepe zinameremeta mabegani, wanakunywa chai...lazima kwanza wale washibe, wapate nguvu za kuwapiga mijeledi wari wao wanaotawishwa vyumbani. Walizungumza kwa kelele na mazungumzo yao yakanoga yakawa ya furaha na vicheko. Lakini vicheko vyao viliwatia wale walio vyumbani kiwewe, wakijua kwamba saa imefika, saa yao ya mateso na idhilali. Vicheko vya wakubwa wale ni ishara ya vilio vyao. Wanapowasikia wakicheka hivyo, wao huingiwa na simanzi, wakazongwa na hofu na wasiwasi, kila mmoja akijiuliza moyoni, “Ni mimi au mwenzangu?” (uk. 46).

Hali hii inajirudia tena huko kwa Ba Mkwe kama inavyodhihirishwa hapa:

Viatu vya maamirijeshi na maafandi wa polisi vilisikika vikiigonga sakafu kwa jeuri na vishindo na kule ofisi, leo kulikuwa kumejaa tele. Wakubwa walikuwa wakicheka kwa furaha na kejeli wakiwa wameshaandaliwa chai itakayonywewa pamoja na kababu, sambusa na katlesi...walikuwa wakizungumza kwa kelele na kucheka kwa

sauti kubwa bila ya kujua kwamba vicheko vyao vile viliwapa kiwewe wale waliosokomeka mle ndani ya vyumba wakisubiri ujudi wa Mungu...(uk. 69).

Kutokana na mifano hii, inabainika kwamba vicheko na sauti za maaskari na maafisa wa kwa Ba Mkwewe zinaposikika huathiri hali ya mahaini waliofungiwa mle vyumbani. Wafungwa hukumbwa na hofu na kiwewe kwa kutojua watarajie nini zaidi ya mateso na dhuluma. Kama tulivyoeleza hapo awali, sauti hizi zinaweza kurekodiwa na kucheza wakati matukio haya yakiigizwa kwenye jukwaa. Mwandishi ametumia sauti kama mbinu mojawapo ya kuwatesa mahaini na wafungwa kule magerezani. Hii inatokana na hofu na wasiwasi wanayopata wafungwa hawa kila wanapozisikia sauti husika. Mwandishi amefanya hivi kwa kuwapa wakubwa wa magereza haya uwezo wa kutumia sauti kama vile kicheko, kugongesha viatu vyao chini kijeuri wanapotembea na kuzungumza kwa sauti za juu makusudi ili wafungwa wao wawasikie, watishike na hatimaye kufanya kama wanavyotaka wao. Kanali Bunju ni mhusika mmojawapo wa wale waliopewa uwezo huu wa kutumia sauti hizi na kuzua hofu na wasiwasi. Tazama anavyohangaika Hamza kutokana na sauti ya Kanali Bunju:

...Sauti yoyote ya mle ndani ilitosha kumrusha roho na kumtia kiwewe akidhani sasa ndio wanakuja. Usiku na mchana, alikuwa katika hali ya hofu, hofu ya vitimbi visivyokwisha vya kwa Ba Mkwewe. Kila wakati hushitushwa na chochote kile na hali hiyo ndiyo iliyompumbaza akawa kama zuzu. Nao walizijua vyema mbinu za kumtia mtu kiwewe, wakamfanya mwendawazimu ilhali ana akili zake timamu. Basi wakamwacha Hamza vilevile, peke yake, katika hali ya hofu na wasiwasi. Hana hakika lini au saa ngapi. Kama anayesubiri mauti. Huingia wakitoka, na pale wanapoingia, Kanali Bunju huzungumza kwa sauti kubwa makusudi. Akitoka, huku nyuma humwacha Hamza akiwayawaya kwani anapoingia, Hamza huona kama nyumba ile imeingiliwa na Ziraili, hajui atachukua roho ya nani atakapotoka...(uk. 96).

Sauti katika muktadha huu inatumiwa kama mbinu ya kuwatesa, kuwatia hofu na kuwaweka wafungwa na wasiwasi. Wakiwa katika hali hiyo, inakuwa rahisi kwao

kushirikiana na wakubwa wa kwa Ba Mkwe. Hali tunayoipata kwa Ba Mkwe wakati Sururu anakamatwa na kupelekwa huko ni sawa na aliyomo Hamza. Si yeye peke yake bali hata wafungwa wengine huhofia maisha yao kila wanapozisikia hizi sauti kutoka kwa maafisa wa kwa Ba Mkwe, na wasiwasi huwazidi ikiwa sauti wanazosisikia ni za wakubwa wa huko. Tazama dondoo hili:

Sururu alihisi kwamba kulikuwa na harakati zisizo za kawaida. Kwa muda wa siku tano alizokaa mle, kwa Ba Mkwe kulikuwa kimya. Ni wale watumishi wa kawaida tu na wakubwa zao ndio waliokuwa wakisikika wakiingia na kutoka. Walio vyumbani wakinong'ona tu hakuna anayethubutu kunyanyua sauti yake. Huko nje ilisikika milio ya gari. Zikija na kuondoka. Kwa ile midundo ya viatu vyao juu ya sakafu, pale wanapoingia kwa mbwembwe na mikogo alijua kwamba wengine walikuwa maafisa wa kijeshi. Sauti zao alizisikia kwa mbali kule ofisini walikokaa, wakiongea na kucheka. Wao wakicheka na wale wa vyumbani wakitetemeka, hawana hakika watu wale wamekuja kuzua balaa gani...(uk. 130).

Baada ya Haramia kutolewa kule *Mashakani Hotel* na kurudishwa chumbani walimokuwa mashahidi wenzake; akiwa katika hali ya kuogopa kutokana na aliyokumbana nayo kule *Mashakani Hotel*, anaisikia sauti ya Kanali Bunju nje ya chumba chao. Huyu ndiye aliyempeleka chumba alimofungiwa na chatu, amle ammalize, maisha yake yaishie hapo. Haramia, licha ya kwamba alimwogopa Kanali Bunju hapo awali, wakati huu anamwogopa hata zaidi, kwa kuwa ashajua hakuna asichokifanya Kanali Bunju. Msimulizi anaeleza kwamba 'Haramia aliposikia sauti ya Kanali Bunju kwa mbali akiongea kule kwa Ba Mkwe, roho ilimpiga, moyo ukamwenda mbio hajui amekuja kuzua balaa gani tena,' (uk. 175). Katika hali hii, msomaji anashawishika kuamini kwamba Kanali Bunju hakuzungumza kwa sauti ya juu bure bilashi, alikusudia hasa Haramia amsikie, aingiwe na hofu na awe tayari kushirikiana naye kwa vyovyote vile. Baadaye kidogo, Kanali Bunju anamwita

Haramia ambako Haramia anajisalimisha kwao. Anakubali kutoa ushahidi wanaomtaka akautoe mahakamani, (uk. 176-177).

2. Kuashiria Hali ya Hatari

Mwandishi wa riwaya ya *Haini* ametumia sauti kuashiria hali ya hatari. Yapo matukio ambapo jambo la hatari linatokea na jambo hili kuashiriwa kwa matumizi ya sauti fulani ambayo wahusika wakiisikia wanafahamu moja kwa moja kwamba kuna hatari pasi na kuambiwa na yeyote. Haya yanadhihirika katika dondoo lifuatalo:

... “Hata sisi tulisikia mlio kama wa bunduki!” Khadija naye aliyarukia maneno. “Nani? Majeshi?” aliuliza. Kabla (Hamza) hakumjibu redio ilisita kupiga muziki wa kijeshi. Hamza akashtuka, akachomoa kalamu kutoka mfukoni, “Hebu niletee kipande cha karatasi!” aliamrisha. Alipokuwa ameinama tayari kuandika chochote kitakachotangazwa, ilisikika sauti iliyojaa hamasa ikitangaza, “Kwa amri ya serikali, hairuhusiwi mtu yeyote kuonekana nje baada ya saa kumi na mbili jioni na yeyote atakayevunja amri hii atachukuliwa hatua kali za kisheria!” “Hee! Kumezidi nini tena? Watu wasitoke, mimi naona hakuna kheri, hiyo ni shari tupu. Sijui balaa gani tena! Mungu atusalim salama,” Khadija aliomba...(uk. 5).

Hali ya hatari inatangazwa katika dondoo hili punde baada ya Kigogo kuuawa. Wahusika hawajui yanayoendelea lakini kwa mujibu wa matukio yanayotokea kabla ya tangazo hili, inafahamika kwamba kuna hatari mji wa Unguja. Watu wamejawa na hofu, hakuna anayejua yaliyotokea na kusababisha matukio yote yaliyotokea, hadi kufikia hali ya hatari kutangazwa.

Sauti imetumika vilevile kuashiria hatari hasa pale wafungwa wanapotoroka gerezani. Katika matukio haya, kipenga ndicho kinachotumika kuashiria kwamba mfungwa fulani ametoroka. Hawa ni watu hatari, na kutoroka kwao huwa ni hatari kwa kila mtu, walenzi wao mle gerezani na wananchi wengine. Tazama mifano hii:

“Nini?” aliuliza Hamza.

“Husikii kitu?”

Hamza naye akatega sikio, “Naskia vipenga kwa mbali!”

“Ni sauti ya vipenga! Nafikiri kuna mwizi anafukuzwa!”
 “Mwizi gani huyo wa ajabu atakayekuja kuiba gereza?” aliuliza Hamza.
 Sauti za vipenga zikasikika kwa karibu zaidi, wote wakavisikia vipenga vikipulizwa. Sauti za vipenga zilikurubia mpaka vikawa vinapulizwa mle ndani ya gereza huku kumetimka vurugu, wafungwa wanarudishwa ndani ya vyumba vyao. Kwanza walirudishwa vyumbani wao, “Haya! Ndani! Ndani nyote! Aliamrisha yule askari, wasiwasi umemjaa. “Ndani! Ndani!” alipiga kelele...
 “Kumezidi nini?” Ambar alimwuliza (mfungwa aliyekuwa amechungulia kwenye tundu la mlango). “Wafungwa watatu wametoroka!” Alimjibu.

Katika matumizi ya sauti kama hii hapa wakati wa utendaji, mwelekezi wa mchezo wa kuigiza anaweza kurekodi sauti hii ya vipenga vikipulizwa, ikachezwa kwa sauti ya chini kwanza (msimulizi anaeleza kwamba inasikika kwa mbali) kisha sauti ikaongezwa hivi kwamba inasikika na watendaji wote kwenye jukwaa na hadhira pia.

Koplo Ngwali anapomwona Sururu akitorokea upande wa nje wa ukuta wa gereza, anafyatua risasi ovyo na baada ya kuona kwamba risasi hizi hazisaidii chochote, anatoa kipenga mfukoni, anakipuliza na kelele zake zinajaa gereza zima, (uk. 123).

Kipenga aghalabu, hata katika hali halisi hutumiwa kuashiria hali fulani ya hatari hasa wakati mwizi anafukuzwa, na katika mazingira ya gereza, anapotoroka mfungwa kama ilivyotukia katika riwaya hii.

3. Kuwasiliana

Sauti katika riwaya ya *Haini* imetumika kupitisha ujumbe kutoka kwa mhusika mmoja hadi mwingine pasipo matumizi ya maneno. Wafungwa wa kule kwa Ba Mkwe wanajipata vyumbani, wanaojuana ni walio katika chumba kimoja pekee. Hawajui chochote cha mle ndani na nje ya kwa Ba Mkwe. Hali hii inabadilika pale ambapo wafungwa hawa wanaanza kuwasiliana kwa vidoto; kupitisha ujumbe kwa kugonga ukuta, mbinu inayotumiwa sana na wanajeshi wakiwa vitani ili kuficha siri.

Tuangalie mifano hii:

Mazungumzo yao (Hamza na Doto) yalikatwa katikati na sauti ya ukuta uliokuwa ukigongwa kutokea upande wa pili wa chumba chao, “Tu tu tu tu tu tu tu.”

“Nini hicho?” Doto aliuliza.

“Labda jamaa wa chumba cha pili wanagonga ukuta.”

Ule mlio wa ukuta ukaendelea. Doto akausikiliza kwa makini, akamwuliza Hamza, “mna wanajeshi humu?” “Wengi,” Hamza akamjibu.

Ule mlio ukaendelea na baada ya muda kidogo ukasita. “Anayegonga ni mwanajeshi,” Doto alisema. “Anazungumza kwa ishara za morse...”

“Sikiliza!” Doto aliamrisha. Kama sajin anayeamrisha kuruta.

Alisikiliza kwa makini mpaka alipomaliza kugonga. Naye Doto akagonga. Akagonga kwa muda, naye akasita kugonga. Akamtazama Hamza aliyekuwa na hamu ya kujua ujumbe alioupelekea na ule alioupeleka.

“Chumba cha pili kuna wanajeshi wawili, wanatuuliza sisi humu ni nani? Tumetokea wapi? Tumekuja lini? Doto alimweleza Hamza...Mazungumzo na jirani zao wa chumba cha pili yakawapa nafuu kubwa kwa kupunguza ule upweke waliokuwa nao chumbani mle. Tokea asubuhi, wakishakunywa uji tu, kazi yao ni kugonga ukuta na kupashana habari...(uk. 52-53).

Hamza na Doto wanapotolewa nje na Mzee Machale wakaoge, Hamza anakaa na kuzungumza na Mzee Machale. Anaporudi chumbani, wawili hawa wanawapasha wenzao yote Mzee Machale aliyosema kwa kule kugota kwenye ukuta, (uk. 58).

Doto na Hamza wakiwa chumbani mwao, ukuta wa chumba unagongwa kutoka chumba cha pili na kutokana na ‘mazungumzo’ haya, wanafahamu kwamba Kumbakumba wapo watu wawili ambao wametoweka na hawajulikani walipo, nako kule chumba cha nne mtu mmoja amekufa, (uk. 70).

Sauti hizi maalum za kugota ukuta zinakuwa muhimu katika kupashana habari kule gerezani pasi na kuonana wala kuongea. Hivyo, japo watu hawa wametengwa kutoka kwa wengine na hawaonani, bado wana uwezo wa kuwasiliana. Utendaji wa tukio hili unaweza kutekelezwa kwa watendaji wanaowasiliana kuwa katika pande tofauti za jukwaa. Kwa mfano, waigizaji watakaochukua nafasi za wahusika Doto na Hamza

wanaweza kuwa kwenye jukwaa (waonekane na hadhira). Wanaoigiza nafasi za wanajeshi waliofungwa chumba tofauti na cha akina Doto wanaweza kuwa nyuma ya jukwaa (wasionekane na hadhira). Wawasiliane kwa kugota ukuta kama wanavyofanya wahusika hawa kwenye riwaya. Sauti hizi za kugota zinaweza kuzidishwa na kipasa sauti ili watazamaji kusikia mgoto wenyewe.

4. Kuwapa Wafungwa Tumaini

Zipo sauti ambazo pindi zinaposikika wafungwa hujua kwamba ama wanatolewa nje wakaoge au ni wakati wa uji au chakula. Sauti hii aghalabu huwa ile ya funguo za Koplo Usi akiandamana na kikosi chake cha wafungwa wanaogawa chakula kule vyumbani. Ingawa sauti ya funguo wakati mwingine huashiria hatari pale mfungwa anapokuja kutolewa akateswe, na wengine kuletwa vyumbani, sauti hii imetumika kwa mapana kama ishara ya mema; wafungwa kufunguliwa watoe mtondoo, kuletewa chakula na kutolewa wakaoge:

Mfano 4.15

Kwa mbali zilisikika funguo zikigongana, “ngeren ngeren” na mgongano wa funguo zile ukakaribia Kumbakumba. Kwa kuwa mlio wa zile funguo umekuwa ishara ya kuja kwa askari, kwa saa zile wakajua tu kwamba mlo sasa ni tayari. Mlio wa ndoo zilizotuliwa juu ya ngazi ya kuingilia Kumbakumba ulisikika waziwazi, kila mtu akajua sasa uji tayari...(uk. 18).

Mfano 4.16

...Lakini asubuhi ya leo hakukuwa na hadithi wala mapishi. Walipokuwa wakigaragara sakafuni, wengine wakibanja chawa, wengine wakichokoa papasi na wengine wakiponda kunguni, walisikia funguo zikigongana na mlio wake ukawa unakurubia kule waliko wao, wakajua Kumbakumba kunakuja kufunguliwa...Sura ya Koplo Fataki ilionekana kama ya mtu asiyelewa kitu. Walimtaazama kwa mshangao wasiamini yale aliyowambia, “kuoga nasema!” aliwashtua kwa kupiga mguu chini, akitabasamu...(uk. 33-34).

Wafungwa walikuwa wakifurahia kutolewa wakaoge na kufua nguo zao kwa kuwa walipata fursa adimu ya kukutana na wafungwa kutoka vyumba vingine, wakajuliana hali na kupashana habari zozote zile.

Mfano 4.17

Mpaka saa tisa ndipo aliposikia watu wakija kule aliko. Akamsikia Koplo Usi kwa mbali akizungumza kwa kelele, “A-a-atakufa njaa yuyu-yule,” alipiga kelele, kigugumizi kimeshika na humzidi pale kazi zinapomwelelea, zikawa nyingi kwake. Hamza aliwasikia wakitua ndoo zao chini ya mlango, mlango ukafunguliwa...(uk. 87).

Hapa ni baada ya Hamza kupelekwa chumba cha kiza na kuwekwa humo bila chakula, hali yake taabani. Anapowasikia Koplo Usi na kikosi chake, anajua kwamba hatimaye ameletewa chakula, japo kidogo.

Mwandishi ametumia sauti katika riwaya ya *Haini* kwa ufaafu na ufanisi mkubwa kuleta athari mbalimbali tulizozijadili hapo juu. Ikiwa mwelekezi wa kazi hii ya kidrama atazijumuisha sauti hizi katika utendaji wa kazi hii basi sauti hizi zitachangia pakubwa katika kufanikisha utendaji wake.

4.3.2 Kimya

George Mercy (2014) akiangazia matumizi ya kimya katika kazi za mwandishi Pinter anadai kwamba mwandishi huyu anafahamika kwa matumizi ya mtuo, alama za dukuduku na kimya katika tamthilia zake. Vipengele hivi huwa sehemu ya kimsingi ya majibizano miongoni mwa wahusika wake.

Kwa maoni yake, kimya katika matini ya kidrama hasa tamthilia huonyeshwa kwa njia tatu kuu: mazungumzo kusitishwa kwa alama za dukuduku, kupitia maelezo ya utendaji au maneno kama vile ‘kimya’ kutumiwa moja kwa moja. Kimya huchangia

katika kubadili mkondo wa mazungumzo na hutokea aghalabu wakati jambo lisilotarajiwa linatokea kuashiria hofu, wasiwasi na vilevile taharuki.

Katika riwaya ya *Haini*, kimya, kama vile sauti, kimetumia kuonyesha hali taharuki na kuashiria hofu na wasiwasi.

(a) Kuonyesha hali ya taharuki

Kimya kimetumika katika riwaya ya *Haini* kuibua hali ya taharuki. Katika hali hii, wahasika hawajui yanayoendelea wala watarajie nini, wamo tu wakisubiri la kutokea litokee. Taharuki hii inaandamana kwa kiasi kikubwa na hali ya woga, hofu na wasiwasi. Baada ya milipuko ya risasi kusikika nje na akina Hamza kutorokea makwao, msimulizi anaeleza kwamba mji wa Unguja ulikuwa kimya ifuatavyo:

Sauti ya Unguja iliendelea kupiga muziki wa kijeshi bila ya kutangaza kitu chochote, au angalau kusikika sauti ya mtangazaji ikisema kitu. Usiku ulikwishaingia, usiku uliokuwa na kimya kizito, kwani huko nje hakuna aliyesikika kwenda wala kurudi. Zile sauti nzuri za watoto wanaocheza usiku wakiimba nyimbo zao za michezo ya ukuti, kinyuki kipenyapenya au saka mke wangu leo hazisikiki, hivyo kuunyima usiku wa siku ile, ile raha ya usiku katika eneo la ng'ambo la mji wa Unguja. Kulikuwa jii, kimya...(uk. 5).

Katika dondoo hili, inabainika kwamba Kigogo ameuawa saa chache zilizopita. Hata hivyo, wananchi hawajui yaliyotokea wala watarajie nini. Redio ya Sauti ya Unguja haijatangaza chochote kwa muda mrefu, inacheza tu nyimbo za kijeshi. Mji mzima umo katika hali hii ya taharuki; kila mtu akisubiri kujua kitakachotokea baadaye na sababu ya kucheza muziki wa kijeshi tu bila tangazo lolote. Hii ndiyo hali inayoukabili mji wa Unguja baada ya kifo cha Kigogo. Watu wanakamatwa na kufungwa, mtu akisema chochote kibaya kuhusu serikali anakamatwa, hivyo suluhu inakuwa ni kukaa kimya. Tunasimuliwa kuwa:

Mji umepwaya, kimya utadhani umeelemewa na jinamizi, nyoyo za watu zimejaa hofu na wasiwasi. Hakuna aliyejua lini au saa ngapi atatiwa mbaroni, watu wnakwenda na kurudi kila mmoja akiwaza labda sasa hivi au halafu...(uk. 148).

Dondoo hili linaashiria hali ya taharuki waliyokuwa nayo wakazi wa mji wa Unguja.

Hakuna aliyejua atarajie nini wala lini. Hofu na wasiwasi zikatawala.

Wale mashahidi tisa wanapopelekwa mahakamani kutoa ushahidi kama walivyoandaliwa, Haramia anakuwa wa kwanza kuulizwa ikiwa anakubali kwamba alihusika katika mauji ya Kiogogo au la. Haramia alijua kwamba wakikubali kwamba walihusika katika kumuua Kigogo wakubwa watauawa. Hivyo, alikuwa amewashawishi wenzake kwamba siku wakifika mahakamani wakatae, na ndio maana anakuwa mhusika muhimu sana katika kikundi cha mashahidi hawa. Kauli yake pale alipo ingeathiri mkondo wa matukio mengine. Anapoulizwa ikiwa anakubali au kukataa, msimulizi anaeleza kwamba:

[Haramia] Ameduwaa, anashindwa kujibu. Kimya, wote wanaisubiri kauli yake. Kanali Bunju na Kifupinyundo wamemkazia macho, wanamtazama kama simba anayetazama swala anayemwinda. “Jibu!” karani wa mahakama alimpigia kelele kwa ukali...(uk. 212).

Katika kunyamaza huku, hakuna ajuaye atakachokisema Haramia. Anazua hali ya taharuki miongoni mwa wahusika hawa; mashahidi wenzake, akina Kanali Bunju na karani wa mahakama.

Baada ya wafungwa 655 kuachiliwa huru na wale 30 kupelekwa wote kwa Ba Mkwe, siku ya kupelekwa mahakamani inakaribia. Hakuna miongoni mwao anayejua lipi atarajie. Wameteswa, wametishwa, wamepigwa nusura roho zao ziwatoke. Walipo hakuna lolote wanalotarajia, labda kifo tu au shari ya aina yoyote ile. Wamo vyumbani tu, taharuki imetanda. Tazama dondoo hili.

Mle mwa akina Hamza hapana anayesema na mwenzake, wote wamekaa kimya kama mabubu... Kwao wote, siku ile ilikuwa ni kitendawili kila mmoja akijaribu kukitegua. Wamekaa vyumbani wanasubiri, wamevalia vizuri utadhani mabwana arusi wanaopelekwa kuingia nyumbani. Baada ya kimya cha muda mrefu mle chumbani mwao, Edi akauliza kwa sauti yake ya kitoto, “Leo nd’o tunatoka?” (uk. 228).

Mfano huu, kama iliyotangulia inadhihirisha zaidi hali ya taharuki waliyomo wahusika katika riwaya ya *Haini*. Wamekaa tu, hawana habari kuhusu yanayoendelea. Wanatolewa vyumbani na kufikishwa mahakamani na kesi ya uhaini kuanza rasmi. Wanapoingia na kukaa mahakamani, taharuki inatawala. Hakuna anayejua kesi yenyewe itakuwaje, wala mwisho wake utakuwa upi:

Kimya kilichokuwemo ndani ya ukumbi wa mahakama kilipotea kidogo pale askari wawili walipoingia na kuwafungua pingu washtakiwa. Kimya kikarudi upya pale kwenye ukumbi wa mahakama mpaka pale mahakimu watau walipoingia kwa kupitia mlango wa kule liliko jukwaa...(uk. 232).

Mwendeshaji mashtaka anapokaribia kumaliza maelezo yake kuhusu kesi ile ya uhaini, anasababisha hali ya taharuki. Wote waliomo mahakamni wamenyamaza, wanamsikiliza kwa makini, hawajui atasema nini zaidi ule uongo aliotoa katika maelezo yake ya kesi ile, (uk. 234).

Hatimaye, baada ya kesi ya uhaini kusikilizwa kwa kipindi cha mwaka mmoja, wakati wa kutoa hukumu ukafika. Mahakimu wakaahirisha kesi kwa nusu saa ili wafanye uamuzi. Katika kipindi hiki, kila mtu roho iko juu, maelezo yametolewa, ushahidi ukatolewa na washtakiwa wenyewe wakajitetea, ila hakuna ajuaye atakavyohukumiwa; ama kifungo, kuachiliwa huru au kifo. Hali hii inajitokeza ifuatavyo:

Kwa muda wa nusu saa nzima ukumbi wa mahakama ulikumbwa na kimya cha mfululizo, hakuna aliyethubutu kufungua mdomo akasema na mwenzake. Hali ya hofu kubwa ilionekana waziwazi kwenye nyuso za washtakiwa. Washajijua kwamba sasa si wa kwa Ba Mkwe tena na ugeni wao kwa Mzee Machale umekwisha. Wakitoka pale ni safari ya moja kwa moja mpaka “Kondem” kule wanakotelekezwa waliohukumiwa kifo, wakilala kitanzi kiko mbele yao, wakiamka kiko mbele yao mpaka siku yao ya kutolewa roho ifike...(uk. 262).

Dondoo hili linaweka wazi zaidi namna kimya kinavyoathiri utendaji. Kimya kinazua taharuki katika ukumbi wa mahakama huku kila mshtakiwa akijiwazia tu. Hakuna anayejua kesi ile itakavyokuwa na wanahofia kuuawa. Kimya kinatumika kusababisha taharuki kwa kutosema chochote. Wahusika katika matukio haya wanakosa kujua yanayoendela na yatakayotokea wakati wowote ule.

(b) Kuashiria Hofu Na Wasiwasi

Kimya katika riwaya ya *Haini*, kama vile sauti, kimetumika kuzua hofu na wasiwasi miongoni mwa wahusika na hadhira kwa jumla. Tazama mifano ifutayo:

Mfano 4.18

Ikiwa jela kuna afadhali yoyote, basi usiku wa Kumbakumba una afadhali kubwa kwani huko, angalau watu hujiliwaza kwa uraibu kwa wale wanaovuta bangi na sigareti na wacha Mungu huvuta uradi na kusoma dua nzito nzito. Lakini huku kwa Ba Mkwe, kuko kimya jii, hakuna hata anayenong'ona. Wa humo huwa wamejiinamia, si mchana si usiku, wanasubiri tu, hawajui nini kimewakabili. Hawaoni kitu ila kiza totoro kimetanda mbele yao. Wamekata tamaa, wako karibu zaidi na mauti kuliko uhai. Hawajui kitu...(uk. 43-44).

Gereza la kwa Ba Mkwe ndiko wafungwa hupelekwa kuteswa, wakakabiliana na dhuluma zaidi ya za kule Kumbakumba. Kule Kumbakumba wafungwa huweza kuwasiliana na wenzao katika vyumba vingine mara moja moja pale wanapotolewa nje kuoga, kufua na kukatana nywele, na wakati mwingine wakipeleka mitondoo nje.

Huku kwa Ba Mkwe mambo ni tofauti. Ni kimya tu, ambayo ni mbinu mojawapo ya kuwazidishia waliomo hofu , wasiwasi na woga.

Sururu anapokamatwa baada ya mpango wake wa kata mbuga kutofaulu, anafungiwa chumbani peke yake kule kwa Ba Mkwe. Msimulizi anaeleza:

Mfano 4.19

Siku zote mbili walimwacha (Sururu) vilevile na pingu zake mikononi na miguuni, akila hivyo hiviyo, akilala hivyo hivyo, kila kitu hivyo hivyo. Yumo chumbani anasononeka peke yake. Hapa hakuna dalili ya uhai. Tofauti na Kumbakumba ambako kumejaa uhai tele, ambako angalau utaiona sura ya binadamu mwenzako au utapata mtu wa kusema naye, huku kukimya na kama utasikia sauti ya mtu basi ni ya kunong'ona tu...(uk. 127).

Kwa mujibu wa msimulizi, 'hofu ya kwa Ba Mkwe huzidi kustawi kwa ule ukimya ulioyazunguka mazingira yote ya nyumba ile. Humo watu husema kwa kunong'ona tu hakuna anayethubutu kunyanyua sauti yake...' (uk. 199).

Kwa upande mwingine, maafisa wa kwa Ba Mkwe huogopwa zaidi ya wale wa Kumbakumba, kutokana na ukatili wao. Wanapoingia wao tu ndio husikika, na wengine huwa mikononi mwao; wao ndio wenye nguvu na satua:

Mfano 4.20

Zile kelele zilizokuwa zikivuma pale uwanjani zilikatika kwa ghafla pakawa kimya kama palipopitwa na ibilisi. Vijana wa kwa Ba Mkwe wakaanza kuingia mmoja mmoja. Waliingia kwa mikogo na maringo. Wa kwanza kuingia alikuwa yule anayevuma sana kule kwa Ba Mkwe kwa ukatili na unyama wake...(uk. 100).

Vijana hawa wa kwa Ba Mkwe ni wale ambao wamekabidhiwa kazi ya kuwatesa mahaini panapokuwa na haja. Wapo wakubwa wao ambao uwepo wao tu huzua hofu hata zaidi ya ile wanayozua vijana wenyewe:

Mfano 4.21

Kilizuka kimya cha ghafula pale watu watatu walipoingia kutoka kule ofisini. Uwanjani palikuwa jii, hapana hata anayetikisika. Wale maafisa usalama waliokuwa wakijibahashua pale uwanjani nao wakakaa juu ya baraza ya banda, mle wanamokula wafungwa...wote watatu walikuwa waheshimiwa. Walifuatana na Mkuu wa Magereza na Chifu wa gereza la Kinoa Miguu...(uk. 102).

Haramia anapopelekwa *Mashakani Hotel*, kimya anachokabiliana nacho kule ni cha kutia hofu. Hiyo ni hali ya kimakusudi inayonuiwa kuzidisha mateso katika hoteli ile:

...Na ukimya wote wa pahala hapo, walinzi wa jumba hilo kila wakati wapo makini, hawasinzii wala hawadorori ila ni wakakamavu usiku na mchana...(uk. 168).

Kutokana na mifano hii, inabainika namna ambavyo kimya kimetumika kuzua taharuki, hofu na wasiwasi miongoni mwa wafungwa. Kama vile sauti, kimya nacho kimetumika kama mbinu ya kuwatesa mateka wa kule kwa Ba Mkwe. Kimya hiki kinapojumuishwa ipasavyo katika utendaji wa kazi hii, kitachangia pakubwa katika kufanikisha utendaji wake. Kama Schechner (1988) anavyodai, vipengele vya sauti na kimya vikijumuishwa na matini, maleba, wakati [vimulimuli na kiza] na rithimu, vitajisuka katika ruwaza itakayofanikisha utendaji kwenye jukwaa.

4.4 Hitimisho

Katika sura hii, tumejadili kwa kina namna ambavyo mwandishi ametumia masimulizi ya utendaji, kimya na sauti, kiza na vimulimuli katika riwaya ya *Haini*. Tumeonyesha namna vipengele hivi vimetumika ili kufanikisha utendaji wa kazi hii kwa njia na ngazi mbalimbali. Katika sura ifuatayo, tunajadili namna taswira za kifilamu, mandhari na maleba yanavyobainika katika riwaya hii, pamoja na mchango wa vipengele hivi vya utendaji katika kufanikisha utendaji wa riwaya ya *Haini*.

SURA YA TANO

TASWIRA ZA KIFILAMU

5.0 Utangulizi

Katika sura ya nne tumeangazia masimulizi ya utendaji, sauti na kimya, na kiza na vimulimuli vinavyoendeleza utendaji katika riwaya ya *Haini*. Katika sura hii, tunachunguza taswira za kifilamu, mandhari, na maleba kama vipengele vya utendaji vinavyochangia katika utendaji wa riwaya ya *Haini*.

5.1 Taswira

Wamitila (2003) anafafanua taswira kama picha ambazo humjia msomaji akilini anapoisoma kazi ya fasihi. Picha hizo hujengwa kutokana na maelezo ya mwandishi au tamathali za usemi alizotumia. Tunaweza kueleza taswira kama matumizi ya lugha ambayo inachora picha za watu, vitu au mahali kwa kutumia ishara. Katika kazi za fasihi ambamo taswira imetumiwa, tunaweza kubainisha maelezo ambayo kwa jinsi yamepangwa na msanii, huweza kuifanya hadhira ipate aina mbalimbali za maana au hisia.

5.1.1 Taswira za Kifilamu

Taswira za kifilamu hurejelea aina za taswira ambazo hufungamana na utendaji na ambazo huteka hadhira kihisia na kimawazo, pamoja na kumfanya ahisi kama ambaye anatazama filamu na sio kusoma au kusigiza kazi husika ya fasihi. Aina zingine za taswira aghalabu hutuchorea picha ya kile ambacho mwanafasihi anazungumzia katika kazi yake. Zipo taswira kwa mfano ambazo hutuchorea picha za wahusika na kutueleza maumbile yao, matendo na hata mahusiano yao, mandhari mbalimbali ambamo matukio katika kazi hiyo hufanyika, hali ilivyo katika tukio fulani na taswira

zingine huibua hisia fulani kwa msomaji; akapenda, akachukia, akafurahi au akakasirishwa na yale anayoyasoma.

Tofauti na taswira hizi, taswira za kifilamu hufungamana zaidi na utendaji. Hali hii humfanya msomaji kuhisi kama ambaye anashuhudia moja kwa moja tukio hilo ambamo taswira hizi zimetumika. Aidha, mbali na kutuchorea picha halisi ya yanayotendeka katika tukio fulani, taswira hizi zinahamisha msomaji kutoka dunia yake halisi na kumpeleka kimawazo na kihisia katika ulimwengu ambamo tukio husika linatendeka. Hali hii ndiyo tunafananisha na kutazama filamu. Hii ni kwa vile imevuka mipaka ya usomaji au usikilizaji. Vinginevyo, taswira za kifilamu huweka tukio fulani wazi zaidi, kwa kumpeleka msomaji kimawazo na kihisia, katika mahali, wakati na kumjumuisha na wahusika wa tukio mahsus. Kutokana na hali hii, ujumbe aliokusudia mwandishi kwa hadhira yake huwa umewasilishwa. Katika riwaya ya Haini, taswira hizi za kifilamu zimefungamana kwa kiasi kikubwa na matukio yanayotokea gerezani na kuweka wazi mateso na dhuluma wanazopitia wafungwa.

Tutazame mifano ifuatayo:

Mfano 5.1

“Sasa utasema au vipi?” Aliuliza yule askari usalama.

“Kama kuna nnalolijua ntasema, lakini hayo ya mauaji mimi siyajui.”

“Hujui? Ngoja basi!”

Yule askari usalama akalivuta gongo la mpera alilokuwa ameliweka chini ya meza akamtwanga nalo Hamza kichwani kwa nguvu zake zote. Damu, mwaa, ikamwagika kama iliyotoka kwenye chemichemi. Ikatapakaa juu ya makaratasi, nyingine imemwagika chini, nyingine inamchururika usoni. Hakuwahi hata kuguna, wengine nao wakamwingilia, kama nyuki waliochokozwa. Alitolewa mle ofisini akatupwa nje juu ya ule uwanja wa sakafu na hapo ikawa

piga, piga, kinyang'anyiro, kobe. Alijaribu kuyakinga yale magongo na kukimbia lakini alizongwa akawa kama aliye ndani ya uzio, hapana hata mwanya wa kupenya. Alipigwa mpaka akashindwa kusimama. Hakuna aliyechagua pa kupiga. Walipiga popote pale. Usoni, kichwani, tumboni, mgongoni. Hamza akapondwapondwa, kachiri saga. Akaanguka kifudifudi. Hapo hapo wakamwinua na kumshika huku na huku kama mwenye kutaka kusulubiwa. Wakamchapa mgongoni shati lote likararuka nyambunyambu. Wakamrudisha kule ofisini. Kamba madhubuti ya mkonge ishafungwa. Kitanzi kinaning'inia kwenye kikuku juu ya boriti ya darini. Alivishwa kitanzi shingoni wakamburura huku na huku na yeye akawafuata kama ng'ombe aliyevishwa shemere. Damu ikimwagika, denda inamchururika. Alipiga kelele kuomba huruma mpaka sauti ikampotea ikawa haitoki tena. Lakini huruma itoke wapi ndani ya nyumba ile. Alibaki kukoroma tu. Sasa wakaona wamnyonge. Wakampandisha juu ya kiti na kitanzi chake shingoni. Waliivuta ile kamba mpaka wakahakikisha kitanzi kimembana sawasawa shingoni, wakampandisha juu ya kiti halafu wakakipiga teke kiti, Hamza akawa ananing'inia na wao wanavuta kamba. Alipiga mikambi, macho yamemtoka, mikojo inamchururika kama mtoto mdogo. Walimning'iniza mpaka akakaribia kukata roho ndipo walipoiachilia kamba. Hamza akaanguka chini. Alinyanyuliwa akatupwa nje na baada ya kutua juu ya ile sakafu tu wakam'mwagia ndoo nzima ya maji kumfufua arudi tena duniani. Walipomwona anazindukana wakaanza tena, "Sasa utasema." Wote wamemzunguka, wamejaa tele pale uwanjani. Hamza amelala chali, povu la kinywa linamtoka. Ameloa damu, anatweta kama mtu anayekata roho sasa hivi na kitanzi bado anacho shingoni. Suruali yote imejaa mikojo. Aliwatazama lakini hakuona watu ila aliona umande mtupu, umetanda tele ndani ya nyumba ile. Yeye mwenyewe hajijui wala hajitambui. Alizisikia sauti zao kwa mbali, mmoja wao akisema, "Tummalize." Akapigwa teke la uso kwa kiatu cha jeshi, na hapo akapoteza fahamu kabisa, akawa kama aliyekufa fo fo fo. Aliwachwa pale pale uwanjani jua la mchana kutwa likimpiga yeye kama ng'onda aliyeantikwa. (uk. 40-41).

Katika mfano huu, wakubwa wa magereza wanamtaka Hamza aseme yote anayoyajua kuhusu mauaji ya Kigogo. Taswira ya kifilamu inatumika hapa kuonyesha namna Hamza anavyoteswa baada ya kukataa, na hii bila shaka inaibua hisia za utazamaji na sio usomaji tu. Msomaji anaona waziwazi namna Hamza anavyovamiwa na askari hawa; anavyochapwa, kutiwa kitanzi shingoni na kuning'inizwa, damu inavyomtoka kila sehemu ya mwili na vilevile denda na mikojo inavyomchururika. Tukio hili linakuwa kama filamu ambayo msomaji 'anatazama' badala ya kusoma tu.

Mfano 5.2

Hamza anatolewa gerezani na kupelekwa asikokujua. Askari bado wanamtaka aseme chochote kile anachokijua kuhusu mauaji ya Kigogo, ingawa yeye tayari amesema yote anayoyajua. Tunasimuliwa:

...Basi baada ya kutolewa ile amri tu, alipigwa munda akatupwa chini, kama ng'ombe anayetaka kuchinjwa. Alitaka kuinuka lakini hapo hapo aliwekewa guu la shingo likamdidimiza chini mpaka pumzi zikampaa. Alilazwa chali, akageuzwa, akalazwa kifudifudi, "Wanani...!" Hakuwahi kumaliza kauli yake, alisokomekwa tambara kinywani likamjaa tele, akabakia kunguruma tu, "M-m-mmmm." Maneno yamezuiwa hayatoki tena, ametiwa kizibo cha mdomo. Alizongwa kamba mwili mzima, tokea shingoni hadi miguuni, kamba ikakazwa sawasawa. Walimlaani na kumtukana, huku wakimsimanga, "Leo utasema! Utake usitake!" alibebwa kitikiti akatupwa, lakini badala ya kuanguka chini Hamza akahisi ananing'inia na kamba nyingine zinamzuia, akaning'inia na kujipigapiga na ukuta. Alihisi kwamba anateremshwa shimoni, ikamjia dhana ya kuzikwa akiwa hai...

"Utasema!" sauti nene ilimpigia kelele na aliisikia ile sauti ikivuma na kujirudia yenyewe kama kwamba kuna mtu aliyekuwa akiifuatisha. Akajua kwamba lile lilikuwa ni shimo, tena la kina kirefu sana... Ile kamba ikasita kupururiwa ikazuiwa palepale ilipo. Sasa alikuwa ananing'inia kichwa chini miguu juu, kamba imemkaza miguuni sawaswa, anayumba huku na huku akijigonga na mawe ya kuta za lile shimo. Yalimchubua na kumchuna usoni na sasa walikuwa wakimfyetulia risasi mle shimoni. Risasi zilimkosa chupuchupu, bado anaisikia ile sauti ikimwambia, "Utasema!"...(uk. 65-66).

Matukio haya yanadhihirisha mateso ambayo washukiwa wa uhalifu hupitia wanapokuwa kule gerezani. Hii inawekwa wazi zaidi na taswira hizi za kifilamu zinazobainika katika matukio haya. Taswira hizi vilevile zinafanikisha utendaji wa matukio haya kwa kuwa zinaweka wazi vipi matukio haya yalitendeka, wapi, lini na wahusika ni akina nani. Hivi ni vipengele muhimu vya kidrama vinavyodhihirika katika matumizi ya taswira hizi na hivyo kufanikisha utendaji wa matukio haya.

Mfano 5.3

Ghafula yule chatu alijizongoa akamchupia Haramia. Kufumba na kufumbua amekwishajizonga kwenye mwili wake. Haramia kazongwa mwili mzima, chatu anajivuta kwa nguvu zake zote kumbana mbavu. Haramia hakuwa na nguvu kama vile alivyodhania mwenyewe. Aliangushwa chini kama kitakataka tu lakini alipokiona kichwa cha yule chatu naye akakikamata kwa nguvu zote alizobakiwa nazo akaanza kumkeketa shingo kwa meno. Chatu alimbana Haramia kwenye mbavu barabara mpaka Haramia akashindwa kupumua. Haramia naye kakidhibiti kichwa cha chatu sawasawa anakikeketa shingo yake kwa meno, ananyofoa minofu na kuitema. Damu imemjaa kinywa kizima anafurukuta pale chini kwenye sakafu. Yeye anafurukuta chatu linapiga mikambi, kivumbi mle chumbani. Haramia alikuwa na meno makali kama kisu na kila alipokeketa alinyofoa pandikizi la minofu wa nyama ya chatu. Hakuona karaha wala kinyaa kuijaza minofu ile kinywani mibichi mibichi, damu chururu imemjaamwili mzima. Hakumwacha yule chatu mpaka alipohakikisha kwamba amekikata kichwa chake kwa meno yake mwenyewe na kuing'oa kutoka katika kiwiliwili chake. Haramia alikuwa taabani naye akaanguka pale chini ya mlango, pumzi ziko juu juu, damu ya chatu imemlevya, amepoteza fahamu...(uk. 173-174).

Mfano wa 3 kwa maoni yetu ndio kilele cha mateso na dhulma wanazopitia wafungwa gerezani katika riwaya hii. Haramia anapelekwa kule *Mashakani Hotel* na kujipata katika hali hii, amekabiliana na chatu ambaye amewekwa pale makusudi ili amle.

Katika kusimulia tukio hili, msimulizi ametumia taswira ya kifilamu kwa ufanisi mkubwa. Msomaji anaona kinyang'anyiro kilivyokuwa kati ya Haramia na Chatu hadi anapomuua kwa meno yake mwenyewe. Katika utendaji wa riwaya hii kwenye jukwaa, mtendaji anayechukua nafasi ya Haramia anaweza kuwekwa chumba kimoja na chatu bandia, kwa mfano aliyetengenezwa kwa mpira, na ndani yake atiwe maji mekundu hivi kwamba mtendaji anapomuuma kwa meno maji yale yatakuwa kama damu ya chatu halisi. Kupitia teknolojia, chatu bandia huyu anaweza kupewa miondoko ili kuwezesha kile kinyang'anyiro chao kutokea kama kilivyosimuliwa katika riwaya.

Kisa hiki kinamwathiri Haramia kisaikolojia, na hata pale anapojumuika na mwenzake, hasemi lolote. Usiku anaota ndoto mbaya kama msimulizi anavyoeleza katika dondo hili:

Haramia akaanza kuweweseka, kwanza kwa sauti ya kunong'ona halafu sauti yake ikawa inapaa taratibu, mwisho akawa anapiga kelele kama mtu anayekabwa roho, “Nyoka! Nyoka! Nyoka!” watu wote mle chumbani wakaamka, kama waliochagawa, nao wakawa wanapiga kelele, “Nyoka! Nyoka! Nyoka!” wota wamesimama kwenye pembe za kuta za kile chumba, mmoja kapanda juu ya mtondo, mwingine kakamata nondo ya dirisha ananing'inia. Kiza, hawaonani, (uk. 174).

Mfano 5.4

Baada ya siku kadhaa na Haramia kuanza kusemezana na wenzake pale chumbani tena, wafungwa hawa tisa isipokuwa Pwacha wanaamua kwamba hawatakubali kwamba walishiriki katika majaribio ya kuipindua serikali, jambo lililopelekea kifo cha Kigogo. Pwacha anaamua kuinusuru nafsi yake kwa kuwasema wenzake. Mara hii hata hivyo, wote, akiwemo Pwacha wanajipata taabani kama inavyoelezwa katika kifungu hiki:

Kanali Bunju na Kifupinyundo walipomaliza mazungumzo yao, Kanali Bunju akatoa amri, “ Haya waleteni. Kila mmoja mbele ya kaburi lake.” Walijipanga mstari mmoja wakawaongoza kama wanaocheza gwaride, wanaelekea kule yalipo makaburi. Nyuso wameziinamisha chini kama wenye kuyaonea haya mauti yaliyowakabili, jasho linawatoka, nyoyo zao zinapiga mapigo ya mshtuko mkubwa, miguu inawatetemeka, manyoya ya mwili yamewasimama. Vingosho machozi yanamtoka, anaomba kimya kimya, “Eh! Mungu tunusuru!” Pwacha alichomoka mbio pale alipokuwa amejipanga na wenzake akaenda mpaka chini ya miguu ya Kanali Bunju, akapiga magoti na kuikumbatia miguu hiyo, “Nakushika miguu! Nakushika miguu Mheshimiwa!” amejitupa chini ameinua macho yake juu, yamejaa hofu tele, anamtazama Kanali Bunju usoni. Kifupinyundo alisukuma teke kwa nguvu zake zote akampiga nalo Pwacha la kifua lakini tumbo lake likamnusuru, teke lake halikumtikisa. Alipoona lile teke halikumfanya kitu, alinyanyua mguu akamtimba bega lake la mkono wa kulia, akamsukuma huko. Pwacha akaanguka chali, tumbo juu, shuka aliyojifunga kiunoni imefunguka, mikojo inamtoka. “Mwondosheni

mpelekeni kule!” aliamrisha Kifupinyundo akionesha kule kwenye makaburi. Pwacha aligaragara pale chini akilia na kuomba, “Msalieni Mtume! Msalieni Mtume!” lakini hakuna hata mmoja aliyetaka kumsalia Mtume. Walimbeba kitikiti wakambwata pale kwenye pembe ya kaburi... Kila mmoja akasimama mbele ya kaburi lake. Kuchi mashuzi yanamtoka, anatemeka kama mgonjwa wa homa, uso kaelekeza mbinguni amenyanyua juu viganja vyake vya mikono, anaomba. Hofu ya mauti imewashukia pale uwandani. Askarijeshi wamenyanyua bunduki zao tayari ziko mabegani, wamelenga shabaha kila mmoja kamwelekeza wake mtutu wa bunduki, wanasubiri amri...Kanali Bunju aliwaangalia wale wanajeshi akanyanyua mkono wake juu. Kwa pamoja wakazikorokocha bunduki zao kuinkiza risasi katika chumba chake cha kufyatulia. Ule mlio wa “korokocho” wa bunduki zote zile kwa pamoja uliondoa lile tone la mwisho la matumaini lililobaki ndani ya moyo wa kila mmoja wa watu wale tisa... Kabla Kanali Bunju hakushusha mkono wake chini kutoa ishara kwa wale wanajeshi wafyatue risasi zao, alinyanyua sauti yake juu akawauliza kwa kelele, “Nakuulizeni mara ya mwisho! Mtakubali mtakataa!” “Tutakubali!” wote walijibu kwa umoja wao. Akawauliza mara ya pili. Wakajibu vilevile, tena sasa kwa kelele zaidi, kelele zao zikavuma pale uwandani, wote wamepiga magoti, vichwa wameviweka upande, viganja vya mikono wamevinyanyua juu, wanaomba kwa unyenyekevu nusura ya roho zao...(uk. 208-210).

Tukio hili ‘linatazamika’ kutoka mwanzo hadi mwisho kutokana na matumizi ya taswira za kifilamu. Kanali Bunju, katika tukio hili, anatumia vitisho na kuwasababishia tisa hawa mateso ya kisaikolojia na ya kimwili, ili wakubali kutoa ushahidi kama walivyokubaliana. Wanafaulu kwa kuwa kila mmoja wao anataka kuinusuru roho yake. Hata hivyo, wanajua kwamba hawakuhusika katika mauaji ya Kigogo na wala hawakuwaona wenzao wanaowasingizia kuwa walihusika, na vilevile kuwa wakiri wasikiri hatima yako ni kifo. Wote tisa wanahukumikiwa kifo kesi ya mauaji ya Kigogo inapokamilika (uk. 264).

Mfano 5.5

...Wakajaa ndani ya basi, msafara ukaanza. Ulikuwa msafara mrefu uliotanguliwa na mapikipiki manane mbele. Mapikipiki yale yalifuatwa na gari la aina ya “Land Rover” lililokuwa na king’ora na kimurimuri chekundu, kikimetameta. Magari sita yasiyokuwa na kipaa yalisheheni askari wa kuzuia fujo wote bunduki zao

wamezilenga kule kwenye lile basi lililowachukua mahaini. Hayo yalikuwa mbele. Magari mengine sita yaliyosheheni askari vilevile, nao pia bunduki zao wamezilenga kwenye lile basi, yalikuwa nyuma. Vyombo vyote hivyo viliwasha taa kali kutoa ishara ya hali ya hatari. Njiani kulikuwa hakuna hata mdudu wa mtu na mwendo wa msafara ule ulikuwa wa kasi sana. Ulipita uwanja wa gofu ukatokezea Mivinjeni, gari zinakwenda marshi marshi utadhani wanakimbilia mwisho wa dunia. Walipita V.I.Lenin Hospital kwa kishindo na walio hospitali wakabaki kuulizana, “Kumezidi nini?”...Magari yote yale na mapikipiki yakasimama kwa vishibdo mbele ya jengo la mahakama kuu ya Zanzibar... (Uk. 229).

Tukio hili linasimuliwa kwa njia inayosababisha kutazamika kwake. Msomaji anapewa uwezo wa ‘kuona’ namna yale magari na pikipiki zinavyoendeshwa kwa kasi sana na vilevile namna bunduki zilivyoelekezwa mahaini. Msomaji pia ‘anashuhudia’ vile ving’ora vinavyolizwa na vile vimulimuli vya magari haya.

Kama tulivyoeleza hapo juu, taswira za kifilamu ni zile ambazo hufungamana zaidi na utendaji kwa namna ambayo huteka hadhira kihisia na kimawazo. Hali hii humfanya msomaji ahisi kama ambaye anatazama filamu na sio tu kusoma husika. Pamoja na hayo, taswira za kifilamu humfanya mtazamaji kuhisi kama ambaye anashuhudia moja kwa moja tukio hilo ambamo taswira hizi zimetumika, hali ambayo hujipambanua zaidi wakati wa utazamaji wa utendaji wenyewe. Sifa hizi za taswira za kifilamu ndizo huwezesha taswira hizi kufanikisha utendaji wa kazi ya kidrama kwa kuwa hujumuisha hadhira katika utendaji. Jambo hili ndilo Bacon (1984) anarejelea kama ‘kuhusika katika maisha ya matini,’ hali inayowezekana kupitia utendaji wake. Hadhira ni nguzo ya utendaji kwa kuwa utendaji huilenga hadhira mahsusi, na hivyo inapohusishwa kimawazo na kihisia kikamilifu, utendaji husika huwa umefanikiwa. Taswira za kifilamu zimejumuishwa kwa kiwango kikubwa katika masimulizi ya riwaya ya *Haini*, sifa ambayo bila shaka itafanikisha utendaji wake kwenye jukwaa.

5.2 Mandhari

Mandhari ni mazingira ya utendaji. Ni yale mambo katika kazi ya fasihi yanayomwezesha msomaji wa kazi hiyo kutambua ni mahali na wakati gani mambo yanayowasilishwa yanatukia.

Gill (1985) anafafanua mandhari kama dhana pana na jumishi. Mawazo yake yanaungwa mkono na Wamitila (2008) ambaye katika maelezo yake kuhusu mandhari anajumuisha dhana za mazingira, mawanda na wakati. Wamitila anaeleza kuwa mandhari sio mazingira ya kijiografia tu bali hurejelea masuala mengine kama kipindi cha wakati wa matukio kama unavyodhihirishwa na matendo ya wahusika.

Akichunguza namna mandhari huchangia kuendeleza maudhui katika kazi za fasihi, Murungi (2013) katika tasnifu yake anaeleza kwamba:

Mandhari huwa ni kipengele muhimu katika uchanganuzi wa maudhui. Sababu ya kimsingi ni kwamba, matukio katika kazi ya fasihi na maudhui yanayosimuliwa hutendeka mahali, wakati na katika mwanda fulani. Nafasi ya mandhari katika kazi ya fasihi hutegemea nafasi yake katika uendelezaji wa maudhui. Kwa mfano, ikiwa tamthilia inawasilisha masuala ya kijamii, sharti mandhari yawe mandhari bayana kijamii ili kutia uzito uthabiti wa kimaudhui.

Mbatia (2001) anahusisha mandhari na drama moja kwa moja anapoeleza kwamba:

Mandhari ni istilahi inayohusishwa hasa na utanzu wa drama. Mandhari yanarejelea sura mahsusi inayotokana na mapambo na vifaa vilivyopangwa kwenye jukwaa. Sura hiyo huwa imedhamiriwa kuiga mazingira halisi yanayoelezwa katika tamthilia inayoigizwa. Mazingira kama hayo yanaweza kuwa nyumbani, njiani au kwenye uwanja wa vita.

Goldfarb na Wilson (2002) wanadai kwamba hadhira inapokaa kwenye thieta huwatazama watendaji kwa makini zaidi. Hata hivyo, hadhira hutambua vilevile taswira inavyojengwa kupitia matumizi ya mandhari, maleba na vimulimuli. Hadhira

pia inaweza kusikia sauti zinazotumika kuhimiza utendaji na ambazo hazikukusudiwa kujumuishwa katika utendaji kama vile mvua, radi, n.k. Wataalam hawa wanaona kwamba vipengele hivi huchangia pakubwa katika kufaulu au kutofaulu kwa utendaji kwa mujibu wa hadhira. Mwelekezi wa mchezo wa kuigiza anapoandaa mandhari hukusudia mambo kadha wa kadha kama Goldfarb na Wilson (2002) wanavyofafanua:

Kwanza, kubainisha aina ya mchezo wa kuigiza. Mandhari huwezesha kubainisha hali (mood), mtindo na namna ya utendaji. Mtindo hapa hurejelea namna ambavyo mchezo fulani wa kuigiza hutendwa, namna mandhari yalivyo, matumizi ya lugha, namna vipengele vingine vya utendaji vilivyotumiwa na vilevile namna watendaji wamesawiriwa. Mchezo wa kuigiza wa kihalisia kwa mfano huakisi namna watu wanavyoishi maisha yao ya kila siku, huku tanzia ikihitaji kwamba miondoko na utendaji kwa jumla udhihirishe udhati. (T.Y)

Ili kufafanua zaidi mandhari, wataalam hawa wanatumia mifano ya michezo ya kuigiza ambapo wanaeleza:

Tuchukue mchezo wa kuigiza, *His Blood Wedding* ulioandikwa na Federico Garcia Lorca ambao unahusu mwanamke ambaye siku ya harusi yake hutorokea msituni na mpenzi wake wa zamani. Yanayoonekana huko msituni ni pamoja na mwezi na ajuza mmoja anayewakilisha kifo. Wawili hawa wanajipata katika njia panda; hawajui ikiwa waende kukaa pamoja na hivyo kutii mapenzi yao au waheshimu aila zao na kuachana. Katika tukio kama hili, mandhari na maleba sharti yatumiwe kuashiria mvutano huu wa fikra na hisia. Kwa mfano, si lazima msitu uwasilishwe kwa miti kwenye jukwaa lakini lazima mandhari yawasilishe hali hii wanamojipata watendaji hawa wawili; yabainishe hisia (*emotions*) na fikra zao. Mwezi na yule ajuza vilevile sio lazima wawepo lakini sharti wawakilishwe kwenye mandhari ili kuonyesha mivutano ya hali inayowakumba watendaji hawa wawili. (T.Y)

Kwa hivyo mandhari katika utendaji huwa muhimu katika kubainishia hadhira ikiwa utendaji husika ni wa kihalisia au wa kimazingaombwe. Wataalam hawa wanasisitiza kwamba:

Ikiwa mchezo wa kuigiza ni wa kihalisia, kila kitu kuhusu utendaji huo sharti kiambatane na namna hali halisi ya maisha ilivyo. Hii inajumuisha namna watendaji wanavyozungumza na kutenda, nguo wanazovaa, matukio yanayotukia katika mchezo huo wa kuigiza na hata mazingira yenyewe yawe ya kihalisia. Watendaji wanaotenda katika sebule au baa kwa mfano wanatarajiwa kuonekana namna watu katika sehemu hizo halisi wanavyotarajiwa kuwa. Kwa upande mwingine, ikiwa utendaji sio wa kihalisia, mambo yote yanayohusiana nao hayafai kuwa ya kihalisia. Kwa mfano, melodrama huwa haina uhalisia kwa kuwa hutawaliwa na watendaji wanaoimba na kucheza ngoma ilhali hali sivyo ilivyo katika maisha halisi. (T.Y)

Wanaeleza zaidi kwamba mandhari hutumiwa katika utendaji ili kubainisha mahali na wakati wa utendaji huo. Pindi wanapoanza kuigiza kwenye jukwaa, watazamaji wanafaa kujua moja kwa moja mahali na wakati wa matukio yanayotendwa. Je, mahali hapo ni chumba cha kulala, kortini, ikulu au ni msituni? Mandhari yabainishe vilevile wakati matukio yanatendeka. Chumba cha kupikia kwa mfano, chenye vyombo vya kizamani visivyotumia umeme huashiria kwamba matukio katika mchezo husika yalitukia enzi kabla ya nguvu za umeme kuanza kutumika; kwamba ni matukio ya kizamani na sio ya kisasa.

Mbali na kueleza mahali na wakati utendaji ulitukia, mandhari hueleza ni watendaji wa aina gani wanaohusika katika mchezo wa kuigiza. Goldfarb na Wilson (2002), wakifafanua hoja hii wanadai kwamba kutegemea mandhari, watazamaji wanaweza kujua moja kwa moja ikiwa wahusika watakuwa maskini au matajiri, wafalme au watumwa, n.k. Wanasisitiza kwamba sharti mandhari yaweke mambo haya wazi moja kwa moja.

Katika utendaji, kama inavyobainika, mandhari huwa na umuhimu wa kukamilisha vipengele vingine vya utendaji. Mandhari hayafai kujisimamia kivyake wala kujitenga na vipengele kama vile maleba, vimulimuli, kiza, sauti au kimya. Kwa mfano, ikiwa masimulizi ya utendaji ni ya kihalisia, mandhari sharti yawe ya kihalisia. Hata hivyo,

Goldfarb na Wilson wanadai kwamba mandhari yanaweza kukiuka madai haya ikiwa mwelekezi wa utendaji husika ananua kwamba mandhari yatumike kijazanda; na hivyo kuwa na uwezekano wa kuwa tofauti na hali inayoashiriwa na vipengele vingine vya utendaji.

Wataalam hawa wanaeleza mambo kadhaa ambayo mwandalizi au mtayarishi wa mandhari anafaa kuzingatia ili mandhari husika yafaulishe utendaji kwenye jukwaa.

Kwanza ni mahali penyewe pa utendaji. Wanadai kwamba:

Jukwaa lazima liwe kubwa kiasi cha watendaji husika kutoshea hapo. Ukubwa au udogo wa jukwaa uzingatiwe ili kukidhi mahitaji ya idadi ya watendaji. Mtayarishi vilevile azingatie namna jukwaa lilivyo. Kwa mfano, ikiwa mtendaji anahitaji kutoka nje ya jukwaa kupitia mlango wa kulia kisha arudi kwenye jukwaa kupitia mlango wa kushoto wa jukwaa, basi inamlazimu mtayarishi huyo aandae mahali nyuma ya jukwaa ambapo mtendaji huyo atapita. Ikiwa watendaji wanahitaji kubadilisha nguo kwa haraka kabla ya kurudi tena jukwaani na kuendelea na utendaji, sharti mwandalizi wa mandhari aandae chumba au mahali maalum pa kuwezesha shughuli hiyo nyuma ya jukwaa. Ikiwa kuna watendaji ambao wanafaa kupigana kwa mfano, jukwaa liruhusu miondoko ya vita hivi; kusonga mbele, kurudi nyuma, kukimbia, n.k. (T.Y)

Miondoko yoyote ile kwenye jukwaa inahitaji jukwaa ambalo litairuhusu kutekelezwa kikamilifu. Hivyo, wataalam hawa wanapendekeza kwamba ili kuhakikisha jambo hili limezingatiwa, ni bora ikiwa mtayarishi wa mandhari atashirikiana na mwelekezi wa mchezo wa kuigiza. Wanaeleza zaidi kwamba:

Namna milango inafaa kufungwa na kufunguka, mahali samani kama vile viti na meza zinafaa kuwa lazima ieleweke na ijitokeze kwenye jukwaa kama ilivyo kwenye maelezo ya utendaji. Watendaji nao sharti waweze kutoka sehemu moja ya jukwaa hadi nyingine bila tatizo, pamoja na kuweza kupanda na kushuka ngazi ikiwa zipo. (T.Y)

Katika miaka michache iliyopita, utayarishaji wa mandhari umerahisishwa na maendeleo ya kiteknolojia. Mandhari changamano na hata mabadiliko ya mandhari wakati wa utendaji yamewezeshwa na matumizi ya teknolojia. Wanafafanua kwamba:

Kwa kutumia tarakilishi kwa mfano, mandhari yanayohitajika yanaweza kujengwa na kubadilika kutoka tukio moja hadi lingine bila kuvuruga wala kusitisha utendaji. Mandhari yenye mwangaza na rangi tofauti tofauti yanawezeshwa na teknolojia. Watendaji vilevile wanaweza kusimama kwenye mashine zinazosonga, baadhi wakiingia na wengine wakiondoka, vivyo hivyo kutegemea mahitaji ya mchezo wa kuigiza. Ujenzi wa mandhari kwa mfano yenye vivuli nyuma ya watendaji katika tukio la kutisha huwezesha kwa kiwando kikubwa na matumizi ya teknolojia. Mashetani, katika baadhi ya matukio huweza kuumbwa na kuwasilishwa kiteknolojia ili kufaulisha utendaji husika.

Ili kufaulu katika uandalizi wa mandhari ambayo yatawezesha utendaji, mtayarishi anapaswa kusoma matini inayoigizwa ili apate picha kamili ya mandhari yanayohitajika. Kisha, ashirikiane na mwelekezi wa mchezo huo wa kuigiza na kwa pamoja, wanaweza kukubali ama mandhari watakayotumia yalingane na aliyoeleza msimulizi au wajumuishe ubunifu wao ili kuyaboresha mandhari hayo.

Msimulizi wa riwaya ya *Haini* ameeleza kwa kina namna mandhari ambamo matukio yanatukia yalivyo. Anaelekea kufuata maelezo ya Ntaragwi (2004) kuhusu matumizi ya mandhari. Ntaragwi anaeleza mandhari kama sura ya mahali, hususan jinsi panavyoonekana katika hali halisi ya maisha. Mtunzi wa kazi ya fasihi anaweza kutumia maelezo ya mandhari kuelezea mazingira halisi ya kisa anachosimulia katika kazi yake. Mathalan, mwandishi anaweza kutuchorea mandhari ya pwani kwa kuwa tukio fulani linatendeka pwani. Hapa, akatuchorea vitu kama minazi, nyumba za makuti na bahari. Haya ni mandhari halisi na huleta ufasaha katika utunzi husika.

Mandhari katika riwaya ya *Haini* ni mengi kadri matukio yalivyo. Mandhari tuliyojadili ni pamoja na kule ambako mahaini wamefungwa, wanakohjiwa na kushawishiwa na hatimaye wanakotesewa. Tutazame mifano ifuatayo.

5.2.1 Mahaini Walikozuliwa

Yapo maelezo yaliyotolewa na msimulizi yanayotufafanulia kwa kina namna mahali ambapo mahaini walizuliwa palivyokuwa. Punde baada ya kukamatwa, washukiwa wa tukio la uhaini wanapelekwa moja kwa moja mpaka Kinoamiguu, jela kuu ya Zanzibar. Mandhari ya jela hii yameelezwa kwa kina. Baada ya Hamza kukamatwa na kufikishwa Kinoamiguu tunaeleza kwamba:

Mfano 5.6

Alifungua [Koplo aliyekuwa akiwaongoza watuhumiwa] lango la kwanza la chuma, wakatokezea sehemu yenye eneo tupu. Akafungua lango la pili la chuma wakatokezea sehemu ya ulinzi pale wanapokaa askari. Akafungua lango la tatu la chuma wakatokezea kwenye uwanja mkubwa wa gereza lile pale wanapokusanywa wafungwa. Akafungua lando la nne la chuma wakaingia sehemu yenye vyumba vya wafungwa. Hapo walingizwa vyumbani kusubiri hatima yao. Hamza alitiwa chumba chake peke yake. Kilikuwa chumba kikubwa cha kiasi mita tano za mraba. Kitupu, hamna chochote ndani zaidi ya ndoo moja tupu, mbovu. Kilikuwa na dirisha moja tu nalo lilikuwa juu ambako huwezi kufika kwa kuchungulia. Chini ni sakafu tupu, hakuna hata kipande cha mkeka cha angalau mtu kuweza kujinyosha. Alisimama katikati ya kile chumba akakitazama, lakini hamkuwa na cha kutazama. Ni kuta nne tu zimemzunguka kama kaburi. Yuko gerezani, (uk. 11).

Katika mfano huu, tunasimuliwa kwa kina namna walikofungiwa mahaini kulivyokuwa. Kuna milango mingi ili kuhakikisha kwamba sio rahisi kwao kutoroka. Namna vyumba vyao vilivyo ni jambo lililowekwa wazi. Mabango yenye michoro hii inaweza kuangikwa kwenye jukwaa ili kuwasilisha mandhari haya. Mandhari haya yanaelezwa yalivyo kijiografia kwa kina zaidi kama yanavyoonekana na mtu aliye juu, anayatazama chini yake:

Pale alipo Koplo Ngwali ni katika ile sehemu ya Kumbakumba, amekwea juu, kila kitu anakiona kimedumaa chini yake. Kaskazini mwake, kilima cha Kinoamiguu kinateremka kwa kasi kuelekea Mivinjeni na kusini kilima hicho kimeinuka ghafula kinapandishia Mazizini. Mashariki ndiko liliko gereza lenyewe, analitazama kwa pale juu alipo na magharibi majumba ya ghorofa ya Kilimani yamejipanga msururu. Koplo Ngwali hakushughulishwa na rangi nzuri ya samawati ya mbingu zilizoshikamana na bahari ya Kizingo kule kwenye upeo wa macho yake upande wake wa magharibi...(uk. 121).

Mfano 5.7

...walipita chini ya lile kuta Hamza akaliangalia jinsi lilivyojizatiti na kusimama imara kuizunguka ile ngome ya wahalifu, watenda maasi. Jinsi lilivyozunguka dunia ile, dunia ya peke yake. Siyo ile dunia iliyojaa raha, starehe na anasa. Siyo ile dunia iliyojaa kila chenye kuweza kukidhi matamano ya binadamu. Hii ni dunia ya wale waliolaaniwa na Mungu akawahizi, akawatupilia mbali humo waone adhabu yake wakiwa hapa hapa duniani...(uk. 99).

Dondoo hili linaweka wazi namna mahali walimojipata wafungwa katika riwaya ya *Haini* palivyo; wamo chini ya ulinzi kila wakati, ukuta mrefu uliolizunguka gereza lote hivi kwamba mandhari yenyewe hayaruhusu mfungwa kutoroka kwa urahisi. Hivi ndivyo mandhari haya yanapaswa kuwasilishwa kwenye jukwaa.

Mfano 5.8

Kule kwa Ba Mkwe mandhari yanatisha hata zaidi kuliko yale ya gereza la Kinoamiguu. Huko ndiko wafungwa hatari, au waliojaribu kutoroka wakashindwa hufungwa. Huko ndiko kulikojaa mateso na dhuluma. Mandhari yenyewe yanavyoonekana yanaashiria hali hii na hivyo kurahisisha utendaji. Msimulizi anayaeleza ifuatavyo:

Kwa Ba Mkwe kulikuwa vilevile, ukiingia utadhani umeingia giningi, nyumba ya mazuzu na mabubu, wote wamefichwa vyumbani kama vizuu. Zile kikiri kakara za wapishi alizokuwa [Hamza] akizisikia kule tokea alfajiri na mchana wote mpaka usiku, leo hazipo, hazisikii tena, yuko mbali nazo. Zile kwake zilikuwa ni

ishara ya uhai, ni dalili ya maisha, hata kama maisha yenyewe ni ya dhiki tupu...(uk. 93).

Aghalabu mandhari haya huwa ya kutisha kwa kuwa hakuna raha inayohusishwa na mahali kama gerezani. Ni mahali pa dhiki na kisirani. Vyumba wanamofungiwa vinakosa vitu muhimu vya kutumia vinavyopatikana nyumbani au mahali pengine pasipo gerezani. Ni pachafu kwa kuwa sio wengi wanaowajali waliofungwa mle, kwani wameletwa huko kusudi wateseke. Tazama:

Mfano 5.9

“Saa wataleta magodoro?” aliuliza, ki-lillahi, hakukusudia mzaha wala kejeli. Abdul alimtaazama akataka kumwambia kitu lakini maneno yakamkwama. Akawa kama ana kigugumizi. Alishusha pumzi chini kama kumwambia maskini roho yako. Halafu akamwambia kwa upole, “Unaiona hii sakafu usiyotaka kuigusa? Hiki nd’o kitanda chako, nd’o godoro lako, nd’o mto wako, nd’o shuka yako ya kujifunika.” “Ehh!” alishtuka. “Manake! Manake!” “Manake utalala hapo juu ya sakafu usiyotaka kuigusa,” Abdul alimaliza maneno yake. Yule kijana alimtaazama Abdul kwa macho ya hasira, bado amechutama, amechukizwa na hali yote ya chumba kile. Amezungukwa na uchafu. Chumba kichafu, waliomo wachafu, hewa ya chumbani mle chafu, kila kitu kichafu isipokuwa yeye tu...(uk. 16).

Hali ya vyumba hivi inahuzunisha na kukatisha tamaa. Haviwapi waliomo matumaini ya kesho, wala lolote la kufurahia. Uwezo wa mandhari kudhihirisha hali za wahusika ni muhimu katika kufanikisha utendaji. Hivyo, Adam Shafi anapobainisha hali ya wahusika wake kule jela anarahisisha utendaji wa kazi hii iwapo itaandaliwa mchezo wa kuigiza na kuwekwa kwenye jukwaa. Msimulizi kwa mfano, anaeleza namna hali ilivyokuwa katika chumba walimofungiwa Hamza na wenzake:

Mfano 5.10

Chumba kile kilikuwa kizito kimesheheni majonzi yaliyojaa yaliyojaa ndani ya nyoyo zao wote. Kimejaa masikitiko na malalamiko yao. Masikitiko na malalamiko ambayo hapakuwa na

yeyote wa kuyasikiliza, angalau akawaangalia kwa jicho la rehema. Wako peke yao, wanasononeka. Wamezungumza wakamaliza mazungumzo yote. Sasa hawana la kuzungumza wamebaki kugombana. Wamepika wamemaliza vyakula vyote...Kumbakumba imekumbwa na jinamizi, kila mtu amejinamia. Wote wamekaa tu, hakuna ajuaye hatima. Wamebaki kubahatisha, “Labda hivi labda vile. Labda leo labda kesho.” Siku zinakwenda...(uk. 91).

Wafungwa walikozuiliwa ni mandhari yanayotusawiria hali halisi ya magereza mengi, na matukio yanayotukia huko yanaaminika kwamba yanaweza kutokea gereza lolote lile barani Afrika.

5.2.2 Mahaini Wanakohojiwa na Kushawishiwa

Mahaini wanakamatwa na kufungiwa vyumbani katika magereza ya Kinoamiguu na kwa Ba Mkwe. Hapo, uchunguzi wa kutafuta aliyemuua Kigogo unaanza, na mahaini hawa wanajipata wakihojiwa waseme chochote wanachokijua kuhusiana na mpango wa uhaini uliopheleka kifo cha Kigogo. Baadhi wanashawishiwa wakubali kuwa walishiriki katika mpango huo ili kufanikisha kesi ya taifa dhidi ya washtakiwa. Wapo wanaokubali huku wengine wakishikilia kutohusika kwao licha ya mateso na dhuluma za pale gerezani. Yapo mandhari mbalimbali ambako kuhoji na kushawishi huku kunatekelezwa. Mahali wanakohojiwa mahaini kunachukua mfumo wa ofisi au chumba chochote maalum kwa ajili ya mazungumzo. Vyumba vya ushawishi kwa upande mwingine vinakuwa vizuri zaidi ili kuzidisha uwezekano wa anayeshawishiwa kushawishika.

Hamza, rafikiye mshukiwa mkuu wa mauaji ya Kigogo anahojiwa mara kadha wa kadha, kutokana na imani kwamba Hamduni hawezi kuhusika katika mauaji ya Kigogo na Hamza, rafikiye wa karibu zaidi kutokuwepo. Mara ya kwanza anapotolewa Kumbakumba kwenda kuhojiwa anajipata katika mandhari haya kama mfano ufuatao unavyodhihirisha:

Mfano 5.11

Hamza akaingizwa ndani ya lile jengo linalokabiliana na uwanja wa sakafu, akajikuta yumo ndani ya chumba kikubwa, mbele yake kuna meza mbili zilizopangwa muundo wa T na viti vilipangwa kwenye pembe za meza zile kama kwamba kuna mkutano...ofisi ile ilikuwa ni chumba kikubwa chenye kuta nene zilizopakwa chokaa. Kilikuwa na dari ndefu iliyozuiliwa kwa boriti nene za chuma. Kwenye moja ya boriti hizo kulikuwa na vikuku viwili vyenye kuonekana kama vya kuning'iniza pembea. Kilikuwa na dirisha moja tu, juu, karibu na dari, na hilo ndilo alilokuwa amelikabili Hamza na mwanga wa jua uliopita pale ukampiga usoni moja kwa moja. Kilikuwa na sakafu inayoteleza na kwa ule ukubwa wake, sauti ndogo tu, huvuma ikatoa mngurumo mnene. "Sasa tueleze!" Alianza yule afisa wa usalama...(uk. 39-40).

Hamza anatolewa Kumbakumba mara tena na kupelekwa mbali na gereza lile, wale askari wakiwa na nia ya kumshawishi akubali kushirikiana nao; akubali kwamba kweli alishiriki katika mauaji ya Kigogo na hivyo kuwa shahidi wa mahakama. Anakopelekwa wakati wa tukio hili ni mahali tofauti na wanakopigiwa na kucharazwa wakati wakiteswa. Tazama mfano huu:

Mfano 5.12

Walielekea njia inayokwenda uwanja wa ndege lakini kabla hawakufika Kiembesamaki gari liliacha barabara, dereva akakata mkono wa kulia, wakaingia kichakani. Hawakwenda mbali, wakatokea mbele ya nyumba kubwa ya kizamani ya ghorofa moja. Nyumba yenyewe ilionekana kama gofu lililohamwa siku nyingi lakini sasa limetengenezwa vizuri likapakwa chokaa linang'ara, jeupeee. Hamza alikuwa na hakika kwamba pale ndio machinjioni, wamemleta kummaliza kabisa. Walipanda juu kwenye ile ghorofa, wakupita kwenye roshani iliyotandikwa mbao za msaji na alipokuwa hapo kwenye roshani aliiona bahari imetanda mbele ya macho yake, maji ya rangi ya ya buluu iliyokoza yanapanda na kushuka na kutifua mawimbi makubwa makubwa, yanajipinda na kujipindua na kujitandaza juu ya uso wa bahari. Halafu hujizongazonga tena na kuangukia tena ufukweni kwa kishindo na kutambaa taratibu juu ya mchanga mweupe wa ufukweni. Siku nyingi hakuona mandhari kama yale na alitamani asimame pale kwenye ile roshani aangalie uzuri ule wa bahari. Alisimama pale kama aliyezugwa, macho kayaelekeza kule baharini...walizunguka upande wa pili wa ile roshani na baada ya kuipa mgongo ile bahari iliyompumbaza walikabiliana na mlango mkubwa uliochongwa kwa nakshi nzuri.

Waliingia ndani na humo mlikuwa na watu sita. Wanne maafisa wa jeshi, wawili wamevaa nguo za kiraia...(uk. 77).

Ofisi ile ilikuwa imepambwa inapendeza. Zulia jekundu limeifunika sakafu yote ya chumba kile. Makochi manne makubwa yametandikwa mito iliyovishwa foronya za rangi ya manjano. Mlikuwa na meza nzuri ya mpingo na kiti chake cha mti huo huo, nacho pia kimetandikwa mto wenye foronya ya rangi ya manjano. Upepo kutoka baharini ulipepea moja kwa moja. Kwenye pembe moja ya chumba palikuwa na mtungi mkubwa ndani yake umemea mti wenye majani mapana mfano wa majani ya mayugwa yenye vidoto vyekundu na vyeupe. Juu ya ukuta, karibu na ile meza ya mpingo imening'inizwa picha kubwaya Kigogo amevaa sare ya jeshi akionesha kidole cha shahadi kama kumwonesha Hamza aliyekaa na kukabiliana uso kwa uso na picha ile, akimwambia, "wewe!" chumba kilikuwa na madirisha matatu makubwa, mawili mkono wa kulia na moja kule iliko ile picha. Chini ya dirisha hilo palikuwa na majalada yaliyotupwa ovyoovyo, yamejaa vumbi, dalili kwamba majalada yale yapo pale siku nyingi...Hamza amekaa lakini hakuelewa chochote katika mazungumzo waliyokuwa wakizungumza wakubwa wale. Ghafula mazungumzo yalisita, akaulizwa Hamza, "Utakunywa nini?" (uk. 78).

Mandhari haya kama mifano hii inavyodhihirisha ni ya kupendeza na yametulia, hayatii hofu wala kutisha kama yale ya wanakofungwa mahaini. Lengo kuu la uzuri wa mandhari haya ni kuwashawishi wahusika kukubaliana na wale maafisa. Mandhari haya yanafanikisha matukio haya ya kushawishi kwani japo baadhi wanakataa, wengi ni wale wanaoshawishika na kuunga upande wa mashtaka mkono.

5.2.3 Mandhari Wanakotesewa Mahaini

Mazingira ya jela yamejaa utesi na udhalimu. Mahaini wanahojiwa na kucharazwa kila uchao huku maafisa wakijaribu kupata aina yoyote ile ya habari kuhusu uhusika wa yeyote yule katika mpango uliophelekea kifo cha Kigogo. Mbali na haya mateso ya kuchapwa kila siku, yapo matukio katika riwaya ya *Haini* yanayosimulia mateso yaliyokithiri dhidi ya wafungwa na mahaini. Yanakotukia matukio haya ndiyo mandhari tunayoshughulikia katika sehemu hii. Mandhari haya aghalabu yanatisha na

kukatisha tamaa zaidi ya kule wanakofungwa kwani lengo lake hasa ni kufanikisha mateso.

Mfano 5.13

Huko ni jela ndani ya jela, wanakosokomekwa wale manunda wasiosarifika. Ndio maana wanakuuta chumba cha kiza...chumba cha kiza kiko katikati baina ya Kumbakumba, chumba cha kunyogea na jiko. Mlango wake ni wa chuma na jua la mchana kutwa hupiga mlangoni hapo. Ukuta wa chumba hicho umeshikana na jiko na kuni zote zinazoteketea jikoni hapo humimina joto lake ndani ya chumba hicho. Mchanganyiko wa joto la moto wa jikoni na joto la jua linalopiga juu ya ule mlango wa chuma mchana kutwa ndio unaotengeneza hali ya hewa ya chumba cha kiza. Joto kali hufukuta chumbani humo kutwa, kucha na inapofika usiku, mbu humiminika humo utadhani wanamiminiwa makusudi...(uk. 85).

Alipoingizwa humo jua lilikuwa limekolea mlangoni. Jikoni nako, maharagwe yanachemshwa na maji ya dona yako jikoni, kuni zinaripeka, jiko limepamba moto. Chumba chenye ni cha mita mbili za mraba na njia pekee ya kupitisha hewa ni kidirisha kidogo juu ya ule mlango wa chuma. Vuke la chumbani lilimfukiza kama aliye ndani ya tanuri. Joto linamwunguza, tundu za mwili zimejiachia anavuja jasho chururu. Mwili wote unanata anachemka kama anayechemshwa kwa jasho lake mwenyewe. Ile hali ya kuwekwa uchi katika joto kama lile ilizidi kumfadhaisha, akajiona kama mnyama aliyetiwa ndani ya kile chumba. Alikaa, akasimama, akachutama. Kila alivyofanya aliona sivyo. Akiegemea, kuta zinaunguza. Akikaa, sakafu inaunguza. Vile alivyosimama, nyayo nazo zinaungua. Afanye nini? Yumo katika nakama. Jahanamu ya hapa duniani. Mwisho alikaa, mwili wake ukalizoea joto taratibu...(uk. 86).

Tukio hili linatukia pale ambapo Hamza anakataa kushirikiana na maafisa wa kule gerezani. Kanali Bunju anakasirika na kuamrisha kwamba awekwe chumba cha kiza kwa wiki moja. Kanali Bunju anafanya hivi akijua kwamba Hamza hawezi kustahimili madhila ya chumba hicho, na inafaa iwe hivyo ili akate tamaa kwa haraka na kuwaunga mkono. Chumba cha kiza, kama msimulizi anavyokieleza, kinatupatia mandhari ambayo yanasikitisha hasa ikiwa mwanadamu atawekwa humo ndani kwa siku nyingi kama alivyowekwa Hamza. Hivyo, yanakuwa mandhari ya kukatisha

tamaa na ambayo yaliwasababisha wengi kukubali kushirikiana na akina Kanali Bunju katika uchunguzi wao wa kesi ya mauaji ya Kigogo.

Mfano 5.14

...Hilo ni pandikizi la jumba lililofichika katikati ya chaka kubwa kandokando ya bahari kaskazini ya kisiwa cha Unguja. Jumba hilo limesimama hapo lilipo kama mzimu na wanaofika hapo ni watumishi maalum wa kwa Ba Mkwe. Kama kuna mwingine anayepelekwa huko, basi huyo huwa anapelekwa huko kutolewa mhanga. Kwa ukubwa wa chaka la hapo jumba hilo limemezwa na kiza kizito kilichojikita pale usiku na mchana na kuzungukwa na ukimya mtupu. Mpaka ufike hapo lilipo, inakubidi ukabiliane na ulinzi mkali wa wanajeshi waliojizatiti sawasawa kwa silaha madhubuti pale kwenye kizuizi cha lango kubwa la chuma. Na ukimya wote wa pahala hapo, walinzi wa jumba hilo kila wakati wapo makini, hawasinzii wala hawadorori ila ni wakakamavu usiku na mchana. Jumba lenyewe limekaa kama gofu na kwa asiyelijua atadhani ni maskani ya wafu na mizuka. Kuta za nje zimejaa ukungu, si kama zimesahauliwa angalau kurashiwarashiwa chokaa ila limeachwa hivyo makusudi lioneshe hali ya kutisha. Ni jumba la kizamani la ghorofa moja lililojengwa kwa mawe na udongo. Lina vyumba chungu nzima na humo ndani hewa yake siku zote imejaa unyevu kwa kutopata nuru ya jua na kukosa loto la binadamu...(uk. 168).

(Haramia) anakiangalia kile chumba. Kikubwa kama ghala, dari iko juu sana, kina mlango mmoja mkubwa wa Kiarabu na madirisha mawili makubwa, yote yamefungwa na kugongomelewa mbao ili yasifunguke kabisa. Juu ya kiladirisha kuna shubaka kubwa. Chumba hicho kilikuwa na taa moja iliyokuwa ikitoa mwanga hafifu. Taa hiyo huwaka kutwa kucha, huwezi kujua kama ni mchana au usiku. Juu ya dari kimejaa mabuibui, kuta zimeshurubu maji, zimeshiba unyevu na pembe moja ya dari imefanya ukungu wa kijani kwa sababu ya unyevu wa muda mrefu. Akajihisi amefika. Yupo Mashakani Hotel, nyumba ya mashaka ya kwelikweli siyo mashaka ya mzaha...(uk. 169).

Katika mfano huu, Kanali Bunju, ambaye ni mmoja wa waliotajwa na Haramia anaamua kumpeleka Haramia *Mashakani Hotel*. Huku ni kule wanakopelekwa watu wasionekane tena. Anapelekwa huko kusudi aliwe na chatu, asipatikane asilani akaja kuwatia wakubwa matatani. *Mashakani Hotel*, kama Adam Shafi anavyoeleza ni mandhari ya kutisha. Ni mahali pa kifo, hapana uhai na hivyo basi yanafanikisha

utendaji wa matukio kama haya. Mandhari haya yawasilishwe kwenye jukwaa kama yalivyosimuliwa ili kuleta athari iliyokusudiwa.

Mfano 5.15

Walikuwa katikati ya uwanda mkubwa hauna kitu chochote isipokuwa vichaka vilivyotawanyika hapa, pale na kule. Kwa mbali kuna mivumo iliyojipanga safu moja na nyuma ya hiyo mivumo kuna utepe mwembamba wa bahari uliotambaa kwenye upeo wa uwanda ule, rangi yake ya feruzi ikimetameta chini ya jua kali la mchana. Makaburi tisa yalikuwa yameshachimbwa yamepangana msafa. Sasa siyo kuchungulia kaburi tena, ni kuingia hasa ndani ya hilo kaburi. Mategemeo yao yote ya uhai yamepeperushwa na upepo wa balaa na hali ya kukata tamaa ilionekana katika nyuso zao. Wingu la kiza lilitandambele yao na ile ishara yya nusura hawaioni tena imemezwa na wingu lile la nakama. Kanali Bunju akatoa amri, “Haya waleteni. Kila mmoja mbele ya kaburi lake.” (uk. 208).

Katika tukio hili, Kanali Bunju anawapeleka mashahidi hawa yalipo makaburi yao. Mandhari hayo yanatisha kwa vile kila mmoja wao anafanywa kusimama mbele ya kaburi lake, hivi kwamba anaona mauti mbele yake. Ni mandhari yanayoogofya na yanafaulu kuwafanya mashahidi hawa kutoa ushahidi wao mahakamani kama alivyotaka Kanali Bunju.

Mwandishi amefanikiwa kwa kiasi kikubwa kuwaweka wahusika wake katika mandhari mbalimbali yanayoafikiana na utendaji wao. Matukio mengi katika riwaya ya *Haini*, kama tulivyotaja hapo awali yamejaa mateso na dhuluma dhidi ya wafungwa. Hivyo, mandhari yanayotumiwa ili kufanikisha utendaji wa matukio haya sharti yawezeshe ule utesi kutekelezwa. Hivi ndivyo hali ilivyo katika riwaya ya *Haini*. Mwandishi ametumia mandhari ya kutisha na kuogofya, kusikitisha, na kuhurumisha, na ambayo yanaendana vyema na matukio yanayotendeka katika mandhari hayo. Mandhari yaliyotumiwa kushawishi yameboreshwa kuliko yale ya kutisha ili kufanikisha shughuli ya kushawishi. Tofauti kati ya aina hizi za mandhari ijitokeze kwenye jukwaa.

5.3 Maleba

Maleba ni mavazi yanayotumiwa katika utendaji wa kazi za kidrama ili kuwabainisha watendaji kwenye jukwaa. Wilson na Goldfarb (2002) wanadai kwamba maleba ni kipengele cha utendaji ambacho huandamana kwa karibu sana na watendaji, kwa kuwa wao ndio huvaa maleba yenyewe. Maleba na watendaji huonekana kwa wakati mmoja na watazamaji. Maleba yametuzunguka kote tuliko ulimwenguni. Kwa mfano, kwa kutazama tu mavazi aliyovaa mtu tunaweza kutambua yeye ni nani; polisi, mchezaji, kasisi, n.k. Zaidi ya hayo, wanaona kwamba maleba yana umuhimu wake katika utendaji.

Maleba huashiria mambo anuwai kuhusu mtendaji; hali na hadhi, jinsia, kazi anayofanya, aina ya sherehe aliyohudhuria, kuwepo au kutokuwepo kwa uhuru wake na ucheshi au unyamavu wake. an Wilson na Goldfarb (2002) waeleza zaidi kwamba punde tunapona alichokivaa mtu, huwa tunapokea taarifa kadhaa kuhusu mtu huyo. Vivyo hivyo, hata katika utendaji, mavazi aliyovaa mtendaji huwa na ujumbe kwa hadhira. Kwa mfano, kazi anayoifanya, jinsia yake na hata hali yake ya uchumi.

Mwandalizi wa maleba, kama anayeandaa mandhari sharti awe na uelewa wa kina wa mchezo husika wa kuigiza; maudhui, wakati, mtindo na dhamira yake. Kisha, aelewe mahitaji ya utendaji. Je, wahusika wanasimama, wanaketi, kucheza ngoma au kupigana katika utendaji wao? Akishajua haya anaweza kuandaa maleba ambayo yatafanikisha aina husika ya utendaji. Hatimaye afahamu sifa za kimaumbile za watendaji ili mavazi hayo yawatoshe na kuwaruhusu kutenda kama maelezo ya utendaji yanavyoelekeza.

Maleba yanafaa kukidhi mahitaji ya kibinafsi ya mtendaji. Kwa mfano, rinda refu linaweza kupendeza machoni mwa hadhira lakini sharti mtendaji aliyelivaa aweze

kutenda bila kutatizwa na urefu huo. Ikiwa watendaji watahitajika kupigana, kucheza ngoma, kuketi au kusimama, waweze kufanya hivyo pasipo kuzuiliwa na mavazi yao. Maleba hatimaye sharti yaingiliane na kukamilishana na vipengele vingine vya utendaji. Utendaji wa kihalisia uambatane na maleba ya kihalisia. Pamoja na maleba, mitindo ya nywele, vipodozi na mapiku hutumika katika utendaji. Goldfarb na Wilson wanaeleza:

Watendaji hupaka vipodozi kama vile rangi, podari, n.k. ili kuwawezesha kujifananisha na wahusika wanaowaigiza. Kwa mfano, ikiwa mtendaji kijana amechukua uhusika wa mzee, mbali na mavazi yanayoashiria uzee, atalazimika kupaka rangi nyeupe kwenye nywele na ndevu ili kuonyesha mvi. Kutokana na rangi hiyo anaonekana mwenye umri mpevu na hivyo kuaminika kwamba yeye ni mzee.

Watendaji kama vile mahakimu hujitambulisha kwa majoho yao meusi pamoja na nywele nyeupe wanazovaa kichwani. Mitindo ya nywele vilevile huonyesha hadhi na hali ya mtendaji ya kiuchumi. Mapiku ndicho kipengele cha kimsingi kinachowafanya watazamaji kujua kwamba kile wanachokitazama ni maigizo tu bali sio uhalisia wa mambo, na kwamba maigizo hayo ni kiwakilishi cha maisha halisi. Mapiku hubadilisha sura ya mtendaji na kumpa hali moja kwa muda anaohitajika kuwa katika hali hiyo (2002). (T.Y)

Katika riwaya ya *Haini*, maleba yametumiwa kuwabainisha wahusika kwa namna mbalimbali. Aina tofauti za maleba yenye rangi tofauti kwa mfano yametumiwa kuwasilishia tukio fulani kama tunavyobainisha katika mifano ifuatayo:

5.3.1 Mavazi Ya Mahaini

Kuna mavazi ambayo kila mmoja wa mahaini alikuwa amevaa wakati akikamatwa, kabla ya kupewa zile sare za gerezani. Tutazame mifano ifuatayo.

Mfano 5.16

(Shadidi) alikuwa kijana maridadi, si mfupi si mrefu. Kavalia shati safi jeupe la mikono mifupi na suruali ndefu ya dreli rangi ya kisamli. Nguo zake zimenyoshwa vizuri kwa pasi na kilichokosekana pale kutimiza uungwana wake ni viatu tu ambavyo

alivuliwa pale mapokezi alipokuwa akisachiwa. Alipoingizwa chumbani akawa kama aliyekifukiza chumba kile kwa marashi makali ya ndevu na uturi wake ukasambaa chumba kizima...(uk. 15).

Mfano 5.17

Abdul amevaa kaptura tu, tumbo wazi na Hamza ana suruali ndefu ya kijivu cha mng'aro na shati la buluu isiyokoza, nguo zile zile alizokamatwa nazo. Tokea siku aliyoingizwa mle hakuoga wala hakupiga mswaki. Nywele zimesokotana na ndevu zimeota ovyo ovyo zimeanza kukutana na masharubu...(uk. 15).

Mfano 5.18

(Shekhe Mandundu) amevaa kanzu ya darzi, nyeupe inameremeta, nyuzi za kikoi cha jabir zimening'inia chini ya ile kanzu. Amevaa kofia ya mkono ya kipande kikali cha jani la mbaazi. Alikunja kanzu yake akakaa kwa kukikalia kile kikoi...(uk. 16).

Mahaini hawa wanapokamatwa na kupelekwa gerezani, kila mmoja wao amevaa mavazi aliyokuwa amevaa wakati akikamatwa. Mavazi haya hayawezi kuwatambulisha kama mahaini, japo yanatambulisha baadhi yao kama vile wanajeshi.

Mfano 5.19

Wapo mahaini waliokamatwa na kabla ya kufungiwa mle vyumbani wakapata kichapo ambacho kiliathiri mavazi waliyokuwa wamevaa. Tofauti na Shadidi na Shekhe Mandundu katika mfano 1 na 3, mahaini hawa waliletwa chumbani nguo walizokuwa wamezaa zikiwa zimechanika kuashiria kile kichapo. Mmoja wa hao alikuwa Kondo:

Shati lake la sufi rangi ya kijani kibichi limekaa ovyo ovyo, amelichomoa kutoka surualini. Suruali yenyewe imekatika vifungo kiunoni, ameikaza kwa uzi wa gunia. Imeanza kunyambuka na magotini imeshafanya alama ya kutaka kuchanika...(uk. 25).

Katika maelezo mengine ni kwamba Sugu alikuwa amejizonga saruni kiunoni, amevaa fulana isiyokuwa na mkono, (uk. 26). Hivi ndivyo waliokamatwa waliletwa gereza la Kinoamiguu; wakiwa safi, nadhifu na wenye heshima zao. Hata hivyo, baada ya kukaa kule gerezani, kukumbana na vichapo na mateso anuwai waliyopatana

nayo kule gerezani, hali zao zinaanza kubadilika na vilevile mavazi yao. Nywele zao pia zinabadilika na kuendana na mavazi yao mabovu mabovu. Mahaini hawa wanasawiriwa kwa namna tofauti na walivyokuwa walipoletwa pale gerezani. Tazama mavazi yao yanavyobadilika wanavyozidi kukaa mle gerezani:

Mfano 5.20

Shati lake (Faraji) limejaa mabaka ya damu. Suruali kaikunja pindo kiunoni ili iweze kutulia isiporomoke. Mapele yamemjaa usoni na zile nywele zake za kipilipili zimegeuka singa kwa njaa na shida, kama zilizotiwa dawa ya “Pandora”...(uk. 100).

Mfano 5.21

Ile kanzu yake (Shekhe Mandundu) aliyoingia nayo Kumbakumba iking'ara, leo ni tambara tu, ameshindwa hata kuivaa ameitupia begani kama aliyebeba kashida...(uk. 100).

Mfano 5.22

[Sururu] alikuwa amekaa, amebanwa katikati. Amevaa fulana yake ile ile aliyokamatwa nayo ambayo jitihada zake zote alizozifanya kuifua, bado mabaka ya damu yanaonekana wazi wazi...(uk. 100)...Alikuwa amevaa kaptura na fulana yake ile ile iliyojaa madoo ya damu...(uk. 119).

Zonga anapotolewa kule mashahidi wengine walipokuwa anaambiwa avae nguo, anachukua kipande cha gunia na kujizonga kiunoni, (uk. 115).

Maleba hapa yanadhihirisha maisha wanayoishi wafungwa kule gerezani. Maisha yaliyojaa dhiki na mateso. Kutokana na mifano tuliyotoa, inaeleweka kwamba wamekuwa wakipigwa vibaya vibaya kwani nguo zao, hata walizofua zina mabaka ya damu. Mara tena, mwandishi anafanikiwa kutumia maleba kwa njia faafu. Ingekuwa vigumu maleba haya kuaminika kwa mfano ikiwa tungesimuliwa kwamba walikuwa nadhifu hata baada ya kukaa muda wote huo gerezani, na kupokea aina ya kichapo walichokuwa wamepokea. Kule kuchanika kwa mavazi ya mahaini kunaashiria mpito wa wakati na maisha magumu wanayoishi pale gerezani.

5.3.2 Sare za Mahaini

Wafungwa wanavishwa kaptura na mashati yenye mabaka meusi na meupe, hivi kwamba mhusika mwingine anapowaona anajua kwamba wao ni wafungwa. Msimulizi anaeleza kwamba sare ya Polo ya magwanda meupe yaliyo na mabaka meusi kila siku ni safi kwa kuwa yeye hufanya kazi sehemu ya ushonaji, (uk. 118). Sururu anapotoroka jela inasemekana hakuwa na nguo, isipokuwa kile kikaptura kilichomsitiri. Msimulizi anasema kwamba hicho hakina stara yoyote kwa kuwa ukikiona tu unajua kwamba ni ile sare ya mahabusu kwa yale mabaka yake meusi yaliyobobekwa ovyo ovyo, (uk. 124). Kwingineko, Sururu anapofika kwenye nyumba iliyokuwa na mwangaza, msichana mwenye nyumba anapofungua anaogopa kwa kuwa mavazi yake yanamtambulisha kama mfungwa, (uk. 125). Sururu anapokamatwa na kupelekwa kwa Ba Mkwe, tunaelezwa kwamba:

Alipotoka kule ndani, mzee Machale alikuwa amechukua nguo mkono mmoja na chupa mkono mwingine. Yalikuwa magwanda mapya, shati na kaptura yake. Siyo kama yale ya Kumbakumba yaliyobobekwa mabaka meusi. Haya meupe, hayana mabaka...(uk. 128).

Hamza anapotolewa nje kuhojiwa, tunaambiwa alitoka vilevile alivyokuwa, na kikaptura, (uk. 140). Mahaini wanapohamishwa kutoka Kumbakumba hadi kwa Ba Mkwe, wanatoka walivyo, wengine na vishuka tu walivyojizonga kiunoni na wengine vikaptura, matumbo wazi, (uk. 205). Hatimaye, mashahidi wanapopelekwa mahakamani tunaelezwa kwamba walikuwa vilevile,, na vikaptura na vishuka, (uk. 210).

5.3.3 Mavazi ya Polisi

Kuna baadhi ya nyakati katika maisha halisi tunamoishi ambapo maafisa wa polisi, hasa wa kitengo cha uchunguzi huvaa mavazi ya kiraia, badala ya sare zao. Lengo

huwa ni kutotambulika kama polisi, na hivyo kurahisisha uchunguzi wao. Kuna baadhi ya maafisa wa polisi wanaovaa mavazi ya kiraia. Tazama mifano hii:

Askari mmoja amesimama nyuma ya meza ya makaribisho. Mtu mmoja mfupi mwembamba amesimama pembeni. Amevaa nguo za kiraia tu, suruali ndefu, shati jeupe, kofia ya mkono na viatu vya makubadhi... Hamza moyo ulimpiga. Anamjua vizuri mtu yule. Maarufu katika kikosi cha usalama chenye kila sifa ya ukali na ukatili, (uk. 36).

Hamza anapotolewa chumbani kwenda kutia saina maelezo yaliyokuwa kwenye jalada, msimulizi anaeleza kwamba alikopelekwa aliwakuta watu watano. Katika hao, wawili walikuwa maafisa wa usalama na ‘nguo zao za kawaida’. (uk. 140).

Japo maafisa hawa wamevishwa mavazi ya kiraia, hatupati sababu maalum ya kufanya hivyo. Wanajulikana kwamba wao ni askari au maafisa wa polisi, na hivyo kuvishwa kwao mavazi ya kiraia hakueleweki. Hata hivyo, hali hii imejitokeza katika matukio machache sana katika riwaya ya *Haini*. Hii haizuii kutendeka kwa riwaya ya *Haini*, japo mabadiliko yanaweza kufanywa, polisi hao wakavishwa sare zao.

5.3.4 Sare za Maafisa wa Usalama

Katika riwaya ya *Haini*, kama inavyotukia katika hali halisi ya maisha, maafisa wa usalama, mbali na kuvishwa sare zinazowatofautisha na wafungwa, wanavishwa tepe zinazowabainisha kwa mujibu wa vyeo vyao. Wapo wenye tepe nyingi ambao wanachukua ngazi ya juu zaidi kuliko wenzao wenye tepe na nyota chache. Vilevile, rangi za sare hizi huenda zikawa tofauti, kwa mfano wapo wanaovaa zenye rangi ya kijani, wengine samawati iliyokoza na baadhi kaki. Rangi hizi zinawatofautisha kutegemea mhusika ni aina gani ya afisa; polisi, koplo au polisi wa uchunguzi. Tofauti na sare za wafungwa ambazo ni chafu na zilizochanika, sare za maafisa hawa ni safi, zilizopigwa pasi na zenye kila heshima anayostahiki afisa.

Mfano 5.23

[Koplo Fataki] alivaa pama ya kitambaa cha kaki akaiteremsha mpaka kipajini ikakurubia kuigusa ile miwani yake. Sare yake ya kaki imetakata. Makali ya pasi yanaonekana wazi wazi jinsi yalivyong'ang'anaa kwa uwanga na tepe zake mbili zikining'inia chini ya bega la mkono wa kushoto. Viatu vyake vyeusi vimekubali rangi, vinametameta na kiunoni amejifunga ukanda mpana wa kitambaa cha turubali wenye vifungio vya shaba vinavyong'ara vizuri...(uk. 34).

Mfano 5.24

Mavazi ya afisa katika ngazi ya ukapteni yanakuwa tofauti na ya Koplo kama mfano huu unavyobainisha:

...leo mlango umefunguliwa na afisa wa jeshi, amesimama mlangoni. Mrefu, mwingi wa mwili, amejaza vizuri, amependeza na ile sare yake ya rangi ya kijani kibichi. Amebeba nyota tatu kila bega zinameremeta kwa ile rangi yake ya dhahabu. Alipofungua ule mlango hewa ya mle chumbani ilijaa riha nzuri ya mafuta ya ndevu aliyojipaka yule Kapteni...(uk. 76).

Katika mfano mwingine, msimulizi anaeleza kwamba Maafandi walikuwa wamejaa juu ya makochi. Wameshiba, vitambi viko juu, nyuso zao zinang'ara kwa mafuta. Sare zao zimekubali pasi, zimenyoka sawasawa, tepe zimejaa mabegani, (uk. 80).

Mavazi ya wakubwa wa magereza yanaelezwa ifuatavyo:

Chifu wa magereza amevaa pama ya rangi ya kijivu, ameivuta mpaka kwenye kipaji cha uso wake. alivaa shati la rangi ya hudhurungi aliloliacha likaning'inia juu ya suruali yake ya dreli ya rangi ya kisamli, (uk. 102)...Sare ya Mkuu wa Magereza inameremeta. Imekolea uwanga. Kaki imeiva barabara kwa pasi. Ukanda mweusi umepita katikati baina ya bega na pembe ya kiuno na kukamatana na ule aliojikaza nao kiunoni kama kibwebwe. Unang'ara kama vinavyong'ara viatu vyake. Tepe zimejaa tele mabegani. Kofia yake yenye kipaa kipajini imemkaa sawasawa kichwani...

Meja Mapanga amevaa sare yake ya kijeshi rangi ya kijani kibichi amekaa juu ya kiti kwa maringo. Kofia yake ya pama ameiweka juu ya meza anatikisatikisa miguu anamtazama Sururu. Wawili ni

maofisa wa polisi, na wao wamevaa sare zao za kaki. Wote wana vyeo vya Inspekta...(uk. 131).

Kutokana na mavazi haya ya maafisa wa usalama, inakuwa rahisi kuwatambua kwa cheo pindi wanapoingia kwenye jukwaa wakati wa utendaji.

5.3.5 Mavazi ya Khadija na Familia Yake

Khadija ni mhusika ambaye kutokana na mavazi yake, anatambulika kama mwanamke wa Uswahilini. Aila yake vilevile inajibainisha kama familia ya Waswahili kutokana na mavazi wanayovaa. Zaidi ya hayo, babake Khadija, mzee Mafta, ana sifa ya kuwa mcha Mungu wa dharti. Mavazi yake ya viongozi wa dini ya Kiislamu yanabainika moja kwa moja kutokana na maelezo ya msimulizi. Tazama:

Roho ilimtua (Khadija) pale aliposikia mlio wa viatu vyake [Mzee Mafta] vya makubadhi, taratibu anarudi nyumbani, amejizonga kashida shingoni na tasbihi yake mkononi. Amevaa kanzu ndefu amekaza kifungo shingoni, amevaa kizibao cheupe na kofia nzuri ya viua aliyoletewa zawadi Makunduchi...(uk. 145).

Kwa upande mwingine, kila Khadija anaposemekana kwamba anatoka nyumbani kwenda popote pale, au kumwona babake, msimulizi anaeleza kwamba alivaa buibui au khanga na kujitandia kichwani. Kwa mfano, msimulizi anaeleza kwamba, ‘Khadija alimlaza mtoto, akajifunga kanga vizuri na ya pili akajitanda kichwani akaenda kumsikiliza babake...’ (uk. 146). Khanga ni mavazi ambayo aghalabu huhusishwa na wanawake wa Uswahilini. Katika tukio lingine msimulizi anasimulia kwamba ‘Khadija alivaa buibui akatoka’ (uk. 148).

5.3.6 Wahusika Kuwa Uchi

Kuna baadhi ya matukio ambapo wahusika wanaonekana kutenda wakiwa uchi, yaani bila mavazi yoyote: mhusika wa kwanza ambaye hadhira inakutana naye akiwa uchi

ni Doto. Anapokea kichapo kutoka kwa vijana wa kwa Ba Mkwewe na kutupwa katika chumba alimo Hamza. Baada ya hapo tunaelezwa:

Mfano 5.25

Matako yanamwuma [Doto] makorodani yanamwuma, mwili mzima unamwuma. Hata hajui akae vipi. Hamza alisimama akavua shati lake, amvalishe ili kuupa stara uchi wake. lakini shati lenyewe si shati si wazimu, ni mararu yaliyonyambuka. Hivyo hivyo lilivyo, alimzonga nalo kiunoni angalau limsitiri ile sehemu ya mbeleni, yasitirike makorodani yake yaliyovimba na kuchunika...(uk. 49).

Hamza anapopelekwa akapokee adhabu yake katika chumba cha kiza tunaelezwa kwamba naye pia alivuliwa nguo, kama wanavyofanywa wengine wanaopelekwa kule:

Mfano 5.26

“Vua nguo!” Aliamrisha tena. Nguo zenyewe za kuazima, sasa anavuliwa wamkashifu tena, akawaza na kusema moyoni, “Ama kweli nguo ya kuazima haisitiri matako.” Lakini hata zingelikuwa si za kuazima, angelizivua tu. Hiyo ni sheria ya hapo. Ukifika hapo lazima wakuvue nguo kudhalilisha ule utu wako na kushusha ubinadamu wako. Alizivua akabaki uchi kama ile siku aliyozaliwa... (uk. 85).

Mlango wa chumba cha kiza ulipofunguliwa Hamza alijibanza ukutani akajikunyata ili kusitiri uchi wake. Ni siku nyingi tokea ahome Kumbakumba ambako uchi si kitu cha kusitiriwa. Hakudhubutu kusimama aadhirike mbele ya Koplo Usi na kikosi chake. Kwa Koplo Usi yale mambo ni ya kawaida tu. Kila siku chumba kile hakikosi mtu. Siku nyingine wawili au watatu, na wa humo lazima wawe uchi...(uk. 87).

Mbali na huku kuwekwa kwa wafungwa wakiwa uchi katika chumba cha kiza, msimulizi anaeleza kwamba kule Kumbakumba wote huoga kwa pamoja, na kwamba uchi hapo si kitu cha stara, (uk. 54).

Ikiwa matukio haya yatatendwa kwenye jukwaa mbele ya hadhira, haiamkiniki kwamba watendaji wawe uchi. Ni jambo la aibu na lisilokubalika. Hata hivyo,

ukarabati unaweza kufanywa na mwandalizi wa maleba, akatengeneza mavazi yanayofanana na ngozi ya mtendaji mahsusi na yambane hivi kwamba mtendaji huyo ataonekana kuwa uchi machoni pa hadhira, na vilevile kusitiri uchi wa mtendaji huyo.

5.4 Hitimisho

Imekuwa rahisi kupata maelezo ya kina kuhusu maleba vilevile mifano mwafaka katika riwaya ya *Haini*, sifa ambayo inaweka riwaya hii katika hali ya kuigizika kwa wepesi. Vivyo hivyo, maleba yametumika kwa njia faafu katika riwaya hii, na kwa kiwango kikubwa yanaingiliana na kukamilishana na vipengele vingine vya utendaji.

Maleba ni kipengele kimojawapo kati ya vinavyotajwa na Schechner (1988) miongoni mwa vipengele vingine vinavyofanikisha utendaji. Anadai kwamba maleba yakijumuishwa na vipengele kama vile kimya, sauti na mandhari vitajisuka kwa pamoja na kufanikisha utendaji husika. Ufaraguzi unaweza kufanywa katika matukio ambamo wahusika wanatenda wakiwa uchi wa mnyama. Katika utendaji kwenye jukwaa, si lazima watendaji wawe uchi wa mnyama bali wanaweza kuvaa chupi au mavazi ambayo yanafanana na ngozi zao hivi kwamba wanaowatazama watapata dhana kwamba watendaji hao wako uchi.

Katika sura hii, tumejadili taswira za kifilamu, mandhari ambamo utendaji unatukia na maleba ya wahusika mbalimbali katika riwaya ya *Haini*. Tumetoa mifano kutoka riwaya teule na kuijadili.

SURA YA SITA

MATOKEO, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

6.0 Utangulizi

Sura hii ni mukhtasari wa utafiti huu. Tumetoa mukhtasari wenyewe kwa kuzingatia suala la utafiti, malengo, nadharia tete, nadharia na hata mbinu za utafiti. Tumetoa maoni wa na mapendekezo ya tafiti za baadaye. Mapendekezo haya huenda yakawapa watafiti wajao ari ya kutafakari na kuona iwapo wanaweza kuendeleza tafiti mbalimbali. Waandishi, hasa wa riwaya, pia huenda wakachochea kuandika kwa namna tofauti.

6.1 Muhtasari Wa Utafiti

Tulichunguza vipengele vya utendaji, kuvibainisha na kuvichanganua. Katika kuchunguza lugha ya majibizano, tulibainisha majukumu ambayo lugha hii imepewa itekeleze, na kuiainisha kwa mujibu wa majukumu hayo. Hapa, tulipata majukumu sita ambayo ni pamoja na kuhoji, kupasha habari, kushawishi, kuliwaza, kuhamasisha na kuendesha mashtaka. Lugha hii ya majibizano imetekeleza majukumu yake kikamilifu. Kwa mfano, inahoji na katika kuhoji, tunapata habari zinazotufichulia mambo yanayotendeka. Mfano wa majibizano haya ni yale ya afisaa sita wa usalama wakimhoji Hamza. Wanamuuliza maswali kuhusu Barakati na Hamduni (mshukiwa mkuu wa mauaji ya Kigogo). Maafisa hawa hawa wanawahoji mahaini wengine kama vile Sururu, Haramia (na mashahidi wengine) ili kuweza kupata ukweli wao kwa nia ya kuubadilisha ushahidi uweze kuafiki kesi ya serikali.

Lugha ya majibizano imetumika kwa wingi katika riwaya ya *Haini*. Majibizano haya yamejitokeza katika muundo wa (ya) sentensi fupi fupi wakati wahusika wakizungumza, hali inayochochea utendaji wa riwaya teule.

Tumechanganua nafasi inayochukuliwa na wahusika katika utendaji wa kidrama kwa kuwaainisha kwa mujibu wa utendaji wao. Hapa tulipata makundi makuu matano ya wahusika. Makundi haya ni: mahaini, mashahidi, wakubwa wa magereza, washikadau mahakamani na waathiriwa wa uhaini. Japo wahusika ni wengi katika kila kundi, tuliwachanganua wale ambao wanahusika katika utendaji wa kipekee. Tumewateua wahusika wanaodhihirisha upekee wa aina fulani katika kutenda kwao, tukawajadili na kutoa mifano. Kwa mfano, kuna mahaini takriban 15, huku mashahidi wakiwa tisa. Miongoni mwa mahaini 15 tuliobainisha, tuliwajadili Hamza, Sururu, Doto, Faraji na Shekhe Mandundu. Japo tumewajadili mashahidi wawili pekee; Haramia na Pwacha, mashahidi wote ni tisa. Tulimjadili Kanali Bunju miongoni mwa wakubwa watano wa magereza. Miongoni mwa washikadau mahakamani, tuliwajadili Chopra na mahakimu na hatimaye, japo nchi nzima iliathiriwa na tukio hili la uhaini, tumemwangazia Khadijah kwa kina.

Wahusika wameteuliwa na kupewa utendaji ipasavyo. Sifa ambazo msimulizi amewapa zinaafiki nafasi za utendaji alizowakabidhi, hali ambayo itafanikisha utendaji wa kidrama wa riwaya ya *Haini* iwapo itaigizwa kwenye jukwaa.

Kwa upande mwingine, tumebaini kwamba wapo baadhi ya wahusika waliopungukiwa kiutendaji; hawajatenda kikamilifu uhusika waliopewa. Kwa mfano, Chopra ameshindwa kuandaa ushahidi wa kutosha dhidi ya wahusika wakuu kama vile Hamza. Hamza anapotoa maelezo yake anadai kwamba ushahidi uliotolewa dhidi yake si thabiti na hata Chopra mwenyewe anapomhoji Hamza anashindwa kumjibu

maswali anayomuuliza badala ya yeye Chopra, kama mwendeshaji mashtaka kumbana Hamza kwa maswali.

Mhusika Zonga, ambaye ni jasusi aliyewekwa chumba walimo Hamza ili kupata habari kutoka kwao hajatekeleza uhusika huu kikamilifu. Anajitokeza katika tukio moja pekee, na akiwa pamoja na mahaini chumbani, badala ya kujihusisha na mazungumzo yao ili adadisi mambo, yeye anajitia kulala kila wakati, utendaji unaomnyima fursa ya kufanikiwa kupata habari zozote zile. Pwacha naye, ambaye ni mmoja wa mahaini anatenda kama jasusi zaidi ya anavyotenda kama haini. Anaduhushi habari zozote pale chumbani na kuwapelekea wakubwa wa magereza, shughuli ambayo ilifaa kutekelezwa na Zonga. Wahusika kama vile mahakimu wametia fora katika utendaji wao, tofauti na ilivyotegemewa, kwa kutoa hukumu ya haki kwa kila mshtakiwa.

Katika sura ya nne, tumejadili masimulizi ya utendaji, vimulimuli na kiza, kimya na sauti. Masimulizi ya utendaji ni kipengele cha kimsingi cha utendaji kwa kuwa hueleza namna tendo fulani linastahili kutekelezwa kwenye jukwaa. Katika riwaya ya Haini, tumebainisha aina nne za masimulizi ya utendaji. Haya ni kama vile masimulizi ya utendaji kuhusu mateso, usafiri, utendaji wa mahakamani na kuhusu faraja.

Masimulizi haya ya utendaji yanaeleza waziwazi namna matukio yanayotendwa yanavyofaa kutekelezwa kwenye jukwaa. Kwa mfano, tumetoa mifano ya masimulizi kuhusu mateso ambayo yanatuchorea picha kamili ya namna mahaini mbali mbali wanavyoteswa na askari jela. Kwa mfano, masimulizi kuhusu namna Hamza anavyopigwa baada ya kukataa kushirikiana na akina Kanali Bunju, (uk. 40-41), Doto

anavyopigwa kabla ya kutupwa kwenye chumba alimo Hamza (uk. 46-48) na vilevile Sururu anvyoteswa baada ya kukataa kutia sahihi kwenye jalada la maelezo ya uongo aliyoandikiwa kwamba ni ushahidi wake (uk. 132-133). Riwaya hii inapoigizwa kwenye jukwaa, mwelekezi anafaa kuzingatia maelezo haya ya utendaji na kuhakikisha kwamba watendaji wanayatekeleza kama yalivyoelezwa. Kwa kufanya hivyo, masimulizi haya yatafanikisha utendaji wa riwaya hii.

Tumechunguza vimulimuli na kiza. Katika kutafitia vipengele hivi tumebaini kwamba, japo vyenyewe si vipengele vya kimsingi vya utendaji, vinaweza kujumuishwa katika kazi za kidrama ili kuboresha utendaji husika. Katika riwaya ya *Haini* kwa mfano, vimulimuli vimetumiwa katika kuwezesha kuona, kuleta matumaini na kuashiria hatari. Kwa upande mwingine, kiza kimetumiwa kubainisha wakati, kuashiria mateso na maovu na vilevile kujenga hali ya kutamauka.

Vipengele vingine tulivyoangazia katika sura ya tatu ni sauti na kimya. Mwandishi amefanikiwa kutumia sauti ili kuzua hofu na wasiwasi, kuashiria hali ya hatari, kuwasiliana na kuwapa wafungwa tumaini. Kimya nacho kimetumiwa hasa kujenga hali ya hofu na wasiwasi na kuibua hali ya taharuki. Ikumbukwe kwamba matukio mengi yanatukia katika magereza, ambako kumeshamiri mateso na hali ngumu ya maisha. Vipengele hivi vinne; sauti na kimya, kiza na vimulimuli vimetumiwa kwa njia faafu kujenga hali inayoashiria maisha ya wafungwa hawa, na hasa maisha ya mahaini yalivyo. Vikitumika vizuri kwenye jukwaa, na kushirikishwa ipasavyo na vipengele vya kimsingi vya utendaji vitafanikisha utendaji wa kidrama wa riwaya ya *Haini*.

Sura ya tano imeangazia taswira za kifilamu, mandhari na maleba. Taswira za kifilamu, kwa maoni yetu, ni zile ambazo zinahamisha msomaji kutoka dunia yake

halisi na kumpeleka kimawazo na kihisia katika ulimwengu ambamo tukio husika linatendeka, na hivyo kuipa kazi husika sifa za kifilamu. Katika kuzichanganua taswira za kifilamu tulizobainisha katika riwaya teule, badala ya kuzigawa katika makundi mbali mbali kama tulivyofanya katika vipengele vingine tulivyojadili, tumejadili matukio ya utendaji ambamo taswira hizi zimetumika kikamilifu. Hapa, tulitoa mifano ya matukio kama vile Hamza kupigwa nusura afe (uk. 40-41), Hamza kutumbukizwa kwenye kisima chenye maji na kupigwa risasi japo hakuna iliyompata, tukio la Haramia kufungiwa chumba kimoja na chatu hadi anamkata na kumuua kwa meno yake, ambalo ni tukio linaloshika hisia za msomaji zaidi katika riwaya hii.

Taswira hapa inalifanya tukio hili kuwa kama filamu ya kutisha na inayoogofya ambayo mtazamaji anatazama, na hutuliza misuli pale tu ambapo Haramia ananusurika baada ya kumuua chatu huyu. Tumejadili tukio la mashahidi wale tisa kupelekwa kwenye uwanja, kila mtu mbele ya kaburi lake na namna utendaji unatekelezwa katika tukio lenyewe. Vilevile, tumejadili namna mahaini walivyosafirishwa hadi mahakamani. Kama tulivyoeleza hapo awali, taswira za kifilamu zinafungamana sana na utendaji. Hii ndiyo sababu inazifanya ziingiliane kwa karibu sana na masimulizi ya utendaji. Tofauti iliyopo ni kwamba matukio ambamo taswira za kifilamu zimetumika yanavuka mipaka ya usomaji na kumwingiza msomaji katika ulimwengu ambamo tukio hilo linatukia. Anakuwa mtazamaji, mbali na kuwa msomaji tu kama ilivyo katika masimulizi ya utendaji.

Mandhari pia yameshughulikiwa katika sura ya tano. Masimulizi ya riwaya ya *Haini* yanahusu mateso na udhalimu, jambo linalomfanya mwandishi ateue mandhari ambayo yataibua hali zinazoambatanishwa na hali hizi. Tumbainisha mandhari kama mahaini wanakofungiwa na kueleza hali mbaya za vyumba hivyo, tukaeleza pia

kuhusu mahaini wanakohojiwa na kushawishiwa na vilevile wanakoteswa. Tumeeleza katika kujadili kipengele hiki kwamba japo wafungwa hawa wapo gerezani, wanapelekwa katika mandhari tofauti wakati wakihojiwa au kushawishiwa, ili kuleta athari ambayo maafisa hawa wanaikusudia. Kwa mfano, Hamza anapelekwa kwenye chumba safi, kinachofanana na ofisi, analetewa chakula kizuri na mwanamke anayependeza na kuna upepo mzuri kutoka kwenye bahari inayomvutia kutoka pale alipo. Mandhari haya yananuiwa kumfanya ashawishike, atoe ushahidi wa uongo wanaoutaka maafisa hawa. Mandhari yameteuliwa kwa ufaafu na yanafanikisha utendaji wa matukio yanayotukia katika mandhari mbalimbali tuliyojadili.

Hatimaye tumeshughulikia kipengele cha maleba. Haya ndiyo mavazi yanayotutambulishia wahusika katika tukio fulani ni akina nani. Yapo mavazi ya wafungwa, yanayowatofautisha na polisi. Polisi na maafisa wa magereza vilevile wana sare zinazotambulisha wao ni aina gani ya maafisa; makoplo na makanali, na hata kuonyesha vyeo vya wahusika mahsus. Mwandishi anateua mavazi anayowavisha wahusika wake hivi kwamba yanaendana na utendaji wao. Kwa mfano, wapo polisi ambao wanavishwa nguo za kiraia ili wasitambulike kwamba wao ni polisi. Hali hii inawawezesha kufanya upelelezi bila kutambulika kwamba wao ni polisi.

Tumbainisha matukio ambamo baadhi ya wahusika hasa mahaini wanatenda wakiwa ama uchi, au wakiwa na mavazi ambayo yamechanika hivi kwamba hayafichi uchi. Hata hivyo, kumfanya mtu, awe mfungwa au huru kukaa uchi wa mnyama ni kukiuka haki za kibinadamu. Tunahitimisha kwamba, maleba katika riwaya ya Haini yamefanikisha utendaji wake kwa kiasi kikubwa. Hata hivyo, matukio ambamo wahusika wanatenda wakiwa uchi yafanyiwe ufaraguzi. Mavazi yanayomfanya

mtendaji kuonekana kama ambaye yupo uchi yanaweza kutumiwa badala yake kwenda kwenye jukwaa akiwa uchi wenyewe.

Misingi ya nadharia tuliyotumia katika utafiti huu imechangia katika kubainisha vipengele vya utendaji katika riwaya ya Haini. Hata hivyo, imedhihirika kwamba pana haja ya ama nadharia mpya ya utendaji kubuniwa au nadharia iliyopo kupanuliwa zaidi. Hii itawezesha Nadharia ya Utendaji kutumiwa kufafanua vipengele vya utendaji kama vile taswira za kifilamu, kipengele ambacho hakijagusiwa popote katika maelezo ya nadharia hii.

Nadharia ya Utendaji ilitupatia msingi wa kuchanganua data. Kwa mfano, baada ya kubainisha vipengele vya utendaji tulivyochunguza katika riwaya ya Haini, tulivigawa katika makundi, hivi kwamba tuliweka wahusika katika kundi moja kando na masimulizi ya utendaji. Baadaye tukagawa makundi haya katika makundi madogo zaidi ya uchanganuzi.

Hatimaye, Nadharia ya Utendaji ilituwezesha kutathmini ufaafu wa vipengele vya utendaji katika utendaji wa kidrama wa riwaya ya Haini. Maelezo ya nadharia hii, kwa mfano kuhusu watendaji, yanaeleza wazi wazi namna ambavyo watendaji wanaoteuliwa kuchukua nafasi za wahusika wanavyofaa kuwa; wawe na sifa zinazowiana na za wahusika wanaowawakilisha na watende kama wahusika hao.

Utafiti huu umeakisi kuwa utendaji sio suala la sanaa za maonyesho na fasihi simulizi pekee bali lipo na linabainika hata katika kazi za kinathari kama riwaya na hadithi fupi.

6.2 Matokeo ya Utafiti

Utafiti huu uliazimia kuchunguza utendaji wa kidrama katika riwaya ya Haini kwa malengo ya: kwanza, kubainisha lugha ya majibizano na wahusika katika riwaya ya Haini. Pili, kuchunguza masimulizi ya utendaji na taswira za kifilamu katika riwaya ya Haini na hatimaye, kutathmini ufaafu wa vipengele vya utendaji katika utendaji wa kidrama wa riwaya ya Haini. Ili kutimiza malengo haya, tulichunguza vipengele vya utendaji ambavyo ni pamoja na lugha ya majibizano, nafasi ya wahusika, masimulizi ya utendaji na taswira za kifilamu. Vipengele visaidizi tulivyochunguza ni pamoja na kimya na sauti, kiza na vimulimuli, mandhari na maleba.

Tuliweza kubainisha lugha ya majibizano na nafasi ya wahusika katika riwaya teule. Tulifanikiwa vilevile katika uchunguzi wetu wa taswira za kifilamu na masimulizi ya utendaji na hatimaye tukatathmini ufaafu wa vipengele hivi katika utendaji wa kidrama katika riwaya ya *Haini*.

Uchunguzi na uchanganuzi wa data ulithibitisha nadharia tete zetu kwamba kwanza, lugha ya majibizano imetumika katika riwaya ya *Haini* na kwamba nafasi ya wahusika itafanikisha utendaji wa kidrama wa riwaya ya *Haini* iwapo itaigizwa kwenye jukwaa. Pili, kwamba masimulizi ya utendaji na taswira za kifilamu zimetumika katika riwaya hii. Tatu, kwamba, vipengele vya utendaji katika riwaya ya *Haini* vitachangia kufanikisha utendaji wa kidrama wa riwaya yenyewe.

6.3 Hitimisho

Kutokana na matokeo ya utafiti huu, tunaona kwamba vipengele vya utendaji; vya kimsingi na visaidizi vimejumuishwa katika masimulizi ya riwaya ya *Haini*.

Vipengele hivi vikitumika kwa pamoja kwa njia ifaayo vitafanikisha utendaji wa kidrama wa riwaya ya *Haini* kwenye jukwaa.

Kuna umuhimu wa riwaya ya *Haini* kutendwa kwenye jukwaa. Kwanza, utendaji wake utanufaisha hadhira kubwa na pana kuliko hali ilivyo katika usomaji wake tu. Hii ina maana kwamba, masuala ya kisiasa yanayotokea katika nchi hasa za Kiafrika, masuala ya kijamii na ya kiuchumi yaliyoangaziwa kwenye riwaya hii yatapokelewa na hadhira hii kubwa.

6.4 Mapendekezo

Kutokana na utafiti huu tumeweza kutambua kwamba pana haja ya utafiti zaidi kufanywa kuhusu suala la utendaji kwa jumla na namna linavyobainika katika tanzu za kinathari. Kufikia sasa, tafiti nyingi zinazohusu utendaji hufanywa tu katika utanzu wa tamthilia, fasihi simulizi na sanaa za maonyesho. Utafiti zaidi kuhusu utendaji katika riwaya mbalimbali ufanywe, kwa mfano katika riwaya kama vile *Unaitwa Nani* ya Wamitila ambamo wahusika wanatumia lugha ya majibizano kwa wingi.

Tunapendekeza kwamba utafiti zaidi kuhusu taswira za kifilamu ufanywe katika riwaya zingine; ama za Shafi Adam au za waandishi wengine wa riwaya za Kiswahili. Hiki ni kipengele muhimu cha utendaji ambacho kinaweza kuchunguzwa katika kazi anuwai za fasihi.

Ni pendekezo letu kwamba riwaya ziandikwe kwa namna ya kuigizika ili ujumbe na maudhui kuifikia hadhira pana zaidi pale zinapoigizwa jukwaani. Riwaya zinazodaiwa kuwa changamano kama vile Babu Alipofufuka zingeigizwa kwenye jukwaa zingepata hadhira pana. Kama tulivyoeleza, utendaji hufaidi hadhira pana zaidi ya usomaji wake.

Hatimaye, tunapendekeza kwamba riwaya ya *Haini* iandikiwe mchezo wa kuigiza na kuwekwa kwenye jukwaa mbele ya hadhira. Hii ni kwa sababu, moja, tumejadili vipengele vya utendaji tulivyobainisha katika riwaya hii na kuonyesha namna vinafanikisha utendaji wake. Ni wazi hivyo kwamba ikiwa patakuwa na juhudi za kuitenda riwaya hii kwenye jukwaa, utendaji wake utafanikiwa.

MAREJELEO

- Banks, R. A. (1985). *Drama and Theatre Arts*. London: Hodder and Stoughton.
- Cuddon, J. (1991). *A Dictionary of Literary Terms and Literary Theory*. Blackwell Publishers Ltd. www.researchgate.net. (Retrieved on 05/05/2016: 11:05 am).
- Diegner, L. (2003) *Mazungumzo na Adam Shafi juu ya Uandishi wake wa Riwaya*. www.qucosa.de/fileadmin/data/qucosa/documents/9837/18-04-shafiDiegner.pdf. (Retrieved on 03/02/2016).
- Elena, B. (2002). 'When Grandfather Came To Life Again: Said Ahmed Mohamed's New Novel Beyond Realism'. Paper presented at the 15th Swahili Colloquium, Beyruth, Germany.
- Epskamp, K. (1984). *Learning by Performing Arts: From Indigenous to Endogenous Cultural Development*. C.E.S.O Paperback. No. 16.
- Etherton, M. (1982). *The Development of African Drama*. Johannesburg: Hutchington University Library for Africa.
- Foster, E. (1927). *Aspects of the Novel*. New York. www.rosettbooks.com/AspectsOfTheNovel.
- Francoise, G. (1981). Masked Dances and Ritual in Tanzania, Mozambique and Zambia. *The Drama Review*. Vol 25, No. 4. Massachusetts Institute of Technology.
- Gill, R. (2006). *Mastering English Literature (Toleo la Tatu.)* Houndmills. Palgrave Macmillan.
- Goldfarb, A., & Wilson, E. (2002). *Theatre: the Lively Art*. New York: McGrawHill Companies.
- Gromov, M. (1998). 'Nagona and Mzingile: Novel, Tale or Parable?' *Katika Jarida la Afrikanische Arbeitspapiere* 55: Kiswahili Forum V. 73-78.
- Gromov, M. (2008). Swahili Popular Literature in Recent Years. *Swahili Forum* 15: 5-13.
- Gromov, M. (1996). 'Tanzanian Prose in the Early 90s'. AAP 47.
- Gromov, M. (2004). 'Post-Modernist Elements in Recent Kiswahili Novels'. *Katika 'The Nairobi Journal of Literature: The Journal of The Department of Literature* (28-36) Nairobi: University of Nairobi.
- Herman, R. (1947). *The Literary Theory Toolkit: A Compendium of concepts and Methods*. (1st. Ed.). Blackwell Publishing Ltd.
- Kisurilia, E. (2000). *Usawiri wa Wahusika katika kazi za Katama G.C Mkangi*. Tasnifu ya Chuo Kikuu cha Moi. Haijachapishwa.

- Kothari, C. (2004) (2nd Rv. Ed). *Research Methodology: Methods and Techniques*. India: New Age International Publishers.
- Longhorn (2011). *Kamusi ya Karne ya 21*. Nairobi: Longhorn Publishers.
- Madison, D. & Hamera, J. (2005) *Performance Studies at the Intersections. The Sage Handbook of Performance Studies*. www.sagepub.com. (Retrieved on 05/12/2015: 9:00 am).
- Madison, D., & Hamera, J. (2005). *Performance of and Beyond Literature. The Sage Handbook of Performance Studies*. www.sagepub.com. (Retrieved on 05/12/2015: 9:00 am).
- Madumula, J. (1995). *Riwaya ya Kiswahili*. Dar-es-Salaam University Press.
- Malas, A. (2012). 'The Darkness in William Shakespeare's Play Macbeth: A Study.' *The Criterion: An International Journal in English*. Vol 3. Issue, 3. www.thecriterion.com. (Retrieved on 09/03/2016 (10:58am).
- Mercy, G. (2014). 'Language of Silence in The Plays of Harold Pinter.' *International Journal of English Language, Literature and Humanities*. Vol, 2. Issue 6. www.ijellh.com. (Retrieved on 08/03/2016 (12:06 pm).
- Mihangwa (2012) *Mwandishi Shafi Adam Shafi*. www.hapakwetu.blogspot.com. (Retrieved on 03/01/2016, 4:41 pm.)
- Mlama, P. (1981). Didubi: A Tanzanian Indigenous Theatre Form. *The Drama Review*, Vol 25, No. 4, Winter. Massachusetts Institute of Technology.
- Mogere, G. (2007). *Taswira ya Gereza Inavyoendeleza Maudhui katika Riwaya ya Haini ya Shafi Adam Shafi*. Tasnifu ya Chuo Kikuu cha Nairobi. Haijchapishwa.
- Muda, Z. (1993). *When People Play People: Development Communication Through Theatre*. Johannesburg: Witwatersrand University Press.
- Muhando, P., na Balisidya (1976). *Fasihi na Sanaa za Maonyesho*. Dar-es-Salaam: Tanzania Publishing House.
- Muir, K. ed. (2004). *The Arden Shakespeare: Macbeth*. New Delhi: East West Press.
- Mulokozi, M. (1996). *Utangulizi wa Fasihi ya Kiswahili*. Dar-es-Salaam: TUKI.
- Mumbo, K. (2012). 'Artistic Techniques of Expression in the Performance of the Mijikenda Naming Ceremony 'Vyalusa' of Kenya'. *Matatu* 41: Amsterdam & New York; Radopi.

- Mumbo, K. (2014). *'Uchunguzi wa Kidrama wa Riwaya ya Kiswahili na Maendeleo ya Fasihi Afrika Mashariki: Unaitwa Nani? K.W.Wamitila'*. Makala iliyowasilishwa katika kongamano la kwanza la kimataifa kuhusu kutafitia fasihi za Kiafrika katika karne ya 21. Chuo Kikuu cha Pwani. Dec, 11-13. (hajachapishwa).
- Mumbo, K. (1997). *Sanaa za Maonyesho za Mijikenda: Mbinu za Uwasilishaji hali Miongoni mwa Wachonyi, Wagiriama na Wajibana*. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Moi. (hajachapishwa).
- Mumbo, K., & Mwari, A. (2016). *Sauti kama Mhusika na Uwasilishaji wa Maudhui katika Tamthilia ya Kimya Kimya Kimya ya Said. A. Mohamed*. Makala iliyowasilishwa tarehe nane Septemba, 2016 kwenye kongamano la CHAKITA la kumuenzi Prof. Abdulaziz. RISSEA.
- Murungi, G. (2013). *Mtindo Unavyoendeleza Maudhui Katika Natala*. Tasnifu ya Chuo Kikuu cha Nairobi. (Hajachapishwa).
- Mwamzandi, I. (2002). *'Majadiliano Tanzu Katika Ushairi wa Kiswahili'*. *Katika Inyani Simala (mh)*. (2002). Utafiti wa Kiswahili. Eldoret: Moi University Press.
- Mwanakombo, N. (2016). *Zaidi ya Burudani: Utendaji Katika Nyimbo za Msondo, Mvita*. Makala iliyowasilishwa tarehe nane Septemba, 2016 kwenye kongamano la CHAKITA la kumuenzi Prof. Abdulaziz. RISSEA.
- Mwenda, M (2001). *Kamusi ya Fasihi*. Nairobi: Standard Textbooks Graphics and Publishing.
- Ngugi wa Thiong'o. (1986). *Decolonising The Mind: The Language of African Theatre*. Nairobi: Heinemann Kenya.
- Njogu, K., & Chimerah, R. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi Nadharia na Mbinu*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.
- Nkwera, F.V (1978). *Sarufi na Fasihi: Sekondari na Vyuo*. Dar-es-Salaam: Tanzania Publishing.
- Nyambura, K. (2014). *Utendaji katika Tamthilia za Sudana na Kimya Kimya Kimya*. Tasnifu ya shahada ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Nairobi. (Hajachapishwa).
- O'Quinn, J. (ed) et al (1981). African Performance Issue. *The Drama Review*, Vol 25. Winter. Massachusetts Institute of Technology.
- Omar, A. (2014). *Kuchunguza Dhamira za Kijamii na Kiutamaduni katika riwaya ya Kiswahili: Mifano kutoka Kuli na Vuta n'Kuvute*. Tasnifu ya Uzamifu, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.
- Ricard, A. (2000). *Ebrahim Hussein: Swahili Theatre and Individualism*. Dar-esSalaam: Mkuki na Nyota Publishers.

- Said, M. (2001). *Babu Alipofufuka*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.
- Sandra, S. et al (ed). (2012). *Language in African Performing and Visual Arts*. Selected Papers from a Conference held at Yale University.
- Schechner, R. (1988). *Performance Theory*. United Kingdom: Routledge.
- Schechner, R. (1985). *Between Theatre and Anthropology*. Philadelphia: University of Pennsylvania Press.
- Schechner, R. (2013). (3rd ed.). *Performance Studies: An Introduction*. USA and Canada: Routledge.
- Senkoro, F. (2011). *Fasihi: Mfululizo wa Lugha na Fasihi, Kitabu cha Kwanza*. Dares-Salaam: KAUTTU Limited.
- Senkoro, F. (1982). *Fasihi na Jamii*. Dar es Salaam: DSM Press and Publicity.
- Shafi, A. (2003). *Haini*. Nairobi: Longhorn Publishers Ltd.
- Shafi, A. (2013). *Mbali na Nyumbani*. Nairobi: Longhorn Publishers.
- Shafi, A. (1978). *Kasri ya Mwinyi Fuad*. Dar-es-Salaam: Tanzania Publishing House.
- Shafi, A. (1979). *Kuli*. Nairobi: Longhorn Publishers.
- Simon, E. (2007). *Uhakiki wa Haini kama Riwaya ya Kihistoria*. Tasnifu ya Chuo Kikuu cha Nairobi. Haijchapishwa.
- Soyinka, W. (1988). *Art, Dialogue and Outrage: Essays on Literature and Culture*. Ibadan: New Horn Press.
- Soyinka, W. (1976). *Myth, Literature and the African World*. Cambridge: Cambridge University Press.
- Stanislavsky, C. (1948). *An Actor Prepares, Theatre Atrs*. New York.
- Swahili Forum 18 (2011) 37-68. 'Mazungumzo na Adam Shafi Juu ya Uandishi wake wa Riwaya': Adam Shafi na Lutz Diegner.
- Toolan, M. (1988). *Narrative, A Critical Linguistic Introduction: Narrative Performance*. (2nd ed.)
- Traore, F. (2002). *Investigating Topics and Style in Vuta n'Kuvute by Shafi Adam Shafi*. Swahili Forum ix, AAP 72 (35-41).
- TUKI (2004). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Nairobi: Oxford University Press.
- TUKI (2006). *Kamusi ya Kiingereza-Kiswahili Toleo la tatu*. Dar-es-salaam: Tanzania.

- Victor, T. (1982). *From Ritual to Theatre: The Human Seriousness of the Play*. New York: Performing Arts Journal.
- Wafula, R.M., na Njogu, K. (2007). *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.
- Walibora, K. (2013). *Ujasiri wa Kujumulika katika Uandishi wa Kiswahili*. www.swahilihub.com. (Retrieved on 06/01 2016).
- Wallace, B. (1894). *The Art of Interpretation. Performance of and Beyond Literature. The Sage Handbook of Performance Studies*. www.sagepub.com. (Retrieved on 05/12/2015: 5:00 am).
- Wamitila, K. (2003) *Uhakiki wa Fasihi. Misingi na Vipengele Vyake*. Nairobi: Phoenix Publishers Ltd.
- Wamitila, K. (2003). *Kamusi ya Fasihi Istilahi na Nadharia*. Nairobi: Focus Books.
- Wamitila, K. (2003). *Kichocheo cha Fasihi Simulizi na Andishi*. Nairobi: Focus Books.
- Wamitila, K. (2008). *Kanzi ya Fasihi, Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*. Nairobi: Vide ~Muwa Publishers.
- Wellek, R., na Warren, A. (1978). *Theory of Literature*. London: Penguin Books.
- Willet, J. ed. (1967). *The Theatre of Bertolt Brecht. A Study From Eight Aspects*. London: Methuen and Co.Ltd.
- Willet, J. Trans & ed. (1978). *Brecht On Theatre: The Development of an Aesthetics*. London: Eyre Methuen.